# KAMATI YA UANGALIZI WA UCHAGUZI TANZANIA

# TEMCO

REDET - LEAD AGENCY OF TEMCO

# RIPOTI YA WATAZAMAJI WA UCHAGUZI MKUU WA TANZANIA, 2015

MAY 2016

## YALIYOMO

**YALIYOMO** ..... I
**ORODHA YA MAJEDWALI** ..... VI
**ORODHA YA VIELELEZO** ..... VIII
**ORODHA YA VIAMBATANISHO** ..... IX
**VIFUPISHO** ..... X
**CHAPTER 1 MFUMO WA TEMCO WA UTAZAMAJI WA UCHAGUZI** ..... 1
1.1 Usuli na Muktadha ..... 1
1.2 Dira na Malengo ..... 1
1.3 Upeo katika Utazamaji wa Chaguzi ..... 2
1.4 Faida Zitokanazo na Utazamaji wa Chaguzi na Vigezo vyaTathmini ..... 4
1.5 Mfumo wa Utazamaji wa Uchaguzi Mkuu ..... 5
1.6 Mpango wa Mgawanyo wa Vituo na Waangalizi ..... 9
1.7 Ripoti za Awali kuhusu Michakato ya Chaguzi ..... 10
1.8 Mbinu za Ukusanyaji wa Taarifa kuhusu Mwenendo wa Uchaguzi ..... 12
1.8.1 Utazamaji wa Kina katika Maeneo ya Uchaguzi ..... 12
1.8.2 Mahojiano ..... 12
1.8.3 Mapitio na Marejeo ya Nyaraka Muhimu ..... 12
1.8.4 Matumizi ya TEHAMA ..... 13
1.8.5 Mitando ya Ushikiano na Mahusiano ..... 16
1.9 Vigezo katika Kutathmini Chaguzi ..... 18
1.10 Mtiririko na Maudhui ya Ripoti ..... 19
1.11 Shukrani ..... 21
**CHAPTER 2 MAZINGIRA YA KISIASA KUELEKEA UCHAGUZI MKUU** ..... 24
2.1 Utangulizi ..... 24
2.2 Serikali ya Umoja wa Kitaifa na Siasa za Uchaguzi Zanzibar ..... 24
2.3 Utendaji wa Serikali ya Awamu ya Nne (2005-2015) ..... 26
2.4 Chaguzi Ndogo na Chaguzi Ngazi Msingi 2014 ..... 31
2.5 Mchakato wa Katiba Mpya ..... 32
2.6 Migogoro na Makundi ya Ndani ya Vyama vya Siasa ..... 36
2.7 Hali ya Uhodhi wa Chama Tawala Kuelekea Uchaguzi Mkuu wa 2025 ..... 42
2.8 Hitimisho ..... 42
**CHAPTER 3 MIFUMO YA KISHERIA NA KITAASISI KWA UCHAGUZI WA MWAKA 2015** ..... 44
3.1 Utangulizi ..... 44
3.2 Mifumo ya Kisheria kwa Uchaguzi wa Mwaka 2015 ..... 44
3.2.1 Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ..... 44
3.2.2 Sheria ya Taifa ya Uchaguzi ..... 45
3.2.3 Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ..... 45
3.2.4 Sheria ya Gharama za Uchaguzi ..... 46
3.2.5 Sheria ya Vyama vya Siasa ..... 46
3.2.6 Katiba ya Zanzibar ..... 46
3.2.7 Athari za Mfumo wa Kisheria katika Uchaguzi wa Mwaka 2015 ..... 48
3.3 Vyombo vya Kusimamia Uchaguzi ..... 49
3.3.1 Tume ya Taifa ya Uchaguzi ..... 49
3.3.2 Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ..... 53
3.4 Uhuru wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ..... 55
3.5 Uhusiano kati ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ..... 55

3.6 Uwekaji wa Mipaka ya Majimbo ya Uchaguzi ........ 56
3.7 Kulinda Kura na Shauri la "Mita 200" ........ 57
3.8 Hitimisho na Mapendekezo ........ 58
3.8.1 Hitimisho ........ 58
3.8.2 Mapendekezo ........ 58
**CHAPTER 4 UANDIKISHAJI WA WAPIGAKURA ........ 60**
4.1 Utangulizi ........ 60
4.2 Uhalali wa Kuanzishwa kwa Teknolojia ya BVR ........ 60
4.3 Mifumo ya Kitaasisi na Kisheria iliyoongoza Uandikishaji wa Wapigakura ........ 62
4.4 Menejimenti ya Mchakato wa BVR ........ 63
4.4.1 Rasilimali Watu ........ 63
4.4.2 Utoshelevu wa Fedha, Vituo vya Uandikishaji na Vifaa vya BVR ........ 66
4.5 Elimu ya Mpigakura Wakati wa Uandikishaji ........ 72
4.6 Ukiukwaji wa Taratibu, Changamoto na Hatua Zilizochukuliwa ........ 73
4.6.1 Uandikishaji wa Wahamiaji Haramu na Wageni ........ 73
4.6.2 Utambuzi wa Alama za Vidole ........ 74
4.6.3 Misururu Mirefu katika Vituo vya Kuandikisha Wapigakura ........ 75
4.6.4 Malipo Haba kwa Waandikishaji wa Wapigakura ........ 75
4.6.5 Uwezo Mdogo wa Waandishi ........ 76
4.7 Makadirio na Idadi Halisi ya Walioandikishwa Kupiga Kura ........ 76
4.8 Tathmini ya Jumla ya Zoezi la Uandikishaji Wapigakura ........ 77
4.9 Hitimisho na Mapendekezo ........ 78
4.9.1 Hitimisho ........ 78
4.9.2 Mapendekezo ........ 79
**CHAPTER 5 UTEUZI WA WAGOMBEA ........ 80**
5.1 Utangulizi ........ 80
5.2 Muktadha wa Kisheria na Utaratibu wa Vyama kufanya Uteuzi ........ 80
5.3 Uteuzi Ndani ya Vyama ........ 80
5.3.1 Uteuzi wa Wagombea Urais ndani ya CCM ........ 81
5.3.2 Uteuzi wa Mgombea Urais wa CHADEMA ........ 84
5.3.3 Uteuzi ndani Vyama Vingine ........ 85
5.4 Uteuzi Nafasi za Ubunge na Udiwani ........ 85
5.4.1 Chama Cha Mapinduzi ........ 87
5.4.2 Uteuzi wa Madiwani ........ 87
5.4.3 Chama cha Wananchi (CUF) ........ 88
5.4.4 CHADEMA ........ 88
5.4.5 Uteuzi wa Udiwani ........ 89
5.5 Uteuzi wa Wabunge na Madiwani ndani ya Vyama Vingine ........ 91
5.6 Malalamiko Juu ya Uteuzi ........ 91
5.7 Hama-hama ya Wanachama baina ya Vyama ........ 92
5.8 Uteuzi wa NEC ........ 94
5.9 Pingamizi na Rufaa za Wagombea ........ 95
5.10 Wagombea Waliopita Bila Kupingwa ........ 95
5.11 Tathmini ya Zoezi Zima la Uteuzi ........ 96
5.12 Hitimisho na Mapendekezo ........ 97
5.12.1 Hitimisho ........ 97
5.12.2 Mapendekezo ........ 97
**CHAPTER 6 MWENENDO WA KAMPENI ZA UCHAGUZI ........ 98**

6.1 Utangulizi ........ 98
6.2 Miongozo ya Kisheria na Kitaasisi kwa ajili ya Kampeni ........ 98
6.3 Gharama za Kampeni ........ 98
6.4 Taratibu za Kampeni na Kanuni za Maadili ........ 100
6.5 Kampeni Hasi ........ 102
6.6 Mbinu na Mikakati ya Kampeni ........ 103
6.6.1 Njia za Usafiri ........ 105
6.7 Ilani za Uchaguzi: Ajenda na Masuala Yaliyojitokeza katika Kampeni za Uchaguzi ........ 106
6.8 Elimu kwa Wapigakura ........ 111
6.9 Taratibu za Kiusalama ........ 112
6.10 Tathmini ya Jumla ya Kampeni za Uchaguzi ........ 114
6.11 Hitimisho na Mapendekezo ........ 115
6.11.1 Hitimisho ........ 115
6.11.2 Mapendekezo ........ 115
**CHAPTER 7 VYOMBO VYA HABARI NA UCHAGUZI ........ 117**
7.1 Utangulizi ........ 117
7.2 Mfumo wa Kisheria na Uendeshaji wa Uchaguzi wa 2015 ........ 117
7.3 Habari na Uandikishaji Wapigakura (BVR) ........ 118
7.3.1 Habari za BVR katika Mitandao ya Kijamii ........ 121
7.3.2 BVR katika Vyombo vya Utangazaji wa Habari ........ 122
7.4 Habari Za Kampeni Na Mchakato Wa Kupiga Kura. ........ 122
7.4.1 Kampeni za Urais katika Television ........ 123
7.4.2 Usawiri wa Uchaguzi kwa Picha na Katuni ........ 124
7.4.3 Magazeti ........ 125
7.4.4 Habari za Magazeti kwa Kuzingatia Dhamira ........ 125
7.5 Hitimisho na Mapendekezo ........ 126
7.5.1 Hitimisho ........ 126
7.5.2 Mapendekezo ........ 127
**CHAPTER 8 USHIRIKISHWAJI WA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU KATIKA CHAGUZI ........ 128**
8.1 Utangulizi ........ 128
8.2 Muktadha wa Sheria Katika Kulinda Makundi Maalum. ........ 128
8.3 Ushirikishwaji wa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu katika Usimamizi wa Uchaguzi ........ 129
8.4 Ushirikishwaji wa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu katika Zoezi la Uandikishwaji wa Wapigakura. ........ 130
8.5 Programu za Elimu ya Mpigakura Zilizolenga Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu. ... 131
8.6 Vyombo vya Habari ........ 131
8.7 Taasisi za Kimataifa ........ 132
8.8 Vyama vya Siasa ........ 133
8.9 Changamoto katika Utoaji wa Elimu ya Mpigakura ........ 135
8.10 Uteuzi wa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu ........ 136
8.10.1 Uteuzi wa ndani ya Vyama vya Siasa. ........ 136
8.10.2 Uteuzi wa Mgombea Urais ndani ya Vyama vya Siasa ........ 137
8.10.3 Uteuzi wa Wagombea Ubunge na Madiwani ndani ya Vyama vya Siasa. ........ 138
8.10.4 Changamoto za Mchakato wa Uteuzi wa Wagombea ndani ya Yyama. ........ 139
8.10.5 Uteuzi wa NEC na ZEC ........ 140
8.10.6 Nafasi za Viti Maalum vya Wanawake ........ 140

8.10.7 Uteuzi wa Wanawake wa Viti Maalum Katika Ngazi ya Tume ya Uchaguzi ........................ 141
8.10.8 Ushirikishwaji katika Kampeni za Uchaguzi ........................................................................ 142
8.11 Vitendo vya Ubaguzi dhidi ya Wanawake ............................................................................... 142
8.12 Ushirikishwaji wa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu kama Wapigakura................ 144
8.13 Matokeo ya Uchaguzi kwa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu ............................... 144
8.14 Mwelekeo Baada ya Uchaguzi ................................................................................................ 146
8.14.1 Uteuzi wa Rais kwa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu ........................................ 146
8.15 Hitimisho na Mapendekezo ..................................................................................................... 147
8.15.1 Hitimisho ............................................................................................................................. 147
8.15.2 Mapendekezo ....................................................................................................................... 147
**CHAPTER 9 MCHAKATO WA KUPIGA KURA, KUHESABU KURA NA KUTANGAZA MATOKEO ........................................................................ 148**
9.1 Utangulizi ................................................................................................................................... 148
9.2 Uandaaji wa Vituo vya Kupigia Kura na Maandalizi ya Kupiga Kura ........................................ 148
9.3 Ufunguaji wa Vituo vya Kupigia Kura na Upigaji Kura ............................................................. 151
9.4 Kufungwa kwa Vituo vya Kupigia Kura .................................................................................... 153
9.5 Utaratibu wa Polisi na wa Usalama katika Siku ya Uchaguzi .................................................... 154
9.6 Utendaji wa Wasimamizi wa Uchaguzi katika Siku ya Uchaguzi .............................................. 155
9.7 Mchakato wa Kuhesabu Kura na Kubandika Matokeo ............................................................... 156
9.8 Utangazaji wa Matokeo ya Uchaguzi ......................................................................................... 158
9.9 Mahudhurio ya Wapigakura ....................................................................................................... 159
9.10 Hali na Matukio Baada ya Uchaguzi ........................................................................................ 159
9.11 Malalamiko ya Uchaguzi wa Urais na Ubunge .......................................................................... 163
9.12 Tathimini ya Jumla ya Shughuli za Siku ya Uchaguzi .............................................................. 163
9.13 Hitimisho na Mapendekezo ..................................................................................................... 164
9.13.1 Hitimisho ............................................................................................................................. 164
9.13.2 Mapendekezo ....................................................................................................................... 165
**CHAPTER 10 UCHAGUZI ZANZIBAR: UTATA NA CHANGAMOTO ............. 166**
10.1 Utangulizi ................................................................................................................................. 166
10.2 Siasa za Zanzibar Kabla ya Uhuru ........................................................................................... 166
10.3 Kurudishwa kwa Mfumo wa Vyama Vingi .............................................................................. 168
10.4 Serikali ya Umoja wa Kitaifa ................................................................................................... 169
10.5 Faida na Mapungufu ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa ............................................................. 171
10.6 Uchaguzi wa 2015 Zanzibar ..................................................................................................... 171
10.6.1 Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar: Mamlaka na Muundo ......................................................... 171
10.6.2 Uhusiano wa ZEC na NEC .................................................................................................. 172
10.6.3 Uandikishaji Wapigakura .................................................................................................... 173
10.6.4 Ugawaji wa Majimbo ........................................................................................................... 173
10.6.5 Uteuzi wa Wagombea kwa Vyama vya Siasa na ZEC .......................................................... 174
10.6.6 Kampeni za Uchaguzi .......................................................................................................... 176
10.6.7 Maandalizi ya Siku ya Uchaguzi .......................................................................................... 179
10.6.8 Kufunguliwa kwa Vituo vya Kupigia Kura ........................................................................... 179
10.6.9 Kuhesabu Kura ..................................................................................................................... 180
10.6.10 Kutangazwa kwa Matokeo na Matukio baada ya Uchaguzi ................................................ 181
10.7 Kubatilishwa kwa Matokeo ya Uchaguzi ................................................................................. 182
10.8 Utatuzi wa Migogoro baada ya Uchaguzi ................................................................................. 185
10.8.1 Kuingilia Mgogoro wa Zanzibar ........................................................................................... 185
10.9 Hitimisho na Mapendekezo ..................................................................................................... 186

10.9.1 Hitimisho ........ 186
10.9.2 Mapendekezo ........ 186
**CHAPTER 11 UHURU, HAKI NA KUAMINIKA KWA UCHAGUZI WA MWAKA 2015 ........ 188**
11.1 Utangulizi ........ 188
11.2 Muhtasari wa Masuala Makuu ........ 188
11.2.1 Njia na Mbinu za Utazamaji wa Uchaguzi ........ 188
11.2.2 Muktadha wa Kisiasa na Mazingira ya Uchaguzi ........ 189
11.2.3 Mfumo wa Kisheria na Kitaasisi ........ 191
11.2.4 Usimamizi wa Michakato ya Uchaguzi ........ 191
11.3 Tathmini ya Michakato ya Mzunguko wa Uchaguzi ........ 192
11.3.1 Utengaji wa Mipaka ya Maeneo ya Uchaguzi ........ 192
11.3.2 Mchakato wa Uandikishaji wa Wapigakura ........ 192
11.3.3 Uteuzi ndani ya Vyama ........ 192
11.3.4 Uteuzi wa NEC ........ 193
11.3.5 Kampeni ........ 194
11.3.6 Kupiga Kura, Kuhesabu Kura na Kutangaza Matokeo ........ 194
11.4 Tathmini ya Michakato yote ya Uchaguzi ........ 195
11.5 Uchaguzi wa Zanzibar ........ 196
11.6 Tathmini ya Jumla ya TEMCO na Uamuzi juu ya Uchaguzi wa 2015 ........ 196
11.7 Mapendekezo ........ 197
11.7.1 Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ........ 198
11.7.2 Tume ya Taifa ya Uchaguzi ........ 198
11.7.3 Vyama vya Siasa ........ 199
11.7.4 Vyombo vya Habari ........ 199
11.7.5 Asasi za Kiraia ........ 199
11.7.6 Wapigakura ........ 199
**MAREJEO ........ 201**
**VIAMBATISHO ........ 203**

## ORODHA YA MAJEDWALI


Jedwali 2-1: Mgawanyo wa kura za Urais Uchaguzi Mkuu 2010 ........................................ 27
Jedwali 2-2: Ushindani wa Vyama vya Siasa katika Uchaguzi wa Ngazi Msingi, 2014 ........ 32
Jedwali 2-3: Mgawanyo wa viti vya Ubunge na Udiwani Uchaguzi Mkuu 2010 .................. 42
Jedwali 3-1: Vigezo vya Uwekaji Mipaka ya Majimbo ya Uchaguzi ................................... 57
Jedwali 3-2: Uwasilishaji wa maoni juu wa uwekaji mipaka ya majimbo ya uchaguzi .......... 57
Jedwali 4-1: Ugumu wa kutumia mashine za BVR ............................................................ 66
Jedwali 4-2: Uandikishaji Wapigakura wa Majaribio .......................................................... 68
Jedwali 4-3: Ratiba ya Uandikishaji wa Wapigakura kwa Mikoa .......................................... 69
Jedwali 4-4: Kufikika kwa Vituo vya Kuandikishia Wapigakura .......................................... 70
Jedwali 4-5: Utoshelevu wa Mashine za BVR ..................................................................... 71
Jedwali 4-6: Uwepo wa Mashine za Dharura za BVR ......................................................... 71
Jedwali 4-7: Idadi ya Wapigakura kwa Mikoa na Jinsia ........................................................ 77
Jedwali 4-8: Tathmini ya Zoezi la Uandikishaji Wapigakura ................................................ 78
Jedwali 5-1: Idadi ya Watia nia na Wagombea wa Viti vya Ubunge .................................... 86
Jedwali 5-2: Idadi ya Watia nia na Wagombea kwenye Uchaguzi wa Madiwani .................. 86
Jedwali 5-3: Idadi ya Watiania na Wagombea wa Viti Maalum ............................................ 87
Jedwali 5-4: Majimbo ambayo Makubaliano ya UKAWA Hayakuheshimiwa ...................... 90
Jedwali 5-5: Malalamiko juu ya teUuzi wa Wagombea Ubunge ndani ya Vyama ................ 91
Jedwali 5-6: Malalamiko juu ya Uteuzi wa Wagombea Ubunge ndani ya Vyama ................ 91
Jedwali 5-7: Malalamiko juu ya Uteuzi ndani ya Vyama ...................................................... 92
Jedwali 5-8: Mambo yaliyosababisha hama-hama ................................................................ 92
Jedwali 5-9: Mitindo ya Uteuzi ............................................................................................. 94
Jedwali 5-10: Uteuzi wa Wanawake kwa Viti Maalum ......................................................... 94
Jedwali 5-11: Orodha ya Wagombea Urais wa Muungano na Wagombea Wenza ................ 95
Jedwali 5-12: Tathmini ya Zoezi la Uteuzi ............................................................................ 96
Jedwali 6-1: Kiwango cha Juu cha Gharama ambacho Mgombea Anaweza Kutumia ........... 99
Jedwali 6-2: Kampeni Hasi kwa Kupitia Maneno ................................................................ 102
Jedwali 6-3: Mbinu na Mikakati Iliyotumiwa na Vyama ..................................................... 104
Jedwali 6-4: Njia za Usafiri kuelekea katika mikutano ya kampeni ..................................... 105
Jedwali 6-5: Mbinu za Vyama vya Siasa katika Kupambana na Rushwa ............................ 107
Jedwali 6-6: Mbinu za Zilizotumiwa na AZAKI katika Kutoa Elimu kwa Mpigakura ........ 111
Jedwali 6-7: Mbinu zilitumiwa na Tume ya Uchaguzi kutoa Elimu ya Mpigakura ............. 111
Jedwali 6-8: Uhusika wa Vyama vya Siasa kutoa Elimu ya Mpigakura .............................. 112
Jedwali 6-9: Mbinu za Kutoa Elimu ya Mpigakura kwa Makundi Maalum ........................ 112
Jedwali 6-10: Tathmini ya Kampeni za Uchaguzi ............................................................... 114
Jedwali 8-1: Wapigakura Waliojiandikisha kwa Umri na kwa Jinsia katika Uchaguzi mkuu wa Mwaka 2015 ........ 130
Jedwali 8-2: Wagombea Ubunge Waliochaguliwa kutoka katika Vyama vya Siasa, 2015 .. 140
Jedwali 8-3: Wanawake Waliochaguliwa Kupitia Viti vya Majimboni ............................... 145
Jedwali 8-4: Wanawake Wabunge na Madiwani Waliochaguliwa Kupitia Mfumo wa Viti Maalum ........ 146
Jedwali 9-1: Kufaa kwa Vifaa vya Uchaguzi ...................................................................... 150
Jedwali 9-2: Mpangilio wa Maboksi ya Kura katika Vituo vya Kupigia Kura .................... 151
Jedwali 9-3: Changamoto katika Kubaini Vitambulisho vya Wapigakura ........................... 153
Jedwali 9-4: Sifa za Wasimaizi Wakuu wa Uchaguzi ......................................................... 156
Jedwali 9-5: Kuwepo kwa Wadau Muhimu wa Uchaguzi wakati wa Mchakato wa Kuhesabu Kura ........ 156
Jedwali 9-6: Urudiaji wa Kuhesabu Kura na Malalamiko Yaliyosikika kabla ya Kutangazwa kwa Matokeo ........ 157

Jedwali 9-7: Kubandikwa kwa Matokeo ya Uchaguzi katika Vituo vya Kuhesabia Kura....157
Jedwali 9-8: Matokeo ya Uchaguzi wa Urais Tanzania........................................................158
Jedwali 9-9: Matokeo ya Uchaguzi wa Ubunge, 2015 .........................................................159
Jedwali 9-10: Matokeo ya Mwitikio wa Watu......................................................................160
Jedwali 9-11: Malalamiko Yaliyofikishwa Makahama kuu Dhidi ya Matokeo ya Uchaguzi wa Ubunge.............................................................................................................................163
Jedwali 9-12: Tathtimini ya Shughuli za Siku ya Uchaguzi.................................................164
Jedwali 10-1: Tathmini ya Uteuzi wa Wagombea ndani ya Vyama vya Siasa .....................176
Jedwali 10-2: Tathmini ya Mchakato wa Kampeni ..............................................................177
Jedwali 10-3: Tathmini ya Siku ya Kupiga Kura..................................................................181
Jedwali 10-4: Tathmini ya Jumla ya Mwenendo wa Uchaguzi ............................................182
Jedwali 11-1: Tathmini ya Michakato yote ya Uchaguzi .....................................................195
Jedwali 11-2: Tathmini ya Jumla ya Uchaguzi wa Mwaka 2015 ..........................................197

## ORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo 1-1: Mzunguko wa Chaguzi Tanzania....4
Kielelezo 1-2: Mgawanyo wa Waangalizi wa Uchaguzi kwa Ajili ya Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura....13
Kielelezo 1-3: Mwonekano wa Teknolojia ya Telerivet....14
Kielelezo 1-4: Taswira ya Mawasiliano kwa kutumia Teleriveti....15
Kielelezo 3-1: Muundo wa Utawala wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi....49
Kielelezo 3-2: Muundo wa Utawala wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar....54
Kielelezo 4-1: Utoshelevu wa vifaa vya kufundishia....63
Kielelezo 4-2: Utendaji wa Jumla wa Maafisa Uandikishaji....65
Kielelezo 4-3: Utoshelevu wa Mafunzo kwa Maafisa Uandikishaji....66
Kielelezo 4-4: Idadi ya matukio ya kuharibika kwa mashine za BVR....71
Kielelezo 4-5: Muda wa Wastani wa Kuandikisha Mpigakura....72
Kielelezo 7-1: Asilimia ya Habari za Uandikishaji Wapigakura....119
Kielelezo 7-2 Matumizi Mitandao kwa Wanasiasa/Vyama....123
Kielelezo 7-3: Vyama vya siasa katika televisheni....124
Kielelezo 7-4: Habari za Uchaguzi katika Magazeti (Januari-Novemba, 2015)....125
Kielelezo 7-5: Habari za kashfa zilizojitokeza magazetini....126
Kielelezo 7-6: Yaliyojiri kweye mikutano ya hadhara....126
Kielelezo 9-1: Muda wa Kufungua Vituo vya upigia kura....152
Kielelezo 9-2:  Muda Aliotumia kila Mpigakura Kupiga Kura....153
Kielelezo 9-3: Muda wa Kufungwa kwa Vituo vya Kupigia Kura....154

## ORODHA YA VIAMBATANISHO

Kiambatanisho namba 1: Orodha ya Asasi shiriki za TEMCO 2015 ........................203
Kiambatanisho namba 2: Maadili ya Waangalizi Uchaguzi wa TEMCO ............................208
Kiambatanisho namba 3: Mgawanyo wa Waangalizi wa TEMCO ......................................210
Kiambatanisho namba 4: Wanachama wa CCM waliochukua Fomu za Kuteuliwa kugombea Urais ndani ya Chama ....................................................................................214
Kiambatanisho namba 5: Mapendekezo ya TEMCO ya Kuboresha Mchakato wa Chaguzi wa 2000.........................................................................................................................216
Kiambatanisho namba 6: Mapendekezo ya TEMCO ya Kuboresha Mchakato wa Chaguzi 2005 ..............................................................................................................................222
Kiambatanisho namba 7: Mapendekezo ya TEMCO ya Kuboresha Mchakato wa Chaguzi 2010 ..............................................................................................................................224
Kiambatanisho namba 8: Sekretarieti ya TEMCO, 2015 ..............................................228

## VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| AATZ | Action Aid Tanzania |
| ACT-Wazalendo | Alliance for Change and Transparency |
| ADC | Alliance for Democratic Change |
| AFP | Alliance for Tanzania Farmers Party |
| ANGOZA | Association of Non-governmental Organizations in Zanzibar |
| APPT | African Progressive Party of Tanzania |
| AROs | Assistant Returning Officers |
| ASP | Afro Shiraz Party |
| AUEOM | African Union Election Observation Mission |
| AZAKI | Asasi za Kiraia |
| BAGODE | Baraka Goodhope Orphanage Development |
| BAKWATA | Baraza la Waislamu Tanzania |
| BAWACHA | Baraza la Wanawake CHADEMA |
| BVR | Biometric Voter Registration |
| CCK | Chama cha Kijamii |
| CCM | Chama Cha Mapinduzi |
| CCT | Christian Council of Tanzania |
| CEMOT | Coalition on Election Monitoring and Observation in Tanzania |
| CHADEMA | Chama Cha Demokrasia na Maendeleo |
| CHAUMMA | Chama cha Ukombozi wa Umma |
| CHAVITA | Chama cha Viziwi Tanzania |
| CHAWATA | Chama cha Walemavu Tanzania |
| CKD | Chuo Kikuu cha Dar es Salaam |
| COG | Commonwealth Observer Group |
| CSOs | Civil Society Organizations |
| CUF | Civic United Front |
| CV | Curriculum Vitae |
| CWT | Chama cha Walimu Tanzania |
| CWZ | Chama cha Wanasheria Zanzibar |
| DKW | Daftari La Kudumu la Wapigakura |
| DP | Democratic Party |
| DPA | Development Promotion Agency |
| EAC | East African Community |
| EATV | The East Africa Television |
| EOM | Election Observation Mission |
| EU | European Union |
| FBOs | Faith-Based Organisation |
| HK | Halmashauri Kuu |
| IFES | International Foundation for Electoral Systems |
| IRI | International Republican Institute |
| ISSU | Idara ya Sayansi ya Siasa na Utawala |
| ITV | Independent Television |
| KK | Kamati Kuu |
| KTT | Kamati Tendaji ya TEMCO |
| KUUM | Kamati ya Uangalizi wa Uchaguzi ya Mkoa |
| LEGCO | Legistlative Council of Tanzania |
| LHRC | Legal and Human Rights Center |
| MCT | Media Council of Tanzania |

| | |
|---|---|
| MKUKUTA | Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania |
| MUUM | Mratibu wa Utazamajiwa Uchaguzi wa Mkoa |
| N.A | Not Applicable |
| NCCR-Mageuzi | National Convention for Construction and Reform |
| NDI | National Democratic Institute |
| NEC | National Electoral Commission |
| NED | National Endowment for Democracy |
| NIDA | National Identity card Authority |
| NLD | National League for Democracy |
| NRA | National Reconstruction Alliance |
| OMR | Optical Mark Recognition |
| OSIEA | Open Society Initiative of East Africa |
| PMO RALG | Prime Minister's Office Regional Administration and Local Government |
| PNVR | Permanent National Voter Register |
| PPRA | Public Procurement Regulatory Authority |
| RECs | Regional Election Coordinators |
| REDET | Research for Education and Democracy in Tanzania |
| ROs | Regional Observers |
| SADC | Southern Africa Development Community |
| CNGO | Council for Non-Governmental Organizations |
| SEOM | Elections Observer Mission |
| SPSS | Statistical Package for the Social Sciences |
| STOs | Short Term Observers |
| SUK | Serikali ya Umoja wa Kitaifa |
| SUMANGO | Sumbawanga Non-Governmental Organizations |
| TACCEO | Tanzania Civil Society Consortium on Election Observation |
| TADEA | Tanzania Democratic Alliance |
| TAKUKURU | Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa |
| TAMISEMI | Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| TAMWA | Tanzania Media Women's Association |
| TANU | Tanganyika African National Union |
| TAWLA | Tanzania Women Lawyers Association |
| TBC | Tanzania Broadcasting Corporation |
| TCD | Tanzania Centre for Democracy |
| TCRA | Tanzania Communications Regulatory Authority |
| TEC | Tanzania Episcopal Conference |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TEMCO | Tanzania Election Monitoring Commitee |
| TEMESA | Tanzania Electrical Mechanical and Electronics Services Agency |
| TGNP | Tanzania Gender Networking Programme |
| THM | Wataalam wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TLP | Tanzania Labour Party |
| TLS | Tanganyika Law Society |
| TTU | Tume ya Taifa ya Uchaguzi |
| AU | African Union |
| UKAWA | Umoja wa Katiba ya Wananchi |
| UKIMWI | Ukosefu wa Kinga Mwilini |

| | |
|---|---|
| ULINGO | Umoja wa Wanawake Wabunge |
| UNDP | United Nations Development Programme |
| UPDP | United People's Democratic Party |
| USAID | United States Agency for International Development |
| WMM | Watazamaji wa Muda Mrefu |
| ZAFELA | Zanzibar Female Lawyers Association |
| ZANAB | Zanzibar National Association of the Blind |
| ZANID | Zanzibar Identity Card |
| ZANVERG | Zanzibar Voter Education Reference Group |
| ZEC | Zanzibar Electoral Commission |
| ZGC | Zanzibar Gender Coalition |
| ZLS | Zanzibar Law Society |
| ZNP | Zanzibar Nationalist Party |
| ZPPP | Zanzibar and Pemba Peoples Party |
| ZYF | Zanzibar Youth Forum |

# CHAPTER 1
# MFUMO WA TEMCO WA UTAZAMAJI WA UCHAGUZI

## 1.1 Usuli na Muktadha

Asasi ya utazamaji wa uchaguzi Tanzania, TEMCO, ni taasisi huru ya waangalizi wa ndani wa uchaguzi ambayo imejemgwa katika misingi ya uzalendo na weledi katika kutimiza majukumu yake na haifungamani wala kuegemea upande wowote wa kisiasa. TEMCO ilianzishwa na asasi 24 zenye malengo yanayofanana na mwelekeo usiokinzana mnamo mwaka 1994. Dhamira kuu ya waasisi wa TEMCO ilitokana na nia yao njema ya kujenga na kukuza demokrasia ya chaguzi nchini Tanzania. Baadhi ya asasi anzilishi za TEMCO ni pamoja na Mpango wa Utafiti na Elimu ya Demokrasia Tanzania, yaani REDET, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (CKD), Baraza la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT) na Chama cha Walimu Tanzania (CWT). Idadi ya wanachama wa TEMCO imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka kutoka 24 mwaka 1994 hadi 183 mwaka 2015. Orodha yao imeambatishwa katika ripoti hii kama Kiambatanisho namba 1

Asasi zinazounda TEMCO, kama vile vikundi vya kiraia, mashirika ya kidini, vyama vya wafanyakazi, vikundi vya taaluma na sekta binafsi hazifanani zote wala kushabihiana kwa kila hali. Asasi hizi nyingi zinatofautina sana katika dira, dhamira, malengo, mwelekeo na mitizamo. Lakini katika masuala ya uchaguzi, asasi hizi zinaunganishwa zaidi na nia yake njema ya kuwa jicho la wananchi wa Tanzania katika kutathmini chaguzi kama zinasimamiwa kwa kuzingatia utawala wa sheria, taratibu na misingi ya chaguzi bora, huru na za haki. TEMCO imeshiriki kama mwangalizi na mwangalizi wa chaguzi kuu na chaguzi ndogo zilizosimamiwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Tume ya Uchaguzi Zanzibar tangu mwaka 1992 baada ya siasa huria kuruhusiwa rasmi na hivyo kupelekea kurejeshwa kwa mfumo wa chaguzi zinazoshirikisha vyama vingi vya siasa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Aidha, TEMCO ilikuwa mwangalizi wa michakato yote ya chaguzi Zanzibar, ikiwa ni pamoja na Kura ya Maoni iliyofanyika tarehe 31 Julai, 2010 hatua iliyopelekea kuanzishwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK). Kwa mujibu wa Hati ya Makubaliano ya asasi shiriki za TEMCO, shughuli za kila siku hufanywa na Mpango wa Utafiti na Elimu ya Demokrasia Tanzania, yaani REDET. Shughuli hizo ni pamoja na uendeshaji, utafutaji rasilimali, na maandalizi ya kazi ya utazamaji wa chaguzi. Aidha wakati wa zoezi la kutazama uchaguzi Sekretarieti ya TEMCO uundwa kwa ajili ya kutekeleza kazi za kila siku za za TEMCO. Masuala na majukumu yanayohusu uongozi na sera husimamiwa na Kamati ya Tendaji yenye idadi ya wajumbe 16 kutoka asasi shiriki za TEMCO.

## 1.2 Dira na Malengo

Kwa niaba ya wananchi, bila upendeleo wa aina yoyote wala kuegemea au kufungamana na upande wowote, TEMCO uangalia chaguzi ili kutathmini na kubainisha kiwango cha amani, uadilifu, uhuru na haki katika chaguzi. Aidha, njia mbalimbali hutumiwa kupima na kuainisha kiasi ambacho matokeo ya chaguzi yanadhihirisha na kuakisi matakwa, uhuru na maamuzi ya wapigakura na jamii kwa ujumla. Malengo mahususi ya TEMCO kwa kiasi kikubwa yanaimarishana na kukamilishana kama ifuatavyo:

(i) Kuangalia na kufuatilia hatua zote za mchakato wa uchaguzi, ikiwa ni pamoja na mchakato wa kutenga maeneo ya uchaguzi, uandikishaji wa wapigakura na uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura (DKW), uteuzi wa wagombea ndani ya vyama vya siasa, kampeni, kupiga kura, kuhesabu na kujumlisha kura, kutangaza matokeo na tathmini ya jumla ya mwenendo mzima pamoja na matukio baada ya uchaguzi;

(ii) Kutizama na kutathmini matukio yanayoonesha kiwango cha kutendeka kwa haki katika usimamizi wa uchaguzi kwa ujumla, hususani umadhubuti wa mfumo wa kisheria (sheria za uchaguzi, kanuni, taratibu na miongozo), muundo wa kitaasisi, vyombo vya usimamizi wa uchaguzi, yaani Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) na matumizi ya vyombo vya dola na vyombo vya kusimamia sheria na taratibu;

(iii) Kutathmini utendaji haki na matumizi ya raslimali za umma katika vyama vya siasa, hususani wagombea wanaoomba kuchaguliwa kwa mara ya pili au zaidi, na kutathmini vyombo vya habari vya umma (radio, televisheni na magazeti ya taifa);

(iv) Kutathmini kiwango ambacho uchaguzi unaweza kuelezwa kuwa wa kuaminika, huru na wa haki; na

(v) Kuainisha mambo yote kuhusu uchaguzi yanayoweza kuwa fundisho kwa wadau wa uchaguzi, kwa nia ya kuleta ufanisi, haki na kuimarisha siasa za ushindani kwa misingi ya kudumisha amani na utulivu wa nchi katika chaguzi nyingine zitakazofuata..


### 1.3 Upeo katika Utazamaji wa Chaguzi

Mbinu na njia za utazamaji wa uchaguzi zinazotumiwa na waangalizi wa TEMCO zinatokana na ujuzi na njia za kisayansi zilizofanyiwa utafiti na kutumiwana wataalam wa sayansi ya siasa wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (CKD) katika utazamaji na utazamaji wa chaguzi kwa muda mrefu tangu mwaka 1965. Utazamaji wa uchaguzi unajumuisha maeneo mengi, ikiwa ni pamoja na: (i) utengaji wa maeneo ya uchaguzi; (ii) uteuzi wa wagombea ndani ya vyama vya siasa; (iii) uteuzi wa wagombea unaofanywa na mamlaka za kusimamia chaguzi; (iv) kampeni za uchaguzi; (v) siku ya uchaguzi na shughuli zake; na (vi) matukio baada ya uchaguzi.




*Maadili ya Waangalizi wa Uchaguzi wa TEMCO*

Aidha jicho la mwangalizi wa uchaguzi, hujielekeza pia kutazama ushiriki wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu wa aina mbalimbali. Eneo jingine ambalo linatazamwa ni mwenendo wa vyombo vya habari hususani vile vya kielekitroniki (televisheni na redio), vinavyochapishwa (magazeti) pamoja na mitandao ya kijamii. Dhamira kuu ya TEMCO katika utazamaji chaguzi ni kuwajengea imani wananchi kwa ujumla, wapigakura na wadau wengine wa uchaguzi, ikiwa ni pamoja na wagombea wa vyama vya siasa imani katika usimamizi wa uchaguzi na hivyo kuamsha hamasa na mshawasha wa kushiriki katika chaguzi, wakitambua kuwa wasimamizi wa uchaguzi hawako peke yao katika hatua zote za mchakato wa uchaguzi bali kauli na vitendo vyao vinafuatiliwa kwa makini na waangalizi huru wa uchaguzi. Maadili yanayoongoza mwenendo na tabia ya waangalizi wa TEMCO katika ufuatiliaji wa chaguzi ni uadilifu, uwazi, weledi, uhalali, uaminifu, kutopendelea na uwajibikaji. Kiambatanisho namba 2 kinafafanua kwa kina maadili ya Waangalizi wa uchaguzi wa TEMCO.




***Kielelezo 1-1: Mzunguko wa Chaguzi Tanzania***

## 1.4 Faida Zitokanazo na Utazamaji wa Chaguzi na Vigezo vyaTathmini

Azma ya TEMCO katika utazamaji wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, ilitokana na ukweli kwamba utazamaji na utazamaji huru wa uchaguzi, unaozingatia maadili na weledi wa mwangalizi chaguzi, ni muhimu sana na unalenga kuleta faida nyingi katika kustawisha na kukuza demokrasia. Faida hizo ni pamoja na: (i) kustawisha na kudumisha demokrasia na utawala bora; (ii) kuimarisha taasisi zinazojenga na kukuza demokrasia; (iii) kuimarisha uhalali wa serikali iliyoundwa baada ya uchaguzi; (iv) kukuza na kuhifadhi haki za kiraia na kisiasa za wapigakura na jamii kwa ujumla; (v) kuzuia na kubainisha mbinu na vitendo vinavyoweza kuchafua mwenendo na matokeo ya uchaguzi, ikiwa ni pamoja na kuwatisha au kuwajengea hofu wapigakura na hata kuhatarisha usalama na amani; ubabaishaji; (vi) kubainisha na kutambua vitendo vya hujuma au dosari katika chaguzi punde zinapojitokeza; (vii) kuwatia moyo wapigakura na umma kwa ujumla kushiriki katika michakato ya chaguzi; (viii) kuwajengea Imani na matumaini wananchi katika michakato ya chaguzi (ix) kuongeza ubora wa chaguzi; (x) kubainisha maeneo katika chaguzi yanayohitaji kuboreshwa na wadau wa uchaguzi ikiwa ni pamoja na taasisi za Serikali na zisizo za kiserikali.

Ili kutambua ni kwa kiwango gani Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 ulikuwa huru, wa haki na wenye kuaminika, waangalizi wa TEMCO walitumia vigezo na viashiria mbalimbali, vikubwa vikiwa ni:

(i) Kiasi au kiwango ambacho mfumo wa kisheria, ikiwa ni pamoja na sheria za uchaguzi, kanuni na taratibu ziliwezesha au kukwaza mchakato wa uchaguzi kwa kuzingatia vigezo vya haki za kiraia na kisiasa zinazotambulika na kuheshimiwa kimataifa;
(ii) Uwazi katika mfumo wa uchaguzi na ushiriki wa wananchi katika mchakato wa kutenga mipaka ya maeneo ya uchaguzi, yaani majimbo na kata;
(iii) Uhuru na uadilifu wa vyombo vya usimamizi wa uchaguzi, ikiwa ni pamoja na taratibu za ajira na mafunzo ya wasimamizi na maafisa uchaguzi pamoja na upatikanaji wa taarifa, takwimu na machapisho ya Tume za uchaguzi;
(iv) Kiasi ambacho mfumo wa kisheria, kanuni na taratibu katika usimamizi wa uandikishaji wapigakura zililindwa na kuhifadhi haki ya wananchi kujiandikisha;
(v) Kiwango ambacho Tume za usizimamizi wa uchaguzi, Asasi za kiraia (AZAKI) na vyama vya siasa vivilijihusisha kikamilifu na kwa ufanisi katika utoaji wa elimu ya mpigakura;
(vi) Kiasi ambacho vyama vya siasa na wagombea walifanya kampeni za uchaguzi kwa uhuru lakini pia kwa kuzingatia sheria;
(vii) Kiwango ambacho sheria, kanuni na taratibu ikiwa ni pamoja na zile zinazohusu Sheria ya matumizi ya fedha katika chaguzi zilisimamiwa na kutekelezwa;
(viii) Kiasi ambacho vyombo vya habari, magazeti, radio na televisheni pamoja na mitandao ya kijamii vilitoa fursa na kukuza upatikanaji wa habari na taarifa kuhusu uchaguzi kwa weledi bila kuingiliwa; na
(ix) Kiwango ambacho malalamiko yaliyohusu uchaguzi yalishughulikiwa na kupatiwa ufumbuzi kwa kuzingatia sheria , kanuni na taratibu;

### 1.5 Mfumo wa Utazamaji wa Uchaguzi Mkuu

Sekretarieti ya TEMCO iliundwa mwezi Oktoba mwaka 2014 na kujitayarisha kwa ajili ya kuratibu shughuli za timu ya waangalizi wa uchaguzi. Mfumo wa utazamaji wa uchaguzi ikiwa ni pamoja na mpango na taratibu za kuwapangia vituo waangalizi wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 uliandaliwa na kuidhinishwa na Kamati ya Utendaji ya TEMCO (KUT). Jumla ya waangalizi wa muda mrefu 201 walichaguliwa na kuteuliwa na hatimaye kupatiwa mafunzo stahiki kwa muda wa siku tatu kuanzia tarehe 14 Februari, 2015 hadi tarehe 16 Februari, 2015. Aidha, timu ya waangalizi 161 iliteuliwa na kukabidhiwa jukumu la kutazama uchaguzi katika hatua ya uandikishaji wapigakura katika zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura (DKW) kwa kutumia mfumo mpya wa kiekitroniki, yaani "Biometric Voter Registration (BVR) system". Mwezi Septemba 2015, waangalizi wengine 150 waliteuliwa baada ya kupatiwa mafunzo kwa takribani siku tatu na kutawanywa katika majimbo teule 150 kwa ajili ya kuangalia mchakato wa uchaguzi ikiwa ni pamoja na kampeni, zoezi la kupiga na kuhesabu kura pamoja na kutangaza matokeo ya uchaguzi.

TEMCO ilipeleka waangalizi wake 161 kutazama zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura (DKW) katika halmashauri za wilaya, miji, manispaa na majiji Tanzania Bara na Visiwani. Ripoti ya awali kuhusu mchakato wa kuboresha DKW ilitolewa kwa umma na wadau mbalimbali wa uchaguzi kupitia vyombo vya habari mwezi Agosti 2015. Ripoti kamili kuhusu zoezi la uboreshaji wa DKW iliandaliwa na kusambazwa kwa umma.




*Mkutano wa TEMCO na Waandishi wa Habari wa Tarehe 14 Februari, 2015 Kuueleza Umma juu ya Utazamaji wa Uchaguzi. Kushoto kwenda Kulia: Bw. Alex Mintah (Mtaalam wa Masuala ya Uchaguzi, USAID),Bw. Benson Bana Meneja wa Mradi wa TEMCO) na Bw. Lupa Ramadhani (Mchambuzi wa Masuala ya Siasa)*

Waangalizi wote wa TEMCO walipatiwa mafunzo mahususi kuhusu utazamaji wa chaguzi, na ni wale tu waliohitimu na kufaulu mafunzo hayo waliteuliwa kuwa waangalizi wa muda ,mrefu au waangalizi wa muda mfupi. Mafunzo kwa ajili ya waangalizi wa muda mrefu kuhusu zoezi la kuboresha DKW yalifanyika kwa muda wa siku mbili. Mafunzo kwa ajili ya utazamaji wa michakato mingine ya Uchaguzi Mkuu yalifanyika kwa muda wa siku nne kwa waangalizi wa muda mrefu na siku moja kwa waangalizi wa muda mfupi.



*Mwenyekiti wa TEMCO, Profesa Rwekaza Mukandala, Akitoa Hotuba ya Ufunguzi wa Mafunzo kwa Ajili ya Waangalizi wa muda mrefu*

Mahudhui ya mafunzo yalijikita katika maeneo mengi muhimu, ikiwa ni pamoja na haya yafuatayo: (i) mfumo wa uchaguzi kisheria na kitaasisi; (ii) zana za kukusanya taarifa za utazamaji wa uchaguzi; (iii) Maadili ya TEMCO na Tume za chaguzi kwa waangalizi wa uchaguzi, (iv) Majukumu na kazi za waangalizi wa uchaguzi; na (v) Uandishi wa Ripoti ya uchaguzi kwa waangalizi wa muda mrefu na waangalizi wa muda mfupi. Maadili ya TEMCO kwa waangalizi wake wa uchaguzi yameambatishwa katika ripoti hii kama Kiambatanisho namba 2.



*Sehemu ya Waangalizi wa muda mrefu Wakati wa Mafunzo*

Wawezeshaji na wakufunzi walioshiriki katika mafunzo ya waangalizi wa muda mrefu walikuwa ni wataalam wa sayansi ya siasa kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (CKD), wataalam wa uchaguzi kutoka Tume ya Taifa ya Uchaguzi (TTU), Wanasheria kutoka Chama cha Wanasheria Tanzania (CWT), Chama cha Wanasheria Zanzibar (CWZ) pamoja na Wataalam wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (THM) kutoka Muungano wa Waangalizi wa Ndani wa Uchaguzi, yaani "CEMOT".



*Mwangalizi wa Uchaguzi Ms. Magret Bwathondi, Akiuliza Swali Wakati wa Mafunzo*

TEMCO iliteua Mratibu wa Utazamaji wa Uchaguzi wa Mkoa (MUUM) kwa kila mkoa kutoka miongoni mwa waangalizi wa muda mrefu. Jukumu la mratibu wa mkoa lilikuwa kuratibu shughuli za waangalizi wa uchaguzi chini ya TEMCO vile vile kujenga mtandao na kukuza mahusiano mema kati ya TEMCO na wadau mbalimbali wa uchaguzi katika ngazi ya mkoa husika. Kamati ya Utazamaji wa Uchaguzi ya Mkoa (KUUM) ilifufuliwa au kuundwa upya katika kila mkoa. Kila KUUM ilikuwa na wajumbe wapatao kumi na wawili waliopatikana kutoka asasi shiriki za TEMCO. Aidha, Kamati ya Mkoa ilijumuisha pia waangalizi wa muda mrefu waliokuwa wakitazama uchaguzi katika majimbo teule katika mkoa husika. Kwa kutambua mahusiano mema baina ya Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) na Mpango wa Utafiti na Elimu ya Demokrasia Tanzania (REDET), uliopelekea kuundwa kwa Muungano wa Waangalizi wa Ndani wa Uchaguzi (CEMOT), kwa muktadha huu, waangalizi kutoka kikundi cha waangalizi wa uchaguzi wa ndani, TACCEO, kilichoongozwa na LHRC, walikaribishwa kuhudhuria mikutano yote ya KUUM.

Kati ya mwezi Septemba 2015 na Oktoba 2015 jumla ya mikutano mitatu ya KUUM iliitishwa katika kila mkoa, kufanya idadi ya mikutano yote ya KUUM kuwa 90 katika mikoa yote, na kuhudhuriwa na wadau wa uchaguzi takribani 1,080. Mikutano hiyo, pamoja na mambo mengine, iliwezesha (i) kubadilishana taarifa, maarifa na uzoefu baina ya waangalizi wa muda mrefu na asasi shiriki mbalimbali chini ya mwavuli wa TEMCO; (ii) uratibu wa shughuli za kutazama uchaguzi ngazi ya mkoa na majimbo; (iii) kuhakiki na kuridhia Ripoti za waangalizi wa TEMCO; (iv) kuridhia na kupitisha majina ya watu waliopendekezwa kuwa waangalizi wa muda mfupi kwa kila Jimbo la uchaguzi; na (v) kushauri kuhusu mgawanyo wa waangalizi wa muda mfupi katika vituo vya kupiga kura kutazama shughuli anuwai za siku ya uchaguzi. Baadhi ya Wajumbe wa Kamati Tendaji ya TEMCO (KTT) na Sekretarieti walifanya ziara mikoani na majimboni ili kufuatilia na kutathmini utendaji kazi wa waangalizi wa uchaguzi na waratibu wa mikoa.



*Menejimenti ya TEMCO Ikiwa na Baadhi ya Waangalizi wa Muda Mrefu mara tu Baada ya Mwenyekiti, Prof. R. Mukandala Kufungua Mafunzo ya Waangalizi wa Uchaguzi*

TEMCO iliandaa, kuchapisha na kusambaza Majarida manne yenye Matoleo manane (8) kwa lengo la kueleimisha na kuhabarisha wapigakura na wananchi kwa ujumla mambo muhimu kuhusu mchakato wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015. Majarida yote yalipakiwa katika tovuti ya TEMCO (http://temco.udsm.ac.tz/), ambayo ilifanyiwa maboresho makubwa, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba taarifa muhimu kuhusu uchaguzi zinawekwa au kupakuliwa mara kwa mara.




*Jalada la Moja ya Majarida Yaliyochapishwa na TEMCO katika Kipindi cha Uchaguzi*

Aidha, ili kurahisisha upatikanaji habari na taarifa za uchaguzi zilizotakiwa kuwafikia wananchi wa Tanzania na kwingineko duniani,TEMCO ilijenga mitandao ya kijamii ikiwa ni pamoja na "*Facebook*" "*Instagram*"na"*WhatsApp*".

### 1.6 Mpango wa Mgawanyo wa Vituo na Waangalizi

Upangaji wa majimbo na vituo kwa ajili ya mgawanyo wa waangalizi wa muda mrefu na muda mfupi uliandaliwa kwa kuzingatia mkakati wa kupata sampuli kutokana na vigezo mbalimbali kama vile: (i) historia ya jimbo kisiasa, (ii) hali ya ushindani wa kisiasa, (iii) idadi ya majimbo na vituo vya kupiga kura, pamoja na (iv) uwiano wa maeneo ya mijini na vijijini. Jumla ya waangalizi 161 walitawanywa katika mamlaka za serikali za mitaa, mijini na vijijini, kuangalia zoezi la uboreshaji wa daftari la wapigakura, ikiwa ni pamoja na uandikishaji wa wapigakura. Kati ya majimbo 265, jumla ya majimbo 161 (asilimia 60.75) yalikuwa na waangalizi kutoka TEMCO kwa ajili ya kutazama zoezi la uandikishaji wa wapigakura kwa kutumia mfumo wa kielektroniki, yaani BVR.

Jumla ya waangalizi wa muda mrefu 150 walitawanywa au kupangwa katika majimbo ya uchaguzi ili kutazama mchakato wa Uchaguzi Mkuu. Kwa hali hiyo, TEMCO ilikuwa na waangalizi wa muda mrefu kwa kiwango cha asilimia 56.6 ya majimbo yote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Waangalizi 128 (asilimia 85) walitawanywa katika majimbo ya uchaguzi ya Tanzania Bara na waangalizi 22 (asilimia 15) walipelekwa kutazama uchaguzi mkuu katika majimbo ya Zanzibar, Unguja na Pemba. Waangalizi wa TEMCO waliopelekwa Zanzibar walitazama asilimia 44 ya majimbo yote ya Zanzibar kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu. Tume ya Taifa ya Uchaguzi iliandaa vituo vya kupigia kura 65,525 (63,525 Tanzania Bara na 1,580 Zanzibar). Idadi ya waangalizi wa uchaguzi waliotazama uchaguzi walikuwa ni 7,350 idadi hii inajumuisha Waangalizi wa muda mrefu na Waangalizi wa muda mfupi. Waangalizi hao walitazama asilimia 11.2 ya vituo vyote vya kupigia kura. Mgawanyo wa waangalizi wa uchaguzi wa TEMCO umeoneshwa katika ripoti hii kama Kiambatanisho namba 3 kinavyoonesha.

**1.7 Ripoti za Awali kuhusu Michakato ya Chaguzi**

TEMCO imejenga utamaduni wa kutoa Ripoti za awali za kuhusu mchakato wa Uchaguzi Mkuu mara tu baada ya kukamilika na Ripoti kamili baada ya uchambuzi wa kina. Taarifa za awali hutolewa kwa umma kupitia vyombo vya habari, tovuti na mitandao ya kijamii.



*Wanahabari wakipokea taarifa ya Awali ya Utazamaji wa DKW*

Ripoti za awali utayarishwa na timu ya wataalamu wa utazamaji wa uchaguzi wa TEMCO, inayoshirikisha Meneja wa Mradi na Naibu Kiongozi wa Timu ya Waangalizi wa Uchaguziwa TEMCO, Mchambuzi wa Masuala ya Kisiasa na Mchambuzi wa vyombo vya Habari na Mchambuzi wa Takwimu. Timu hii iliandaa taarifa za awali na kuziwasilisha kwa njia ya mjadala na maamuzi katika Kamati Tendaji. Taarifa zilizowasilishwa ni pamoja na uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura na Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 25, 2015.




*Baadhi ya Wajumbe wa KTT Wakishiriki Kuwasilisha Ripoti ya Awali Kupitia Vyombo vya Habari*

Ripoti ya awali kuhusu uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura, yaani BVR, ilitolewa kwa vyombo vya habari na kupakuliwa katika tovuti na mitandao ya kijamii ya TEMCO mnamo tarehe 23Mwezi Agosti, 2015. Aidha wadau wengine walipelekewa ripoti hii kupitia katika anwani zao za barua pepe na posta. Taarifa ya awali kuhusu Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 25, 2015 ilitangazwa kupitia mkutano na vyombo vya habari tarehe 3 Novemba, 2015. Usambazaji wa taarifa hii kwa wananchi na wadau wengine wa uchaguzi ulifanyika kupitia tovuti ya TEMCO, njia ya barua pepe, posta na mitandao ya kijamii.




*Naibu Kiongozi wa Timu ya Waangalizi wa TEMCO, Dr. Benson Bana, Akiwasilisha Ripoti ya Awali ya Uchaguzi Mkuu kwa Waandishi wa Habari*

### 1.8 Mbinu za Ukusanyaji wa Taarifa kuhusu Mwenendo wa Uchaguzi

Waangalizi wa uchaguzi wa TEMCO walitumia mbinu mbalimbali kukusanya taarifa zilizohitajika kuhusu mwenendo wa Uchaguzi Mkuu wa 2015. Matumizi ya njia na mbinu tofauti kukusanya taarifa yaliwezesha kufanya uhakiki ili kupata taarifa sahihi na zisizotiliwa mashaka.

#### *1.8.1 Utazamaji wa Kina katika Maeneo ya Uchaguzi*

Utazamaji wa kina katika maeneo ya uchaguzi ilikuwa njia kuu iliyotumiwa na waangalizi wa muda mrefu na wale wa muda mfupi kupata na kukusanya taarifa za michakato yote ya uchaguzi, hususani uteuzi wa ndani ya vyama vya siasa, kampeni na uendeshaji wa shughuli katika siku ya uchaguzi. Waangalizi walikuwa na zana mahususi au kitini kilichotumika kama rejea yao katika utazamaji wa mambo mahususi kuhusu hatua mbalimbali katika mchakato wa uchaguzi. Kitini hicho kiliwaongoza waangalizi kuelekeza macho na masikio yao katika matukio mbalimbali ambayo ni muhimu katika uchaguzi. Waangalizi walielimishwa ipasavyo ikiwa ni pamoja na kuwa makini, kufuatilia kikamilifu na kuchunguza kwa kina mambo yote muhimu kuhusu uchaguzi na kuweka kumbukumbu zao kimaandishi kwa usahihi kuhusiana na mchakato wote wa uchaguzi. Katika kutumia mbinu hii, waangalizi waliongozwa na kauli ya Waingereza kwamba “Kuona ni Kuamini”.

#### *1.8.2 Mahojiano*

Waangalizi wa muda mrefu walitumia hojaji iliyoandaliwa mahususi kwa ajili ya kuongoza mahojiano ya kina na watu au wadau mbalimbali wa uchaguzi katika majimbo ya uchaguzi. Mahojiano hayo yaliwawezesha waangalizi kupata taarifa muhimu na za kina kuhusu mtazamo na uzoefu wa wadau kuhusu usimamizi wa uchaguzi na mwenendo wake katika maeneo yao. Taarifa walizokusanya ziliwawezesha kupata picha kamili na halisi ya hali ilivyokuwa kabla ya waangalizi kufika katika maeneo hayo kwa ajili ya utazamaji wa zoezi la uchaguzi katika hatua zake mbalimbali. Kwa hali hiyo waangalizi waliweza kupata taarifa sahihi na za kina kuhusu utengaji na ugawanyaji wa mipaka ya maeneo ya uchaguzi pamoja na uteuzi wa wagombea ndani ya vyama vya siasa. Wadau wa uchaguzi waliohojiwa ni pamoja na: (i) viongozi wa vyama vya siasa; (ii) wasimamizi na maafisa wa uchaguzi, (iii) wagombea nafasi za ubunge na udiwani; (iv) viongozi na maafisa wa serikali; (v) makamanda na maafisa wa Jeshi la Polisi; (vi) makamanda wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU); na (vi) viongozi wa Asasi za Kiraia (AZAKI) hususani wale walioshiriki katika kutoa mafunzo ya elimu ya mpigakura. Mbinu ya mahojiano ilisaidia kwa kiasi kikubwa katika ukusanyaji wa taarifa kuhusu Uchaguzi Mkuu wa Tanzania wa mwaka 2015.

#### *1.8.3 Mapitio na Marejeo ya Nyaraka Muhimu*

Waangalizi walifanya mapitio ya nyaraka mbalimbali zenye vyanzo vya taarifa na habari za Uchaguzi Mkuu zilizopatikana kutoka ofisi za mamlaka za uchaguzi, yaani ofisi za Tume na wadau mbalimbali wa uchaguzi. Nyaraka zilizofanyiwa mapitio ni pamoja na: (i) sheria mbalimbali zinazohusu chaguzi; (ii) ilani za uchaguzi za vyama vya siasa; (iii) kanuni na taratibu zinazoongoza uteuzi wa wagombea ndani ya vyama vya siasa; (iv) maadili ya waangalizi wa uchaguzi yaliyoandaliwa na Tume za uchaguzi; (v) machapisho mbalimbali

kuhusu hali ya kisiasa na kiuchumi Tanzania; na (vi) maadili ya wagombea wa vyama vya siasa yaliyoandaliwa na Tume za uchaguzi.





***Kielelezo 1-2:*** **Mgawanyo wa Waangalizi wa Uchaguzi kwa Ajili ya Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura**

### *1.8.4 Matumizi ya TEHAMA*


Michakato ya ukusanyaji, uwasilishaji na uchambuzi wa taarifa zilizokusanywa na waangalizi ilirahisishwa kutokana na kuanzishwa kwa taratibu za matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika shughuli za TEMCO, ikiwa ni pamoja na utazamaji na utazamaji wa chaguzi. Waangalizi wa muda mrefu katika majimbo ya uchaguzi waliweza kuwasilisha taarifa zao katika Kituo cha pamoja cha Utazamaji wa Uchaguzi ambacho kilianzishwa kwa ushirikiano kati ya Mpango wa Utafiti na Elimu ya Demokrasia Tanzania, REDET, na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, LHRC. Taarifa zilitumwa na kupokelewa katika kituo hicho kwa kutuma ujumbe mfupi kwa simu ya mkononi kwa kutumia mfumo au teknolojia inayoitwa *Magpi*.

Waangalizi wa muda mrefu na Waangalizi wa muda mfupi walitumia teknolojia hiyo kuwasilisha kituoni taarifa zote zilizohusu shughuli mbalimbali zilizofanyika katika siku ya uchaguzi. Aidha, mawasiliano kati ya Waangalizi wa muda mrefu na Makao Makuu ya TEMCO yaliwezeshwa na kurahisishwa kwa kutumia teknolojia ya mawasiliano inayojulikana kama*Telerivet*. Teknolojia hiyo iliongeza kiwango cha ufanisi kwa hali ya juu katika mfumo wa mawasiliano ambapo ujumbe ulitumwa kiweledi na kupokelewa kwa muda mfupi katika mtandao wa mawasiliano kupitia ujumbe mfupi wa simu ya kiganjani.





***Kielelezo 1-3: Mwonekano wa Teknolojia ya Telerivet***

Teknolojia hii ya mawasiliano iliwawezesha waangalizi wa muda mrefu kurahisisha mawasiliano kati yao na makao makuu ya TEMCO. Aidha *Telerivet* ilirahisisha mawasiliano kati ya Sekretarieti na waangalizi katika majimbo ya uchaguzi kwa kutuma ujumbe mfupi kwa waangalizi wote kwa wakati mmoja. Ujumbe uliwafikia walengwa kwa muda mfupi na kwa wakati mmoja. Aidha, waliweza kutuma mrejesho wa mawasiliano hayo makao makuu ya TEMCO kwa muda mfupi sana.



*Makarani wa Data Wakitumia Fomu za Google Kuingiza Data katika Mfumo kwa Kutumia TEHAMA*

Pamoja na matumizi ya Telerivet kurahisisha mawasiliano, uongozi wa TEMCO ulijenga mitandao ya kijamii ili kupanua wigo wake wa mawasiliano na utoaji habari za uchaguzi. Mitandao iliyojengwa na kutumiwa ni pamoja na ukurasa wa*Facebook*,*WhatsApp*, *Instagram*, *twitter*,na *YouTube n.k.*. Pia TEMCO ilijenga kanzidata yake ya kutunza kumbukumbu na taarifa zake kwa kutumia teknolojia ya habari. Tovuti ya TEMCO (http://temco.udsm.ac.tz/) ilifanyiwa ukarabati mkubwa ili kuboresha mwonekano wa sura yake, ikiwa ni pamoja na kipeperushi cha habari, kikokotoo cha wanaovinjari tovuti n.k.




***Kielelezo 1-4: Taswira ya Mawasiliano kwa kutumia Teleriveti***

Taarifa zilizokusanywa na kuwasilishwa kutoka kwa waagalizi wa uchaguzi wa muda mrefu na waagalizi wa uchaguzi wa muda mfupi zilichambuliwa kwa kutumia fomu maalum za *google* zilizotokana na matumizi ya TEHAMA.  Seti za data ziliandaliwa na kuchapishwa kwa

ajili ya matumizi ya waandishi wa ripoti hii. Hii ilikuwa ni mara ya kwanza kwa Ripoti ya uchaguzi ya TEMCO kuandikwa kwa kutumia uchambuzi wa taarifa za waangalizi wa muda mfupi kutoka katika vituo vya kupiga kura kwa kutumia TEHAMA.

Matumizi ya fomu za *google* yameleta mapinduzi ya kiteknolojia katika shughuli za utazamaji uchaguzi zinazofanywa na TEMCO. Kwa ujumla matumizi ya TEHAMA hususani fomu za *google*yalileta maboresho makubwa na kuongeza idadi ya taarifa za uchaguzi zilizotumika kuandaa ripoti ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 na fomu hizo ziliongeza ufanisi katika matumizi ya taarifa za waangalizi wa uchaguzi. Taarifa za waangalizi wa muda mrefu zilichambuliwa kwa kutumia programu ya kompyuta ya uchambuzi wa Takwimu katika fani ya Sayansi ya Jamii inayojulikana kwa kifupi kama "SPSS". Seti za taarifa zilizochambuliwa zilitumiwa katika maandalizi au matayarisho ya ripoti hii.


***1.8.5 Mitando ya Ushikiano na Mahusiano***

Vikundi vya utazamaji wa uchaguzi vya ndani ya nchi, kwa mujibu wa shughuli zake, hupaswa kujitahidi kupata na kuongeza uzoefu na maarifa mapya mara nyingi kutoka kwa waangalizi wengine hususani wa kimataifa kutoka nje ya nchi. Ni kwa jinsi hii vikundi vya waangalizi wa ndani hujijengea mazingira ya kuwa asasi endelevu zinazojifunza na kujielimisha mara zote. Mafunzo hupatikana kwa njia nyingi, ikiwa ni pamoja na kujenga mitandao na mahusiano ya kikazi.Katika shughuli zake za utazamaji wa uchaguzi, TEMCO iliweza kujenga mitandao ya mahusiano na ushirikiano na taasisi mbalimbaliza kitaifa na kimataifa zinazojishughulisha na utazamaji wa chaguzi ndani na nje ya nchi.



*Meneja wa TEMCO akiwa kwenye Mazungumzo na Wawakilishi wa Jumuiya ya Ulaya, Margarida Ramos na Xavier Nockatika ofisi za TEMCO kuhusu Utazamaji wa Uboreshaji wa DKW na Uchaguzi Mkuu*

Taasisi za kimataifa ni pamoja na Taasisi ya Kitaifa ya Demokrasia, yaani, National Democratic Institute (NDI)ya Marekani; Taasisi ya Kimataifa ya Republican, yaani International Republican Institute (IRI) ya Marekani;Mfuko wa Kimataifa wa Mifumo ya Chaguzi, yaani International Foundation for Electoral Systems (IFES); Taasisi ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali katika Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika, yaani Southern Africa Development Community Council for Non-Governmental Organizations (SADC-CNGO);Taasisi ya Wazi ya Kijamii Afrika Mashariki, yaani Open Society Initiative of East Africa (OSIEA); na Taasisi ya Majaliwa kwa Demokrasia, yaani National Endowment for Democracy (NED).



*Maafisa wa NDI na REDET/TEMCO wakiwakatika Mkutano wa Mashauriano*

Katika kukuza ushirikiano na taasisi za kitamataifa, viongozi wa TEMCO walialikwa kwa ajili ya mazungumzo ya kikazi na vikundi mbalimbali vya kimataifa vilivyokaribishwa rasmi na mamlaka husika Serikalini kuja Tanzania kutazama Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015. Baadhi ya vikundi hivyo ni Waangalizi kutoka Jumuiya ya Nchi za Ulaya, yaani, European Union Election Observation Mission (EU-EOM); Jumuiya ya Madola, yaani Commonwealth Observer Group (COG); Waangalizi kutoka nchi zinazounda Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, yaani SADC Electoral Observation Mission (SEOM), Jumuiya ya Afrika Mashariki, yaani East African Community Election Observation Mission (EAC-EOM); na Muungano wa nchi za Kiafrika, yaani the African Union Election Observation Mission (AU-EOM).



*Rais mstaafu wa Nigeria na kiongozi wa waangalizi wa uchaguzi kutoka Jumuiya ya Madola, Mhe. Goodluck Jonathan, akiagana na Naibu kiongozi wa Waangalizi wa uchaguzi wa TEMCO baada ya kutembelea Kituo Cha Uchaguzi, katika Hotel ya Hyatt Regency-Kilimanjaro, katika Jiji la Dar es Salaam*

Katika kukuza mtandao wa mahusiano na vikundi vya waangalizi wa uchaguzi wa ndani, REDET,asasi kiongozi ya TEMCO, ilianzisha mahusiano na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, kilichoratibu mtandao wa asasi za kiraia katika utazamaji na utazamaji chaguzi, yaani TACCEO. Mahusiano kati ya asasi hizi mbili yaliwezesha kuanzishwa kwa Muungano wa Waangalizi na Watazamaji wa Uchaguzi Tanzania, yaani CEMOT. Aidha, chini ya umoja huu, kilianzishwa Kituo cha Utazamaji wa Uchaguzi ambacho kilipokea taarifa za mwenendo wa mchakato wa uchaguzi kutoka kwa waangalizi wa TEMCO na TACCEO waliopelekwa katika majimbo yote ya uchaguzi na vituo teule vya kupiga kura Tanzania Bara na Zanzibar.

### 1.9 Vigezo katika Kutathmini Chaguzi

TEMCO imejijengea utamaduni na desturi ya kutoa C*heti* kwa uchaguzi kulingana na matokeo ya tathmini yake ya jumla ya mchakato mzima wa uchaguzi husika. Tathmini na aina ya *Cheti* kinachotolewa hutokana na *Alama* zilizotolewa na *Daraja* lililotolewa kwa kila zoezi muhimu katika mchakato wa uchaguzi kwa kuzingatia ubora na kiwango cha kuaminika, uhuru na haki kwa mujibu wa tathmini ya waangalizi wa uchaguzi wa TEMCO.Vyeti vinavyotolewa huanzia *Cheti cha Uchaguzi Safi wa Kuaminika, Huru na wa Haki* hadi *Cheti cha Uchaguzi Uliovia au Kuharibika Kabisa*. Maelezo na ufafanuzi kwa kila aina ya Cheti husika ni kama ifuatavyo:

(i) *Cheti cha Uchaguzi Safi, wa Kuaminika, Huru na wa Haki:* Cheti hiki utolewa kwa uchaguzi safi na wa kiungwana wenye mapungufu na dosari kidogo sana, ambazo kwa ujumla wake haziwezi katu kuathiri kwa namna yoyote ile matokeo ya uchaguzi. Kwa ujumla ni uchaguzi halisi, wa viwango na kuaminika unaoonesha matakwa ya wapigakura na wananchi kwa ujumla. Alama zinazotolewa kwa uchaguzi wa namna hii huanzia asilimia 80 hadi 100, sawa na Daraja “A”.

(ii) *Cheti cha Uchaguzi Unaoridhisha, kwa ujumla ni Huru na wa Haki***:** Cheti hiki utolewa kwa uchaguzi ambao kwa kiwango kikubwa ni safi, huru na wa haki lakini una mapungufu na dosari kadhaa ambazo kwa kiwango kidogo unaweza kuathiri kwa namna mbalimbali fursa za ushindi kwa baadhi ya wadau, ikiwa ni pamoja na wapigakura, wagombea na vyama vya siasa. Alama zinazotolewa kwa uchaguzi wa namna hii huanzia asilimia 60 hadi 79, sawa na Daraja "B".

(iii) *Cheti cha Uchaguzi Huru lakini Usio wa Haki*: Cheti hiki hutolewa kwa uchaguzi ulioruhusu bila vikwazo vyovyote ushiriki wa wadau wote, yaani vyama vya siasa, wagombea na wapigakura lakini kukawepo matukio ya vyama vikubwa, au chama tawala, kutokuzingatia sheria na kanuni za uchaguzi na kutokuadhibiwa kwa hilo. Aidha, kuwepo kwa upendeleo dhahiri unaoathiri ushiriki au mafanikio ya baadhi ya wadau wengine wa uchaguzi. Kwa ujumla uwanja wa ushindani haukusawazishwa inavyopaswa na sheria ya matumizi ya fedha katika chaguzi haikufuatwa au kusimamiwa kikamilifu.Alama au Maksi zinazotolewa kwa uchaguzi wa namna hii huanzia asilimia 50 hadi 59, sawa na Daraja "C".

(iv) *Cheti cha Uchaguzi usio Safi, Huru na wa Haki:*Cheti hiki hutolewa kwa uchaguzi uliogubikwa na mapungufu na dosari nyingi kutokana na ukiukwaji wa baadhi ya sheria, kanuni, taratibu na maadili. Aidha, ni uchaguzi ambao ulitawaliwa na udhaifu mkubwa katika usimamizi na vitisho na upendeleo.Alama zinazotolewa kwa uchaguzi wa namna hii huanzia asilimia 40 hadi 49, sawa na Daraja "D".

(v) *Cheti cha Uchaguzi Uliovurugika Kabisa:* Cheti hiki hutolewa kwa uchaguzi uliovurugika au kuborongwa kabisa kiasi kwamba ni vigumu kufahamu kilichotokea na wadau wengi wa uchaguzi wanashindwa kukubali matokeo yote ya uchaguzi. Uchaguzi wa aina hii unaweza kabisa kulinganishwa na mwanafunzi aliyeshindwa kabisa mtihani**.** Alama zinazotolewa kwa uchaguzi wa namna hii huanzia asilimia 0 hadi 39, sawa na Daraja "E".

*(vi) Uchaguzi Uliovia na Kuharibika Kabisa*: Cheti hiki hutolewa kwa uchaguzi uchaguzi uliosimamiwa kwa udhaifu mkubwa sana na sheria, kanuni na taratibu zote za uchaguzi zilikiukwa Aidha, utawala wa sheria haukuzingatiwa na haki za binadamu zilikiukwa. Ni uchaguzi ulioghubikwa na vitisho vikubwa sana, ghasia na vurugu kila mahali na hata kusababisha vifo, kiasi kwamba baadhi ya wagombea waliamua kujiondoa. Uchaguzi wa aina hii unaweza kabisa kulinganishwa na mimba iliyoharibika au yai lililovia au kuoza kabisa. Alama zinazotolewa kwa uchaguzi wa namna hii huanzia asilimia 0 hadi 0.9, sawa na Daraja "F".

### 1.10 Mtiririko na Maudhui ya Ripoti

Ripoti hii imegawanyika katika sura kumi na moja. Sura ya hii ya kwanza inatoa usuli, muktadha na utangulizi wa ripoti ya TEMCO kuhusu Uchaguzi Mkuu wa 2015. Aidha sura hii inaangaza chimbuko la TEMCO kama asasi ya utazamaji na utazamaji wa uchaguzi Tanzania, muundo wa utendaji katika utazamaji wa chaguzi na hususani Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 pamoja na vigezo au viwango vinavyotumiwa na TEMCO kutathmini na kufanya maamuzi kuhusu ubora, kuaminika, kulinda uhuru na kuzingatia haki katika chaguzi.

Sura ya pili ni tafakuri kuhusu mazingira na muktadha wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015. Sehemu hii ya Ripoti inajadili mazingira na hali ya siasa ya nchi katika kipindi cha kuelekea Uchaguzi Mkuu wa 2015. Matukio Muhimu yaliyojitokeza katika nyanja za kijamii, kisiasa na kiuchumi, ambayo kwa namna moja au nyingine yalikuwa na athari katika mchakato wa Uchaguzi Mkuu yanawekwa bayana katika sura hii. Kwa kufanya hivyo, sura inajenga msingi madhubuti kwa sura nyingine za Ripoti hii. Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 ulifanyika miaka takribani 20 baada ya Serikali ya Jamuhuri ya Muugano wa Tanzania kurejesha siasa huria mwaka 1992, ikiwa ni pamoja na mfumo wa uchaguzi unaoshirikisha vyama vingi vya siasa tangu mwaka 1995. Aidha Serikali ya awamu ya nne ilikuwa inahitimisha muhula wake wa miaka kumi (1995-2015) katika uongozi wa taifa na hivyo, kwa vyovyote vile, taifa lilitarajia kumpata Rais mpya ama kutoka chama tawala (CCM) au chama chochote cha upinzani.

Sura ya tatu inajadili masuala mbalimbali yaliyohusiana na uboreshaji wa Dafari la Kudumu la Wapigakura (DKW) kwa kutumia mfumo wa kieletroniki, zoezi ambalo lilitangulia michakato mingine ya Uchaguzi Mkuu wa 2015. Uboreshaji wa daftari ulihusu pia uandikishaji wa wapigakura wapya kwa mujibu wa sheria.

Sura ya nne inachambua mifumo ya kisheria na kitaasisi inayoongoza Uchaguzi Mkuu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar. Lengo la uchambuzi huu ni kubainisha nguvu na udhaifu katika mifumo hiyo ikiwa ni pamoja na mianya, vikwazo na changamoto katika mifumo, hali inayoweza kudhoofisha au kuathiri upatikanaji wa uchaguzi bora, wa kuaminika ulio huru na wa haki. Zaidi ya hapo, Sura hii inatathmini uwezo na ufanisi wa mamlaka zilizokabidhiwa dhamana kikatiba kusimamia uchaguzi, yaani Tume ya Taifa ya Uchaguzi, NEC na Tume ya Uchaguzi Zanzibar, ZEC.

Uteuzi wa wagombea ndani ya vyama vya siasa na katika ngazi ya Tume ya uchaguzi unachambuliwa katika sura ya tano. Uchambuzi huu unajikita kwenye maeneo ya sheria zinazoongoza uteuzi wa wagombea ndani ya vyama vya siasa ili waweze kugombea nafasi za uchaguzi katika ngazi za Urais, Ubunge na Udiwani. Kanuni na taratibu za uteuzi ndani ya vyama zinamulikwa ili kuainisha kiwango ambacho haki za wananchi na makundi anuwai katika jamii, kama vile wanawake, vijana na watu wenye ulemavu zinazingatiwa katika uteuzi wa wagombea ngazi zote za uchaguzi na uteuzi.

Sura ya sita inabainisha na kujadili yaliyojiri wakati wa kipindi cha kampeni za uchaguzi, na kiwango ambacho vyama vya siasa na wagombea walitekeleza matakwa ya sheria za uchaguzi na maadili stahiki katika kujinadi kwa wapigakura. Masuala yanayohusu utekelezaji wa sheria ya gharama za uchaguzi, matukio ya kampeni chafu, maudhui na mwelekeo wa ilani za uchaguzi za vyama vya siasa, mipango ya ulinzi na usalama katika mikutano ya kampeni yanabainishwa na kujadiliwa katika sura hii.

Sura ya saba inajikita kwenye mwenendo wa vyombo vya habari katika kuandika na kutangaza habari za uchaguzi hususani wakati wa kipindi cha uchaguzi. Vyombo vya habari vinavyojadiliwa ni magazeti, radio na televisheni (luninga) na mitandao ya kijamii. Muundo wa kisheria na udhibiti wa vyombo vya habari, ikiwa ni pamoja na kiwango ambacho uhuru

wa vyombo vya habari unalindwa na kuzingatiwa ni mambo ambayo yanachambuliwa kwa kina katika sura hii. Dhamira kuu ya sura hii ni kutathmini kiwango ambacho vyombo vya habari vilizingatia misingi yake na weledi wake katika kuandika na kutangaza habari na taarifa za uchaguzi bila upendeleo au kuegemea upande mmoja.

Sura ya nane inatathmini na kujadili ushiriki wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika Uchaguzi Mkuu kama wapigakura au wagombea. Uchambuzi na tathmini inayofanywa katika sura hii inalenga kubaini hatua mahususi zilizochukuliwa na wadau mbalimbali wa uchaguzi kuhakikisha usawa wa kijinsia kati ya wanawake na wanaume kwa upande mmoja na usawa katika fursa kwa watu wenye ulemavu kwa upande mwingine, ikiwa ni pamoja na kuwepo kwa nafasi za upendeleo katika mchakato wa uteuzi ndani ya vyama vya siasa.

Sura ya tisa inahusu Uchaguzi wa Zanzibar uliofanyika tarehe 25 Oktoba, ambao ulighubikwa na changamoto na sintofahamu nyingi na hivyo kuuibua maswali mengi kuliko majibu miongoni mwa wadau wa uchaguzi huo. Kwa kuzingatia hisia na maoni ya wadau, sura hii inachambua muktadha wa uchaguzi, hali ya siasa Zanzibar, mamlaka ya Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar, yaani ZEC, uhuru wa Tume, uhusiano kati ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi, yaani NEC na ZEC; na mamlaka ya Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania katika kushughulikia masuala yanayohusu Zanzibar. Aidha sura hii inaangazia hali ya siasa Zanzibar, ikiwa ni pamoja na mitafaruku ya kisiasa katika muktadha mzima wa historia ya chaguzi kabla na baada ya mapinduzi mwaka 1964. Lengo ni kuleta uelewa mpana wa hali ya siasa inayojitokeza Zanzibar.

Sura ya kumi inarejelea shughuli anuwai katika siku ya uchaguzi, ikiwa ni pamoja na mchakato wa kupiga kura, kuhesabu kura, kutangaza matokeo, na hali iliyojitokeza na inayoendelea kujitokeza, ikiwa ni pamoja na matukio chanya na hasi yanayodhihirisha mtizamo wa wananchi kuhusu Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 kwa ujumla wake.

Sura ya kumi na moja ni majumuisho ya Taarifa ya sura zote zilizotangulia. Uchambuzi na mijadala yote kuhusu mchakato wa uchaguzi inaunganishwa pamoja ili kupata picha halisi ya usimamizi wa uchaguzi. Matokeo ya tathmini ya kila hatua ya uchaguzi tangu utengaji wa mipaka ya maeneo ya uchaguzi (kata na majimbo) hadi matukio yaliyojitokeza mara tu baada ya uchaguzi na yanayoendelea kujitokeza kama yanavyoainishwa na kujadiliwa katika sura mbalimbali zinazokamilisha ripoti hii. Lengo la hatua hii ni kuthibitisha pasipo shaka tathmini na tamko la TEMCO kuhusu kiwango ambacho Uchaguzi Mkuu wa 2015 ulikuwa bora, wa kuaminika, huru na wa haki, ili kuweza kutoa Alama, Daraja na Cheti au Hati stahiki kwa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015.

### 1.11 Shukrani

Ripoti hii isingeweza kukamilika bila juhudi na michango ya hali na mali kutoka kwa watu na taasisi mbalimbali. Michango yao ndiyo iliyowezesha TEMCO kushiriki kama mwangalizi wa ndani wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015. Uongozi na menejimenti ya TEMCO tunapenda kuwashukuru na kuwatambua kwa namna ya pekee watu wote na taasisi mbalimbali kwa jitihada, dhamira na nia zao njema zilizowezesha kuandaa, kukamilisha na hatimaye

kusambaza ripoti hii kwa umma na wadau mbalimbali wa uchaguzi. Hatuwezi kuwataja wote itoshe baadhi yao kuwakilisha wengine wengi.

Fedha za kuwezesha TEMCO kuwa mwangalizi wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 zilipatikana kutokana na hisani ya watu wa Marekani kupitia Shirika la Misaada ya Maendeleo la Marekani, yaani USAID. Tunapenda kuwashukuru kwa dhati na kwa namna ya pekee watu wa Marekani kupitia USAID kwa msaada wao rasilimali fedha uliowezesha TEMCO kutazama mchakato wote wa Uchaguzi Mkuu. Uongozi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (CKD) unastahili shukrani za pekee, kama ambavyo umekuwa ukifanya huko nyuma, kwa kuiwezesha REDET, kuongoza TEMCO katika utazamaji wa Uchaguzi Mkuu wa 2015. Ufanisi katika utazamaji wa uchaguzi na maandalizi ya ripoti hii ni matunda ya kazi nzuri ya kiweledi iliyofanywa, kwa kiasi kikubwa, na baadhi ya wanataaluma wa CKD hususani kutoka katika Idara ya Sayansi ya Siasa na Utawala (ISSU).

Tunaishukuru Taasisi ya Kidemokrasia Kitaifa, yaani National Democratic Institute (NDI) ya Marekani kwa kuunga mkono jitihada za REDET, asasi kiongozi ya TEMCO, kuhusu kuanzisha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika shughuli za utazamaji wa uchaguzi. Taasisi hii ilitoa rasilimali fedha na wataalam waliowezesha matumizi ya TEHAMA katika shughuli za utazamaji wa uchaguzi. Tunatoa shukrani za dhati kwa Asasi za Kiraia 183 washirika wa TEMCO, waangalizi wote, ikiwa ni pamoja na waratibu wa mikoa, waangalizi wa muda mrefu takribani 180 na wa muda mfupi 7,350 kwa kufanya kazi kama timu moja, kuzingatia maadili ya mwangalizi chaguzi, bidii na uwajibikaji kazini, moyo wa kujitoa na kujituma pamoja na kutoa ushirikiano mzuri kwa uongozi na Sekretarieti ya TEMCO.

Ni dhahiri kuwa bila ushirikiano mzuri na mamlaka za usimamizi wa chaguzi, yaani Tume ya Taifa ya Uchaguzi, NEC na Tume ya Uchaguzi Zanzibar, ZEC shughuli za utazamaji uchaguzi zisingefanyika. TEMCO inazishukuru Tume zote mbili za uchaguzi kwa kutoa vibali vya kuangalia uchaguzi kwa wakati, na kwa ushirikiano mzuri uliotolewa na wasimamizi na Maafisa Uchaguzi katika ngazi zote kwa waangalizi wake wa Uchaguzi Mkuu. Tunapenda kushukuru Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, kinachoratibu TACCEO, kwa ushirikiano wake na REDET, asasi kiongozi wa TEMCO, kuanzisha CEMOT na Kituo cha Utazamaji wa Uchaguzi (KUU), yaani EOC. Takwimu zilizokusanywa na KUU zimetumiwa katika ripoti hii.

Tutakuwa wezi wa fadhila endapo hatutatambua kazi kubwa na nzuri iliyofanywa kwa umakini na weledi mkubwa na timu ya waandishi wa rasimu ya ripoti hii hususani katika kuchambua, kujadili na kutathmini taarifa anuwai zilizowezesha ripoti ya Uchaguzi Mkuu mwaka 2015 kukamilika. Kwa namna ya pekee tunawashukuru wafuatao: Prof. Rwekaza Mukandala, Dkt. Benson Bana, Dkt. Lupa Ramadhani, Dkt. John Jingu, Dkt. Victoria Makulilo, Dkt. Ambrose Kessy, Mr. Richard Mbunda, Dkt. Deogratias Rugaimukamu, Prof. Bernadeta Killian, Mr. Charles Kayoka, Dkt. Bruce Heilman, Bw. Audax Kweyamba, Dkt. Rasul Minja na Dkt. Edwin Babeiya.

Shukrani hizi hazitakamilika endapo tutashindwa kutambua kazi nzuri iliyofanywa na Sekretarieti ya TEMCO chini ya uongozi mahiri wa Prof. Rwekaza Mukandala (Makamu Mkuu wa CKD, Kiongozi Mkuu wa Timu ya Waangalizi wa Uchaguzi wa TEMCO na Mwenyekiti wa REDET); Dkt. Benson Bana (Meneja wa TEMCO na Naibu Kiongozi Mkuu wa Timu ya Waangalizi wa Uchaguzi wa TEMCO), Dkt. Lupa Ramadhani (Mchambuzi wa Masuala ya Kisiasa), Dkt. Deogratias Rugaimukamu (Mchambuzi wa Takwimu), Bw. Dunia Saidi Nassoro (Mhasibu), Bi Sandra Tetty (Afisa Utawala), Bi Judith Kapinga (Mchambuzi wa Sheria), Bi Perpertua John (Mtaalam wa Teknolojia ya Habari), Bw. Charles Kayoka (Mchambuzi wa Vyombo vya Habari), Bi Shani Adam (Afisa Utawala Msaidizi), Bw. Captain Patrick (Mtaalam wa TEHAMA), Bw. Herbert Tenson (Mtaalam-Ufuatiliaji na Tathmini) na Bw. Julius David (Mhudumu wa Ofisi). Timu hii ilifanya kazi kwa bidii, weledi na kwa kujituma ili kuhakikisha majukumu ya kila siku ya TEMCO yanatekelezwa kwa ufanisi. Juhudi za ziada zilizofanywa na baadhi ya wataalam miongoni mwa maafisa wa Sekretariat hususani katika kuandika na kutetea Muswada wa Mradi (Project Proposal) zinastahili kupongezwa.

Tunaomba ieleweke kuwa TEMCO pekee ndiyo yenye dhamana ya ripoti hii yakiwemo maoni, dosari na upungufu wowote uliomo. Aidha ripoti hii haiakisi au kuwakilisha mawazo, fikra, hisia, misimamo na maoni ya watu binafsi au kikundi chochote, au asasi yoyote iliyotajwa. ripoti hii ni ya TEMCO na siyo vinginevyo.

Kwa hiyo basi, ripoti hii ni mchango wetu kwa wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wadau wa uchaguzi, ikiwa ni pamoja na Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Tume ya Uchaguzi Zanzibar, taasisi za serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zinazohusika na chaguzi, vyama vya siasa, asasi za kiraia, jamii kwa ujumla na wadau wote wa siasa za Tanzania kutoka ndani na nje ya nchi. Tuna matumaini kuwa ripoti hii itachangia katika kuboresha chaguzi zijazo, ili hatimaye ziweze kukidhi vigezo na viwango stahiki vya chaguzi bora, za kuaminika, huru na za haki.

# CHAPTER 2
# MAZINGIRA YA KISIASA KUELEKEA UCHAGUZI MKUU

## 2.1 Utangulizi

Chaguzi ufanyika katika muktadha fulani. Mara zote chaguzi huakisi mazingira halisia ya kijamii, kiuchumi na kisiasa ya nchi mahalia na wakati mwafaka. Uchaguzi mkuu wa 2015 ulifanyika baada ya miaka 20 tangu mfumo wa siasa za uliberali uliporudishwa nchini, ikiwa ni pamoja na kuruhusu mfumo wa vyama vyama vingi. Sura hii inachambua muktadha ambao uchaguzi mkuu wa 2015 ulifanyika.Kwa ufupi, uchaguzi huu ulifanyika katika mazingira mahususi hususani matukio muhimu yaliyotokea kipindi cha kuelekea uchaguzi huu kwa upande wa Tanzania Bara na Zanzibar. Yamkini matukio haya (hasa ya kisiasa) yalichagiza katika kuufanya uchaguzi huu uwe na ushindani mkubwa na wa muwashawasha wa aina yake ilinganishwa na chaguzi zilizotangulia tangu kurudishwa kwa mfumo wa vyama vingi nchini.

Kwa upande wa Zanzibar, yalikuwepo matumaini kuwa kuwepo kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK) ungechagiza kuwa na uchaguzi ambao ungeisha kwa amani pasipo na matatizo makubwa, kama ilivyokuwa kwa uchaguzi wa 2010. Hali kadhalika kwa upande wa Tanzania Bara, changamoto na kutoridhisha kwa utendaji wa muhula wa pili wa Rais Kikwete uliashiria uwezekano mkubwa wa kuwepo uchaguzi wenye ushindani mkubwa baina ya Chama Tawala (CCM) na vyama vya upinzani. Mbali na haya, uchaguzi wa Tanzania Bara pia ulitegemewa kuchagizwa na matukio mengine makubwa ya kisiasa ikiwa ni pamoja na mchakato wa Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ushindani ndani ya vyama vya siasa na makundi ya kuwania nafasi za uongozi ndani ya vyama vya siasa. Pamoja na hali hii ya kisiasa hususani kuimarika kwa nguvu ya vyama vya siasa vya upinzani Tanzania Bara kuelekea uchaguzi mkuu wa 2015, mazingira yaliyoonesha bado chama tawala kilikuwa na faida ya kuwa na dola na hata kuwa na nguvu katika mhimili wa Bunge. Hali kama hii ya kuingia uchaguzi wa 2015 CCM ikiwa na faida, ilikuwa dhahiri hata kwa upande wa Zanzibar.

## 2.2 Serikali ya Umoja wa Kitaifa na Siasa za Uchaguzi Zanzibar

Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK), iliyoundwa baada ya uchaguzi wa 2010 ilikuwa ni sehemu ya jitihada za hivi karibuni katika siasa za uchaguzi Zanzibar katika kutafuta suluhu ya matatizo na changamoto zihusuzo chaguzi za Zanzibar tangu uchaguzi wa kwanza wa 1995 baada ya kurejeshwa kwa mfumo wa vyama vingi. Uchaguzi wa 1995 ulihitimishwa kukiwepo dhana na hisia kuwa haukuakisi matakwa halisi ya wananchi wa Zanzibar. Kulikuwa na hisia za kibaguzi (hasa zikisisitizwa na Chama cha Wananchi CUF) baina ya waarabu na waafrika zilizokuwepo tangu kipindi cha kabla ya ukoloni,ukoloni na hata baada ya Mapinduzi ya Zanzibar ambazo zilisababisha kuminywa kwa demokrasia na uchaguzi ulio huru na wa haki (IFES 1995; ZEMOG 1995; Bakari 2001).



*Waasisi wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar (SUK), Mhe. Rais Dkt. Ali Mohamed Shein Akiwa na Makamu wa Kwanza wa Rais na Makamu wa Pili wa Rais*

Madai ya CUF ya kutaka yawepo marudio ya uchaguzi yalikataliwa na dola na matokeo yake kulikuwa na mgogoro mkubwa wa kisiasa ambao hatimaye ulifikia hatua ya kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK) baada ya uchaguzi wa 2010. Ni serikali hii ya Umoja wa Kitaifa iliyowezesha kushirikishwa kwa Chama Cha Wananchi CUF katika Serikali na hivyo kupunguza uhasama kwa kiwango kikubwa baina ya vyama vikuu shindani Zanzibar, yaani CCM na CUF. Ni kupitia SUK pia Zanzibar iliweza kuondokana na mfumo wa uchaguzi wa anayeshinda hata kwa tofauti ndogo ndiye yeye pekee anayeunda serikali na vyombo vingine kama vile vya wawakilishi wa wananchi (Baraza la Wawakilishi kwa upande wa Zanzibar). Pamoja na haya, hali ya kisiasa Zanzibar kuelekea uchaguzi wa 2015 pia iliashiria kuwepo kwa dalili za baadhi ya wananchi na hata viongozi kutaka kujitenga kutoka Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na kuwa na Serikali kamili. Kuibuka kwa kikundi chenye msimamo mkali Zanzibar kilichojulikana kama UAMSHO ni mfano wa hisia hizi za kutaka kujitenga. Madhara ya kikundi hiki yalikuwa makubwa ikiwa ni pamoja na kuchomwa moto kwa nyumba za ibada na kuuawa kwa askari mmoja. Hata hivyo serikali iliingilia kati na kukipiga marufuku kikundi hiki.

**2.3 Utendaji wa Serikali ya Awamu ya Nne (2005-2015)**

Kuchaguliwa na kuingia madarakani kwa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania aliye kijana na aliyeonekana kupendwa na wananchi karibu wa rika mwaka 2005 (kwa kupata 82 asilimia ya kura zilizopigwa na wananchi) huku akiwa na kauli mbiu ya *maisha bora kwa kila Mtanzania*) ilileta matumaini mapya kwa watanzania na iliwavutia wengi. Matumaini haya yalitokana na ukweli kwamba, pamoja na Rais Benjamini Mkapa (mtangulizi wa Rais Kikwete) alifanya vizuri katika kukuza uchumi (kufikia asilimia 7 wakati wa kipindi chake chote cha mihura miwili), uchumi huu haukuweza kuonekana miongoni mwa wananchi kwa ujumla kwani mwananchi wa kawaida aliendelea kuishi katika umaskini (World Bank, 2015).

Kauli mbiu ya *Maisha bora kwa kila Mtanzania* ilikuwa na nia ya kumtangaza Rais mpya kwa matumaini kuwa angeleta unafuu katika hali ya maisha ya mwananchi wa kawaida, hususani kumpunguzia makali ya umaskini. Kauli mbiu hii pia ilichagizwa na mikakati mingine kama vile MKUKUTA (National Strategy for Growth and Poverty Reduction) and *Kilimo Kwanza* (“*Agriculture First*”).



*Rais Mstaafu Dkt .Jakaya Mrisho Kikwete (2005-2010)*

Benki ya Dunia (2015) ilikadiria kuwa Serikali ya Kikwete ilijitahidi kupunguza umaskini kwani kiwango cha wananchi ambao walikuwa hawana uwezo wa kupata mahitaji msingi kilishuka kutoka asilimia 34.4 mwaka 2007 mpaka asilimia 28.2 mwaka 20111/2012 kwa kutumia vigezo vya Tanzania vya kupima kiwango cha umaskini. Ripoti hii ya Benki ya Dunia pia ilionesha kuwa kipindi cha Rais Kikwete kulikuwa na uboreshaji kidogo wa maisha ya watanzania walio wengi hususani katika kupata huduma za msingi kama vile elimu, umri wa kuishi na kupata chakula. Pamoja na haya, hisia na ripoti za kwenye magazeti na mitandao ya kijamii kwa ujumla zilionesha ni kwa kiwango kidogo kauli mbiu ya *maisha bora kwa kila Mtanzania* ilitekelezeka kinyume na matarajio ya wengi.

Hata hivyo, ni vema kueleza kuwa uchaguzi wa nne chini ya mfumo wa vyama vingi Tanzania uliofanyika 2010 uligubigwa na dosari ya watu wachache kujitokeza kupiga kura kwani, asilimia ya waliojitokeza ilishuka kutoka asilimia 70 uchaguzi wa 2005 mpaka asilimia 43 uchaguzi wa 2010. Tafti zilizofanyika zilionesha sababu kadha wa kadha kuhusu hali hii ya kushuka kwa idadi ya watu waliojitokeza kupiga kura. Sababu moja kubwa ilikuwa ni kutoridhishwa kwa utendaji kazi wa Serikali ya Kikwete hususani kutokutekelezwa kwa ahadi

nyingi alizozitoa wakati akijinadi mwaka 2005. Hali hii ya utendaji wa Rais Kikwete imeoneshwa katika Jedwali 2-1: Mgawanyo wa kura za Urais Uchaguzi Mkuu 2010 linaloonesha kura alizopata katika mgawanyo wa kura za urais za uchaguzi wa 2010.

***Jedwali 2-1: Mgawanyo wa kura za Urais Uchaguzi Mkuu 2010***

| Mgombea Urais | Chama cha Siasa | Kura | Asilimia |
|---|---|---|---|
| JakayaMrishoKikwete | CCM | 5,276,827 | 62.84 |
| Wilbrod Peter Slaa | CHADEMA | 2,271,941 | 27.05 |
| Ibrahim HarunaLipumba | CUF | 695,667 | 8.28 |
| Peter Kuga Mziray | APPT-Maendeleo | 96,933 | 1.15 |
| HashimRungweSpunda | NCRR-Mageuzi | 26,388 | 0.31 |
| MutamwegaMugayhwa | TLP | 17,482 | 0.21 |
| FahmiNassoroDovutwa | UPDP | 13,176 | 0.16 |
| Jumla | | 8,398,414 | 100.00 |

Chanzo: Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), 2011

Takwimu kwenye Jedwali 2-1: Mgawanyo wa kura za Urais Uchaguzi Mkuu 2010 zinaonesha kuwa mgombea Urais kupitia CCM alishinda uchaguzi kwa kiwango cha kura zilizoshuka karibu ya asilimia 20 ya kura ililinganishwa na kura alizopata mwaka 2005. Hii ni uthibitisho kuwa utendaji wa CCM na mgombea wake wa urais ulishuka na hata kukubalika kwake kulikuwa kumeshuka. Hii ilikuwa na madhara kwa CCM ilipoingia kwenye kinyanganyiro cha uchaguzi wa 2015.

Changamoto nyingine zilizoukabili utawala wa Kikwete ni suala la ugunduzi wa gesi asilia mkoani Mtwara ambayo ilichukuliwa na watu wa Mtwara kama njia ya kuifanya Mtwara kuwa "Dubai" ya Tanzania. Dhana hii ilipelekea suala la gesi asilia kuwa na matukio makubwa ya mapambano baina ya serikali na wananchi wa Mtwara na mara nyingine kusababisha uharibifu wa mali na majeruhi hasa mwaka 2013. Changamoto nyingine iliyotia doa serikali ya Kikwete (hasa wakati wa muhura wake wa pili) ni tatizo la rushwa. Kati ya kashfa za rushwa zilizolitikisa Taifa na kuvuta hisia za watanzania na wadau wa maendeleo ya Tanzania ni ya *Tegeta* Escrow iliyohusisha malipo tata ya serikali kupitia benki kwa mfanyabiashara maarufu James Rugemalira. Vyama vya upinzani vilitumia kashfa hii kushinikiza uwajibikaji wa viongozi na wanasiasa waliohusika na kashfa hii. Hii ilifikia hatua yakajitokeza hata majibizano makali bungeni hususani kati ya Mheshimiwa David Kafulila (Mb.) na Mwanasheria Mkuu wa Serikali Fredrick Werema kwa maneno kama vile *tumbili, mwizi, fisadi*.

Mwisho wa siku kashfa hii iliondoka na aidha kutimuliwa kazi au kujiuzulu kwa vigogo wa Serikalini ikiwa ni pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali Fredrick Werema, Waziri wa Nishati Sospeter Muhongo, na waziri wa Ardhi Anna Tibaijuka. Kashfa hii pia iliwahusisha hata mawaziri wa zamani Andrew Chenge, William Ngeleja, na Daniel Yona, hata viongozi wa dini ikiwa ni pamoja na Askofu Msaidizi Methodius Kilaini (Gray 2015 and Butahe and Elias 2014).



*Wahanga wa Sakata la Akaunti yaTegeta Escrow na Mmoja Aliyenusulika kama Ilivyochorwa na Mchora katuni*


Suala jingine lililotia dosari utawala wa Rais Kikwete ni la vyombo vya ulinzi na usalama kuwaumiza au kuwadhuru wananchi wanaoishi aidha jirani na hifadhi za Taifa za wanyama pori au karibu na maeneo ya machimbo makubwa ya madini yanayoendeshwa na wawekezaji. Kwa mfano yalikuwepo malalamiko kuwa wananchi walikuwa wakinyanyaswa au kuumizwa na wana vyombo vya ulinzi na usalama wakati vikidhibiti ujangili.



*Moja ya Picha Zilizothibitisha Hatua Zilizotia Mashaka  Kuhusu Kudhibiti Suala la Ujangili*

Hatua za kudhibiti ujangili zilizokuwa tata ni pamoja na "*Operesheni tokomeza ujangili*" iliyoanzishwa mwezi Oktoba 2013. Operesheni hii ilibidi isimamishwe baada ya mwezi mmoja kwani ilionekana kugubikwa na ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu (Makoye 2014).

Matatizo mengine yaliyochafua utawala wa Rais Kikwete ni kuongezeka kwa migogoro mingi ya ardhi hususani mapigano kati ya wakulima na wafugaji kwenye maeneo kama vile Kilosa na Loliondo. Pia kuibuka kwa migogoro yenye sura za kidini ni jambo lililotia doa serikali ya awamu ya nne hasa kipindi cha muhura wa pili. Mfano mzuri ni maandamano na mashambuliano ya Mbagala, Dar es Salaam, iliyohusisha baadhi ya waislamu kutaka kulipiza kisasi kwa wakristo kwa kile kilichoelezwa kuwa ni mtoto mkiristo kukojolea kitabu kitakatifu cha dini ya kiislamu (Kuruani Tukufu). Harakati hizi zilidaiwa kumuhusisha kiongozi wa waislamu, Sheikh Issa Ponda na wanachama wengine 52 toka jumuia za taasisi za kiislamu.



*Kiongozi wa Waislamu Sheikh Issa Ponda Akiwahutubia Wafuasi Wake*

Tukio jingine lilokuwa na sura ya mgogoro wa kidini ni ule wa mwanzoni mwa mwaka 2013 uliohusisha kuuawa kwa mchungaji wa Kanisa la Kilutheri Tanzania huko mkoani Geita. Mauaji haya yalitokea kutokana na mgogoro baina ya wakristo na waislamu. Pia mwezi Mei 2013 tukio jingine lilihusisha kulipuka kwa bomu lililoua watu watatu na kujeruhi wengine 60 katika maeneo ya Kanisa la Mtakatifu St. Joseph Olasiti Mkoani Arusha ambapo hata Balozi wa Vatikani hapa nchini na Askofu Mkuu wa Jimbo Katoliki la Arusha walikuwepo.

Matukio mengine yaliyojiri wakati wa utawala wa awamu ya nne ambayo yalitikisa nchi ni pamoja na kutoridhisha kwa serikali katika utoaji wa huduma za umma kama vile afya, elimu, maji na umeme. Mgomo wa madaktari wa mwaka 2012 uliohitimika kwa kutekwa nyala na kuumizwa (na kuachwa nusu mfu huko Mabwepande nje kidogo ya jiji la Dar es Salaam) kwa kiongozi wa Madaktari Steven Ulimboka. Hili ni tukio lililotia doa serikali ya awamu ya nne. Pia kushindwa kwa wanafunzi wengi wa kidato cha nne, tishio la mgomo wa walimu, ukosefu wa maji safi na salama hususani katika jiji la Dar es Salaam na kukosena kwa uhakika wa huduma ya umeme navyo vilitikisa nchi.

Katika kilichoonekana kama juhudi za CCM kujisafisha kutoka doa la kashfa za rushwa, mwaka 2011 Rais Kikwete aliahidi kusafisha chama kwa kutoa siku 90 kwa mafisadi na wala rushwa kuondoka wenyewe kutoka kwenye chama.



*Vigogo wa CCM Waliokuwa kwenye Orodha ya Wanachama Waliokuwa Wanatupiwa "Mashambulizi" toka Ndani na Nje ya Chama ili Wajisafishe kama Njia ya Kukisafisha Chama*

Mafanikio makubwa ya mkakati huu wa kukisafisha chama ulioratibiwa na Kamati ya Maadili ya chama kupitia kauli mbiu ya "*kujivuagamba*" lilikuwa ni kujiuzulu kwa Rostam Aziz mwezi wa Julai 2011 kutoka nafasi yake ya kuwa mbunge wa Jimbo la Igunga (kupitia tiketi ya CCM) na pia nafasi yake kwenye Kamati Kuu ya Chama (Butahe and Yamola 2014).



*Bwana Rostam Aziz, Alijiuzulu Nafasi yake ya Ubunge kwa kile Alichoeleza kuwa ni Kuachana na Siasa za Majitaka*

Jitihada za kujisafisha mbele ya macho ya umma ndani ya CCM pia zilidhihirika mwishoni mwaka 2014 ambapo Kamati ya Maadili ya Chama iliwasimamisha kufanya kampeni za mapema makada wake sita waliokuwa wanaonesha wazi nia ya kutaka kugombea nafasi ya Urais. Makada hawa walikuwa Edward Lowassa, Bernard Membe, Fredrick Sumaye, January Makamba, Stephen Wasira, and William Ngeleja.








*Makada wa CCM Waliopigwa "stop" kwa Kuanza Kampeni za Kuwania Nafasi ya Urais kwa tiketi ya CCM Mapema*

**2.4 Chaguzi Ndogo na Chaguzi Ngazi Msingi 2014**

Chaguzi ndogo na chaguzi za ngazi msingi 2014 zilikuwa ni pimajoto nyingine kwa vyama vya siasa kuelekea uchaguzi mkuu 2015. Kufuatia kujiuzulu kwa Rostam Aziz uchaguzi mdogo ulifanyika jimbo la Igunga mwezi Oktoba 2011. Katika uchaguzi huu mdogo mgombea wa CCM Dalaly Kafumu alimshinda mgombea wa CHADEMA Kashindye Mwandu kwa kura 26,484 dhidi ya 23,260 (Tume ya Taifa ya Uchaguzi, 2011). Mwaka uliofuta kufuatia kifo cha Mbunge wa Jimbo la Arumeru Mashariki kwa tiketi ya CCM, CHADEMA ilishinda uchaguzi huu mdogo uliokuwa na ushindani mkubwa. Mgombea wa CHADEMA Joshua Nassari ndiye alishinda. Mwaka 2013 CUF iliendelea kutetea kiti cha jimbo la Chambani wakati wa uchaguzi uliofanyika kufuatia kifo cha mbunge wa jimbo hili marehemu Salim Khamis. Aliyeshinda ni Yussuf Salim Hussein ambaye alishinda kwa ushindi wa kishindo. Mwaka 2014 CCM ilishinda kwa kishindo chaguzi ndogo mbili yaani uchaguzi katika majimbo ya Kalenga and Chalinze kufuatia vifo vya wabunge wa majimbo haya.

Mtihani wa mwisho kuhusu nguvu ya vyama vya siasa ilikuwa ni kwenye chaguzi za ngazi msingi 2014 zilizoratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI). Jedwali 2.2 linaonesha matokeo ya chaguzi hizi ambapo inaonesha CCM ilishinda kwa asilimia 74.5 ikifuatiwa na CHADEMA kwa ushindi wa asilimia 16. Pamoja na kupoteza zaidi ya nafasi 3,000 kwenye chaguzi hizi, CCM iliingia kwenye kinyanganyiro cha uchaguzi wa 2015 ikiwa na hali ya kujiamini zaidi ikilinganishwa na vyama vya upinzani (Chidawali and Chibwete 2014).

*Jedwali 2-2: Ushindani wa Vyama vya Siasa katika Uchaguzi wa Ngazi Msingi, 2014*

| Chama cha siasa | idadi ya mitaa ambayo chama kilishinda | idadi vijiji ambayo chama kilishinda | Jumla | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| CCM | 2,116 | 7,290 | 9,406 | 74.5 |
| CHADEMA | 753 | 1,248 | 2,001 | 15.9 |
| CUF | 235 | 946 | 1,181 | 9.4 |
| NCCR-Mageuzi | 8 | NA | 8 | 0.1 |
| Jumla | 3,112 | 9,454 | 12,596 | 100.0 |

## 2.5 Mchakato wa Katiba Mpya


Desemba 31, 2010 katika hotuba ya mwaka mpya, Rais Kikwete alianzisha hoja ambayo ilikuja kuwa katika masuala muhimu yaliyoathiri, kwa namna moja au nyingine, uchaguzi wa 2015. Katika hotuba hiyo Rais alitangaza nia yake ya kuanzisha mchakato wa Katiba mpya. Tamko hili liliibua hamasa baina ya wadau mbalimbali wa siasa na mwisho wa siku ilikuja kusababisha hata uundwaji wa makundi mbalimbali kama njia ya kujipanga kushindana kushika dola katika uchaguzi wa 2015.



*Rais Dkt Kikwete (mstaafu kwa sasa) na Rais Dkt Shein Wakizindua Katiba Pendekezwa*

Rais Kikwete aliunda Tume ya Marekebisho ya Katiba iliyokuwa na idadi ya wajumbe 30, 15 kutoka Tanzania Bara na 15 kutoka Zanzibar. Wajumbe hawa walitoka katika taasisi mbalimbali ikiwa ni pamoja na vyama vya siasa, asasi za kiraia, taasisi za kidini, vyama vya wafanyakazi, wafanyabiashara, wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Tume hii ilianza

rasmi kazi yake mwezi Aprili, 2012 chini ya uongozi wa Makamu wa Rais na Waziri Mkuu Mstaafu, Joseph Sinde Warioba




*Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Katiba, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu Mstaafu, Joseph Sinde Warioba*

Tume ya Marekebisho ya Katiba ilitembea nchi nzima kuwafikia na kupata maoni ya wananchi kuhusu Katiba mpya.Wadau na makundi mbalimbali ya jamii ikiwa ni pamoja na wananchi wa kawaida walifikiwa kupitia njia mbali kama vile mikutano ya hadhara, mitandao ya kijamii, vyombo vya habari, n.k. Inakadiliwa watu wapatao 1.4 milioni walifikiwa wakati wa mchakato wa kutafuta maoni kuhusu Katiba mpya. Tume ya Marekebisho ya Katiba ilitoa rasimu ya kwanza ya Katiba tarehe 3 mwezi Juni 2013, ikifuatiwa na mwezi mmoja wa mjadala wa rasimu hii katika mabaraza 169 katika ngazi ya wilaya. Baada ya kuifanyia marekebisho rasimu ya kwanza (kutokana na mapendekezo yaliyotokana na mabaraza ya ngazi ya wilaya), Tume ya Warioba iliandaa na hatimaye kuwasilisha rasimu ya pili ya Katiba kwa Rais tarehe 30 Desemba 2013. Hatua hii ilifuatiwa na Rais kuunda Bunge Maalumu la Katiba lilionekana kuwa na uwakilishi mpana.Hata hivyo, wajumbe wengi wa Bunge hili maalum walikuwa wanatoka kundi la wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tokea Zanzibar. Bunge Maalumu la Katiba liliapishwa tarehe 18 Februari 2014 baada ya mijadala na maelekezo juu ya kanuni za kutumika wakati wa Bunge hili. Wajumbe wa Bunge Maalum la Katiba walianza kujadili rasimu ya Katiba tarehe 21 mwezi Machi 2014.

Mara baada ya kuanza kwa mijadala ya Bunge Maalumu la Katiba, ilionekana wazi mijadala iligawanyika katika kambi kuu mbili za kivyama (vyama vya siasa). Utaratibu ambao ungetumika kuongoza mijadala, hoja za kanuni za kuongoza mijadala hususani kuhusu utaratibu ambao ungetumika katika kupiga kura za maamuzi (kura ya siri au ya wazi) vilionekana kulipasua Bunge Maalumu katika makundi mawili yaani kundi la CCM na kundi la vyama vya upinzani.

Ni vema kubainisha kuwa pasua kichwa katika mijadala ya Bunge ilikuwa ni suala la muundo wa serikali kwa maana ya muundo wa serikali moja au tatu. Hatma ya mjadala mkali huu juu ya muundo wa serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilikuwa ni ‘kuzaliwa” kwa kambi mbili yaani “Tanzania Kwanza” likiwajumuisha hasa baadhi ya wajumbe wa CCM na lile la Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA) likiwaunganisha baadhi ya wabunge toka vyama vya upinzani. Kambi hii ya pili iliundwa na vyama vinne vya upinzani ambavyo ni CUF, CHADEMA, NLD na NCCR-Mageuzi.




*Rasimu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*

UKAWA ilijikita katika kuleta umoja hasa baina ya vyama vikuu vya upinzani. Ukawa pia ilichukua msimamo wa kuitetea rasimu ya Katiba iliyoandaliwa na Tume ya Warioba waliyodai ndiyo yenye mawazo na mapendekezo ya wananchi. Kambi ya CCM kupitia mwavuli wa “Tanzania Kwanza” (ambao wajumbe wake ndio walikuwa wengi) walisitiza kuwa Bunge Maalumu la Katiba lina mamlaka ya kubadilisha kilichomo kwenye rasimu. Wazo hili la Bunge Maalum kuwa na mamlaka ya kubadili vifungu vya rasimu ya Katiba na kuifanyia marekebisho makubwa lilipingwa vikali na kambi ya UKAWA.




*Viongozi wa Vyama Vinne vya Siasa chini ya Mwavuli wa UKAWA Wakitia saini Makubaliano ya Ushirikiano Wao*

Huku wakiwa wamechefuliwa na wingi wa wajumbe wa kundi la "Tanzania Kwanza constitutional draft", tarehe 17 Aprili, 2014 kundi la liliamua kutoka nje ya ukumbi wa Bunge na kususia vikao vyake. Pia wajumbe wake waliapiza kususa ushiriki wao katika mchakato wa kupata Katiba mpya. Kama njia mbadala ya kuweza kushiriki kwenye uchaguzi wa 2015 vyama vinavyounda umoja wa UKAWA waliingia katika mazungumzo yaliyoratibiwa na Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD) kwa minajili ya kuangalia uwezekano wa kufanyika kwa marekebisho ya baadhi ya sheria zinazobana mianya ya kufanyika kwa uchaguzi ulio huru na wa haki.



*Viongozi wa UKAWA Wakiongea na Waandishi wa Habari*

Maeneo yaliyokuwa yanapendekezwa kufanyiwa marekebisho ni pamoja na: (i) kuundwa kwa Tume huru ya Taifa ya uchaguzi; (ii) kuruhusiwa kwa mgombea binafsi wakati wa uchaguzi; (iii) kuwepo kwa utaratibu wa mgombea urais kupata asilimia zaidi ya 50 ya kura zote kwa mgombea anayetangazwa kuwa mshindi wa kiti cha urais badala ya utaratibu wa yeyote atakayemzidi mgombea mwenzake; na (iv) kuruhusiwa kwa matokeo ya urais kuweza kupingwa mahakamani. Pia yalikuwepo makubaliano kuwa UKAWA wangeendelea kususia mchakato wa Katiba mpya mpaka baada ya uchaguzi mkuu. Makubaliano haya yalikuwa hayana nguvu ya kisheria hivyo utekelezaji wake ulitegemea zaidi uungwana wa wahusika ambao hata hivyo haukutekelezwa.



*Bunge Maalum la Katiba Likiwa Kazini*

Pamoja na hali iliyoelezwa, mchakato wa Katiba mpya hususani Bunge Maalum la Katiba liliendelea huku likikosa chachu ya michango ya wajumbe wa Bunge wa upinzani toka vyama vinavyounda UKAWA. Mwisho wa siku Bunge Maalum la Katiba liipitisha Katiba Pendekezwa mnamo tarehe 2 Oktoba, 2014. Kwa mujibu wa ratiba ya mchakato wa Katiba uliokuwepo, hatua iliyokuwa inafuatia ilikuwa ni kuipeleka Katiba Pendekezwa kwa wananchi kuipigia kura ya ama kuikubali au kuikataa. Hata hivyo hatua hii haikuweza kufikiwa mpaka kipindi cha Uchaguzi mkuu wa 2015. Cha kusisitiza hapa ni kwamba pamoja na kwamba mchakato wa Katiba ulikuwa umesitishwa wakati wa kuelekea uchaguzi mkuu 2015, vyama vinavyounda umoja wa UKAWA vilitumia fursa ya umoja wao huo kuunganisha nguvu kama mkakati wa kuing'oa CCM madarakani na kutoa ushindani mkubwa kwake.

**2.6 Migogoro na Makundi ya Ndani ya Vyama vya Siasa**

Kipindi cha kuelekea uchaguzi mkuu wa 2015 kiligubikwa na matukio makubwa ndani ya vyama vikubwa vya siasa, CCM, CHADEMA, CUF na NCCR-Mageuzi. Baadhi ya matukio haya yaliathiri, kwa namna moja au nyingine, uchaguzi huu. Matukio haya makubwa yamegawanyika katika sura au makundi makubwa mawili: (i) ushindani na migogoro ya kiuongozi ndani ya vyama na (ii) mipango ya kisera na kimkakati kuelekea uchaguzi wa 2015.

Rais wa anayemaliza muda wake akiwa hana nafasi ya kugombea tena alitoa fursa ya kuongezeka kwa ushindani mkubwa wa kuwania nafasi ya urais ndani ya chama tawala, CCM. Hata ndani ya vyama vya upinzani nako migogoro na makundi ya kuwania nafasi ya urais haikuwa haba. Kwa ujumla, hali hii ilipelekea vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kuongeza hamasa na muwashawasha wa wananchi kuhusu uchaguzi mkuu wa 2015. Wakati mwingine hata uvumilivu wa kisiasa miongoni mwa viongozi ndani ya vyama ulionekana kufifia kadri za kuelekea uchaguzi mkuu zilivyokaribia. Viongozi hao walioonekana kutaka

kutia nia ya kugombea nafasi mbalimbali hasa urais. Matokeo ya haya ilikuwa ni kuibuka kwa makundi ya kimkakati ndani ya CCM na hata kwa upande wa vyama vya upinzani.

Kwa upande wa vyama vya upinzani, yalishuhudiwa makundi ya migogoro ya kiuongozi ndani ya CUF na CHADEMA. Katika CUF, Hamad Rashid, mbunge wa jimbo la Wawi, alionesha nia ya kutaka kuwania nafasi ya uongozi aliyokuwa nayo Seif Sharif Hamad ndani ya chama yaani Ukatibu Mkuu wa Chama. Kutokana na hali hii Hamad Rashid alitimuliwa kutoka CUF mwezi Januari 2015, hali iliyopelekea (kwa mujibu wa sheria za uchaguzi Tanzania) "kupoteza" nafasi ya kiti chake cha ubunge. Akijua yatakayomkuta baada ya kutimuliwa kutoka CUF, Hamad Rashid alikimbilia mahakamani na kuweka pingamizi akipinga uamzi wa CUF kumtimua. Hali hii ilipelekea mahakama kuamuru Hamad Rashid aendelee kuwa mbunge almaarufu kama "mbunge wa mahakama" mpaka mwezi Julai 2015 alipoamua kuhama rasmi CUF na kuunda kujiunga chama kipya cha Alliance for Democratic Change (ADC) na baadaye kugombea nafasi ya urais wa Zanzibar kwa tiketi ya chama hiki.

Hali kama hii ya mashindano na migogoro ya kuwania nafasi za uongozi ndani ya vyama vya siasa pia ilijitokeza ndani ya CHADEMA. Hii ilikuwa ni baina ya mwenyekiti Freeman Mbowe na 'kijana' ambaye nyota yake ya uongozi ilionekana kung'ara yaani Zitto Kabwe hususani mwaka 2009, alipoonesha dalili na mwendendo wa kuinyemelea nafasi ya uenyekeiti wa chama.



*Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe na Mhe. Zitto Kabwe*

Migogoro na dalilli za kutoelewana baina ya kundi la Mbowe na la Zitto ndani ya chama zilikuwa dhahiri mwaka 2013 wakati taarifa ya chama ya "wazi" ilimtuhumu Zito Kabwe kuwa amekuwa akifadhiliwa hela nyingi (dola robo milioni) na CCM ili kukihujumu na kukiangamiza chama cha CHADEMA. Katika hali iliyoonekana kumdhibiti Zitto Kabwe, chama chake kilijaribu kumtimua na hatimaye hazma hii ilifanikiwa mwezi Machi 2015 CHADEMA kiliposhinda kati kesi ya Mahakama Kuu aliyokuwa ameifungua Zitto Kabwe akipinga uamzi wa chama chake kumtimua.



*Katibu Mkuu wa Zamani wa CHADEMA, Dr.Wilbrod Slaa, Akiteta Jambo na Mwenyekiti wake Freeman Mbowe na Bwana Zitto Kabwe kabla Hawajasambaratika*

Baada ya kutoka CHADEMA Zitto Kabwe alikaa "kijiweni" kwa muda baada ya uamuzi wa Mahakama Kuu kumuamuru aachie kiti chake cha ubunge kupitia CHADEMA. Baadaye alijiunga na chama kipya cha siasa cha Alliance for Change and Transparency (ACT-Wazalendo). Zitto Kabwe alichaguliwa kuwa kiongozi mkuu wa ACT-Wazalendo, huku Anna Mghwira akishika nafasi ya uenyekiti wa chama.

Ndani ya CCM ambapo Rais aliyepeperusha bendera yake 2005 alikuwa anamalizia kipindi chake cha uongozi wa miaka kumi, vuguvugu la makundi na migogoro ya kutaka kumrithi katika uchaguzi wa 2015 ilidhihirika miongoni mwa makada na wanachama. Kwa mara ya kwanza katika historia ya Tanzania walijitokeza jumla ya wanachama 42 waliochukua fomu na kuzilipia kwa nia ya kuwania nafasi ya uteuzi wa chama katika nafasi ya urais. Kati ya hawa 14 walikuwa ni mawaziri wastaafu. Pia kati ya watia nia hawa 42, ni thelathini na nane (38) ndio walirudisha fomu zilizojazwa itakiwavyo na hivyo kuwa watia nia rasmi kwa ajili ya uteuzi wa mgombea nafasi ya urais ndani ya chama. Kati ya watia nia hawa 38, Edward Lowassa, Waziri Mkuu Mstaafu, aliyeonekana kuungwa mkono kifedha na mbunge na Mweka Hazina wa zamani wa CCM, Rostam Aziz alionekana kuwa na nguvu na wafuasi wengi. Hata hivyo kashfa ya ufisadi ya Richmond iliyosababisha ajiuzulu nafasi ya Uwaziri Mkuu mwaka 2008 ilionekana kuendelea kuandama harakati za Lowassa za kutaka kuwania nafasi ya kugombea urais kwa tiketi ya CCM. Pamoja na Lowassa, watia nia wengine ndani ya CCM walikuwa ni pamoja na Harrison Mwakyembe na Samuel Sitta kutoka kambi iliyojipambanua kuwa ni "safi" (wapinga rushwa), Naibu Waziri "kijana" January Makamba, Mark Mwandosya (waziri mwandamizi mstaafu kutoka Kanda za Juu Kusini), Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa (wakati wa Utawala wa Kikwete) Bernard Membe, Waziri Mkuu Mstaafu Fredrick Sumaye, Waziri Mkuu aliyekuwa madarakani Mizengo Pinda na Makamu wa Rais aliyekuwa madarakani Mohamed Gharib Billal.




Katika hali ya kutokuamini wafuasi wa Edward walijikuta wakipatwa na mshangao zilipovuja habari kuwa jina la Lowassa (waliyekuwa na imani angesonga mbele katika hatua mbalimbali za mchakato wa kumpata mgombea urais ndani ya chama) ‘lilikatwa’ katika hatua ya mwanzo kabisa ya Kamati ya Maadili ya CCM. Kwa maana hiyo jina la Lowassa halikuwa mojawapo kati ya majina matano yaliyopelekwa na Kamati Kuu ya CCM mbele ya Kamati kuu Taifa ya CCM kwa maamuzi zaidi mnamo mwezi Julai 2015. Kati ya majina matano yaliyowasilishwa mbele ya Kamati Kuu Taifa ya CCM, yaliondolewa majina ya January Makamba na Bernard Membe kutoka katika kinyang’anyiro na hivyo kubakiza majina ya Amina Salum Ali, Asha Rose Migiro, na John Pombe Magufuli ambayo ndiyo yalipelekwa ngazi ya Mkutano Mkuu wa CCM kwa maamuzi zaidi.




*Watia nia Watatu wa Nafasi ya Uteuzi wa Urais ndani ya CCM Walioweza Kufika Hatua ya Mkutano Mkuu wa CCM kwa Maamuzi zaidi*

Alikuwa ni John Magufuli ambaye hatimaye aliteuliwa na Mkutano Mkuu wa CCM kupeperusha bendera yake katika uchaguzi wa 2015. Uteuzi wa Magufuli ulionekana kukipa hafueni Chama cha Mapinduzi kutokana na rekodi ya utendaji kazi wa Magufuli katika nafasi

mbalimbali za uongozi alizopitia hususani unaibu na baadaye uwaziri. Magufuli pia alionekana 'kuuzika' machoni pa watanzania wengi kutokana na misimamo yake ya kujiamini na kutokuwa na kashfa za rushwa. Sifa hizi za mgombea huyu zilisaidia kupunguza makali ya chuki na kutopendeka kwa CCM machoni pa watanzania kulikosababishwa na, pamoja na mambo mengine, kukithiri kwa vitendo vya rushwa na ufisadi na huduma za jamii zisizoridhisha hasa katika kipindi cha pili cha uongozi wa awamu ya nne.

Uteuzi wa Magufuli kuwa mgombea urais kwa tiketi ya CCM pia uliacha maswali mengi kuliko majibu hususani miongoni mwa baadhi ya wale walioshindwa katika kinyang'anyiro hiki. Hali hii iikuwa hasa kwa upande wa Edward Lowassa ambaye kama isharaya kutoridhika na mchakato wa uteuzi wa nafasi kugombea urais ndani ya CCM alikihama Chama cha Mapinduzi na kujiunga chama cha upinzani CHADEMA, mnamo mwezi Agusti 2015 kwa nia ya kutafuta uwezekano wa kuteuliwa kuwania nafasi ya urais kwa tiketi ya chama kipya alichojiunga. Zikiwa hesabu za kisiasa, vyama vinne vinavyounda umoja wa UKAWA viliamua kumuunga mgombea mmoja ngazi ya urais kupitia CHADEMA naye si mwingine bali ni Edward Lowassa kama njia ya kukusanya nguvu za kuing'a CCM toka madarakani kwenye uchaguzi wa 2015. Hata hivyo, uteuzi huu wa Lowassa uliibua hisia tofauti tofauti miongoni mwa watanzania, baadhi wakihoji ni kwa vipi CHADEMA wameweza kumpokea na kumteua Edward Lowassa ambaye kipindi cha nyuma walikuwa wanamwita ni "fisadi mkubwa" (mmoja kati ya waliomo kwenye orodha ya aibu-list of shame iliyoasisiwa na CHADEMA) na hata kuwa mmoja wa walengwa wa mashambulizi ya CHADEMA dhidi ya kampeni maalumu za kupambana na mafisadi almaarufu kama "Operation Sangara" na "Movement for Change-M4C".




*Katibu Mkuu wa CHADEMA, Dkt Wilbroad Slaa na Mwenyekiti wa CUF, Prof. Ibrahim Lipumba*

Ujio wa Lowassa ndani ya CHADEMA ulisababisha kupanguliwa kwa safu za uongozi hususani kwenye vyama vinavyounda UKAWA. Katibu Mkuu wa CHADEMA Dkt Wilbroad Slaa na Mwenyekiti wa CUF Prof Ibrahim Lipumba waliachia ngazi nafasi zao (walijiuzulu) kama ishara ya kupinga ujio wa Lowassa akiwa na nia ya kugombea nafasi ya Urais. Baadhi

ya viongozi na wanachama walimuona Lowassa kama mtu asiyekuwa na sifa za kupeperusha bendera ya UKAWA kwani vyama vingi vya upinzani (hasa CHADEMA na CUF) vilishamchafua sana kama fisadi katika kashfa ya Richmond miaka ya 2007 na 2008 na hivo kutokuwa tayari kumuunga mkono kama mgombea urais. Kashfa hii ya Richmond ndiyo ilimlazimisha Edward Lowassa kujiuzulu nafasi yake ya Uwaziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 2008.



*Mawaziri wakuu wastaafu, Lowassa na Sumaye kabla hawajahama toka CCM kwenda CHADEMA*

Pamoja na Lowassa, vigogo wengine waliomfuata baada ya kujiunga chama cha upinzani cha CHADEMA ni pamoja na Frederick Tluway Sumaye (Waziri Mkuu Mstaafu), Kingunge Ngombale Mwiru, Juma Mwapachu, Naibu Waziri mmoja na wenyeviti watatu wa mkoa.



*Katika hali kama ya kutoamini vile, eh, msemo wa wahenga wa "hakuna adui wa kudumu katika siasa" ukidhihirika baada ya Lowassa kuwa katika mazungumzo ya 'dili' ya kuhama kutoka CCM kwenda CHADEMA*

Hatma ya mchakato wa kumpata mgombea urais kwa tiketi ya CCM uliogubikwa na hamasa na makundi yaliyokuwa yakipingana ilikuwa ni kumpata mgombea ambaye kwa kiwango

kikubwa alikonga nyoyo za watanzania wengi. Mgobea huyu hakuwa na mbwembwe wakati wa harakati za kuwania nafasi hii. Pia agenda yake ya 'magufuli kwa ajili ya mabadiliko' iliweza kusaidia chama chake kusafishika kwa kiwango fulani dhidi ya mapungufu yaliyoikumba serikali ya awamu ya nne hususani katika muhula wake wa pili. Kwa upande wa UKAWA kama kambi ya vyama vya upinzani, uteuzi ulihitimishwa kwa kumpata Edward Lowassa 'aliyekatwa' na CCM katika uteuzi wa ndani ya chama. Uteuzi huu wa Lowassa, hata hivyo uliambatana na umegukaji wa safu ya uongozi ya CHADEMA na CUF kufuatia kujiuzulu kwa Katibu Mkuu wa CHADEMA Dkt. Willibroad Slaa na Mwenyekiti wa CUF Prof Ibrahim Lipumba. Hata hivyo, ilionekana ujio wa Lowassa ulikiimarisha chama cha CHADEMA hasa kwa upande wa raslimali fedha na hata mtaji wa kisiasa katika uchaguzi wa 2015. Pia ni katika kipindi cha kuelekea uchaguzi CHADEMA ilishuhudia kutimuliwa kwa Zitto na kujiunga na chama kipya cha upinzani cha ACT-Wazalendo na baadaye kuweza kuchaguliwa kuwa kiongozi mkuu wa chama hicho na hivyo kuongeza nguvu katika kumnadi mgombea urais kwa tiketi ya ACT-Wazalendo, Anna Elisha Mghwira. Kwa ufupi, uteuzi wa wagombea urais miongoni mwa vyama vya upinzani hususani CHADEMA (ikiwakilisha UKAWA) na ACT-Wazalendo kwa ajili ya uchaguzi wa 2015 kwa mara ya kwanza katika historia ya Tanzania ulionekana kutoa changamoto za kiushindani kwa CCM, chama ambacho kimekuwa madarakani kwa miaka zaidi ya hamsini tangu kupata uhuru.

## 2.7 Hali ya Uhodhi wa Chama Tawala Kuelekea Uchaguzi Mkuu wa 2025

Kabla ya kuanza kwa mchakato wa uchaguzi wa 2015 CCM ilikuwa na nafasi ya pekee kutokana na ukongwe (kimekuwa chama tawala tangu uhuru) wake ikiwa ni pamoja na kuwa raslimali nyingi (ikiwa ni pamoja na zile zilizorithiwa baada ya kuisha kwa mfumo wa chama kimoja) ikilinganishwa na vyama vingine. Hii ni pamoja na kuwa na mtandao mkubwa mpaka ngazi msingi kwa maana ya ofisi na matawi ya chama. Hali hii ya uhodhi ilikuwa ni dhahiri hata wakati wa uchaguzi wa 2010 ambao matokeo yake yanaonesha uhodhi huu katika matokeo ya uchaguzi wa ubunge kwenye Jedwali 2-3: Mgawanyo wa viti vya Ubunge na Udiwani Uchaguzi Mkuu 2010.

***Jedwali 2-3: Mgawanyo wa viti vya Ubunge na Udiwani Uchaguzi Mkuu 2010***

| Na. | Chama cha siasa | viti | Viti maalum vya wanawake | Jumla | Madiwani |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | CCM | 186 | 67 | 253 | 2,803 |
| 2. | CHADEMA | 24 | 25 | 49 | 326 |
| 3. | CUF | 23 | 10 | 33 | 126 |
| 4. | NCCR-Mageuzi | 4 | 0 | 4 | 28 |
| 5. | UDP | 1 | 0 | 1 | 28 |
| 6. | TLP | 1 | 0 | 1 | 20 |
| 7. | Vingine | 0 | 0 | 0 | 4 |
| Jumla | | 239 | 102 | 341 | 3,335 |

Chanzo: TEMCO, 2011

## 2.8 Hitimisho

Wakati vyama vya siasa vikizindua kampeni zao kwa ajili ya uchaguzi mkuu wa 2015 Tanzania ilikuwa katika hali ya muhamasiko wa hali ya juu huku vyama hivyo na wanachama wao

(hususani vyama vilivyokuwa na ushindani mkubwa baina yao) wakitambiana kuibuka mshindi. Zipo sababu au vichocheo kadhaa vilivyopelekea mwamuko na hamasa hii katika uchaguzi wa 2015. Sababu au au vichocheo vikubwa ni pamoja na: (i) Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK) kwa upande wa siasa za chaguzi Zanzibar; (ii) kiwango cha utendaji cha uongozi wa awamu ya nne; (iii) chaguzi ndogo ; (iv) mchakato wa Katiba mpya; (v) misuguano na ushindani ndani ya vyama vya siasa; na (vi) kuendelea kuwa na nafasi hodhi kwa chama tawala (CCM) katika siasa za uchaguzi na siasa za Tanzania kwa ujumla. Kwa ujumla, sababu hizi haziwezi kukwepeka katika kuelezea na kuuelewa uchaguzi mkuu wa Tanzania wa mwaka 2015.

## CHAPTER 3

## MIFUMO YA KISHERIA NA KITAASISI KWA UCHAGUZI WA MWAKA 2015

### 3.1 Utangulizi


Sura hii inatathmini mifumo ya kisheria na kitaasisi iliyotumika katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 kwa lengo la kubainisha kama iliwezesha kufanyika kwa uchaguzi unaoaminika, huru na wa haki. Sura hii imegawanyika katika vipengele saba, ikijumuisha utangulizi huu. Kipengele cha pili kinajikita katika kutathmini mfumo wa kisheria wa uchaguzi. Kipengele cha tatu kinahusu mifumo ya kitaasisi. Kipengele cha nne kinaongelea dhana ya uhuru wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na kipengele cha tano kinahusu uhusiano baina ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC). Kipengele cha sita kinajadili dhana ya "kulinda kura" na shauri la mita 200. Kipengele cha mwisho kinatoa majumuisho na mapendekezo.

### 3.2 Mifumo ya Kisheria kwa Uchaguzi wa Mwaka 2015

Mfumo wa sheria unaohusu uchaguzi mkuu katika Jamhuri ya muungano wa Tanzania unapata uhalali wake kutoka kwenye katiba ya jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, pamoja na sheria zingine zinazohusiana na chaguzi. Sheria hizi ni (i) Sheria ya taifa ya Uchaguzi (Sura ya 343) ya mwaka 1985; (ii) Sheria ya Uchaguzi wa serikali za mitaa (Sura 292) ya mwaka 1979, ikiwa ni pamoja na kanuni zake; (iii) Sheria ya gharama za uchaguzi namba 6 ya mwaka 2010 (iv) Sheria ya vyama vya siasa (Sura ya 258) ya mwaka 1992 (v) Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984; na (vi) Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar namba 11 ya mwaka 1984.

#### *3.2.1 Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*

Kwa kiwango kikubwa, katiba ya jamhuri ya muungano wa Tanzania inazingatia vipengele vya msingi vya kimataifa na kikanda ikiwa ni pamoja na tamko la umoja wa mataifa kuhusu haki za binadamu la mwaka 1948; agano la kimataifa kuhusu haki za kiraia na kisiasa la mwaka 1966; agano la kimataifa kuhusu haki za kiuchumi, kijamii na kiutamanduni la mwaka 1966 na hati idhini ya Afrika kuhusu haki za binadamu ya mwaka 1981.




*Katiba ya Jamhuri ya muungano wa Tanzania ya mwaka 1977*

Katiba hii inatoa haki za kiraia na kisiasa, ikiwa ni pamoja na haki ya kushiriki katika uchaguzi sambamba na haki za mtu binafsi; uhuru wa kujieleza, uhuru wa kijiunga na taasisi na uhuru

wa kushiriki katika masuala ya kijamii kama yalivyobainishwa katika ibara za 15, 18, 20, 21, 39 na 67. Katiba pia inatoa fursa kwa uwakilishi wa wanawake kupitia viti maalumu katika ngazi ya ubunge na udiwani kama ilivyobainishwa katika ibara ya 78 na sheria ya uchaguzi wa serikali za mitaa sura ya 292. Katiba hii pia inaweka ukomo wa mihula miwili ya vipindi vya miaka mitano mitano kwa mtu anayechaguliwa kuwa raisi wa jamhuri ya muungano wa Tanzania. Katiba hii pia inatoa uhuru wa mtu kupiga kura, kwa kuzingatia sheria zingine za nchi.

Pamoja na mazuri ya katiba hii, yapo mapungufu kadhaa yanayoweza kuathiri kufanyika kwa uchaguzi unaoaminiwa, huru na wa haki. Mapungufu makubwa ni (i) kuzuiliwa kwa mgombea binafsi (ii) kunyimwa haki ya kushiriki kwenye uchaguzi raia wa Tanzania wanaoishi ughaibuni na wafungwa wanaotumikia adhabu ya kifungo chini ya miezi sita (iii) kukosekana kwa uwazi wa kutosha katika uteuzi wa mwenyekiti wa tume ya taifa ya Uchaguzi, makamishina wa tume na mkurungenzi wa uchaguzi; na (iv) kuzuia kupingwa kwa matokeo ya kura za urais mahakamani.

Kwa kuzingatia mazuri na mapungufu ya vifungu vya katiba kuhusu chaguzi nchini Tanzania, ni wazi kwamba katiba ya jamhuri ya muungano wa Tanzania haiathiri kwa kiwango kikukwa kufanyika kwa uchaguzi unaoaminika, huru na wa haki.

### *3.2.2 Sheria ya Taifa ya Uchaguzi*

Sheria ya taifa ya uchaguzi (Sura ya 343) ya mwaka 1985 ni sheria mahususi inayohusu utekelezaji wa vipengele mbalimbali vya michakato ya uchaguzi kwa uchaguzi wa urais na ubunge wa jamhuri ya muungano wa Tanzania. Sheria hii inatoa mwongozo katika uwekaji mipaka ya majimbo ya uchaguzi; uteuzi wa wagombea, kampeni, upigaji kura, kuhesabu kura na kutangaza matokeo. Sheria hii pia inaeleza namna ya uundwaji wa tume ya taifa ya uchaguzi na mamlaka ya tume hiyo. Sheria hii vile vile inaelekeza jinsi ya kutatua migogoro ya uchaguzi. Kwa ujumla, sheria hii si kandamizi kiasi cha kuathiri michakato ya uchaguzi. Japokuwa sheria hii haitoi mwanya kwa matokeo ya urais kuhojiwa mahakamani, inaruhusu kuhojiwa kwa matokeo ya ubunge. Kwa ujumla, sheria hii haimnyimi raia haki zake za msingi za kushiriki katika uchaguzi.

### *3.2.3 Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa*

Uchaguzi wa madiwani katika serikali za mitaa anaongozwa na sheria ya uchaguzi wa serikali za mitaa (sura ya 292) ya mwaka 1979. Sheria hii ipo chini ya ofisi ya waziri mkuu –Tawala za Mikoa na Serikali za mitaa (PMO-RALG), ambayo ni taasisi ya serikali kuu. Ofisi hii imepewa jukumu la kusimamia uchaguzi wa serikali za mitaa Tanzania bara. Sheria hii inatoa mwongozo wa uchaguzi wa madiwani hivyo kuilazimisha tume ya Taifa ya Uchaguzi kuitumia katika kusimamia uchaguzi mkuu.

Kama ilivyo sheria ya taifa ya uchaguzi, sheria hii inatoa mwongozo wa uwekaji mipaka ya maeneo ya uchaguzi katika ngazi ya serikali za mitaa, uteuzi wa wagombea, kampeni, upigaji kura, uhesabuji kura na utangazaji wa matokeo. Pia sheria hii inaeleza muundo na mamlaka ya chombo cha kusimamia uchaguzi. Sheria hii pia inatoa mwongozo wa kushughurikia

mapingamizi ya uchaguzi katika mahakama. Kwa ujumla, sheria hii inakidhi vigezo vya msingi vya sheria ya haki.

### *3.2.4 Sheria ya Gharama za Uchaguzi*

Sheria ya gharama za uchaguzi, namba 6 ya mwaka 2010 ina vifungu mbalimbali vinavyohusiana na kugharimia michakato ya uchaguzi, ikiwa ni pamoja na uteuzi wa wagombea, kampeni na shughuli mbalimbali siku ya kupiga kura. Sheria hii inaweka ukomo wa michango ya hiari, ikiwa ni pamoja na misaada ya kifedha kutoka nje ya nchi na uridhiaji wake sambamba na uwekaji wazi gharama za kampeni za uchaguzi. Sheria pia inabainisha makosa na adhabu dhidi ya mambo yaliyozuiliwa na sheria (mfano, kuwashawishi wapigakura kwa fedha au vitu vingine vya thamani; kusafirisha wapigakura na gharama nyingine zozote zilizo kinyume na sheria hii).

Sheria hii ipo chini ya msajili wa vyama vya siasa ambaye amepewa mamlaka ya kuchunguza nyaraka, taarifa na vitabu vya kumbukumbu za matumizi ya fedha vya vyama vya siasa kwa lengo la kubainishi ukiukwaji au utii wa sheria hii. Sheria ya gharama za uchaguzi inatumika tu katika uchaguzi mkuu wa Tanzania Bara. Hivyo basi, sheria hiyo haitumiki katika uchaguzi wa Zanzibar.

### *3.2.5 Sheria ya Vyama vya Siasa*


Sheria ya vyama vya siasa (Sura ya 258) ya mwaka 1992 inaeleza vigezo, masharti na utaratibu wa kusajili vyama vya siasa. Sheria hii inatoa tafsiri na kazi ya chama cha siasa nchini Tanzania, ikiwa ni pamoja na wajibu wa chama cha siasa kushiriki na kushindana katika uchaguzi ili kuunda serikali. Sheria hii pia inakitaka chama cha siasa kuweka au kuunga mkono wagombea wakati wa uchaguzi. Ofisi ya msajili wa vyama vya siasa ndiyo yenye jukumu la kusimamia shughuli zote za vyama vya siasa nchini na pia ni mlezi wa vyama hivyo na demokrasia kwa ujumla nchini Tanzania.

### *3.2.6 Katiba ya Zanzibar*

Michakato ya uchaguzi Zanzibar inaendeshwa chini ya katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984. Katiba hii inatoa haki kwa raia kushiriki katika uchaguzi kwa kuzingatia sheria mbalimbali zinazohusu uchaguzi Zanzibar. Ibara ya 7(1) ya katiba hii inatoa haki kwa raia kupiga kura. Katika kueleza haki hii katiba inasema “Mzanzibari yeyote mwenye umri wa miaka 18 na kuendelea ana haki ya kupiga kura katika uchaguzi unaofanyika Zanzibar na haki hii itatimizwa kwa kuzingatia sheria zingine zenye vipengele vinavyozuia mzanzibari kutimiza haki yake ya kupiga kura”. Katiba hii pia inatoa mamlaka kwa baraza la wawakilishi kutunga sheria inayohusu ushiriki wa wananchi katika uchaguzi wa rais wa Zanzibar, wajumbe wa baraza la wawakilishi au madiwani kwa upande wa serikali za mitaa. Katiba hii vile vile inatoa mwongozo wa michakato ya kusajili wapigakura na kuweka mipaka ya majimbo ya uchaguzi.

Katiba hii pia inaeleza uundwaji wa tume ya uchaguzi ya Zanzibar na inabainisha uhuru wa tume wa kufanya maamuzi kwakuwa hakuna mahakama yoyote yenye mamlaka ya kuhoji jambo lolote linalohusu utendajikazi wa tume ya uchaguzi ya Zanzibar. Pia, katiba hii inatoa mwanya kwa tume ya uchaguzi ya Zanzibar kuwa shirikishi kwa kuwa inataka kiongozi wa

shughuli za serikali bungeni na kiongozi wa upinzani bungeni kuteua wajumbe wawili watakaoidhinishwa na rais wa Zanzibar kuwa wajumbe wa tume. Katika kutekeleza majukumu yake, tume ya uchaguzi Zanzibar pia inatakiwa kuwasiliana na tume ya uchaguzi ya jamhuri ya muungano wa Tanzania. Kwa ujumla, katiba ya Zanzibar inazingatia vigezo vya sheria inayoruhusu ufanyikaji wa uchaguzi unaoaminiwa, huru na wa haki.




*Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984*

3.2.7 Sheria ya Uchaguzi Zanzibar

Uchaguzi Zanzibar unafanya kwa mujibu wa sheria ya uchaguzi ya Zanzibar namba 11 ya mwaka 1984. Sheria hii inaorodhesha taratibu na usimamizi wa uchaguzi, ikiwa ni pamoja na uanzishaji wa tume ya uchaguzi Zanzibar, muundo wake na mamlaka yake. Sheria pia inabainisha vigezo vya mtu kuwa mpigakura au kukosa sifa ya kupiga kura; utaratibu wa kukata rufaa na utaratibu wa kuchagua rais na wajumbe wa baraza wa wawakilishi. Sheria pia inabainisha mambo yanayoruhusiwa na yasiyoruhusiwa wakati wa kampeni, kupiga kura na wakati wa kutangaza matokeo. Sheria pia inabainisha makosa yanayohusiana na michakato ya uchaguzi na mapingamizi yanayoweza kushughulikiwa na mahakama. Tofauti na mfumo wa kisheria kwa uchaguzi wa Jamhuri ya Muungano, Sheria ya uchaguzi ya Zanzibar pia inatoa mwongozo wa uchaguzi wa serikali za mitaa.

Japokuwa sheria hii kwa ujumla wake haimzuii raia kushiriki katika uchaguzi, sheria ya ukaazi ya Zanzibar, namba 7 ya mwaka 2005 inawanyima baadhi ya wazanzibari haki yao ya kushiriki katika uchaguzi. Kifungu namba 12 (3) (iia) kinaeleza kwamba " mtu atatambuliwa kuwa mkaazi wa jimbo husika ikiwa ana makazi ya kudumu na amekuwa akiishi katika jimbo husika kwa kipindi cha miezi 36 mfululizo toka kuanza kutumika kwa sheria hii hadi siku ya uchaguzi". Kwa kiasi fulani, kigezo hiki kinawanyima baadhi ya watu haki na uhuru wa kutimiza haki yao ya kiraia na kisiasa.

### *3.2.7 Athari za Mfumo wa Kisheria katika Uchaguzi wa Mwaka 2015*

Kwa ujumla, sheria zilisosimamia uchaguzi wa mwaka 2015 zilizingatia vigezo na viwango vya kimataifa vinavyohusu uchaguzi wa kuaminika, huru na wa haki. Uchambuzi wa sheria hizi hauonyeshi kwamba zinajikanganya, au kwamba zinakosa vigezo vya kutosha vya kuhakikisha kwamba raia wanatimiza haki zao za kiraia na kisiasa. Sheria hizi zilitumika kwa usawa nchi nzima na hazikutumiwa kinyume na ilivyokusudiwa. Pamoja na mapungufu kadhaa yaliyobainishwa awali, sheria hizi zilizingatia matakwa ya sheria za kimataifa za haki za binadamu. Pia hakukuwa na ushahidi wowote wa mikinzano ya sheria za uchaguzi. Waangalizi wa uchaguzi kutoka TEMCO hawakuweza kubaini matukio yaliyohusu utekelezaji wa sheria kwa misingi ya ushabiki wa vyama au ukiukwaji wa haki ambayo yangeweza kuathiri hadhi ya michakato ya uchaguzi. Aidha, kanuni na taratibu ndogo ndogo hazikukinzana na malengo ya sheria za uchaguzi. Kwa kuzingatia yaliyojitokeza wakati wa uchaguzi, haishangazi kuona kwamba hakuna mdau mkuu wa uchaguzi aliyejitokeza kupinga sheria hizi mahakamani, au kususia uchaguzi kwa kigezo cha kupinga sheria mbovu.

Pamoja na ukweli huu, uchambuzi wa TEMCO unabainisha kuwa baadhi ya vifungu vya sheria havikuungwa mkono na wadau wakuu wa uchaguzi mwaka 2015. Minong’ono ya baadhi ya wadau hawa ilihusu mambo mbalimbali yatokanayo na katiba na sheria za uchaguzi. Kuhusiana na uchaguzi, kama ilivyokuwa katika chaguzi zilizopita, hakukuwa na marekebisho ya sheria kuruhusu vyama kuunda mseto au ushirika kwa lengo la kuimarisha nguvu yao ya ushindani katika uchaguzi wa rais, wabunge na madiwani. Pili, watanzania walienda katika uchaguzi mkuu bila ya sheria inayoruhusu mgombea binafsi katika ngazi zote. Tatu, hakukuwa na mabadiliko ya kikatiba kuruhusu watanzania waishio ughaibuni kushiriki katika uchaguzi wa mwaka 2015 wakiwa kama wagombea au wapigakura. Nne, masuala yanayohusu uhuru wa tume ya taifa ya uchaguzi hayakupatiwa ufumbuzi. Tano, haki ya mtu kupinga mahakamani kuchaguliwa kwa rais haikutolewa.


Pamoja na mapungufu ya kikatiba yaliyobainishwa awali, kulikuwa na sheria zinazohusu michakato ya uchaguzi ambazo kwa maoni ya TEMCO ziliathiri kwa kiasi fulani michakato ya uchaguzi katika misingi ya kuamininiwa, uhuru na haki. Kwanza, japokuwa sheria ya gharama za uchaguzi ya mwaka 2010 inaweka ukomo wa gharama hizi kwa wagombea na vyama vya siasa, ushahidi wa jumla ulionesha kwamba ukomo huu haukuzingatiwa wala kuheshimiwa. Hakukuwa na mikakati thabiti ya kusimamia utekelezaji wa sheria hii. Pili, mfumo wa sheria haukuweka ukomo wa muda ambao mtu anaweza kuhamia chama kingine na kuteuliwa kuwa mgombea katika uchaguzi wa urais, ubunge na udiwani. Tatu, sheria ilikuwa kimya kuhusu vyama vya siasa kuanzisha na kumiliki vikundi vyao vya ulinzi na usalama. Nne, chaguzi zinaendeshwa kwa kutumia sheria na vyombo tofauti vya kusimamia uchaguzi. Wakati uchaguzi wa rais na wabunge unafanyika chini ya sheria ya taifa ya uchaguzi ya mwaka 1985, uchaguzi wa madiwani unafanyika chini ya sheria ya uchaguzi wa serikali za mitaa ( uchaguzi ambao unafanyika sambamba na uchaguzi wa rais na wabunge) ya mwaka 1979 ambayo haipo chini ya mamlaka ya tume ya taifa ya uchaguzi. Mwisho, japokuwa sheria haiwazuii kupiga kura watuhumiwa walio rumande au wafungwa wanaotumikia adhabu ya kifungo cha chini ya miezi sita, hakukuwa na mipango ya kiutekelezaji ili kuwawezesha kutimiza haki yao ya kupiga kura katika uchaguzi wa mwaka 2015.

## 3.3 Vyombo vya Kusimamia Uchaguzi

Kuna mamlaka kuu mbili za kusimamia uchaguzi wa jamhuri ya muungano wa Tanzania na uchaguzi wa Zanzibar ambavyo ni tume ya taifa ya uchaguzi (NEC) na tume ya uchaguzi ya Zanzibar (ZEC). Ili kuweza kufanya kazi zake kwa ufanisi, mamlaka hizi zinahitaji kuwa na muundo wa kiutendaji na zana mbalimbali kama muundo wa utawala, mpango mkakati, raslimali fedha na raslimali watu na mkakati wa mawasiliano ya nje na ndani.

### *3.3.1 Tume ya Taifa ya Uchaguzi*

Usimamizi wa michakato yote ya uchaguzi mkuu katika jamhuri ya muungano wa Tanzania upo chini ya tume ya taifa ya uchaguzi ambayo ina makamishina saba wanaoteuliwa kwa mujibu wa sheria na mkurugenzi wa uchaguzi ambaye ndiye mtendaji mkuu wa tume. Tume ina watumishi wasaidizi (wa kiufundi na kiutawala) ambao wanatoka kwenye kada mbalimbali za utumishi wa umma. Watumishi hawa hawaajiriwi moja kwa moja na tume na badala yake wanaazimwa kutoka wizara na idara za serikali kuu. Tume ina idara na vitengo mbalimbali ambavyo vinafanya kazi tofauti kama inavyoonyeshwa katika mchoro wa muundo wa utawala katika Kielelezo 3-1 hapa chini.




***Kielelezo 3-1: Muundo wa Utawala wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi***

Chanzo: Tume ya Taifa ya Uchaguzi, 2015

Kama inavyoonekana katika Kielelezo 3-1, tume ya taifa ya uchaguzi ina muundo wa utawala unaoeleweka na unaoonesha vizuri mgawanyo wa majukumu muhimu ya tume. Umbo hili la muundo wa utawala lina vipengele vyote muhimu katika kuiwezesha tume kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Tume ina vitengo ambavyo ni muhimu kwa mamlaka za usimamizi wa uchaguzi ambavyo ni: ufuatiliaji na tathmini; elimu kwa mpigakura; utunzaji na usimamizi wa kumbukumbu za mpigakura na GIS.

Muundo wa utawala pia unaonesha kanda saba za uchaguzi ambazo hata hivyo hazijaelezwa kwa kina na ambazo uwepo wake unaweza kuwa wa muda mfupi, hasa tu wakati wa uchaguzi. Vile vile, huduma za technolojia ya habari na mawasiliano hazionekani kupewa kipaumbele katika muundo huu wa utawala. Muundo huu pia hauonyeshi uhusiano wa tume na serikali kuu, japokuwa bajeti ya tume inawasilishwa bungeni na ofisi ya waziri mkuu. Itakumbukwa kwamba suala la bajeti ya tume limekuwa chanzo cha minong'ono mingi hasa juu ya uhuru wa tume. Pia, japokuwa mawasiliano ni jambo muhimu katika uhai wa taasisi, kitengo cha mahusiano ya umma hakionekani katika muundo wa utawala wa tume ya taifa ya uchaguzi. Vile vile, kitengo cha uwezeshaji ambacho ni muhimu katika kuiboresha tume kuwa taasisi inayokwenda na wakati hakijajumuishwa katika muundo wa utawala.

Katika uchaguzi wa mwaka 2015, tume ya taifa ya uchaguzi ilianzisha kamati saba za dharura na kila kamati ilikuwa chini ya utazamaji wa kamishina mmoja wa tume. Kamati hizi zilikuwa shirikishi na zilijumuisha wadau mbalimbali wa uchaguzi. Kamati hizi ni (i) Kamati ya uratibu wa mamlaka za uchaguzi (ii) Kamati ya elimu kwa mpigakura na asasi zisizo za kiserikali (iii) Kamati ya habari na mawasiliano (iv) Kamati ya uhusiano wa serikali na vyama vya siasa (v) Kamati ya waangalizi wa uchaguzi na mashirika ya kimataifa (vi) kamati ya ununuzi na ugavi; na (vii) Kamati ya kuratibu uchaguzi mkuu. Waangalizi wa TEMCO hawakutathmini ufanisi wa kamati hizi kiutendaji lakini uanzishwaji wake ulisaidia kuongeza ukaribu wa tume kwa wadau mbalimbali wa uchaguzi. Kamati hizi ziliifanya tume ifikike kwa urahisi, iwe na mwingiliano wa karibu na wadau mbalimbali na pia uliiwezesha tume kukabiliana na changamoto zilizojitokeza wakati wa uchaguzi. Tume hizi ziliyafanyia kazi maoni ya wadau ili kuboresha utendaji wake. Kwa ujumla, muundo wa utawala wa tume ya taifa ya uchaguzi unakidhi vigezo vya taasisi rasmi.


#### *3.3.1.1 Manunuzi na Fedha*

Tume ya taifa ya uchaguzi ilipata fedha kwa ajili ya uchaguzi mkuu wa waka 2015 kutoka bajeti ya serikali kuu. Kwa bahati mbaya, hadi TEMCO inakamilisha kuandaa ripoti hii tume ya taifa ya uchaguzi ilikuwa haijaweka wazi makadirio ya matumizi kwa uchaguzi wa mwaka 2015 wala kiasi halisi cha fedha ambazo tume ilizipokea kutoka serikali kuu. Kwa mantiki hiyo, TEMCO haina taarifa kamili kuweza kuelezea matumizi ya fedha kwa tume ya taifa ya uchaguzi katika uchaguzi wa mwaka 2015. Hata hivyo, TEMCO inatambua kuwa utoaji wa fedha kwa ajili ya kununulia mashine na vifaa vya kuandikisha wapigakura (BVR) haukuwa katika mpangilio mzuri hivyo kusababisha ucheleweshaji katika ununuzi wa vifaa hivyo.
Ushahidi wa wazi na wakuaminika unabainisha kuwa utendaji wa vitengo vya ununuzi na ugavi, pamoja na uhasibu na fedha haukuwa wa kuridhisha. Ripoti ya mdhibiti na mkaguzi

mkuu wa serikali kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015 ilibainisha maeneo kadhaa ambayo tume ya taifa ya uchaguzi haikuzingatia taratibu za kiuhasibu na kimanunuzi. Ripoti hiyo inaonesha kwamba: (i) vifaa kadhaa vya uandikishaji wa wapigakura vyenye thamani ya Tshs 827, 046, 942/= vilinunuliwa na havikutumiwa hadi zoezi la uandikishaji wapigakura lilipohitimishwa; (ii) baaadhi ya taarifa za malipo zilikuwa hazipatikani (iii) kitabu chenye kumbukumbu ya raslimali zisizohamishika kilikuwa hakijulikani kilipo (iv) baadhi ya vifaa vilivyonunuliwa vilikuwa havipatikani kwenye bohari (v) baadhi ya vifaa vilitolewa boharini bila kibali (vi) matengenezo ya magari yalifanyika katika karakana za watu binafsi bila idhini ya wakala wa ufundi na umeme Tanzania (TEMESA) (vii)manunuzi yalifanyika bila mikataba. Vile vile, ripoti ya hivi karibuni ya wakala wa udhibiti wa manunuzi ya umma (PPRA) inabainisha ukiukwaji wa taratibu za manunuzi katika taasisi za umma, ikiwa ni pamoja na utaratibu wa kutangaza zabuni kwa ajili ya manunuzi ya mashine za kuandikisha wapigakura ( gazeti la Mwananchi, 15/05/2016).

#### *3.3.1.2 Habari na Mawasiliano*

Habari na mawasiliano ndani na nje ya taasisi ni vichocheo muhimu katika utendaji kazi wa mamlaka ya kusimamia uchaguzi. Mambo haya yanaweza kuleta ufanisi katika taasisi iwapo kuna mkakati mathubuti wa habari na mawasiliano kama mojawapo ya zana za usimamizi, pamoja na mpango mkakati. Tofauti na tume ya uchaguzi ya Zanzibar ambayo ina mpango mkakati wa kina, tume ya taifa ya uchaguzi haikuwa na mpango mkakati wowote. Wakati wa zoezi la kuandikisha wapigakura kati ya April na Julai, 2015, ubadilishanaji wa taarifa baina ya tume ya taifa ya uchaguzi na wadau wengine wa ndani na nje ya nchi ulikuwa mgumu kwa kiasi fulani mgumu. Japokuwa tume ya taifa ilikuwa na tovuti iliyosanifiwa vizuri, tovuti hiyo ilikuwa haitumiki kama chombo muhimu cha mawasiliano kwa sababu ilikosa taarifa muhimu na pia taarifa hizo zilikuwa haziboreshwi mara kwa mara na kwa wakati. Vile vile tume ilikuwa haijaandaa jukwaa madhubuti kurahisisha ufanisi wa mawasiliano.



*Mheshiniwa Jaji (Mstaafu) Damian Lubuva, Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Ndugu Ramadhan Kailima, Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi*

Hata hivyo, tume iliongeza mawasiliano na wadau wa uchaguzi baada ya zoezi la kuandikisha wapigakura ambapo mabadiliko yaliyofanywa yaliwezesha kuboresha utendaji kazi wa kitengo cha mawasiliano cha tume. Baada ya mabadiliko hayo, tume ilianza kufikika kirahisi na wadau kupitia mikutano na vyombo vya habari na mijumuiko mingine. Zana za mawasiliano za tume ziliweza kuboreshwa hasa katika maeneo yafuatayo (i)Tovuti ya tume ilihuishwa (ii) taarifa muhimu ziliweza kuwekwa kwa wakati katika tovuti hiyo (iii)ukurasa wa facebook ulifunguliwa na ulisheheni taarifa muhimu za uchaguzi. Maboresho ya mawasiliano yaliwezesha wadau wa uchaguzi, ikiwa ni pamoja na TEMCO, kuifikia tume ya taifa ya uchaguzi kwa urahisi, ikiwa ni pamoja na uongozi wa juu wa tume.

#### *3.3.1.3 Uimarishaji Uwezo wa Maafisa Uchaguzi*

Waangalizi wa uchaguzi kutoka TEMCO walibaini kuwa tume ya taifa ya uchaguzi iliajiri na kutoa mafunzo kwa maafisa uchaguzi kwa ajiri ya kusimamia uchaguzi wa mwaka 2015. Tume ilichukua hatua za kuimarisha uwezo wa watumishi wake katika ngazi za taifa, mkoa hadi jimbo. Mpango wa kuwaongezea uwezo maafisa wa uchaguzi ulitekelezwa katika awamu mbili. Awamu ya kwanza ilihusisha kutoa mafunzo kwa maafisa wa tume waliohusika katika zoezi la uandikishaji wapigakura kupitia BVR kama itakavyojadiliwa kwa kina katika sura ya nne ya ripoti hii. Awamu ya pili ilijikita katika kuwajengea uwezo maafisa wa tume walioshiriki katika michakato iliyofuata baada ya zoezi la uandikishaji wapigakura kama ilivyoelezwa katika sura ya nane na ya tisa ya ripoti hii. Taarifa za waangalizi wa TEMCO zinabainisha kwamba waratibu thelathini (30) wa uchaguzi katika ngazi ya mkoa (RECs); wasimamizi wa uchaguzi na wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi 972 (ROs na AROs) katika ngazi ya jimbo; na wasimamizi wasaidizi katika ngazi ya kata wapatao 7914 walipewa mafunzo mbalimbali kuhusu usimamizi wa uchaguzi.

#### *3.3.1.4 Utoaji wa Vibali kwa Waangalizi wa Uchaguzi na Watoaji wa Elimu kwa Mpigakura*

Tume ya taifa ya uchaguzi ina mamlaka ya kutoa vibali kwa watoaji elimu kwa mpigakura na waangalizi wa uchaguzi wa ndani na wa kimataifa. Taarifa za waangalizi wa TEMCO zinabainisha kuwa jumla ya vikundi 75 vya waangalizi wa ndani wa uchaguzi na vikundi 12 vya waangalizi wa kimataifa vilipewa vibali vya utazamaji wa uchaguzi wa mwaka 2015. Tume ya taifa ya uchaguzi iliweka kituo maalumu katika ukumbi wa mikutano wa kimataifa wa Mwalimu Nyerere kwa lengo la kutoa vibali hivi na utaratibu huu ulisaidia kuondoa mrundikano wa kazi katika makao makuu ya tume na hivyo kuwezesha mchakato wa kutoa vibali kwa waangalizi kuendeshwa bila matatizo. Pamoja na ubunifu huu, uwezo wa tume ya taifa ya uchaguzi kutoa vibali kwa waangalizi wote katika kituo kimoja ulikuwa mdogo. Kwa vyovyote vile, na kwa kuzingatia uwezo wa tume ya taifa ya uchaguzi, tume isingeweza kusajili zaidi ya waangalizi wa uchaguzi wa muda mfupi (STOs) 10,000 kupitia kituo kimoja. Vile vile, tume ya taifa ya uchaguzi ilitoa kanuni za maadili kwa waangalizi wa uchaguzi ambazo ziliandaliwa kupitia njia shirikishi iliyowajumuisha wadau mbalimbali.

Tume ya taifa ya uchaguzi pia ilisambaza sheria na kanuni muhimu za uchaguzi na kanuni za maadili kwa waangalizi wa uchaguzi, vyama vya siasa na wagombea, sare na mikoba ya

kubebea nyalaka mbalimbali kwa waangalizi wa uchaguzi. Wasimamizi wengi wa uchaguzi walitoa ushirikiano mzuri kwa waangalizi wa uchaguzi. Baadhi walitoa ushirikiano zaidi kwa kutoa barua za utambulisho na vitambulisho kwa waangalizi wa uchaguzi wa muda mfupi bila kusubiri amri kutoka makao makuu ya tume.

Pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na tume katika kutoa vibali kwa waangalizi wa uchaguzi, kulikuwa na matukio machache yaliyoashiria ukosefu wa ufanisi katika makao makuu ya tume na katika ngazi ya jimbo. Katika ngazi ya makao makuu ya tume, mpango wa tume wa kusajili na kutoa vibali kwa waangalizi wote wa muda mfupi wa uchaguzi (STOs) haukufanikiwa kwa sababu ya kukosa uwezo wa kuhimili idadi kubwa ya waangalizi hawa ambao walitakiwa kupewa vibali. Katika ngazi ya jimbo, baadhi ya wasimamizi wa uchaguzi waliweka masharti yao binafsi katika utoaji wa vibali kwa waangalizi wa uchaguzi. Kwa mfano, katika jimbo la Kibondo, msimamizi wa uchaguzi, ambaye pia ni mkurugenzi mtendaji wa halmashauri ya wilaya hakupenda TEMCO iwaajiri walimu kama waangalizi wa uchaguzi wa muda mfupi, pamoja na ukweli kwamba chama cha walimu Tanzania (CWT) ni mwanachama mwenza wa TEMCO. Mfano mwingine ni katika jimbo la Igalula ambapo msimamizi wa uchaguzi aliamuru waangalizi wote 51 wa uchaguzi wa muda mfupi wale viapo mahakamani kabla ya kuwapa vibali vya utazamaji. Vile vile katika majimbo ya Lindi, Kalambo na Karagwe wasimamizi wa uchaguzi waliweka idadi yao ya waangalizi wa uchaguzi wa muda mfupi, kinyume na idadi iliyokuwa imepangwa na TEMCO. Katika jimbo la Mbulu mjini, msimamizi wa uchaguzi alidai kwamba majina yote yaliyowasilishwa ofisini kwake kwa ajili ya kuombewa vibali vya utazamaji wa muda mfupi yalikuwa ni ya mashabiki wa CHADEMA na UKAWA. Kutokana na mifano hii, ni wazi kwamba baadhi ya wasimamizi wa uchaguzi hawakuelewa majukumu yao kuhusiana na utoaji vibali kwa waangalizi wa uchaguzi wa muda mfupi.


Kuhusu utoaji elimu kwa mpigakura, TEMCO ilibaini kwamba jumla ya asasi sa kiraia 451 ziliomba kupewa vibali vya utoaji elimu hii wakati wa zoezi la uandikishwaji wa wapigakura ambapo asasi 447 zilipewa vibali. Tume ya taifa ya uchaguzi pia ilitoa vibali kwa waangalizi wote wa ndani na wa kimataifa ambao walitimiza vigezo na masharti yaliyowekwa na tume. Waangalizi wa uchaguzi kutoka TEMCO hawakupata taarifa ya kikundi chochote cha utazamaji kunyimwa kibali au kunyang'anywa kibali cha utazamaji.

### *3.3.2 Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar*

Usimamizi wa michakato yote ya uchaguzi Zanzibar uko chini ya tume ya uchaguzi ya Zanzibar iliyoanzishwa mwaka 1997 na ambayo tangu kuanzishwa kwake imesimimia chaguzi kuu nne zilizopita, uchaguzi kadhaa wa marudio na kura ya maoni. Tume hii ina makamishina saba walioteuliwa kwa mujibu wa sheria na pia kuna mkurugenzi wa uchaguzi ambaye ni afisa mtendaji mkuu wa tume. Tofauti na tume ya taifa ya uchaguzi, tume ya uchaguzi ya Zanzibar ina watumishi (wa kiufundi na utawala) iliyowaajiri yenyewe. Tume ina vitengo vitano, ikiwa ni pamoja na ofisi ndogo ya Pemba, ambazo zinatekeleza majukumu mbalimbali kama ilivyooneshwa katika muundo wa utawala katika Kielelezo 3-2.



*Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar Akipokea Fomu za Uteuzi kutoka kwa Mgombea Uraisi wa Zanzibar Kupitia CUF*




***Kielelezo 3-2: Muundo wa Utawala wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar***

Chanzo: Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, 2015-2019 Mpango Mkakati

Kama inavyoonekana katika muundo wa utawala, tume ya uchaguzi Zanzibar ina muundo kamili wa kiutawala unaoiwezesha tume kutekeleza majukumu yake bila matatizo. Vile vile,

tume ya uchaguzi Zanzibar ina mpango mkakati 2015-2019 unaobainisha mikakati mikuu ya kiutendaji, ikiwa ni pamoja na kushirikiana na wadau muhimu wa uchaguzi, mifumo ya kisheria, uimarishaji wa mamlaka ya utendaji kazi, utatuzi wa migogoro ya uchaguzi, elimu kwa mpigakura, utengaji mipaka ya majimbo ya uchaguzi na uboreshaji kitaasisi na kitaaluma. Tume ya taifa ya uchaguzi ina dira na mwelekeo na kanuni zinazoiongoza katika kutekeleza majukumu yake. Muhimu zaidi ni kwamba tume ya uchaguzi ya Zanzibar inatekeleza majukumu yake kwa mujimu wa mpango kazi wake unaosimamiwa na kamati ambayo iko chini ya mwenyekiti wa tume, mkurugenzi wa uchaguzi, mshauri wa kisheria na wakuu wa vitengo.

**3.4 Uhuru wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar**

Mamlaka ya kusimamia uchaguzi inaweza kuwa huru ikiwa itatimiza vigezo vifuatavyo: (i) uwepo wake uwe ni kwa mujibu wa sheria za nchi; (ii) wajumbe wake wanatakiwa kuteuliwa kupitia mfumo ambao ni wazi na wenye ushindani; (iii) tume inatakiwa kuwa na mamlaka ya kuajiri na kuwawajibisha watumishi wake; (iv) tume inatakiwa kuwa na uhuru wa kutumia bajeti yake kama ilivyoidhinishwa na bunge.

Uchambuzi wa kina unabainisha kuwa tume hizi mbili za uchaguzi zipo kwa mujibu wa katiba na zina mamlaka ya kutumia bajeti zake kama zilivyoidhinishwa na bunge. Hata hivyo, tume hizi hazina mamlaka kamili kwa watumishi wake na pia makamishina wa tume hizi hawapatikani kwa njia za uwazi na zenye ushindani. Kutokana na ukweli huu, kumekuwa na manung'uniko kutoka kwa wadau wa uchaguzi kwamba tume hizi hazikidhi vigezo vya kuitwa tume huru za uchaguzi kulingana na viwango vya kimataifa.




*Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar Mh. Jecha Salim Jecha, Makamishina na Mkurugenzi wa Uchaguzi*

**3.5 Uhusiano kati ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar**

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na katiba ya Zanzibar zinazitaka tume ya Taifa ya Uchaguzi na tume ya uchaguzi ya Zanzibar kuwasiliana mara kwa mara hasa katika mambo

yanayohusiana na usimamizi wa uchaguzi nchini Tanzania kama vile uwekaji mipaka ya majimbo ya uchaguzi, usajili wa wapigakura na siku ya kupiga kura. Katika uchaguzi wa mwaka 2015 kulikuwa na manung'uniko kutoka kwa wadau wa uchaguzi juu ya kukosekana kwa mawasaliano ya kuridhisha baina ya tume hizi. Kulikuwa na hisia za kuweko kwa hali ya kutokukubaliana baina ya tume hizi hasa kuhusiana na idadi ya majimbo ya uchaguzi Zanzibar.



*Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi Mh Lubuva na Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar Mh. Jecha Wakiwa Pamoja na Mkurugenzi wa Uchaguzi Bw Kailima na Msajili wa Vyama vya Siasa Mh. Mutungi*

Kwa mara ya kwanza idadi ya majimbo kwa uchaguzi wa Zanzibar na Uchaguzi wa Jamhuri ya muungano ilitofautiana. Wakati tume ya uchaguzi ya Zanzibar ilipopitia mipaka ya majimbo ya uchaguzi na kuongeza majimbo manne mapya Unguja kwa uchaguzi wa Zanzibar, tume ya taifa ya uchaguzi iliendelea na idadi yake ya majimbo 50 ya Zanzibar kwa uchaguzi wa jamhuri ya muungano. Pamoja na tofauti hizi za kitakwimu, taarifa za waangalizi wa uchaguzi kutoka TEMCO zinaonesha kwamba ushirikiano baina ya tume hizi mbili katika kipindi chote cha uchaguzi wa mwaka 2015 ulikuwa ni mzuri na ulikuwa kwa mujibu wa katiba.

### 3.6 Uwekaji wa Mipaka ya Majimbo ya Uchaguzi

Uwekaji wa mipaka ni mchakato wa kubainisha mipaka ya majimbo ya uchaguzi na kata. Ni njia muhimu ya kuhakikisha uwakilishi wenye tija unazingatiwa. Ni jambo muhimu ambalo kama halitekelezwi kwa uangalifu linaweza kusababisha migogoro ya uchaguzi. Kutokana na umuhimu huo, ushirikishwaji wa wadau wa uchaguzi katika uwekaji mipaka unahitajika ili kuwezesha kufanyika kwa uchaguzi wa kuaminiwa, huru na wa haki. Katika uchaguzi wa mwaka 2015 kulikuwa na uanzishwaji wa majimbo mapya na kata. Waangalizi wa uchaguzi kutoka TEMCO walitakiwa kubainisha kama uwekaji mipaka ulizingatia vigezo vilivyowekwa kwa mujibu wa sheria. Taarifa za waangalizi wa uchaguzi kutoka TEMCO juu ya suala hili zinaonyeshwa katika Jedwali 3-1.

*Jedwali 3-1: Vigezo vya Uwekaji Mipaka ya Majimbo ya Uchaguzi*

| Vigezo | Ndiyo | | Hapana | | Haihusiki | | Hakuna majibu | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | F | % | F | % | F | % | F | % | F | % |
| Idadi ya watu | 38 | 25.3 | 11 | 7.3 | 98 | 65.3 | 3 | 2.0 | 150 | 100.0 |
| Ongezeko la wilaya mpya | 10 | 6.7 | 31 | 20.7 | 98 | 65.3 | 11 | 7.3 | 150 | 100.0 |
| Ongezeko la halmashauri mpya | 16 | 10.7 | 21 | 14.0 | 98 | 65.3 | 15 | 10.0 | 150 | 100.0 |
| Hali ya kijiografia | 34 | 22.7 | 9 | 6.0 | 98 | 65.3 | 9 | 6.0 | 150 | 100.0 |
| Hali ya kiuchumi ya jimbo | 17 | 11.3 | 22 | 14.7 | 98 | 65.3 | 13 | 8.7 | 150 | 100.0 |
| Mipaka ya kiutawala | 25 | 16.7 | 12 | 8.0 | 98 | 65.3 | 15 | 10.0 | 150 | 100.0 |
| Mwenendo wa makazi ya watu | 18 | 12.0 | 20 | 13.3 | 98 | 65.3 | 14 | 9.3 | 150 | 100.0 |
| Uwezo wa ukumbi wa bunge | 4 | 2.7 | 31 | 20.7 | 98 | 65.3 | 17 | 11.3 | 150 | 100.0 |
| Viti maalum kwa wanawake | 2 | 1.3 | 29 | 19.3 | 98 | 65.3 | 21 | 14.0 | 150 | 100.0 |
| Vigezo vingine | 1 | 0.7 | 26 | 17.3 | 98 | 65.3 | 25 | 16.7 | 150 | 100.0 |

Chanzo: Taarifa za Waangalizi wa Uchaguzi kutoka TEMCO, 2015

Kama taarifa zinavyoonesha katika Jedwali namba 3.1, kwa kiwango fulani, vigezo mahususi vilitumika katika kuweka mipaka ya majimbo ya uchaguzi. Kwa ujumla, hakukuwa na migogoro iliyotokana na mitazamo ya uwekaji mipaka ya majimbo kwa misingi ya matakwa ya kisiasa au upendeleo. Vile vile, taarifa za waangalizi wa uchaguzi kutoka TEMCO zinabainisha kwamba asilimia 18% ya wapigakura kwenye maeneo ambapo mapitio ya mipaka yalifanyika walipewa fursa kuwasilisha maoni yao kwa mamlaka husika kuhusu mchakato huo kama inavyoonesha kwenye Jedwali 3-2

*Jedwali 3-2: Uwasilishaji wa maoni juu wa uwekaji mipaka ya majimbo ya uchaguzi*

| Jibu | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|
| Ndiyo | 27 | 18.0 |
| Hapana | 12 | 8.0 |
| Haihusiki | 98 | 65.3 |
| Hakuna majibu | 13 | 8.7 |
| Jumla | 150 | 100.0 |

Chanzo: Taarifa za Waangalizi wa Uchaguzi kutoka TEMCO, 2015

Kama taarifa zinavyoonesha katika Jedwali 3-2, kulikuwa na matukio ambapo wapigakura walinyimwa fursa ya kuwasilisha maoni yao juu ya uwekaji mipaka ya majimbo ya uchaguzi. Hata hivyo, waangalizi wa uchaguzi kutoka TEMCO hawakubainisha tukio ambapo chama cha siasa au mgombea alipinga mahakamani uwekaji wa mipaka ya majimbo ya uchaguzi. Kwa kuhitimisha, ni wazi kwamba zoezi la uwekaji mipaka ya majimbo ya uchaguzi lilifanywa kwa mujibu wa sheria na liliridhiwa na wadau wengi wa uchaguzi.

### 3.7 Kulinda Kura na Shauri la "Mita 200"

Mojawapo ya mambo yaliyovuta hisia za watu wakati wa uchaguzi wa mwaka 2015 ni mwongozo wa CHADEMA kwa wanachama na wafuasi wake wa kuwataka kulinda kura zao siku ya kupiga kura. Hoja ya kulinda kura iliongezwa nguvu na mgombea wake wa urais, Bw

Edward Lowassa aliyedai kwamba CCM ina tabia ya kuiba kura. Kwa nyakati tofauti, Lowassa aliwahimiza wafuasi wake kujitokeza kwa wingi kupiga kura ili kwamba hata CCM wakiiba bado CHADEMA waendelee kuwa washindi. Tume ya taifa ya uchaguzi iliweka wazi kwamba mikusanyiko yoyote kwa lengo la kulinda kura ilikuwa ni kinyume cha sheria kwakuwa kila chama kilikuwa na mawakala katika vituo vya kupigia na kuhesabia kura ambao mojawapo ya majukumu yao ni kulinda maslahi ya vyama vyao. Kutokana na sintofahamu hii, CHADEMA walipeleka shauri mahakamani wakipinga tangazo la mwenyekiti wa tume ya Taifa ya Uchaguzi. Waliiomba mahakama kutoa tafsiri sahihi ya kifungu 104 (1) cha sheria ya uchaguzi kinachosema:

> “ Hakuna mtu atakayeitisha mkutano siku ya uchaguzi au katika majengo yanayotumika katika zoezi la kupiga kura, au eneo lolote lililoko katika umbali wa mita mia mbili, kuvaa au kuonesha kadi, picha, au nembo inayoashiria kuunga mkono au kupendelea mgombea yeyote siku ya uchaguzi”.

Hukumu ya shauri hili ilitolewa siku ya ijumaa tarehe 23 Oktoba 2015, siku mbili kabla ya siku ya uchaguzi na ilikazia msimamo wa tume ya taifa ya uchaguzi kwa kusistiza kwamba sheria inazuia kufanya kampeni siku ya uchaguzi bila kujali umbali kutoka kituo cha kupigia kura. Kwa hiyo mahakama ilizuia mikusanyiko karibu na vituo vya kupigia kura na iliwataka watu kupiga kura na kuondoka. Taarifa za waangalizi wa uchaguzi kutoka TEMCO zinaonesha kwamba watu waliheshimu uamuzi huu, japokuwa maafisa wa polisi walionekana kuwa tayari kukabiliana na mikusanyiko yoyote karibu na vituo vya kupigia kura iwapo ingejitokeza.

## 3.8 Hitimisho na Mapendekezo

### *3.8.1 Hitimisho*

Uchambuzi wa mifumo ya kisheria na kitaasisi kwa uchaguzi wa mwaka 2015 umebainisha mafanikio na mapungufu kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya uchaguzi umaoaminika, huru na wa haki. Hata hivyo, kwa ujumla mapungufu yaliyobainishwa hayakusababisha matatizo makubwa ambayo yangeweza kuathiri kufanyika kwa uchaguzi wa kuaminika, huru na wa haki. Pamoja na mazuri ya mfumo wa kisheria katika mambo kadhaa, umuhimu wa maboresho ya kisheria haukwepeki ikiwa Tanzania inahitaji kukidhi viwango vya kimataifa vya uchaguzi huru na wa haki.

### *3.8.2 Mapendekezo*

TEMCO inapendekeza kwamba wadau wa uchaguzi Tanzania wachukue hatua kutatua mapungufu kadhaa katika mifumo ya kisheria na kitaasisi inayosimamia michakato ya uchaguzi. Maboresho ya kisheria na kitaasisi yanahitajika ili:

(i) Kuifanya serikali ifikirie kutunga sheria itakayowezesha uanzishwaji wa chombo huru cha kufuatilia kampeni na matumizi ya fedha katika shughuli za kisiasa hasa wakati wa uchaguzi

(ii) Vyama vya siasa viwe huru katika kutengeneza miseto na ushirika kwa lengo la kuongeza nguvu ya ushindani

(iii) Kuruhusu mgombea binafsi katika uchaguzi wa rais, wabunge na madiwani

(iv) Kuwezesha watanzania waishio Ughaibuni kushiriki katika michakato ya uchaguzi

(v) Kuimarisha uhuru wa tume za uchaguzi

(vi) Kuimarisha utelekezaji na utii wa sheria ya gharama za uchaguzi

(vii) Kuweka ukomo wa muda kwa mwanachama wa chama cha siasa kuhama chama na kusimama kama mgombea katika uchaguzi wa rais, wabunge na madiwani

(viii) Kudhibiti vikundi vya ulinzi na usalama vinavyoanzishwa na kumilikiwa na vyama vya siasa

(ix) Kuwa na mfumo mmoja wa kisheria wa kusimamia uchaguzi, ikiwa ni pamoja na kuipa mamlaka tume ya Taifa ya uchaguzi kusimamia uchaguzi wa serikali za mitaa; na

(x) Kuweka utaratibu wa kiutekelezaji utakaowawezesha mahabusu na wafungwa wanaotumikia adhabu ya kifungo kisichozidi miezi sita kutimiza haki yao ya kupiga kura.

# CHAPTER 4
# UANDIKISHAJI WA WAPIGAKURA

## 4.1 Utangulizi

Kwa mara ya kwanza teknolojia ya kielektroniki ya kuandikisha wapigakura ijulikanayo kama *Biometric Voter Registration* ilitumika kuandikisha wapigakura katika Daftari la Kudumu la Wapigakura. Matumizi ya vitambulisho vya kupigia kura vilivyotolewa tangu mwaka 2004 kwa kutumia teknolojia ya utambuzi wa alama yaani, *Optical Mark Recognition* yalisitishwa. Kimsingi uandikishaji huu wa wapigakura kwa kutumia mfumo wa kieletroniki ulihusisha wapigakura waliokwisha kujiandikisha kabla na wale wapya. Sura hii inatathmini zoezi la uandikishaji wa wapigakura kwa kutumia mfumo wa kielektroniki. Sura imegawanyika katika sehemu tisa, ikianza na utangulizi. Sehemu ya pili inaangazia sababu za kuanzishwa kwa mfumo huu wakati sehemu ya tatu inachunguza mifumo ya kisheria na kitaasisi iliyoongoza mchakato wa BVR. Sehemu ya nne inaangalia menejimenti ya zoezi la uandikishaji wa wapigakura ikifuatiwa na elimu ya mpigakura katika sehemu ya tano. Ukiukwaji wa sheria, kanuni na taratibu na namna ulivyoshughulikiwa ni mada ya sehemu ya sita. Sehemu ya saba imejikita katika idadi ya wapigakura waliojiandikisha ikilinganishwa na makisio ya Tume. Tathmini ya jumla ya mchakato wa uandikishaji wa wapigakura ni mada ya sehemu ya nane. Sehemu ya tisa na ya mwisho ni hitimisho na mapendekezo.

## 4.2 Uhalali wa Kuanzishwa kwa Teknolojia ya BVR

Kadri uchaguzi wa mwaka 2015 ulivyozidi kusogea ndivyo ambavyo Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) iliendelea kukosolewa na wadau wa uchaguzi kwa kushindwa kuboresha daftari la kudumu la wapigakura kwa mujibu wa sheria tangu kumalizika kwa uchaguzi wa mwaka 2010. Uboreshaji wa mwisho wa daftari la kudumu ulifanyika mwaka 2008 ambapo wapigakura wapya milioni mbili waliandikishwa.

NEC ilijitetea kuwa ucheleweshaji wa pesa kutoka serikalini ndiyo ilikuwa sababu ya kushindwa kuandikisha wapigakura. Katikati ya sintofahamu hii wadau wengi walishangaa kusikia kuwa NEC iliamua kutumia teknolojia ya BVR kuandikisha wapigakura. Wadau wengi walidhani tangazo la NEC halikuzingatia uhalisia ikichukuliwa kuwa mwaka ulikuwa umezongwa na mambo mengi, ikiwemo machakato wa upatikanaji wa katiba mpya pamoja na kura ya maoni ya kupitisha Katiba Inayopendekezwa iliyokuwa imepangwa kufanyika mwezi Aprili 2015. Wasiwasi ulikuwa juu ya upatikanaji wa fedha kutoka serikalini na muda mfupi uliokuwa umebaki kabla ya uchaguzi wa 2015.

BVR ni "mfumo unaojiendesha wa kuchukua alama za vidole, uso na sainii ya dijitali kwa kutumia skana za kompyuta kuchukua habari za kibaolojia za mwombaji".[1] Ingawa teknolojia ya OMR ilikuwa bora zaidi kuliko uandikishaji wa mkono uliotumika kwa uchaguzi wa mwaka 1995 na 2000, bado haukuwa wa kidijitali kikamilifu. Picha zilichukuliwa kwa kutumia kamera za *Polaroid* na kisha kubandikwa katika kitambulisho. Mpigakura pia alitakiwa kuweka sahihi katika kadi. Maelezo mengine ya mpigakura yalichukuliwa kwa kutumia fomu maalum na

[1] Mwighusa, Dennis M (2015) "Transforming Voter Registration Paradigm in Tanzania: From OMR to BVR"; International Journal of Science and Research, Vol. 4 Issue 8, pp 1064-1068. Emphasis added.

kisha kutambazwa (scan) na kuhifadhiwa kielektroniki mwishoni mwa zoezi la uandikishaji. Mfumo huu haukujengewa uwezo wa utambuzi wa urahisi wa uandikishaji zaidi ya mara moja. Tofauti na OMR, mfumo wa BVR ni wa kidijitali kikamilifu na kwa kila kipengele kuanzia sahihi, picha na alama za vidole. Hivyo NEC ilihalalisha utumiaji wa BVR kwa kuzingatia ubora wake kiteknolojia, ikiwemo: (i) kuongezeka kwa tija na uwazi katika uandikishaji; (ii) kuongezeka kwa kasi na uhakika wa kutambua wapigakura; (iii) uwezo mkubwa wa kuwatambua wapigakura waliojiandikisha zaidi ya mara moja kwa urahisi; (iv) urahisi wa kuandaa, kurekebisha na kuboresha daftari la kudumu la wapigakura; (v) upunguzaji wa uwezekano wa vitendo vya kihalifu kwenye uchaguzi; (vi) usahihi wa data kwa kuchukua alama na taarifa na uwezekano wa mpigakura kuzihakiki kabla ya kuzihifadhi; na (vii) urahisi wa kuunda *dataset* kwa wepesi wa uhakiki wa taarifa.




*Uandikishaji wa Wapigakura kwa Teknolojia ya BVR Ukiendelea katika Moja ya Vituo vya Uandikishaji*

Pamoja na maelezo ya kina yaliyotolewa na NEC, bado wasiwasi wa wadau kuhusu uwezekano wa kuwa na daftari la kudumu na kuendesha kura ya maoni tarehe 30 Aprili 2015 na uchaguzi ulibakia. Mashaka haya yalitokana na sababu kadhaa zikiwemo: (i) muda mrefu ulitakiwa kwa ajili ya kumpata mzabuni wa kuleta mashine za BVR, mchakato wa ununuzi, majaribio na kisha kuanza rasmi kwa uandikishaji; (ii) nchi haikuwa na mfumo ya kuwezesha utekelezaji wa BVR: umeme wa uhakika, vifaa vya kuhifadhia taarifa n.k.; (iii) NEC haikuwa imejiandaa kikamilifu kushughulikia changamoto za kiteknolojia na kilojistiki ambazo zilijitokeza katika nchi nyingine za Kiafrika zilizoamua kutumia teknolojia ya BVR; (iv) BVR ilikuwa ghali sana na NEC ingeweza kushirikiana na Mamlaka ya Utambulisho ya Taifa (NIDA) ambayo ilikuwa pia ikitoa vitambulisho vya taifa. Inakadiriwa kuwa NEC ilitumia takriban shilingi bilioni 180 kuandikisha wapigakura takriban milioni 20 wakati NIDA ilitumia takribani kiasi hicho hicho cha pesa kuandikisha watu milioni 2.5.[2]; (v) BVR isingeweza kuwazuia viongozi wenye nia ovu kuvuruga uchaguzi.

[2]Mwandishi Wetu (2016) "Siri waliotumbuliwa NIDA yaanikwa"; *Mwananchi* Newspaper, 27/1/2016. See also Lyimo, Karl (2014) "Biometric Voter Registration vis-à-vis national ID card: Who is right?, Business Times, 1/8/2014

### 4.3 Mifumo ya Kitaasisi na Kisheria iliyoongoza Uandikishaji wa Wapigakura

Katika muktadha wa kisheria, uandikishaji wa wapigakura unaweza kupatikana katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hasa Ibara ya tano ikisomwa pamoja na Sheria na kanuni mbalimbali za uchaguzi. Ibara ya tano inatoa haki ya kupiga kura kwa kila Mtanzania mwenye umri wa miaka 18. Ibara ya 5 (2) inabainisha sababu zinazoweza kumzuia mtu kupiga kura: (a) kuwa na uraia wa nchi nyingine; (b) kuwa na ugonjwa wa akili; (c) kutiwa hatiani kwa makosa fulani ya jinai; na (d) kukosa au kushindwa kuthibitisha au kutoa kitambulisho cha umri, uraia au uandikishwaji kama mpigakura. Kwa kuzingatia kipengele (d), tofauti na nchi chache kama Switzerland, ingawa ni kigezo cha lazima cha kupiga kura, kujiandikisha inabaki kuwa ni hiari ya mpigakura na kutojiandikisha sio kosa la jinai.

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaipa Tume ya Uchaguzi mamlaka ya kusimamia zoezi la uandikishaji wa wapigakura. Katiba na sheria ya uchaguzi zimefanyiwa marekebisho kadhaa. Itakumbukwa kuwa uandikishaji wa mkono ulitumika mwaka 1995 na 2000. Baada ya wadau kueleza kutoridhishwa kwao na utaratibu huu, na kwa kuzingatia matakwa ya *Muafaka wa Kwanza wa mwaka* 1999, Katiba na sheria ya uchaguzi vilibadilishwa ili kutoa mwanya kwa kuanzishwa kwa Daftari la Kudumu la Wapigakura (Permanent National Voter Register-PNVR).[3] Hata hivyo PNVR ilianzishwa mwaka 2004 kwa kutumia teknolojia ya OMR na ikaanza kutumika rasmi katika uchaguzi wa 2005 na 2010.



*Mwangalizi wa muda mrefu wa TEMCO Long term akiangalia mchakato wa uandikishaji wapiga kura kwa kutumia mfumo wa BVR*

Katika kutazama mchakato wa BVR, TEMCO ilitaka kutathmini kama, kwa ujumla, mifumo ya kisheria na kitaasisi iliyoongoza uandikishaji ilikuwa ya haki na iliendana na vigezo vya kimataifa na desturi za uchaguzi unaoheshimika, huru na wa haki. Ingawa kwa ujumla sheria na mifumo ya kitaasisi inaonekana kukidhi matakwa, sheria haitoi fursa kwa Watanzania waishio nje ya nchi kujiandikisha. Pia, katika uhalisia, wafungwa wanaotumikia adhabu

[3] TEMCO (2005) Preparation of a Permanent Voters' Register for Tanzania Mainland, Dar es Salaam, TEMCO


zisizozidi miezi sita hawapewi fursa ya kujiandikisha. Hisia za NEC kutokuwa huru nazo ziliendelea kutawala mijadala kuhusu msimamo wa kisheria wa asasi za kusimamia chaguzi Tanzania na kupata nguvu.

### 4.4 Menejimenti ya Mchakato wa BVR

Uandikishaji wa wapigakura, kama ilivyo kwa michakato mingine katika mzunguko wa uchaguzi (electoral cycle), unahitaji umakini mkubwa katika upangaji wa lojistiki, wafanyakazi wa kutosha na wenye uwezo, pamoja na fedha za kutosha kununua bidhaa na huduma. Uamuzi wa NEC wa kuhamia katika teknolojia ya BVR ulifanya mambo haya kuwa na umuhimu wa kipekee. Kwa kuanzia, NEC ilibidi ibainishe teknolojia mujarabu kwa mazingira ya Tanzania, itangaze tenda kwa ajili ya ununzi wa vifaa, ifanye majaribio ya mashine za BVR na ihakikishe malipo yanafanywa kwa muda ili zipatikane mashine kwa idadi ya kutosha kwa wakati.

#### *4.4.1 Rasilimali Watu*

Mchakato wa BVR ulisimamiwa katika ngazi mbalimbali na kuhusisha maafisa wa ngazi mbalimbali na wenye majukumu tofauti. Katika ngazi ya mkoa, Mratibu wa Uchaguzi wa Mkoa (Regional Elections Coordinator) alikuwa na jukumu la kuhakikisha uandikishaji unakwenda kama ulivyopangwa. Wakurugenzi wa majiji, manispaa, miji na wilaya walihudumu kama Wasimamizi wa Uchaguzi (Returning Officers) katika maeneo yao. Wasimamizi hawa wa uchaguzi waliteuliwa na NEC kwa mujibu wa vifungu cha 7A (1) na 8 (1 na 2) vya Sheria Na. 13 ya 2004 na Na. 8 ya 1995, kutokana na nafasi zao. Katika ngazi ya kata, Maafisa Watendaji wa Kata waliteuliwa kuwa Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi (Assistant Registration Officers), wakiwasaidia wasimamizi wa uchaguzi katika maeneo yao ya kazi. Katika ngazi ya kituo cha kuandikisha wapigakura, afisa mwandikishaji na karani wa uandikishaji ndio walikuwa na jukumu la kuandikisha wapigakura na walikuwa wasimamizi wakuu wa kituo cha kujiandikishia. Wataalamu wa TEHAMA waliajiriwa ili kuzifanyia ukarabati mashine za BVR. Katika majimbo mengi ripoti za waangalizi wa TEMCO zinaonesha upungufu wa wataalam wa TEHAMA. Ripoti zinaonesha kuwa kila kata ilipewa mtaalam mmoja wa TEHAMA na ilipotokea mashine nyingi kuharibika kwa wakati mmoja ilichukua muda mrefu kwa mtaalam huyu kuvifikia vituo vyote.




***Kielelezo 4-1: Utoshelevu wa vifaa vya kufundishia***

*Chanzo: Ripoti za Waangalizi wa Uchaguzi wa TEMCO, 2015*

TEMCO ilitathmini utoshelevu wa vifaa vya kufundishia na matokeo yake yanaoneshwa kwenye Kielelezo 4-1. Kwa ujumla, asilimia 78 ya wahojiwa walikiri kuwa vifaa vya kufundishia vilikuwa vya kutosha.

Mbali na sifa za elimu na weledi, maafisa uchaguzi wote walitakiwa kuwa waadilifu, wenye heshima, wajiamini na wasiwe na upendeleo. Walitakiwa pia kuwa wakazi wa majimbo husika. Kazi ya kuajiri ilifanywa na afisa uandikishaji na kisha mkataba ulisainiwa kuonesha kuwa wahusika walikuwa watumishi wa Tume kwa kipindi chote cha uandikishaji wa wapigakura. Waandishi wasaidizi walipewa mafunzo ya siku mbili. Mafunzo yalijikita katika maeneo makuu saba: (i) sheria na taratibu zinazoongoza uandikishaji wa wapigakura kwa kutumia teknolojia ya BVR; (ii) uendeshaji wa mashine za BVR; (iii) ujazaji wa fomu mahsusi; (iv) utunzaji wa mashine za BVR; (v) matengenezo madogomadogo na usafishaji wa mashine za BVR; (vi) utatuzi wa matatizo madogomadogo ya kiteknolojia BVR; na (vii) utambuzi wa wapigakura wenye sifa.



*Mafunzo ya Waendeshaji wa Mitambo ya BVR Kwimba*




*Mafunzo ya Waendeshaji wa Mashine za Kwimba*

Inatia moyo kugusia kuwa ingawa kwa ujumla waendeshaji wa mashine za BVR walionesha viwango vikubwa vya ufanisi, matukio machache ya upungufu yalijitokeza. Huko Geita watu 150 kutoka vituo tofauti vya kuandikishia wapigakura walilalamikia viwango vya chini vya kadi zilizotolewa. Baadhi ya kadi katika kituo cha Nyerere Road, kata ya Kilangalanga ziligeuzwa. Kufikia mwisho wa zoezi la uandikishaji tarehe 23 Juni 2015 katika kata ya Buhalahala, Mwatutole, kiasi cha watu 400 hawakuandikishwa, pamoja na uamuzi wao wa kugomea kutoka kituo cha kujiandikisha mpaka saa tatu usiku. Wasimamizi wa kituo walipojaribu kuondoa mashine za kuandikishia, vurugu iliibuka na vioo vya madirisha vya magari mawili vilivunjwa kwa kupigwa mawe.





*Vioo vya Gari Vikiwa Vimevunjwa baada ya Kupigwa Mawe na Watu wenye Hasira Kufuatia Kutokuelewana na Maafisa Uandikishaji huko Geita*




***Kielelezo 4-2: Utendaji wa Jumla wa Maafisa Uandikishaji***
Chanzo: Ripoti za Waangalizi wa Uchaguzi wa TEMCO, 2015

Kielelezo 4-2 unaonesha viwango vya juu vya kuridhisha vya utendaji wa maafisa uandikishaji. Ni asilimia nne tu ya vituo vilivyotazamwa na TEMCO ndio walionesha utendaji hafifu.

Ripoti za waangalizi wa TEMCO zinaonesha kuwa waendeshaji wa mashine za BVR walikuwa wakipata uzoefu na ufanisi kadri siku zilivyokuwa zinakwenda. Ilionekana kuwa katika siku mbili za mwanzo uandikishaji ulikuwa wa chini hasa kwa waendeshaji mashine kujifunza na kuzizoea mashine. Kadri siku zilivyosonga mbele ufanisi wao uliongezeka na watu wengi zadi walikuwa wakiandikishwa kwa siku. NEC iliweka utaratibu wa kutumia siku saba tu katika kila kata. Ripoti za waangalizi wa TEMCO zinaonesha kuwa hali ilikuwa tofauti pale ambapo NEC iliamua kutumia timu ileile ya waandikishaji katika kata zaidi ya moja ndani ya jimbo.




***Kielelezo 4-3: Utoshelevu wa Mafunzo kwa Maafisa Uandikishaji***
Chanzo: Ripoti za Waangalizi wa Uchaguzi wa TEMCO, 2015

Kama inavyoonekana katika Kielelezo 4-3, asilimia 48 ya waangalizi wa TEMCO walitathmini mafunzo ya maafisa uandikishaji na kuripoti kwamba mafunzo hayo yalikuwa mazuri. Aidha, asilimia 36 walisema yalikuwa mazuri sana. Ni asilimia nane tu ndio walisema yalikuwa hafifu au mabaya.

***Jedwali 4-1: Ugumu wa kutumia mashine za BVR***

| **Jibu** | **Idadi** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| **Ndio** | 109 | 67.7 |
| **Hapana** | 52 | 32.3 |
| **Jumla** | 161 | 100.0 |

Chanzo: Ripoti za Waangalizi wa Uchaguzi wa TEMCO, 2015

Kwa ujumla, kama inavyoonekana katika Jedwali 4-1, asilimia 68 ya maafisa uandikishaji walimudu utumiaji wa mashine za BVR. Matatizo mengi waliyokumbana nayo maafisa uandikishaji yalihusu "software" (asilimia 67) na yaliyobaki yalihusu "hardware".

### *4.4.2 Utoshelevu wa Fedha, Vituo vya Uandikishaji na Vifaa vya BVR*

Ili kutekeleza kwa ukamilifu zoezi la uandikishaji wa wapigakura, NEC ilipaswa kuwa na idadi ya kutosha ya vituo vya kuandikisha wapigakura katika kila kata. Vituo vya uandikishaji vilitakiwa kuwa na vifaa vyote muhimu ikiwemo mashine za BVR. Ripoti za waangalizi wa TEMCO zilionesha kuwa NEC sio tu ilikuwa kwa kiasi fulani ikikabiliwa na upungufu wa pesa lakini haikupata pesa za kununulia mashine za BVR kwa muda mwafaka. Utoaji wa pesa kutoka serikalini ulikuwa wa kusuasua na hivyo kuathiri mpango wa manunuzi wa Tume. NEC ilipanga kununua mashine 15,000 za BVR lakini baada ya mashauriano na serikali idadi ikapunguzwa mpaka mashine 8,000 za BVR kwa ajili ya uandikishaji wa Watanzania takribani milioni 24 waliokadiriwa.

#### *4.4.2.1 Ununuzi wa Mashine za BVR*

Kufikia wakati wa zoezi la majaribio ya mashine za BVR mwezi Desemba 2014 NEC ilikwishanunua mashine 250 za BVR. NEC iliahidi kuwa mashine 7,500 zingeingia nchini muda wowote ili uandikishaji uendelee kwa kasi. Hata hivyo, ununuzi wa mashine za BVR

ulichelewa na hivyo kuchelewesha zoezi la uandikishaji. NEC ilitoa taarifa kwa umma kuwa mashine za BVR ziliagizwa kutoka kwa kampuni ya Lithotech Exports ya Afrika Kusini, ingawa mchakato wa tenda haukuwekwa wazi. Mathalani, tarehe 23 Septemba 2014 Mwenyekiti wa NEC Jaji Mstaafu Damian Lubuva alinukuliwa na gazeti la *ThisDay* akithibitisha kuwa serikali ilifanya malipo ya awali ya shilingi bilioni 290 (kati ya shilingi bilioni 298) kwa ajili ya kununulia mashine za BVR. Kufikia mwezi Machi, 2015 mashine za BVR zilizoahidiwa zilikuwa hazijawasili nchini. Shauku na tashwishwi ya jamii ilikuwa inaongezeka na hivyo kuipa Tume wakati mgumu.[4] Tarehe 25 Machi, 2015, Waziri Mkuu, Mhe. Mizengo Pinda alisema serikali ilikuwa imetoa asilimia 70 ya pesa iliyotakiwa kununulia mashine za BVR.[5]



*Mashine za BVR Tayari Kusambazwa wakati wa Uandikishaji*

Mkanganyiko huu uliwafanya wabunge kudai majibu kutoka serikalini wakati wa kikao cha 18 cha bunge kilichokutana mwezi Aprili, 2015. Wakati akiahirisha kikao cha bunge, Waziri Mkuu alisema kuwa serikali ilikuwa imelipa asilimia 100 ya pesa zilizotakiwa kununulia mashine za BVR. Pia alikiri kuwa kura ya maoni iliyokuwa ifanyike tarehe 30 Aprili, 2015 isingewezekana, na Tume ingetangaza tarehe nyingine.[6] Siku iliyofuata Mwenyekiti waTume alithibitisha kuahirishwa kwa kura ya maoni ya katiba mpya mpaka itakapotangazwa tena.

#### *4.4.2.2 Ratiba na Ugawaji wa Vifaa na Malighafi*

Tarehe 16 Desemba, 2014 NEC iliendesha zoezi la uandikishaji wa majaribio kwa kutumia BVR katika majimbo matatu: Mlele (Katavi), Kawe (Dar es Salaam) na Kilombero (Morogoro). Zoezi hili lilikuwa limeshaahirishwa mara nyingi baada ya kushindikana mwezi

[4] TEMCO Newsletter, Vol 1, Issue 1&2 Combined, March-April, 2015
[5] Daily News, 25/3/2015
[6] The Citizen, 10/04/2015

Agosti, Septemba na Oktoba, 2014 kama ilivyotangazwa awali[7]. Ilikuwa muhimu kufanya uandikishaji wa majaribio ili kutoa nafasi ya kutathmini ufanisi wa mashine za BVR pamoja na changamoto zake katika mazingira tofauti na kutoa mwanya wa marekebisho kabla ya kuanza zoezi nchi nzima. Baadhi ya changamoto zilizojitokeza ni pamoja na matatizo ya hardware kushindwa kufanya kazi, kuathirika na hali mbaya ya hewa (hasa Morogoro na Dar es Salaam) na kutokujua kusoma na kuandika. Tatizo la hardware lilicheleweshа uandikishaji katika vituo vingi Dar es Salaam na kuleta manung'uniko mengi. NEC iliahidi kuyafanyia kazi matatizo yote yaliyojitokeza kabla ya zoezi la uandikishaji nchi nzima.

***Jedwali 4-2: Uandikishaji Wapigakura wa Majaribio***

| Na. | Jimbo | Makadirio | Walioandikishwa | Tofauti |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | Katavi | 11,394 | 11,210 | -184 |
| **2.** | Kawe | 35,426 | 21,323 | -14,103 |
| **3.** | Kilombero | 17,790 | 19,188 | +1,398 |

Chanzo: Majumlisho ya Takwimu za NEC, 2015

Kama inayoonekana katika Jedwali 4-2, zoezi la majaribio lilidhihirisha kuwa teknolojia ya BVR inaweza kufanya kazi Tanzania, licha ya changamoto zilizojitokeza hususani upatikananji wa umeme zilizojitokeza.

Zoezi la uandikishaji lilianza rasmi katika mkoa wa Njombe tarehe 23 Februari, 2015 kwa kutumia mashine 250 za BVR zilizokuwa zimenunuliwa mpaka wakati huo. Uandikishaji uliendelea kushika kasi taratibu katika kipindi cha miezi sita iliyofuata kadri mtengenezaji, Lithotech Export ya Afrika Kusini alivyoendelea kuingiza mashine za BVR kwa awamu.Uandikishwaji ulikamilishwa katika mkoa wa Dar es Salaam ambako ulifanyika kwa siku 14 (22 Julai mpaka 4 Agosti, 2015). NEC hatimaye ilitoa ratiba kamili ya uandikishaji wapigakura kwa kila mkoa tarehe 22 Mei, 2015, miezi miwili baada ya kuanza kwa zoezi la uandikishaji, kufuatia malalamiko ya vyama vya siasa na wadau wengine. Hata hivyo ratiba hiyo iliendelea kufanyiwa marekebisho kulingana na mazingira yaliyojitokeza wakati wa uandikishaji.

Ripoti za waangalizi wa TEMCO zinaonesha kuwa uandikishaji mkubwa ulifanyika kati ya miezi ya Mei-Julai, 2015. Katika mikoa mingi uandikishaji ulifanyika kwa siku 30 ingawa siku chache ziliongezwa pale ilipoonekana haja ya kufanya hivyo, hasa pale ambapo watu wengi walikuwa hawajajiandikisha kufikia siku ya mwisho iliyowekwa. Kuelekea ukingoni na hasa baada ya mashine za BVR nyingi zaidi kuwasili, siku za kuandikisha kwa kila mkoa zilipunguzwa kwa kuwa mashine nyingi zaidi zilipelekwa mikoani. Mathalani undikishaji wa wapigakura kwa mkoa wa Dar es Salaam lilikomalizikia zoezi ulipangwa kufanyika kwa siku 10 tu, ingawa ziliongezwa siku chache baada ya kuonekana ulazima wa kufanya hivyo. Katika mkoa wa Pwani uandikishaji wa wapigakura ulifanyika kwa siku 14. Kwa Zanzibar zilitengwa siku tatu tu kwa ajili ya wapigakura ambao hawakuandikishwa na ZEC lakini walikuwa na sifa za kushiriki uchaguzi wa Serikali ya Muungano. Wapigakura wa aina hii ni wachache na

[7] ThisDay, 12/11/2015

kufikia mwisho wa siku ya tatu wote walikwishaandikishwa. NEC ilipanga utaratibu wa kuandikisha katika kanda iliyohusisha idadi ya mikoa kadhaa. Ndani ya kanda na mkoa uandikishaji pia ulifanyika kwa awamu kwa kuanzia na idadi iliyopangwa ya kata na kisha kuendelea na kata nyingine mpaka zote zilipomalizika. Uandikishaji katika kata ulifanyika kwa siku saba tu. Ratiba ya awali ya uandikishaji wa wapigakura inaoneshwa katika Jedwali 4-3.

***Jedwali 4-3: Ratiba ya Uandikishaji wa Wapigakura kwa Mikoa***

| Na. | Mkoa | Kuanza | Kumaliza | Na. | Mkoa | Kuanza | Kumaliza |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **1.** | Njombe | 23/02/2015 | 23/03/2015 | 14. | Geita | 02/06/2015 | 04/07/2015 |
| **2.** | Lindi | 24/04/2015 | 24/05/2015 | 15. | Mwanza | 02/06/2015 | 04/07/2015 |
| **3.** | Mtwara | 24/04/2015 | 24/05/2015 | 16. | Shinyanga | 02/06/2015 | 04/07/2015 |
| **4.** | Ruvuma | 27/04/2015 | 28/05/2015 | 17. | Simiyu | 02/06/2015 | 04/07/2015 |
| **5.** | Iringa | 29/04/2015 | 29/05/2015 | 18. | Kilimanjaro | 12/06/2015 | 12/07/2015 |
| **6.** | Katavi | 18/05/2015 | 17/06/2015 | 19. | Arusha | 12/06/2015 | 12/07/2015 |
| **7.** | Mbeya | 19/05/2015 | 18/06/2015 | 20. | Mara | 12/06/2015 | 12/07/2015 |
| **8.** | Dodoma | 20/05/2015 | 19/06/2015 | 21. | Manyara | 12/06/2015 | 12/07/2015 |
| **9.** | Rukwa | 24/05/2015 | 23/06/2015 | 22. | Morogoro | 18/06/2015 | 18/07/2015 |
| **10.** | Kigoma | 21/05/2015 | 18/06/2015 | 23. | Pwani (Coast) | 18/06/2015 | 18/07/2015 |
| **11.** | Kagera | 21/05/2015 | 18/06/2015 | 24. | Tanga | 18/06/2015 | 18/07/2015 |
| **12.** | Singida | 21/05/2015 | 18/06/2015 | 25. | Zanzibar | 14/06/2015 | 16/06/2015 |
| **13.** | Tabora | 21/05/2015 | 18/06/2015 | 26. | Dar es Salaam | 04/07/2015 | 16/07/2015 |

Chanzo: Mawasiliano mbalimbali ya NEC, 2015

Kama tulivyogusia awali, Tume ilichelewa sana kutoa ratiba kamili ya uandikishji wa wapigakura mikoani. Hata ratiba ilipotolewa bado kulikuwa na mikanganyiko katika ngazi ya mkoa na watu wengi hawakujua uandikishaji katika kata zao ungefanyika lini. Baadhi ya watu waliolazimika kusafiri walishindwa kujiandikisha kwa kukosa taarifa sahihi.

#### *4.4.2.3 Uandaaji na Uendeshaji wa Vituo vya Kuandikishia Wapigakura*

NEC ilikuwa na jukumu la kuhakiki utoshelevu wa vituo vya kupigia kura ili uandikishaji ufanyike bila bughudha kwa mpigakura. Ilikuwa ni muhimu kuhakikisha kuwa vituo vya kuandikishia wapigakura viliwekwa karibu na makaziya eneo ambalo lingefikika kwa mguu. Kwa mujibu wa sheria vituo vya kuandikishia wapigakura vilitakiwa viwe katika majengo ya umma, na ripoti za waangalizi wa TEMCO zinaonesha kuwa asilimia 99.4 ya vituo vyote vilikidhi matakwa haya. Asilimia 0.6 ya vituo vyote vilikuwa katika maeneo ya ibada. Huko Tabora watu walidai kituo kilichokuwa eneo la ibada kihamishwe na NEC ilikubaliana na madai haya. Asilimia 26 ya vituo vya uandikishaji wapigakura vilikuwa katika majengo ya muda, chini ya miti au maeneo ya wazi yaliyowekewa maturubai kukinga jua. Vituo kama hivi havikuwa tu hatarishi kwa mashine za BVR lakini havikuwa mazingira sahihi ya kazi kwa waendeshaji wa mashine za BVR.



*Kituo cha Kuandikisha Wapigakura,Bahi, Dodoma*



*Watu Wakisubiri Zamu ya Kuandikishwa wakiwa Wamekaa kwenye Madawati ya Mojawapo ya Darasa, Shule ya Msingi Mlela, Kata ya Kandaga, Kigoma*

***Jedwali 4-4: Kufikika kwa Vituo vya Kuandikishia Wapigakura***

| **Majibu** | **Idadi** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| Vilifikika na vilikidhi mahitaji ya watu wenye mahitaji maalum | 119 | 73.9 |
| Havikufikika kwa urahisi na watu wenye mahitaji maalum | 37 | 23 |
| Vilikuwa maeneo ya miinuko mikali na watu wangeshindwa kuvifikia | 1 | 0.6 |
| Vilikuwa mbali zaidi ya kilomita tatu | 4 | 2.5 |
| **Total** | 161 | 100.0 |

Chanzo: Ripoti za Waangalizi wa Uchaguzi wa TEMCO, 2015

Kama inavyoonekana katika Jedwali 4-4, asilimia 74 ya vituo vya kuandikishia wapigakura vilikuwa katika maeneo muafaka na viliweza kufikiwa kwa urahisi na makundi yote ya watu wakiwemo wenye mahitaji maalum na wajawazito. Hata hivyo, asilimia 23 ya vituo vya kuandikishia wapigakura havikuweza kufikika kwa urahisi na watu wenye mahitaji maalum na asilimia 3 vilikuwa mbali na maeneo ya makazi. Changamoto ya vituo kuwa mbali na maeneo ya makazi ilijitokeza zaidi maeneo ya wafugaji ambako makazi yalikuwa yametapakaa na watu walikuwa wanahamahama kutafuta maeneo ya kuchungia mifugo yao.

Ripoti za waangalizi wa TEMCO zinaonesha kuwa vituo vya kuandikishia wapigakura vilifunguliwa na kufungwa kwa wakati. Kati ya vituo 10,432 vilivyotazamwa, vituo 8,398 (asilimia 80.5) vilifunguliwa kwa wakati, na vituo 2,034 (asilimia 19.5) vilifunguliwa baada ya saa mbili asubuhi, kwa sababu mbalimbali ikiwemo uhamishaji wa mashine za BVR kila siku kuzirudisha stoo. Muda wa kufunga vituo vya uandikishaji ulionesha kuwa asilimi 64 ya vituo vyote vilimaliza zoezi la uandikishaji kila siku saa 12 jioni. Katika baadhi ya maeneo ilibidi uandikishaji uendelee kutokana na idadi kubwa ya watu waliokuwa kwenye foleni au kufidia muda uliopotea kwa kuchelewa kufungua vituo.


Vifaa vilikuwepo vya kutosha na hakukuwa na matukio ya kufungwa vituo kwa sababu ya upungufu wa vifaa. Asilimia 67 ya vituo vilivyokuwa na matatizo ya mashine kushindwa kufanya kazi iliripotiwa. Katika asilimia 33 ya vituo mashine ziliharibika na kuchukua muda kurekebishwa, muda mrefu kabisa ikiwa ni siku moja.

*Jedwali 4-5: Utoshelevu wa Mashine za BVR*

| Majibu | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|
| **Ndio** | 102 | 63.4 |
| **Hapana** | 59 | 36.6 |
| **Total** | 161 | 100 |

Chanzo: Ripoti za Waangalizi wa Uchaguzi wa TEMCO, 2015

Kama inavyoonekana katika Jedwali 4-5, asilimia 63 ya vituo vya uandikishaji vilikuwa na idadi ya kutosha ya mashine za BVR na asilimia 37 kulikuwa na upungufu. Kiasi hiki cha upungufu ni kikubwa.




***Kielelezo 4-4: Idadi ya matukio ya kuharibika kwa mashine za BVR***

Chanzo: Ripoti za Waangalizi wa Uchaguzi wa TEMCO, 2015


Kama inayoonekana katika Kielelezo 4-4 tunaweza kuhitimisha kuwa matatizo ya kuharibika kwa mashine za BVR yalikuwa machache na hayakutokea mara kwa mara. Waangalizi wa TEMCO waligundua kuwa matatizo mengi ya kiufundi yalitatuliwa ndani ya muda mafaka. Katika takriban nusu ya vituo vilivyotazamwa na TEMCO, matatizo yalitatuliwa ndani ya saa moja.

*Jedwali 4-6: Uwepo wa Mashine za Dharura za BVR*

| Majibu | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|
| **Ndio** | 136 | 84.5 |
| **Hapana** | 25 | 15.5 |
| **Jumla** | 161 | 100 |

Chanzo: Ripoti za Waangalizi wa Uchaguzi wa TEMCO, 2015

Jedwali 4-6 linaonesha uwepo wa mashine za BVR za dharura katika asilimia 85 ya vituo vya uandikishaji vilivyotazamwa na TEMCO. Maana yake ni kuwa katika vituo hivi iliwezekana uandikishaji kuendelea hata kama mashine iliyokuwepo ilipata hitilafu.




***Kielelezo 4-5: Muda wa Wastani wa Kuandikisha Mpigakura***
Chanzo: Ripoti za Waangalizi wa Uchaguzi wa TEMCO, 2015

Kielelezo 4-5: Muda wa Wastani wa Kuandikisha Mpigakura unaonesha kuwa katika zaidi ya nusu ya vituo vya uandikishaji vilivyotazamwa, ilichukua wastani wa dakika tano kuandikisha mpigakura wakati katika asilimia 36 ilichukua dakika 10. Ni katika asilimia 3 pekee ya vituo vilivyobainika kuwa na uandikishaji uliochukua zaidi ya dakika 15. Hii ni ishara ya uwezo wa kutosha wa maafisa uandikaji.

Mashine moja ya BVR ilikadiriwa kuandikisha wapigakura kati ya 80 mpaka 150 kwa siku na hali ilikuwa hivyo kwa sehemu kubwa wakati wa zoezi la uandikishaji. Changamoto kubwa ilikuwa ni mipangilio wakati wa uandikishaji. Tatizo lilikuwa kubwa pale watu wengi zaidi walipojitokeza. Huko Nyamagana maafisa uandikishaji walitoa namba kiasi kwamba wale waliozidi namba 150 waliambiwa warudi kesho yake. Katika mtaa wa Nchenga wasimamizi wa BVR walifungiwa ndani ya kituo cha uandikishaji tarehe 18 Juni, 2015 na kundi la watu waliokasirika baada ya kuambiwa warudi kesho yake baada ya kukaa siku nzima wakijaribu kuandikishwa. Polisi walilazimika kuingilia kati na kuandikisha majina na kuwaahidi kuwapa nafasi ya kwanza kesho yake. Sehemu nyingine kama Shule ya Msingi Kagunguli mashine za BVR ilibidi zihamishiwe katika vituo vingine vilivyokuwa na foleni ndefu mara baada ya uandikishaji kukamilika ndani ya siku nne tu tarehe 13 Juni, 2015. Usalama wa mashine za BVR ulileta mushkeli katika baadhi ya maeneo. Tarehe 23 Juni, 2015 mashine ya BVR iliibwa katika nyumba ya kulala wageni Magu katika kata ya Kayenze wakati mashine zikiwa zinachajiwa usiku. Hata hivyo mashine hiyo ilikutwa imetelekezwa kesho yake ikiwa katika hali nzuri.

Pamoja na kutokuwepo kwa maafisa wa polisi katika vituo vingi vya kuandikisha wapigakura, katika vituo takribani vyote TEMCO ilipokuwa na waangalizi hakukuwa na dalili za vitisho wala vurugu zilizotishia mchakato. Viongozi wa serikali za mtaa walijitahidi kuhakikisha kuwa wananchi wanaendelea kuwa watulivu wakati wakisubiri zamu zao za kuandikishwa katika foleni.

### 4.5 Elimu ya Mpigakura Wakati wa Uandikishaji

NEC ina mamlaka ya kikatiba ya kutoa elimu ya mpigakura na kuratibu shughuli za watoa elimu wengine. Matokeo ya utazamaji wa TEMCO yanaonesha kuwa elimu ya mpigakura

wakati wa mchakato wa uandikishaji wa wapigakura ilikuwa haba, ilikosa fedha, haikuratibiwa vizuri na ilikuwa ya viraka.Waangalizi wa TEMCO waligundua kuwa taarifa za uandikishaji zilikuwa haba na hazikutosheleza. Hata hivyo baadhi ya asasi zilijihusisha na utoaji wa elimu ya mpigakura kama ifuatavyo: NEC (asilimia 55), vyama vya siasa (asilimia 33.5), vyombo vya habari (asilimia 5.3), asasi za kidini (asilimia 3.6) na asasi za kiraia (asilimia 2.0). Njia kuu zilizotumika kutoa elimu ya mpigakura kwa wahusika zilikuwa mabango, matangazo ya magari, (NEC); mikutano ya hadhara (vyama vya siasa); na mahubiri katika nyumba za ibada (FBOs). Waangalizi wa uchaguzi wa TEMCO waligundua ushiriki hafifu wa vyama vya siasa na asasi za kiraia katika utoaji wa elimu ya mpigakura. Vilevile taarifa zinazohusu uandikishaji katika BVR zilitolewa zaidi katika maeneo ya mijini kuliko maeneo ya vijijini.

Taarifa zilizotolewa na waangalizi wa uchaguzi wa TEMCO kuhusu kiasi cha watu waliohitaji msaada katika kujaza fomu za kujiandikisha, ikiwemo utiaji wa saini kilishtusha. Wengi wao hawakuweza kusoma herufi na hivyo ilitiliwa shaka hata uwezo wao wa kusoma mabango ya NEC juu ya mchakato wa BVR. Hali hii ilidhihirisha ongezeko la viwango vya ujinga katika jamii hasa maeneo ya vijijini. Vilevile waangalizi walionesha tabia ya upotoshaji na udanganyifu wa makusudi kuhusu madhumuni ya zoezi la BVR. Mathalani, baadhi ya watu huko Lindi walidhani kuwa watu ambao mashine za BVR zinashindwa kusoma alama zao za vidole walikuwa wachawi. Huko Simiyu na Geita baadhi ya watu walidhani kuwa zoezi la uandikishaji kwa kutumia BVR lilikuwa na lengo la kukamata wauaji wa watu wenye ualbino, wakati huko Tunduma watu walidai kuwa mashine za BVR pia zilikuwa zinapima UKIMWI. Upotoshaji huu unaweza kuhusishwa na kutamalaki kwa imani za kishirikina zitokanazo na kuendeleza ukale. Ilionekana pia kuwa watu wengi katika maeneo ya mipakani hawakuweza kufuata maelekezo ya BVR kwa Kiswahili. Hii ilionekana zaidi Mpanda, Misenye, Kyerwa, Karagwe, Msalala, Maswa, Mbogwe na Nyang'wale.

### 4.6 Ukiukwaji wa Taratibu, Changamoto na Hatua Zilizochukuliwa

Baadhi ya matukio ya ukiukwaji wa taratibu na changamoto zilizojitokeza wakati wa zoezi la uandikishaji wa wapigakura ni: (i) uandikishaji wa wageni na wasio Watanzania; (ii) kushindwa kutambua alama za vidole; (iii) mistari mirefu ya foleni za kujiandikisha; (iv) malipo yasiyoridhisha ya waendeshaji wa mashine za BVR; na (v) uwezo mdogo wa waendeshaji wa mashine za BVR.

#### *4.6.1 Uandikishaji wa Wahamiaji Haramu na Wageni*

Waangalizi wa uchaguzi wa TEMCO walikutana na kesi chache za ukiukwaji wa utaratibu na hasa uandikishaji wa wahamiaji haramu hasa katika mikoa ya pembezoni ikiwemo Kagera, Kigoma, Mbeya, Mtwara, Lindi, Mara, Kilimanjaro, Arusha na Tanga kinyume na sheria ya uchaguzi. Huko Kagera waangalizi wa uchaguzi wa TEMCO waligundua majaribio 185 ya wahamiaji haramu kutaka kujiandikisha. Matukio mengi yaligundulika kabla na hivyo wahusika wakazuia kujiandikisha. Ilisemekana kuwa tatizo hili lilichochewa na ubadilishaji wa mipaka ya Uganda/Tanzania mwaka 1995 na kugawa sehemu ya kijiji cha Bugango huko Misenyi ambacho kilikuwa Tanzania. Wakazi watatu wa kijiji hicho walifutiwa usajili ilipobainika kuwa hawakuwa wakazi. Maeneo mengi ya mipakani yana changamoto hii kwani

baadhi ya watu huweza kuwa na nyumba upande wa pili wa mpaka na katika maisha ya kila siku wanaingiliana bila shida yoyote.

Jambo lingine lililovutia hisia ni lile lililohusu hatma ya wakazi 300 wa kijiji cha Nduta wilayani Kibondo katika mkoa wa Kigoma waliokataliwa kuandikishwa. Nduta iliandaliwa kuwa kijiji cha mfano mara baada ya wakimbizi kutoka nchi jirani waliokuwa wakiishi hapo kuondoka. Hata hivyo, mpango huu ambao ulikuwa ukisukumwa na mbunge wa Muhambwe, Felix Mkosamali (NCCR-Mageuzi), haukupendwa na serikali. Mvutano huu uliishia mahakamani ambapo wakazi wa Nduta walishinda. Kulikuwa na hisia kuwa uamuzi wa kuruka kijiji cha Nduta wakati wa uandikishaji ulikuwa na uhusiano mkubwa na hasira za serikali baada ya kushindwa mahakamani.

Huko Tanga, timu ya maafisa uhamiaji 5 ilipewa jukumu la kuzuia uandikishaji wa wageni na wahamiaji. Hata hivyo, waangalizi wa walibaini kuwa idadi hii haikutosheleza kushughulikia tatizo la wahamiaji kutoka Kenya, Somalia na Msumbiji kikamilifu. Ilikuwa vigumu kutambua umri na uraia wa waliokuja kujiandikisha kwani wengi hawakwenda na vyeti vya kuzaliwa au vitambulisho vingine.

### *4.6.2 Utambuzi wa Alama za Vidole*

Tatizo la mashine za BVR kushindwa kusoma alama za vidole za baadhi ya watu liliripotiwa sana na vyombo vya habari. Ubora wa alama za vidole unaweza kuathiriwa na mambo mengi ikiwemo kazi ngumu za mikono, umri, utumiaji wa vipodozi na ujauzito. Huko Newala, kufuatia tatizo la utambuzi wa alama za vidole kuongezeka, baadhi ya watu walianza kueneza uvumi kuwa watu ambao alama za vidole hazitambuliwi na mashine za BVR ni wachawi. Hii iliwatisha baadhi ya watu waliohofia kuhisiwa kuwa ni wachawi. Huko Songea watu walisita kujiandikisha wakidhani kuwa mashine za BVR pia zinapima UKIMWI. Huko Songea na Liwale mashine za BVR zilihusishwa na imani za “Freemasons”. Huko Liwale katika Shule ya Msingi Nabuya, katika siku ya kwanza ya uandikishaji iliwachukua waandikishaji dakika 10 kuwatuliza watu na kuwahakikishia kuwa mashine za BVR hazihusiki kwa namna yoyote na imani ya “Freemason”.

Utatuzi wa matatizo ya utambuzi wa alama ulichukuwa muda mrefu wakati mwingine mpaka dakika 15. Wakati mwingine iliposhindikana kabisa, wahusika waliambiwa warudi kesho yake. Inatia shaka kama wote walirudi kesho yake. Huko Iringa tatizo la utambuzi wa alama za vidole lilitatuliwa kwa kuwaelekeza wahusika kunawa mikono yao na kusugua vidole taratibu. Mwangalizi wa TEMCO huko Tunduru alitaarifu kuwa mafuta maalum ya kulainisha yalipakwa kwenye vidole vya watu waliokuwa na tatizo la alama za vidole kushindwa kutambuliwa. Mbinu zote hizi zilisaidia kwa kiasi fulani. Katika kituo cha Namihu, wilaya ya Liwale, kama pia ilivyokuwa huko Shinyanga, waangalizi wa TEMCO walikutana na tabia ya ajabu kwa waandikishaji ambao waliwaorodhesha wote ambao alama za vidole hazikutambuliwa kama “walemavu”. Hii haikuwa sahihi na ilivuruga taarifa za watu na NEC inapaswa kufuatilia kujua ukweli wa wote walioandikwa kama walemavu.

Katika mkoa wa Simiyu tatizo la kushindwa kutambua vidole lilishughulikiwa ipasavyo na kwa weledi kwa kujaza katika fomu "no finger print option" (hakuna chaguo la alama za vidole), badala ya "mlemavu". Katika baadhi ya maeneo ya wilaya ya Kondoa tatizo la utambuzi wa vidole lilipatiwa ufumbuzi baada ya kugundua mmea uliojulikana kama *makayukayu* ambao ulikuwa na ubora kuliko sabuni za kawaida zilizotumika kuosha mikono. Watu wengi walianza kutumia mmea huu na kurahisisha zoezi la uandikishaji. Kabla ya hapo watu walikuwa wakijaribu kuosha mikono lakini inashindikana.

### *4.6.3 Misururu Mirefu katika Vituo vya Kuandikisha Wapigakura*

TEMCO ilibaini hamasa kubwa ilikuwepo miongoni mwa wapigakura kutaka kujiandikisha. Misururu ya watu wanaotaka kujiandikisha ilikuwa ni kitu cha kawaida katika mikoa mingi. Katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam na miji mingine mikubwa watu walivumbua mbinu mablimbali za kukwepa foleni ndefu. Mkoani Arusha, mathalani, baadhi ya vijana waligeuza suala la foleni kuwa ajira na kujipatia kipato. Waliamka alfajiri mapema kwenda vituoni. Vijana hawa kisha waliuza nafasi hizo za mbele kwa watu waliokuja baadaye kujiandikisha. Maeneo mengine baadhi ya watu waliazima watoto ili wafikapo vituoni wapewe kipaumbele cha kuandikishwa. Wengine walibuni mbinu ya kupanga mawe ili kuchukua nafasi katika foleni na mtindo huu ukaja kujulikana kama "mfumo wa mawe". Tatizo la foleni ndefu lingeweza kupungua kama NEC ingekuwa na utaratibu mzuri wa kuandikisha watu. Ingewezekana, mathalani, kuanza na mtaa mmoja na kisha kuhamia mtaa mwingine mpaka kumaliza kata nzima. Dar es Salaam tatizo lilijitoeza pale watu walipoanza kusaka vituo vyenye watu wachache na kwenda kujiandikisha huko hata kama ilikuwa ni mbali na maeneo yao ya makazi. Kulikuwa na mashaka iwapo watu hawa kweli walikuwa na nia ya dhati ya kupiga kura kwani ingewalazimu kusafiri umbali mrefu kwenda kwenye vituo vyao vya kupigia kura siku ya uchaguzi.



*Misururu Mirefu katika Kituo cha Mtaa wa Nchenga, Mwanza*

### *4.6.4 Malipo Haba kwa Waandikishaji wa Wapigakura*

TEMCO ilibaini kuwa waandikishaji na wataalam wengine wa BVR hawakuwa wakilipwa vizuri. Wengi wao walisema kuwa kiasi cha shilingi 20,000 walicholipwa hakikulingana na

uzito na unyeti wa kazi walioifanya. Wale waliopelekwa maeneo ya mbali walilazimika kutafuta malazi karibu na vituo vyao. Katika maeoneo kama Shilabela na Sengerema, kata ya Iyogelo, waandikishaji walilazimika kuazima samani kutoka kwa watu wanaoishi jirani na vituo vya kuandikishia kwani hakukuwa na fungu la bajeti kwa ajili hiyo. Katika maeneo ambayo taarifa za uandikishaji wa BVR hazikuwa zimesambaa vya kutosha iliwalazimu pia waandikishaji kuwahamasisha watu kujitokeza kuandikishwa. Msimamizi wa Uchaguzi wa Sengerema alikiri kuwa malipo yalikuwa duni lakini akawataka waandikishaji wawe na moyo wa uzalendo. Katika wilaya ya Rufiji waandikishaji wengi waliamua kusitisha mikataba yao baada ya kumaliza awamu ya kwanza ya uandikishaji, wakilalamikia malipo yasiyoridhisha. Huko Nyamagana ilizuka hali ya taharuki baada ya posho ya usafiri kupunguzwa kutoka sh. 5,000 mapka sh. 2,000 kwa siku. Hii iliwalazimisha waandikishaji kuanza kutumia usafiri wa pikipiki maarufu kama "bodaboda" kusafirishia mashine za BVR kutoka na kurudi vituoni. Tarehe 28 Juni 2015 waandikishaji wa BVR wa kata za Mabatini na Mbugani walisimamisha zoezi la uandikishaji wakitaka maelezo ya uamauzi wa kupunguza posho.

#### *4.6.5 Uwezo Mdogo wa Waandishi*

Ripoti za waangalizi wa TEMCO zilibaini kuwa waandishi walishindwa kushughulikia matatizo madogomadogo ya kiteknolojia na ilibidi wawasubiri wataalam wa TEHAMA. Katika sehemu zilizokuwa na misururu hali ya taharuki ilizuka pale watu walipohofia kuwa hawataweza kuandikishwa. Katika kata ya Nguruka tarehe 27 Mei, 2015 zogo lilizuka watu walipoanza kusukumana ili wapate nafasi ya kuandikishwa. Amani ilirejea baada ya msimamizi msaidizi wa uchaguzi kuwahakikishia kuwa wote wataandikishwa. Katika kata ya Gungu watu walilalamika kuwa waandikishaji walikuwa wanaacha vituo kwa muda mrefu kwa kisingizio cha kwenda kutafuta chakula. Baadaye walipewa maelekezo kuwa wachukue chakula na kwenda nacho vituoni.

### 4.7 Makadirio na Idadi Halisi ya Walioandikishwa Kupiga Kura

Mpaka wakati wa kuandaa ripoti hii NEC haikuwa imetoa jumla ya makadirio na idadi halisi ya walioandikishwa kupiga kura. Hata hivyo, NEC ilipotoa matokeo ya urais ilionesha kuwa wapigakura walioandikishwa walikuwa 23,161,440 (asilimia 96.9) kati ya 23,913,184 waliokadiriwa. Mgawanyo wa wapigakura walioandikishwa kwa mikoa na jinsia unaoneshwa katika Jedwali Na. 4.9[8].

[8] Takwimu hizi katika Jedwali Na. 4.9 zinapaswa kuthibitishwa na mamlaka husika.

*Jedwali 4-7: Idadi ya Wapigakura kwa Mikoa na Jinsia*

| Na. | Mkoa | Wanaume | Wanawake | Jumla | %Ke |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Arusha | 494,699 | 514,593 | 1,009,292 | 51 |
| 2 | Dar es Salaam | 1,319,202 | 1,456,093 | 2,775,295 | 52 |
| 3 | Dodoma | 510,581 | 560,802 | 1,071,383 | 52 |
| 4 | Geita | 374,137 | 513,845 | 887,982 | 58 |
| 5 | Iringa | 254,095 | 275,792 | 529,887 | 52 |
| 6 | Kagera | 508,537 | 543,144 | 1,051,681 | 52 |
| 7 | Kaskazini Pemba | 7,066 | 4,504 | 11,570 | 39 |
| 8 | Kaskazini Unguja | 5,856 | 3,746 | 9,602 | 39 |
| 9 | Katavi | 142,363 | 179,764 | 322,127 | 44 |
| 10 | Kigoma | 339,157 | 453,394 | 792,551 | 52 |
| 11 | Kilimanjaro | 382,600 | 417,749 | 800,349 | 52 |
| 12 | Kusini Pemba | 5,645 | 3,341 | 8,986 | 37 |
| 13 | Kusini Unguja | 3,295 | 1,782 | 5,077 | 35 |
| 14 | Lindi | 245,256 | 269,302 | 514,558 | 52 |
| 15 | Manyara | 352,627 | 325,959 | 678,586 | 48 |
| 16 | Mara | 413,679 | 479,062 | 892,741 | 54 |
| 17 | Mbeya | 659,516 | 738,138 | 1,397,654 | 53 |
| 18 | Mjini Magharibi | 7,289 | 5,659 | 12,948 | 44 |
| 19 | Morogoro | 624,947 | 647,004 | 1,271,951 | 51 |
| 20 | Mtwara | 336,016 | 392,965 | 728,981 | 54 |
| 21 | Mwanza | 723,984 | 724,900 | 1,448,884 | 50 |
| 22 | Njombe | 175,993 | 207,373 | 383,366 | 54 |
| 23 | Pwani | 349,423 | 348,110 | 697,533 | 50 |
| 24 | Rukwa | 222,521 | 237,052 | 459,573 | 52 |
| 25 | Ruvuma | 359,643 | 380,131 | 739,774 | 51 |
| 26 | Shinyanga | 360,557 | 412,716 | 773,273 | 52 |
| 27 | Simiyu | 304,717 | 414,060 | 718,777 | 58 |
| 28 | Singida | 313,199 | 335,698 | 648,897 | 52 |
| 29 | Tabora | 522,564 | 575,196 | 1,097,760 | 52 |
| 30 | Tanga | 481,426 | 528,327 | 1,009,753 | 52 |
| | Jumla Kuu | | | 22,750,791 | 53 |

Chanzo: NEC, 2015

## 4.8 Tathmini ya Jumla ya Zoezi la Uandikishaji Wapigakura

TEMCO ilitathmini ufanisi wa jumla wa zoezi la uandikishaji wa wapigakura ili kujiridhisha ni kwa kiasi gani zoezi hili liliweza kuchangia katika uchaguzi huru, wa haki na wa kuheshimika. Matokeo yanaoneshwa katika Jedwali namba. 4.10.

*Jedwali 4-8: Tathmini ya Zoezi la Uandikishaji Wapigakura*

| Na. | Hali ya uandikishaji | Alama (%) | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mchakato wa kuandikisha wapigakura ulikuwa na matukio machache ya ukiukwaji ambayo hayakuathiri kwa namna yoyote matokeo. Kwa ujumla uandikishaji ulikuwa safi, huru na haki. | A (80-100) | 24 | 14.9 |
| 2 | Kwa ujumlam mchakato wa uandikishaji wapigakura ulikuwa huru na wa haki lakini kulikuwa na matukio machache ya ukiukwaji ambayo katika ujumla wake hayakuharibu matokeo ya mwisho na wala hayakuathiri mafanikio ya wadau (vyama vya siasa, wagombea na wapigakura). | B (60-69) | 112 | 69.6 |
| 3 | Mchakato wa uandikishaji wapigakura uliruhusu ushiriki huru wa wadau (vyama vya siasa, wagombea na wapigakura), lakini kulikuwa na matukio mengi ya ukiukwaji wa sheria na taratibu bila ya hatua stahiki kuchukuliwa dhidi ya wahusika na kulikuwa na upendeleo ulioathiri mafanikio ya baadhi ya wadau. | C (50-59) | 24 | 14.9 |
| 4 | Mchakato wa uandikishaji wapigakura uligubikwa na matukio mengi ya kutozingatia sheria, kanuni na taratibu, matatizo ya menejimenti na matukio ya vitisho na upendeleo. | D (40-49) | 1 | 0.6 |
| 5 | Uandikishaji wa wapigakura ulivurugwa na kuingiliwa kiasi kwamba wadau walikataa orodha ya wapigakura iliyotolewa. Ni kama mwanafunzi aliyefeli mtihani. | E (1-39) | 0 | 0 |
| 6 | Mchakato wa uandikishaji wapigakura uligubikwa na matukio makubwa ya ukiukwaji. Kulikuwa na upendeleo, rafu, na rushwa kiasi kwamba baadhi ya vyama vya siasa na wagombea waliamua kujitoa, walichukua hatua za kisheria au walitoa malalamiko rasmi. Mchakato wa uandikishaji ulikuwa kama mimba iliyoharibika. | F (0) | 0 | 0 |
| Jumla | | | 161 | 100.0 |

Chanzo: Ripoti za Waangalizi wa Uchaguzi wa TEMCO, 2015

## 4.9 Hitimisho na Mapendekezo

Sura hii imefanya tathmini ya ujumla ya mchakato wa uandikishaji wa wapigakura ili kuona kama sheria, kanuni na taratibu zilifuatwa ilivyotakiwa na kama zoezi hili lilichangia katika kuufanya uchaguzi kuwa huru, wa haki na wa kuaminika. Sehemu hii ya mwisho ni hitimisho na mapendekezo.

### *4.9.1 Hitimisho*

Kwa ujumla, mchakato wa uandikishaji wapigakura kwa kutumia teknolojia ya BVR ulifanyika vizuri kwa mujibu wa sheria zinazoongoza uchaguzi Tanzania. Ukiukwaji wa sheria na

upungufu wa kimenejimenti ulikuwa mdogo na usingeweza kuathiri ubora wa zoezi zima la uandikishaji kwa namna yoyote. Serikali ilibeba gharama za mchakato mzima wa uandikishaji wa wapigakura na hii ilikuwa hatua kubwa katika kupunguza utegemezi kutoka nje ya nchi kwa mambo nyeti kabisa ya kitaifa. Uamuzi wa NEC wa kuhama kutoka kwenye teknolojia ya OMR na kwenda kwenye BVR ulikuwa wa msingi na wa kupongezwa kwa kuzingatia manufaa ya BVR hususani katika kutambua na kuondoa utaratibu wa watu wanaojiandikisha zaidi ya mara moja katika daftari la kudumu la wapigakura. Matumizi ya teknolojia ya BVR yalihakikisha kuwa daftari zuri na lililoboreshwa linakuwepo. NEC ilitekeleza wajibu wake kwa weledi licha ya uhaba wa rasilimali fedha na muda ambavyo kwa kiasi fulani viliathiri utendaji na ufanisi wake.

Kufikiwa kwa asilimia 96.9 ya lengo la makadirio ya wananchi wenye sifa ni kielelezo cha ufanisi na umakini wa maafisa wote wa NEC waliohusika na zoezi la uandikishaji wa wapigakura waliofanya kazi kwa bidii bila kujali mazingira ya kazi wala kipato ambavyo sehemu nyingine havikutosheleza. Uamuzi wa NEC kuhakikisha kuwa watu wote waliotaka kujiandikisha kwa kuongeza muda pale ilipobidi ni wa kupongezwa. Ni ukweli kuwa wadau wengi wa uchaguzi waliiunga mkono NEC kwa namna moja au nyingine na kuiwezesha kukamilisha zoezi kwa mafanikio. Awali, vyama vya siasa, kikiwemo chama tawala, vilionesha wasiwasi kuhusu uwezekano wa kutekeleza uandikishaji kwa kutumia teknolojia ya BVR lakini wasiwasi huu ilipungua kadri siku zilivyokwenda.

### *4.9.2 Mapendekezo*

Baada ya kutazama kwa undani na kwa kuzingatia sheria, kanuni na utaratibu ulioongoza uandikishaji katika daftari la kudumu la wapigakura kwa kutumia teknoljia ya BVR, TEMCO inatoa mapendekezo yafuatayo:

(i) Mchakato wa ununuzi wa mashine za BVR haukuwa wazi vya kutosha na NEC inabidi kuongeza uwazi wakati ikitekeleza majukumu yake nyeti kwa mustakabali wa taifa;

(ii) NEC itazame upya utaratibu wake wa malipo kwa maafisa wanaoajiriwa kufanya sughuli mbalimbali. Kiasi walicholipwa maafisa uandikishaji hakukutosheleza na hakikulingana na ugumu na unyeti wa kazi yenyewe;

(iii) NEC itazame namna ya kuzitumia mashine za BVR katika kipindi kati ya uchaguzi mmoja na mwingine. Pamoja na kuwa zitaendelea kutumika wakati wa kuboresha daftari la kudumu la wapigakura, zinaweza pia kutumiwa na NIDA katika mchakato wa kutoa vitambulisho vya taifa; na

(iv) NEC iwe na utaratibu mzuri zaidi wa kusimamia mazoezi yake na kuhakikisha kuwa utekelezaji wake hausababishi usumbufu usiokuwa wa lazima kwa wananchi. Ingawa uandikishaji wa wapigakura ulifanyika kwa mafanikio, watu walilazimika kuvumilia foleni ndefu na wengine iliwachukua zaidi ya siku moja kujiandikisha.

## CHAPTER 5
## UTEUZI WA WAGOMBEA

### 5.1 Utangulizi

Uteuzi wa wagombea ni hatua mahususi katika zoezi la uchaguzi. Kitovu cha sura hii ni uteuzi wa wagombea ndani ya vyama vya siasa na vyombo vilivyoendesha uchaguzi mkuu (Tume za Uchaguzi) wa mwaka 2015. Sura hii imegawanyika katika sehemu kuu nane ikiwa ni pamoja na utangulizi huu. Sehemu ya pili ni muktadha wa kisheria na utaratibu wa uteuzi ndani ya vyama, ikifuatiwa na sehemu ya tatu ambayo inahusu uteuzi wa ndani ya vyama. sehemu ya nne, tano na sita zinahusu uhamaji wa wanachama baina ya vyama, uteuzi wa NEC na ZEC na wagombea waliopita bila kupingwa. Sehemu ya saba inatoa tathmini ya jumla juu ya zoezi zima la uteuzi na sehemu ya nane ni hitimisho na mapendekezo.

### 5.2 Muktadha wa Kisheria na Utaratibu wa Vyama kufanya Uteuzi

Mfumo wa sheria unaoratibu chaguzi nchini Tanzania huelekeza uteuzi wa wagombea wa nafasi mbalimbali (ambazo ni urais, ubunge, uwakilishi na udiwani) ufanywe kupitia vyama vya siasa vilivyosajiliwa. Nyaraka za kisheria zinazotoa utaratibu wa uteuzi wa wagombea walioshiriki katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 kwa ufadhili wa vyama vya siasa vyenye usajili wa kudumu ni pamoja na (i) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977; (ii) Katiba ya Zanzibar, 1984; (iii) Sheria ya Uchaguzi Na. 343, 1985; (iv) Sheria ya Uchaguzi Zanzibar Na. 11 ya 1984; na (v) Sheria ya Uchaguzi, Serikali za Mitaa, 1979.

Vyombo vyote viwili vinavyoratibu uchaguzi (NEC and ZEC) vimepewa mamlaka ya kuchagua siku kwa ajili ya uteuzi wa wagombea kwa kutoa tangazo kwenye *Gazeti la Serikali*. Kwa upande wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, siku ya uteuzi majimboni ilipaswa kupangwa ndani ya siku zisizopungua tano na zisizozidi ishirini na tano baada ya kuvunjwa kwa Bunge la Jamhuri na Baraza la Wawakilishi.[9]

Uteuzi wa wagombea nchini Tanzania wakati wa uchaguzi mkuu ulikuwa wa aina tatu; uteuzi wa wagombea urais, ubunge, na udiwani.

### 5.3 Uteuzi Ndani ya Vyama

Uteuzi wa wagombea ndani ya vyama vya siasa kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 ulivuta hamasa nyingi ndani ya vyama vikubwa, hasa ndani ya chama tawala na ndani ya chama kikuu cha upinzani, CHADEMA. Sababu kubwa ya hamasa hiyo ndani ya CCM ni mbio za kurithi 'rungu la uongozi.' Haikushangaza kuona mhemko mkubwa wa vyombo vya habari pale watia nia 42 walipojitokeza kuchukua fomu za uteuzi.

5.4 Uteuzi wa Wagombea Urais

Ripoti za TEMCO zinaonesha kuwa ni vyama viwili vya siasa, CCM na CHADEMA tu ndivyo vilikuwa na utaratibu wa uteuzi unaoeleweka katika ngazi zote. Vyama vingine vya siasa havikuwateua wagombea urais kwa taratibu za kidemokrasia zinazoakisi uwazi na ushindani.

[9]Article 37(1) (a) oft he National Elections Act Cap 343 (made under section 124) and Article 45 (1) (a) of the Zanzibar Elections Act, No. 11 of 1984.

### *5.3.1 Uteuzi wa Wagombea Urais ndani ya CCM*

Zoezi la uteuzi wa mgombea urais wa chama tawala lilikuwa jaribio tosha kupima umoja na mshikamano, na demokrasia ndani ya chama hicho. Kiti cha urais kiliwavutia wanachama 42 wa CCM ikiwa ni pamoja na Mawaziri kumi na wawili (12), Makamu wa Rais na Waziri Mkuu; Wakuu wa Usalama wa Taifa wawili (2) wastaafu, na Jaji Mkuu mstaafu. Hatimaye wagombea 38 walikidhi vigezo vya zoezi la mchujo kwenye uteuzi ndani ya chama. Majina ya wanachama wa CCM waliochukua fomu kuomba uteuzi wa chama kwenye nafasi ya urais yameambatanishwa kwenye ripoti hii kama kiambatisho namba 4.




*Mchoro wa Katuni Kuonesha Watiania wa CCM kwenye Kinyang'anyiro cha Kugombea Urais*

Tarehe 11 Julai 2015, Kamati Kuu (KK) ilitoa majina matano ambayo ni; January Makamba, Dkt. Asha-Rose Migiro, Balozi Amina Salum Ali, Dkt. John Pombe Magufuli na Bernard Kamilius Membe. Siku hiyo hiyo, Halmashauri Kuu (HK) ilitoa majina ya washindi watatu; Asha-Rose Migiro, Amina Salum Ali na John Pombe Magufuli. Tarehe 12 Julai, 2015 wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM walipiga kura kumchagua mgombea wa nafasi ya urais.




*Mchoro wa Katuni Kuonesha Watiania wa CCM kwenye Kinyang'anyiro cha Kugombea Urais*



*Rais na Mwenyekiti wa CCM Dkt. Jakaya Kikwete Akimtambulisha Ugombea Urais wa CCM Dkt. John Pombe Magufuli*

Asha-Rose Migiro alipata kura 59 (2.44%), Amina Salum Ali alijikusanyia kura 254 (10.5%), na john Pombe Magufuli alipata kura 2,104 (87.05%). Hivyo, John Pombe Magufuli alitangazwa kuwa mpeperusha bendera wa CCM kwenye kinyang'anyiro cha urais.



*Mwenyekiti wa CCM, Jakaya Mrisho Kikwete, mgombea mteule wa urais, Ndg.. John Pombe Magufuli, na mgombea mwenza, Samia Suluhu Hassan, wakiwapungia kwa furaha wajumbe wa mkutano mkuu wa chama hicho uliofanyika mjini Dodoma.*

Maamuzi ya zoezi la uteuzi ndani ya CCM yalipokelewa kwa namna tofauti tofauti. Wajumbe watatu miongoni mwa wajumbe 36 wa Kamati Kuu ambao ni Dkt. Emmanuel Nchimbi, Adam Kimbisa na Sophia Simba walionesha wazi wazi kutokuridhishwa na uamuzi wa Kamati Kuu kuliondoa jina la Bw. Edward Lowassa.



*Mh. Edward Lowassa baada ya Jina lake Kuondolewa kwenye Kinyang'anyiro cha Urais*

Ripoti za waangalizi wa TEMCO zilionesha kuwa Bw. Lowassa alikuwa na wafuasi wengi ndani na nje ya CCM kama ambavyo imedhihirishwa na maandamano yaliyolenga kupinga kuondolewa kwake kwenye kinyang'anyiro hicho cha urais. Pamoja na hali hiyo ya kutoridhika, zoezi la uteuzi liliendelea kama lilivyopangwa.



*Wafuasi wa Ndg. Edward Lowassa Wakiandamana Dodoma baada ya Lowassa Kuondoshwa katika Kinyang'anyiro cha Uteuzi wa Mgombea Urais kwa Tiketi ya CCM (Chanzo: The Citizen, Jumapili, July12, 2015).*

Licha ya madai ya wafuasi wake, Bw. Lowassa aliendelea kushiriki zoezi la uteuzi hadi mwisho. Wiki mbili baadaye aliamua kuhamia CHADEMA, uamuzi uliobainisha kuwa hakuridhishwa na zoezi la uteuzi ndani ya CCM.



*Mh. Edward Lowassa na Mkewe Wakionesha Kadi za Uanachama baada ya Kupokelewa CHADEMA*

### *5.3.2 Uteuzi wa Mgombea Urais wa CHADEMA*

Kama ilivyodokezwa kwenye sehemu ya kwanza, kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, vyama vinne vya CHADEMA, CUF, NCCR-MAGEUZI na NLD viliunda umoja wa UKAWA. Moja ya makubaliano ya umoja huu ni kuwa na mgombea mmoja wa kuwakilisha vyama shirika katika ngazi zote, ikiwemo nafasi ya urais wa muungano, ubunge na udiwani.

Wakati zoezi la uteuzi linaendelea, Bw. Lowassa alihamia CHADEMA tarehe 28 Julai 2015. Lowassa alidai kuwa uteuzi ndani ya CCM uligubikwa na ukiukwaji wa kanuni, kinyume na taratibu za uteuzi ndani ya chama.



*Mgombea Urais wa CHADEMA/UKAWA na Mgombea Mwenza wake na Viongozi wa juu wa CHADEMA na CUF*

Mara tu baada ya kujiunga CHADEMA, Lowassa alichukuwa fomu za uteuzi tarehe 30 Julai 2015 na kuzirudisha kwa Sekretarieti ya Chama mnamo Agosti 1, 2015. Tarehe 4 Agosti 2015 CHADEMA kilimpitisha Bw. Lowassa kuwa mgombea wake wa urais na Juma Duni Haji kama mgombea mwenza wake. Bw. Juma Duni Haji alihamia CHADEMA tarehe 3 Agosti 2015 akitokea CUF ili kutimiza matakwa ya kisheria ya kwamba sharti mgombea wa urais na mwenza wake watoke chama kimoja. Utazamaji wa TEMCO umebaini kuwa uteuzi wa ndani ya CHADEMA uliomtoa mpeperusha bendera wa UKAWA haukuwa wazi wala wa kiushindani, hivyo haukuweza kukidhi viwango vya uteuzi wa kidemokrasia.

Kama ilivyokuwa kwa CCM, uteuzi wa Bw. Lowassa kama mpeperusha bendera wa UKAWA ulizua hisia tofauti tofauti. Baadhi ya wanachama waliunga mkono uteuzi huo lakini wengine waliupinga kwa nguvu.Tarehe 6 Agosti 2015 mwenyekiti wa CUF, Professa Ibrahim Lipumba alitangaza kwenye mkutano wake na waandishi jijini Dar es Salaam kujiuzulu uwenyekiti na kubaki kuwa mwanachama wa kawaida. Alisema kuwa alifanya uamuzi huo kwa sababu UKAWA iligeuka na kuanza kuwapokea watu walioihama CCM ambao awali waliipinga Rasimu ya Katiba, ambao ndiyo ilikuwa msingi mkuu wa umoja huo. Uamuzi wa Lipumba kuacha uongozi wa CUF ulihusishwa pia na nia yake ya kutaka kugombea urais.
Kwa muktadha huo huo, tarehe 1 Septemba 2015 Katibu Mkuu wa CHADEMA, Dkt. Wilbroad Slaa alitangaza sio tu kujiuzulu ukatibu mkuu bali kuacha siasa na shughuli zote za chama pia. Kuondoka kwa Slaa kulisababishwa na uamuzi wa chama wa kumpitisha Lowassa, mtu ambaye yeye binafsi alimpinga kuwa hafai kwa ofisi ya rais kutokana na kashfa za ufisadi. Hata hivyo, Slaa aliamini kuwa yeye ndiyo alikuwa chaguo la CHADEMA kwenye kinyang’anyiro cha urais kutokana na mafanikio aliyoyapata kwenye uchaguzi wa mwaka 2010.

#### *5.3.3 Uteuzi ndani Vyama Vingine*

Pia, vyama vingine kumi (10) vilisimamisha wagombea wa urais. Vyama hivyo ni CCK (Christopher Malisa), UPDP (Fahmi Dovutwa), TLP (Macmillan Lyimo), ACT-Wazalendo (Anna Mghwira), ADC (Chief Lutalosa Yomba), DP (Rev. Christopher Mtikila), CHAUMMA (Hashim Spunda Rungwe), TADEA (John Chipaka), AFP (Omar Sombi), NRA (Janken Malik Kasambala). Ni vyama viwili tu; ACT-Wazalendo na TLP viliitisha Mkutano Mkuu kupitisha wagombea urais. Vyama vingine vilitumia utaratibu wa tofauti kuwapata wagombea wao wa urais. Kwa ujumla, zoezi la uteuzi ndani ya vyama hivi haukuwa wazi wala wa kiushindani.

### 5.4 Uteuzi Nafasi za Ubunge na Udiwani

Utazamaji wa TEMCO unaonesha kuwa vyama vichache tu ndivyo vilivyokuwa na utaratibu wa uteuzi wa kidemokrasia unaoeleweka, ulio wazi na wa kiushindani. TEMCO ilielekeza sana utazamaji wake kwenye vyama vitano; ACT-Wazalendo, CCM, CHADEMA, CUF na NCCR-Mageuzi. Vyama vingine vya siasa vilijumuishwa. Idadi ya wanachama ya vyama hivi vitano waliojitokeza kuomba uteuzi kwenye nafasi za ubunge, udiwani na viti maalum imeonyeshwa kwenye

Jedwali 5-1.

*Jedwali 5-1: Idadi ya Watia nia na Wagombea wa Viti vya Ubunge*

| Chama cha Siasa | Watia nia | | | | Wagombea | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wanaume | Wanawake | Jumla | % K | Wanaume | Wanawake | Jumla | % K |
| ACT-Wazalendo | 189 | 19 | 208 | 9.1 | 109 | 10 | 119 | 8.4 |
| CCM | 1071 | 97 | 1168 | 8.3 | 254 | 29 | 283 | 10.2 |
| CHADEMA | 475 | 75 | 550 | 13.6 | 148 | 14 | 162 | 8.6 |
| CUF | 182 | 20 | 202 | 9.9 | 57 | 8 | 65 | 12.3 |
| NCCR-Mageuzi | 20 | 5 | 25 | 20.0 | 16 | 5 | 21 | 23.8 |
| Total | 1937 | 216 | 2,153 | 10.0 | 584 | 66 | 650 | 10.2 |

Kama inavyoonyeshwa kwenye Jedwali 5-1, vyama havikuwa na idadi sawa ya watia nia wala wagombea. Ripoti za waangalizi wa TEMCO zinaonesha kuwa baadhi ya vyama havikuwasimamisha wagombea kwenye majimbo yote. Hata hivyo, CCM ilikuwa na wagombea kwenye majimbo yote, ikifuatiwa na CHADEMA. Hii inategemea nguvu za chama na uwezo wake wa kuwahamasisha wanachama kugombea nafasi za uongozi kwenye uchaguzi. Ushiriki wa wanawake kama wagombea majimboni haukuwa mzuri. Hii inaamanisha kuwa juhudi zinahitajika kuwawezesha wanawake kuona haja na kujenga shauku ya kushindania nafasi za uongozi. Kiulinganifu, CCM na CHADEMA vilipata idadi kubwa ya watia nia wanawake, ambapo CCM ilipitisha idadi kubwa ya wanawake kushinda vyama vingine vya siasa.

Kwa uteuzi wa viti vya udiwani, idadi ya wanachama waliojitokeza ilikuwa nzuri. Hata hivyo, idadi ya watia nia wanawake ilikuwa ndogo ikilinganishwa na idadi ya wanaume. Ni asilimia 10 tu ya watia nia walikuwa wanawake, kama inavyoonyeshwa kwenye Jedwali 5-2

*Jedwali 5-2: Idadi ya Watia nia na Wagombea kwenye Uchaguzi wa Madiwani*

| Chama cha Siasa | Watiania | | | | Wagombea | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wanaume | Wanawake | Jumla | % K | Wanaume | Wanawake | Jumla | % K |
| ACT-Wazalendo | 876 | 95 | 971 | 9.8 | 582 | 52 | 634 | 8.2 |
| CCM | 5,916 | 694 | 6,610 | 10.5 | 1,130 | 203 | 1,333 | 15.2 |
| CHADEMA | 2,952 | 293 | 3,245 | 9.0 | 1,456 | 134 | 1,590 | 8.4 |
| CUF | 896 | 126 | 1,022 | 12.3 | 568 | 153 | 721 | 21.2 |
| NCCR-Mageuzi | 154 | 12 | 166 | 7.2 | 97 | 8 | 105 | 7.6 |
| Total | 10,794 | 1,220 | 12,014 | 10.2 | 3,833 | 550 | 4,383 | 12.5 |

Chanzo: Ripoti za Waangalizi wa TEMCO

Kama ilivyoonekana kwenye uteuzi wa wagombea ubunge, CCM na CHADEMA vilipata watiania wengi na walipitisha wagombea wengi zaidi ya vyama vingine. Kwa ujumla, vyama vyote ndani ya UKAWA vilikuwa na watiania wachache wa viti vya udiwani (4,433) kuliko CCM ambacho kilikuwa na watiania 6,610. Kwa ujumla, vyama vya UKAWA viliwapitisha watiania wengi zaidi (2,416) ikilinganishwa na CCM ambayo ilipitisha watiania 1,333. Kwa uteuzi wa wanawake kwa nafasi ya viti maalum, CCM iliwavutia watiania wengi kuliko vyama vingine vinne (UKAWA). Hata hivyo, ACT-Wazalendo iliwapitisha wanawake wengi zaidi (52.4%), ikifuatiwa na CHADEMA (48.3%), NCCR-Mageuzi ikibaki nyuma kwa idadi (53) na kwa asilimia pia (asilimia 15 tu).

***Jedwali 5-3: Idadi ya Watiania na Wagombea wa Viti Maalum***

| Chama cha Siasa | Watiania | Wagombea | Wagombea % |
|---|---|---|---|
| ACT-Wazalendo | 315 | 165 | 52.4 |
| CCM | 1,909 | 788 | 41.3 |
| CHADEMA | 1,306 | 631 | 48.3 |
| CUF | 380 | 174 | 45.8 |
| NCCR-Mageuzi | 53 | 8 | 15.1 |
| Total | 3,963 | 1,766 | 44.6 |

Chanzo: Ripoti za Waangalizi wa TEMCO

### *5.4.1 Chama Cha Mapinduzi*

Uteuzi wa wagombea ndani ya CCM ulifanywa kwa kufuata taratibu za chama ili kuhakikisha kuwa watiania wamekidhi vigezo vilivyowekwa na chama, yaani *Kanuni za Uongozi na Maadili Toleo la Mwaka 2012*. Miongoni mwa vigezo vingine, kanuni hujumuisha kura za maoni, mchujo na uteuzi wa majina ya watiania kabla ya kupeleka majina ya watiania walioshinda kwenye ngazi za juu kwa ajili ya kufanyiwa maamuzi na kupitishwa. Mbio za uteuzi kwenye nafasi za ubunge ndani ya CCM zilikuwa na ushindani mkali. Jumla ya watiania 2,721, ambapo 781 (asilimia 28.7) kati yao walikuwa wanawake, walichukua fomu za kugombea ubunge kwenye majimbo 265. Umri wa watiania ulikuwa kama ifuatavyo; (i) 620 (22.8%) walikuwa na umri wa miaka 21-40 (ii) 1,775 (65.2%) miaka 41-60 (iii) 326 (12.0%) miaka 61 na kuendelea.

Baada ya kura za maoni, Halmashauri Kuu ya CCM iliyapitia na hatimaye kupitisha majina ya wagombea wa chama kwa nafasi za Ubunge, Agosti 2015. Hata hivyo, Halmashauri Kuu iliagiza kurudiwa kwa kura za maoni kwa baadhi ya majimbo kutokana na uvunjaji wa kanuni ikiwa ni pamoja na shutuma za rushwa, ukiukwaji wa taratibu za uteuzi na wizi wa kura. Ukiukwaji wa taratibu ulibainika kwenye majimbo tisa ya uchaguzi, ambayo ni Ukonga, Kilolo, Makete, Rufiji, Namtumbo, Mbinga Vijijini, Kiteto, Singida Mashariki and Busega.
Baadhi ya watiania walioongoza kwenye kura za maoni walitupiliwa mbali na Halmashauri Kuu na badala yake mshindi wa pili au wa tatu alipitishwa na chama kuwa mgombea. Mfano, katika jimbo la Muhambwe, Atashasta Ndite ambaye alikuwa mshindi wa tatu kwa kura 1,937 alipitishwa badala ya Jamal Tamimu aliyeongoza kwa kishindo kwenye kura za maoni kwa kujizolea kura 9, 592 na Emmanuel Gwegenyeza ambaye alimfuata kwa kura 2, 910. Vile vile, Mboni Mhita ambaye alikuwa mshindi wa pili kwa John Sallu kwenye kura za maoni katika jimbo la Pangani Vijijini, alinufaika na mchujo wa Halmashauri Kuu ambao ulimpatia tiketi ya uteuzi. Halmashauri Kuu iliagiza kurudiwa kwa kura za maoni Busega kutokana na shutuma za wizi wa kura.

### *5.4.2 Uteuzi wa Madiwani*

CCM iliandaa ratiba ya uchaguzi iliyoonesha hatua mbalimbali za zoezi la uteuzi. Pia, maelekezo juu ya utaratibu wa uteuzi yalitolewa.Watiania walipaswa kukidhi vigezo vinne ili kuweza kupitishwa kugombea kwenye uchaguzi wa udiwani; (i) kulipa shilingi 50,000 wakati wa kurudisha fomu za uteuzi, (ii) uwezo wa kugharamia kampeni, (iii) kuheshimu maadili ya

CCM na mwongozo wa uchaguzi, (iv) kudhaminiwa na wanachama. Vile vile kila mtiania alitakiwa kuchangia kifedha kwenye uendeshaji wa kura za maoni. Kiasi kiliamualiwa na wilaya na hakukuwa na kiasi kilitofautiana kwa sehemu na sehemu. Kibaha, watiania wa nafasi ya udiwani walilipa shilingi 300,000 kama mchango wao kugharamia kura za maoni.

Kura za maoni zilitumika katika zoezi la kuwachuja wagombea na kama njia ya kusaidia mamlaka za juu ndani ya CCM kufanya maamuzi. Hata hivyo kuongoza kwenye kura za maoni haikuwa kigezo pekee kuhalalisha kupitishwa moja kwa moja. Katika kata za Isanga na Malambo, jimbo la Bariadi CCM iliwapitisha wagombea walioshika nafasi ya pili kwenye kura za maoni. Hivyo hivyo, katika jimbo la Busega, mshindi wa kwanza kata ya Malili aliondolewa kwa sababu kipindi anachukua fomu ya uteuzi bado alikuwa mtumishi wa umma katika Wizara ya Mifugo. Kwa jimbo la Mtwara Mjini, maamuzi ya kamati ya siasa ya mkoa kuwapitisha wagombea walioshika nafasi ya pili na ya tatu kwenye kura za maoni yalitupiliwa mbali na Kamati Kuu ya CCM baada ya kupokea rufaa. Hivyo, walioshinda kwenye kura za maoni walirejeshewa ushindi wao.Baadhi ya watiania ambao hawakuridhika na uendeshaji wa zoezi la uteuzi waliamua kuhamia vyama vingine. Aliyekuwa diwani wa kata ya Mzinga, jimbo la Morogoro Mjini alihamia CUF, na kupitishwa kugombea udiwani kata ya Kiwanja cha Ndege na hatimaye alishinda.

### *5.4.3 Chama cha Wananchi (CUF)*
CUF iliwapitisha wagombea wake wa nafasi za ubunge na udiwani kwa utaratibu ulio wazi na shindani kwa kiasi fulani hasa kwa upande wa Zanzibar. Hatua ya kwanza ya zoezi la uteuzi ilikuwa ni kutangaza nafasi mbalimbali za kugombaniwa. Zoezi liliambatana na mwaliko kwa wanachama wenye nia ya kuchukua fomu za uteuzi kutoka katika ofisi za chama wilaya. Majina ya watiania yalichujwa na majina matatu yalipelekwa kwenye Baraza la Taifa la chama kwa maamuzi ya mwisho na upitishaji. Baada ya hapo kura za maoni zilifanywa na matokeo yalitumwa kwa Baraza la Taifa.

Kwa upande wa Zanzibar, mbali na kura za maoni, utaratibu mwingine ulitumika kuwachuja wagombea. Zoezi lilianza kwa makao makuu kupokea maombi ya watiania ambayo yaliambatanishwa na wasifu (CV) wa mtiania. Timu ya wataalamu ilipewa kuwasaili na kuwapa alama. Watiania watatu walichaguliwa na majina yao yalitumwa ngazi ya wilaya ili kupigiwa kura za maoni. Watiania wa nafasi ya udiwani walipaswa kulipa ada uteuzi shilingi 5,000.

### *5.4.4 CHADEMA*
CHADEMA iliandaa waraka ambao ulitoa vigezo vitakavyotumika katika uteuzi wa wagombea ubunge na udiwani. Miongoni mwa mambo mengine, waraka huu uliwataka viongozi wa chama kujiepusha na vitendo vya rushwa na matumizi yeyote mabaya ya madaraka wakati wote wa uendeshaji wa zoezi la kura za maoni kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka 2015. Licha ya kuzingatia vigezo vyote kulingana na sheria za uchaguzi, waraka huu wa chama uliweka vigezo vifuatavyo ili vitumike kupata wapeperusha bendera wake: Uzoefu wa uongozi ndani ya chama;Uhusiano mzuri na viongozi wengine ndani ya chama; (i) uadilifu katika uongozi wa kisiasa na kijamii; (ii) uwezo wa kumudu majukumu ya nafasi anayoomba;

(iii) uwezo wa kushirikiana na wengine kutimiza majukumu husika; (iv)uelewa wa malengo, itikadi na falsafa ya chama; (v) awe mwanachama hai katika tawi la chama atokalo, na (vi) uwezo wa kusoma na kuandika kwa Kiswahili au Kiingereza

Uteuzi wa nafasi za ubunge na udiwani ndani CHADEMA uliendeshwa kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza ilijumuisha majimbo ambayo hayakuwa na wabunge wala madiwani wa CHADEMA. Zoezi hili lilifanyika mapema, yaani kuanzia tarehe 18 hadi 25 Mei 2015. Awamu ya pili ilihusisha majimbo ambayo yalikuwa na wabunge wa CHADEMA, na zoezi la uteuzi lilianza mwezi Julai 2015. CHADEMA iliendesha utaratibu wa kura za maoni kwa watiania wa nafasi za ubunge na udiwani kwa majimbo mengi. Halmashauri Kuu ndiyo ilihusika kupitisha wagombea.

Halmashauri Kuu haikutegemea tu matokeo ya kura za maoni katika kufanaya maamuzi ya mwisho ya uteuzi. Kwa mfano, Kwa mfano, mshindi wa kura za maoni Magu (aliyejulikana kwa jina la Dkt. Msuka) ambaye alipata kura 162 alikataliwa na Halmashauri Kuu na badala yake Bw. Ngongoseke Julius Kalwinzi, ambaye alipata kura 84 akapitishwa. Hii ilitokana na pingamizi lilofikishwa Halmashauri Kuu na washindani wake kuwa alitumia rushwa kununua kura. Vile vile, katika jimbo la Bunda Mjini mwenyekiti wa CHADEMA mkoa alimpitisha Bi. Esther Bulaya ambaye alipata kura 37 kuwa mgombea ubunge badala ya Pius Masumin aliyeongoza kwa kura 65 katika uchaguzi wa kura za maoni.

Uamuzi wa kuhamia vyama vingine kama njia ya kupinga maamuzi ya uteuzi ndani ya chama ulibainika. Hassan Majaribu, jimbo la Nanyumbu alihamia CUF alidai kuwa aliahidiwa kwamba angekuwa mgombea pekee lakini aligundua kuwa watiania wengine walikuwa wanachukua fomu za uteuzi pia. Alipitishwa na CUF kuwa mgombea.

### *5.4.5 Uteuzi wa Udiwani*

Kwa ujumla, uteuzi wa wagombea udiwani ndani ya chama haukuwa na matatizo makubwa. Utaratibu wa uteuzi wa chama ulifuatwa vema isipokuwa kwa baadhi ya maeneo. CHADEMA ilifuta matokeo ya kura za maoni katika kata ya Matelea na Msamala Jimbo la Songea Mjini kufuatia tuhuma za rushwa na tetesi kuwa walioongoza kura za maoni ‘walipandikizwa’ na CCM ili kukihujumu chama. Katibu wa CHADEMA wilaya ya Songea Mjini alidai kuwa wale walioshindwa walifadhiliwa na CCM na walikuwa na mpango wa kujitoa kwenye mchakato (kusaliti chama). Mkoani Morogoro, mwanachama wa CHADEMA ambaye hakupitishwa katika kata ya Boma alihamia ACT-Wazalendo na kupitishwa.
Muungano wa Vyama Vinne

Tarehe 26 Oktoba 2014, vyama vinne vya upinzani; CHADEMA, CUF, NCCR-Mageuzi na NLD vilikubaliana kusimamisha mgombea mmoja kwa nafasi ya urais, ubunge, uwakilishi na udiwani kwa uchaguzi mkuu wa mwaka 2015. Hili lilikuwa jambo jipya kwa siasa za uchaguzi nchini Tanzania ambapo kwa sasa sheria hairuhusu vyama kuungana kwa lengo la kushinda uchaguzi. Vigezo vilivyotumika kugawanya majimbo miongoni mwa vyama vya umoja wa UKAWA ni pamoja na; (i) idadi ya viti vya udiwani katika jimbo, (ii) nguvu ya chama katika maeneo husika, (iii) utamaduni na desturi za eneo husika, na (iv) sifa binafsi za watiania.

Kufuatia makubaliano yaliyofanyika kila chama shirika cha UKAWA kilipangiwa idadi ya majimbo kwa uchaguzi wa wabunge na madiwani. Kati ya majimbo 264, CHADEMA ilipangiwa majimbo 138 (54.3%); CUF ilipangiwa majimbo 99 (39.0%); NCCR-Mageuzi 14 (5.5%); na NLD ilipangiwa majimbo 3 (1.2%).

Hata hivyo makubaliano ya kusimamisha mgombea mmoja wa ubunge hayakuheshimiwa katika majimbo 26, kama inavyooneka kwenye Jedwali 5-4

***Jedwali 5-4: Majimbo ambayo Makubaliano ya UKAWA Hayakuheshimiwa***

| S/No. | Jimbo | Vyama |
|---|---|---|
| 1 | Biharamulo Magharibi | CUF na CHADEMA |
| 2 | Bukoba Vijijini | CUF na CHADEMA |
| 3 | Jimbo | Vyama shirika vya ukawa vyenye wagombea |
| 4 | Geita | CUF na CHADEMA |
| 5 | Geita Mjini | CHADEMA and CUF |
| 6 | Handeni Vijijini | CUF na CHADEMA |
| 7 | Itilima | CUF na CHADEMA |
| 8 | Kibaha Vijijini | CUF na CHADEMA |
| 9 | Kilosa Kati | CUF na CHADEMA |
| 10 | Korogwe Vijijini | CUF na CHADEMA |
| 11 | Korogwe Mjini | CUF, CHADEMA na NCCR-Mageuzi |
| 12 | Kwimba | CUF na CHADEMA |
| 13 | Magu | CUF na CHADEMA |
| 14 | Mkinga | CUF na CHADEMA |
| 15 | Mtama | CUF na CHADEMA |
| 16 | Muleba Kusini | CHADEMA na NCCR-Mageuzi |
| 17 | Mwanga | CHADEMA na NCCR-Mageuzi |
| 18 | Ngara | CHADEMA na NCCR-Mageuzi |
| 19 | Nkenge | CUF na CHADEMA |
| 20 | Nyamagana | CUF na CHADEMA |
| 21 | Nzega Vijijini | CUF na CHADEMA |
| 22 | Segerea | CUF na CHADEMA |
| 23 | Singida Magharibi | CUF na CHADEMA |
| 24 | Solwa | CUF na CHADEMA |
| 25 | Ubungo | CUF na CHADEMA |
| 26 | Ukonga | CUF na CHADEMA |

Chanzo: Ripoti za Waangalizi waTEMCO, 2015

Kushindwa kwa vyama shirika vya UKAWA kuheshimu makubaliano ilikuwa Baraka kwa CCM, angalau kwa jimbo la Segerea na Mwanga. Kama makubaliano yangeheshimiwa, Julius Mtatiro wa CUF alikuwa na nafasi kubwa ya kushinda katika jimbo la Segera ambapo alipata kura 75,744 dhidi ya Bonna Kalua wa CCM aliyepata kura 94,640 dhidi ya Anatropi wa CHADEMA aliyepata kura 48,623. Ni dhahiri kuwa Mtatiro angepata kura 124,367. Kwa upande mwingine uchaguzi wa marudio ungefanyika Mwanga kwani Kileo wa CHADEMA

alipata kura 17,366 na Msuya wa NCCR-Mageuzi alipata kura 4,616, ambazo kwa jumla ni kura 21,982 dhidi ya Jumanne Maghembe wa CCM ambaye alipata idadi sawa ya kura.

### 5.5 Uteuzi wa Wabunge na Madiwani ndani ya Vyama Vingine

Kwa sehemu kubwa vyama vingine ikiwa ni pamoja na washiriki wapya katika uchaguzi mkuu, kama ADC na ACT-Wazalendo, waliwapitisha wagombea wao bila mchujo. Kwa TLP, DP, CUF, na ACT-Wazalendo, watiania ama 'walijitolea' au waliomba uteuzi.

### 5.6 Malalamiko Juu ya Uteuzi

Malalamiko mengi yalighubika zoezi la uteuzi ndani ya vyama kwa uchaguzi mkuu wa mwaka 2015. Utazamaji wa TEMCO katika majimbo 150 umebaini kuwa majimbo 73 yalikuwa na malalamiko juu ya uteuzi kwenye nafasi ya ubunge; (i) CCM (46), (ii) CHADEMA (19), (iii) CUF (4), na (iv) ACT-Wazalendo (4) kama inavyoonyeshwa kwenye Jedwali 5-5

***Jedwali 5-5: Malalamiko juu ya teUuzi wa Wagombea Ubunge ndani ya Vyama***

| Chama cha Siasa | Marudio (%) | | |
|---|---|---|---|
| | Ndiyo | Hapana | Hakuna Jibu |
| ACT-Wazalendo | 4 (2.7) | 111 (74.0) | 35 (23.3) |
| CCM | 46 (30.7) | 88 (58.7) | 16 (10.7) |
| CHADEMA | 19 (12.7) | 97 (64.7) | 34 (22.7) |
| CUF | 4 (2.7) | 80 (53.3) | 66 (44) |

Chanzo: Ripoti za Waangalizi wa TEMCO, 2015

Kama inavyooneshwa kwenye Jedwali 5-6, CCM ilikuwa na malalamiko mengi zaidi ikifuatiwa na CHADEMA

***Jedwali 5-6: Malalamiko juu ya Uteuzi wa Wagombea Ubunge ndani ya Vyama***

| Political party | Frequency (%) | | |
|---|---|---|---|
| | Yes | No | No response |
| ACT-Wazalendo | 4 (2.7) | 105 (70) | 41 (27.3) |
| CCM | 44 (29.3) | 90 (60) | 16 (10.7) |
| CHADEMA | 27 (18) | 89 (59.3) | 34 (22.7) |
| CUF | 7 (4.7) | 70 (46.7) | 73.48.7) |

Chanzo: Ripoti za Waangalizi wa TEMCO, 2015

Vile vile, kwenye zoezi la uteuzi wa madiwani ndani ya vyama CCM ilikuwa na malalamiko mengi ikifuatiwa na CHADEMA. Hali hii inathibitisha dhana kuwa malalamiko huongezeka kulingana na ukubwa wa chama. Utazamaji wa TEMCO juu ya zoezi la uteuzi ndani ya vyama katika majimbo 150 umetolewa kwa ufupi kwenye

Jedwali 5-7

*Jedwali 5-7: Malalamiko juu ya Uteuzi ndani ya Vyama*

| Chama cha Siasa | Ubunge (%) | | | Udiwani (%) | | | Viti Maalum (%) | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Ndiyo | Hapana | Hakuna Jibu | Ndiyo | Hapana | Hakuna Jibu | Ndiyo | Hapana | Hakuna Jibu |
| ACT-Wazalendo | 4 (2.7) | 111 (74) | 35 (23) | 4 (2.7) | 105 (70) | 41 (27.3) | 5 (3.3) | 103 (68.7) | 42 (28.0) |
| CCM | 46 (30.7) | 88 (58.7) | 16 (10.7) | 44 (29.3) | 90 (60) | 16 (10.7) | 23 (15.3) | 108 (72) | 19 (12.7) |
| CHADEMA | 19 (12.7) | 97 (64.7) | 34 (22.7) | 27 (18) | 89 59.3) | 34 (22.7) | 10 (6.7) | 103 (68.7) | 37 (24.7) |
| CUF | 4 (2.7) | 80 (53.3) | 66 (44) | 7 (4.7) | 70 (46.7) | 73 (48.7) | 1 (0.7) | 78 (52.0) | 71 (43.7) |

Chanzo: Ripoti za Waangalizi wa TEMCO, 2015

## 5.7 Hama-hama ya Wanachama baina ya Vyama

Moja ya mambo yaliyojitokeza katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 ni hama-hama ya wanachama maarufu, wagombea na hata viongozi wa chama. Kulikuwa na aina mbili za hama-hama; kabla na baada ya uteuzi/kura za maoni. Mbali na hama-hama za baada ya uteuzi ndani ya vyama kulikuwa na hama-hama chache kabla ya zoezi la uteuzi. Mbunge machachari James Lembeli (Kahama) na wenzake wawili; Zakaria Soko na Bobson Shaban Wambura walihamia CHADEMA na ACT-Wazalendo, mtawalia majuma machache kabla mchakato wa uteuzi kuanza ndani ya CCM. Vile vile, aliyekuwa mwanachama wa CHADEMA, jimbo la Shinyanga Mjini, Bw. Kaheza Shilungushera alihamia ACT-Wazalendo. Hama-hama nyingi zilishuhudiwa baada ya uteuzi ndani ya vyama. Hama-hama ya wanachama ilisababishwa na mambo mbalimbali ambayo yamebainishwa na Waangalizi wa TEMCO kama inavyoonyeshwa kwenye Jedwali 5-8

*Jedwali 5-8: Mambo yaliyosababisha hama-hama*

| SN | Sababu | Ndiyo | Hapana | Hakuna Jibu |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ukosefu wa demokrasia ndani ya chama. | 67 (44.7%) | 27 (18%) | 56 (37.3%) |
| 2 | Migogoro ndani ya chama | 52 (34.7%) | 35 (23.3%) | 63 (42.0%) |
| 3 | Kutokuwa na uhakika wa kuchaguliwa tena. | 35 (23.3%) | 44 (29.3%) | 71 (47.3%) |
| 4 | Kutoridhia umoja/muungano wa vyama | 19 (12.7%) | 53 (35.3%) | 78 (52.0%) |
| 5 | Ushawishi wa watu mashuhuri waliohamia vyama vingine | 34 (22.7%) | 41 (27.3%) | 75 (50.0%) |
| 6 | Sababu za kiitikadi | 15 (10.0%) | 55 (36.7%) | 80 (53.3%) |
| 7 | Sababu nyingine | 10 (6.7%) | 41 (27.3%) | 98 (65.3%) |

Chanzo: Ripoti za Waangalizi wa TEMCO, 2015

Kama inavyoonyeshwa kwenye Jedwali 5-8 hakuna sababu moja amabayo kwa peke yake inatosheleza kuelezea hama-hama. Hata hivyo, migogoro na ukosefu wa demokrasia ndani ya vyama inaonekana kuwa sababu kuu. Uchunguzi unaonesha kuwa tofauti za kiitikadi hazikuwa sababu za muhimu kusababisha hama-hama.

Kufuatia kukamilika kwa zoezi la uteuzi ndani ya vyama vikubwa vinne, baadhi ya watiania hasa wale walioshindwa walihamia vyama vingine. Hama-hama haikuwa kwa mwelekeo mmoja tu. Kulikuwa na hama-hama za namna tofauti; (i) chama tawala kwenda upinzani (ii) upinzani kwenda chama tawala (iii) chama tawala-upinzani-chama tawala (iv) upinzani kwenda upinzani. Mfano, katika jimbo la Vwawa, ACT-Wazalendo ndiyo ilipokea wahamiaji wengi kutoka CCM na CHADEMA. Katika wilaya ya Mbozi, kulikuwa na hama-hama nyingi kutoka CHADEMA kwenda ACT-Wazalendo. Katibu wilaya wa CHADEMA Mbozi, Bw. Michael Mwamlima, alithibitisha kuwa hama-hama nyingi zilikuwa katika ngazi ya kata.

Utazamaji wa TEMCO umebaini kuwa uteuzi wa wagombea ndani ya vyama vingi haukukidhi vigezo vya kidemokrasia. Mitindo minne ya uteuzi ilitumika; (i) Uteuzi bila Mchujo ( yaani usiohusisha kura za maoni), (ii)Uteuzi kwa Kupitia Maombi (iii)Uteuzi wa Kusubiri Watakaohama (iv)Uteuzi wa ushirikishwaji/demokrasia kiasi (v)Mtindo wa Kidemokrasia/Ushirikishwaji. Uteuzi bila mchujo ulifanyika pale ambapo viongozi wa vyama vya siasa walifanya uamuzi binafsi kuwateau watu 'waliowataka' wagombee. Mtindo huu wa uteuzi ulitumiwa na vyama vidogo, hasa vile visivyo na viti bungeni na kwenye baraza la madiwani, vina ofisi Dar es Salaam tu na kwenye mikoa michache sana.

Mtindo wa uteuzi kwa kupitia maombi ulikuwa mtindo mpya ambapo baadhi ya vyama hasa vile vidogo viliwaalika watu wenye nia ya kugombea kuchukua fomu za uteuzi na kukiwakilisha chama kwenye nafasi mbalimbali kwenye uchaguzi kwa ngazi za jimbo na kata. Uteuzi wa kusubiri watakaohama ulitumiwa na baadhi ya vyama vya siasa kutoa fursa kwa viongozi mashuhuri walioshindwa kupata uteuzi ndani ya vyama vyao. Mtindo huu ulitumiwa na vyama shirika vya UKAWA na kwa namna fulani ulikiuka nguzo muhimu ya uteuzi wa kidemokrasia. Mtindo wa uteuzi wa demokrasia kiasi ulikuwa na sura ya ushirikishwaji lakini bado viongozi wa vyama walikuwa na maamuzi ya mwisho. Mtindo huu "ulitumiwa kwa kiasi kikubwa na chama tawala na CUF, hasa kwa upande wa Zanzibar ambapo wanachama wenye nia walikaribishwa kueleza nia zao za kutaka uteuzi wa chama kugombea nafasi mbalimbali, ikiwemo ya urais. Uteuzi uliendeshwa kwa kuzingatia sifa za wagombea kulingana na vigezo vya uteuzi vilivyowekwa na chama.

Baadhi ya vyama vya siasa viliamua kutumia taratibu zisizo za kidemokrasia pengine kwa sababu sheria ya vyama vya siasa nchini Tanzania hairuhusu vyama kuungana au kushirikiana wakati wa uchaguzi. Kwa ujumla, utazamaji wa TEMCO unadhihirisha kuwa hata baada ya miaka 23 sasa, vyama vya siasa nchini Tanzania bado havijaweza kujibadilisha kuwa taasisi za kidemokrasia na havijatimiza kikamilifu moja ya majukumu yao muhimu ambayo ni kulea na kuandaa viongozi. Aidha, kasi yao ya kujenga na kuimarisha demokrasia ya ndani ni ndogo.
Utazamaji wa TEMCO kwenye majimbo 150 unaonesha kuwa mtindo wa demokrasia kiasi ulitumiwa hasa na CCM kwenye majimbo 133 (88.7%), ikifuatiwa na CHADEMA kwenye

majimbo 88 (39.3%) na ACT-Wazalendo kwenye majimbo 48 (32%). Mitindo iliyotumiwa na vyama kupata wagombea inaonyeshwa kwenye Jedwali 5-9.

***Jedwali 5-9: Mitindo ya Uteuzi***

| Chama cha Siasa | Mtindo wa Uteuzi | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kidemokrasia | | | Bila Mchujo | | |
| | Ndiyo | Hapana | Hakuna Jibu | Ndiyo | Hapana | Hakuna Jibu |
| ACT-Wazalendo | 48 (32%) | 72 (48%) | 30 (20.0%) | 58 (38.7%) | 61 (40.7%) | 31 (20.7%) |
| CCM | 133 (88.7%) | 12 (8.0%) | 5 (3.3%) | - | - | - |
| CHADEMA | 88 (58.7%) | 33 (22.0%) | 29 (19.3%) | 18 (12%) | 99 (66%) | 33 (22%) |
| CUF | 59 (39.3%) | 36 (24.0%) | 55 (36.7%) | 14 (9.3%) | 79 (52.7%) | 57 (38.0%) |

Chanzo: Ripoti za Waangalizi wa TEMCO

Vile vile matumizi ya mtindo wa demokrasia kiasi na uteuzi bila mchujo yalionekana kwenye uteuzi wa wagombea wa viti maalum kama inavyoonyeshwa kwenye Jedwali 5-10.

***Jedwali 5-10: Uteuzi wa Wanawake kwa Viti Maalum***

| Chama cha Siasa | Mtindo wa Kidemokrasia (%) | | | Uteuzi Bila Mchujo (%) | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Ndiyo | Hapana | Hakuna Jibu | Ndiyo | Hapana | Hakuna Jibu |
| ACT-Wazalendo | 31 (20.7) | 61 40.7) | 58 (38.7) | 43 (28.7) | 47 (31.3) | 60 (40.0) |
| CCM | 124 (82.7) | 17 (11.3) | 9 (6.0) | 0 | 0 | 0 |
| CHADEMA | 90 (60.0) | 31 (20.7) | 29 (19.3) | 13 (8.7) | 100 (66.7) | 37 (24.7) |
| CUF | 49 (32.7) | 40 (26.7) | 61 (40.7) | 18 (12.0) | 65 (43.3) | 67 (44.7) |

Chanzo: Ripoti za Waangalizi wa TEMCO

## 5.8 Uteuzi wa NEC

Vyama kumi na tatu (13) vilichukua fomu za uteuzi wa nafasi ya urais kutoka Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Tume ilitenga siku 21 (tarehe 1 hadi 21 Agosti, 2015) kwa ajili ya kuchukua na kurudisha fomu. Wagombea urais walipaswa kutimiza masharti mbalimbali ya sheria za uchaguzi, kama kuwa na wadhamini wasiopungua mia mbili (200) ambao ni wapigakura walioandikishwa kutoka mikoa kumi ya Tanzania, mbili kati yake kutoka Zanzibar; kulipa dhamana ya shilingi milioni moja (1,000,000/=) na kuwasilisha kiapo cha kisheria. Hadi kufika saa kumi alasiri, tarehe 21 Agosti 2015, ni vyama 9 tu kati ya 13 ndivyo vilivyoweza kurudisha fomu kwa muda uliopangwa (yaani kati ya saa moja na nusu asubuhi hadi saa kumi kamili alasiri). Vyama hivyo ni CHADEMA, CCM, TLP, ADC, UPDP, CHAUMMA, ACT-WAZALENDO, NRA na ADA-TADEA.

CHAUSTA na DP hawakurudisha fomu za uteuzi. CCK na ADA-TADEA walirudisha fomu ingawaje walishindwa kutimiza masharti yote. Fomu na.8 ya CCK haikuwa na majina ya wadhamini kama ambavyo sheria inaagiza. Kwa upande mwingine, mgombea urais wa ADA-

TADEA hakula kiapo. Katika moja ya kioja, mgombea urais wa UPDP, Fahmi Dovutwa alikwama kwenye lifti kwa muda wa dakika kumi wakati akitoka kuchukua fomu za uteuzi katika ofisi za Tume ya Taifa ya Uchaguzi jijini Dar es Salaam. Alidhihaki chama tawala kwa kudai kuwa "tukio hilo halikuwa ajali bali lilipangwa na CCM." Majina ya wagombea urais na wagombea wenza wao waliosimama kuwakilisha vyama vyao kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 yanaonyeshwa kwenye Jedwali 5-11:

***Jedwali 5-11: Orodha ya Wagombea Urais wa Muungano na Wagombea Wenza***

| S/N | Chama cha Siasa | Mgombea Urais | Mgombea Mwenza |
|---|---|---|---|
| 1 | CHADEMA | Edward Ngoyai Lowassa | Juma Duni Haji |
| 2 | CCM | John Pombe Magufuli | Samia Suluhu Hassan |
| 3 | TLP | Macmillan Elifalio Lyimo | |
| 4 | ADC | Chief Lutalosa Yomba | Said Miraji Abdallah |
| 5 | UPDP | Fahmi Nassoro Dovutwa | Hamadi Mohammed Ibrahimu |
| 6 | CHAUMMA | Hashim Rungwe Spunda | Issa Abas Hussein |
| 7 | ACT-WAZALENDO | Anna Elisha Mghwira | Hamad Mussa Yussuf |
| 8 | NRA | Janken Malik Kasambala | Simai Abdulrah Abdulla |

Jumla ya wagombea ubunge 1,218 walipitishwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi. 233 (19.1%) kati yao walikuwa wanawake na wanaume 985 (80.9%). Aidha, Tume ilipitisha wagombea udiwani 10, 879, 679 (6.3%) kati yao ni wanawake na wanaume10, 191 (93.7%).

### 5.9 Pingamizi na Rufaa za Wagombea

Tume ilipokea rufaa 56 zilizowasilishwa na wagombea ubunge walioondolewa na wasimamizi wa vituo kwa sababu mbalimbali. Tume iliwarudisha wagombea ubunge 14. Tume ya Uchaguzi ilikataa rufaa 40, kwa maana kwamba ilikubaliana na uamuzi wa wasimamizi wa uchaguzi. Vile vile, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilipokea jumla ya rufaa 223 kutoka kwa wagombea udiwani walioondolewa na wasimamizi wa vituo. Tume iliwarudisha wagombea udiwani 50 waliokuwa wameondolewa na wasimamizi wa vituo kugombea na kuwaondoa 173.

### 5.10 Wagombea Waliopita Bila Kupingwa

Habari za wagombea ubunge waliopita bila kupingwa ni chache. Mkoani Mtwara, mgombea pekee aliyepita bila kupingwa ni Abdallah Daudi Chikota wa CCM jimbo la Nanyamba. Ukosefu wa upinzani dhidi ya mgombea wa CCM ulizungukwa na aina fulani ya maigizo. Mtazamaji wa TEMCO aliripoti tukio hivi:

Mazingira yaliyopelekea kukosekana kwa mpinzani wake (Chikota) ni ya kustaajabisha. Kwa mujibu wa taarifa kutoka kwa mamlaka husika mkoani humo, ikiwa ni pamoja na maafisa wa uchaguzi zinaeleza kuwa mgombea wa CUF aliyechukua fomu za uteuzi hakuzirudisha fomu hizo kwa msimamizi wa kituo siku ya mwisho ya urejeshaji fomu. Juhudi za viongozi wa CUF na wafuasi wao jimboni humo za kumtafuta mgombea huyo ili azirejeshe fomu hizo

hazikufanikiwa…kikundi cha watu -bila shaka wafuasi wa CUF, walienda nyumbani kwa mgombea wao ambapo hata hivyo hawakumkuta, kwa hasira waliamua kuchoma nyumba yake. Ni kata 10 zilikuwa na wagombea waliopita bila kupingwa katika majimbo 150 ambamo TEMCO ilikuwa na waangalizi wa muda mrefu. Kata hizo ni Kihungu, Kitanda, Mbinga Mhalule, Peramiho wilayani Mbinga; kata za Endonyong, Langa, na Terati katika mkoa wa Manyara; kata za Mkalama na Madege katika majimbo ya Gairo na Kilosa; kata ya Mmale katika jimbo la Igalula; na kata ya Zuzu jimbo la Dodoma Mjini.

### 5.11 Tathmini ya Zoezi Zima la Uteuzi

Tathmini ya jumla ya zoezi la uteuzi katika majimbo 150 ambayo yalikuwa na utazamaji wa TEMCO inaonyeshwa kwenye Jedwali 5-12

***Jedwali 5-12: Tathmini ya Zoezi la Uteuzi***

| Namna na Mtindo wa Uteuzi | Alama | Marudio | Asilimia |
|---|---|---|---|
| Uteuzi wa wagombea uligubikwa na mapungufu mengi. Kulikuweko upendeleo mkubwa, ukiukwaji wa taratibu na vitendo vya rushwa kiasi kwamba baadhi ya wagombea waliamua kujiondoa katika kura za maoni au waliweka pingamizi. Uteuzi umekuwa kama mimba iliyoharibika. | F (0%) | 0 | 0.00 |
| Uteuzi wa wagombea umevurugika au kuborongwa (mismanaged) kiasi kwamba inashindikana kwa wadau kuwakubali walioteuliwa. Ni kama mwanafunzi aliyefeli mtihani. | E (1-39%) | 0 | 0.00 |
| Uteuzi wa wagombea uligubikwa na dosari nyingi kutokana na ukiukwaji wa baadhi ya sheria, kanuni, na udhaifu wa kiuendeshaji na kuwepo kwa vitisho na upendeleo. | D (40-49%) | 5 | 3.51 |
| Uteuzi wenye kuruhusu wadau wote (vyama, wagombea, wapigakura) washiriki, lakini kukawepo matukio mengi ya kutokuzingatia sheria na kanuni za uchaguzi (na kutokuadhibiwa kwa hilo) na ukawepo upendeleo unaoathiri ushiriki au mafanikio ya baadhi ya wagombea. | C (50-59%) | 16 | 10.53 |
| Uteuzi ambao kwa jumla ni huru na wa haki, lakini bado kuna mapungufu ambayo hayakuweza kuathiri sudi za baadhi ya wadau (vyama, wagombea, wapigakura). | B (60-69%) | 68 | 45.61 |
| Uteuzi ambao, japo una mapungufu kadhaa, ni mapungufu ya kawaida na yasiyoweza kuathiri matokeo ya jumla ya wagombea uteuzi. Ni uteuzi safi, huru na wa haki. | A (80 – 100%) | 61 | 40.35 |
| Jumla | | 150 | 100 |

Chanzo: Ripoti za Waangalizi wa TEMCO, 2015

## 5.12 Hitimisho na Mapendekezo

### *5.12.1 Hitimisho*

Maoni ya TEMCO juu ya zoezi la uteuzi katika uchaguzi wa mwaka 2015, ni kwamba kwa ujumla uteuzi ulikuwa huru na wa haki lakini bado kulikuwa na kasoro chache. Vyama vikubwa hasa CCM na CHADEMA vilikuwa na utaratibu wa uteuzi unaoeleweka ambao kwa kiasi kikubwa umekidhi vigezo vya msingi vya uteuzi wa kidemokrasia. Hata hivyo, namna ambayo CHADEMA na vyama shirika vya UKAWA vimempitisha mgombea wao wa urais inazua maswali mengi. Uteuzi huo haukikidhi vigezo vya kidemokrasia. Vyama vingi vidogo havikutumia njia za demokrasia-shirikishi kupitisha wagombea wao.

Kwa upande wake Tume ya Taifa ya Uchaguzi iliendesha zoezi la uteuzi kwa mujibu wa sheria. Wasimamizi wa vituo waliwapa haki ya kukata rufaa wagombea ambao hawakuridhika. Waangalizi wa TEMCO walibaini kuwa Tume haikuzingatia rufaa ambazo zilikatwa kwa sababu ya makosa ya kawaida (kibinadamu). Waangalizi wa TEMCO hawakubaini manung'uniko yeyote baada ya Tume kuamua rufaa zilizokatwa. Tofauti na chaguzi zilizopita suala la wagombea kupita bila kupingwa halikuwa na nafasi kubwa kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka 2015. Hili ni jambo zuri katika kuhakikisha kuwa haki za kisiasa na kiraia zinaheshimiwa na kulindwa nchini Tanzania pamoja na kuhimiza ushindani na hamasa.

### *5.12.2 Mapendekezo*

Kutokana na utazamaji wa zoezi la uteuzi kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, tunapendekeza yafuatayo:

(i) Vyama vya siasa vichukue hatua kujenga na kuimarisha demokrasia ndani ya vyama ili kutoa mwanya kwa uteuzi wa kiushindani na wazi katika uchaguzi wa rais, wabunge na madiwani.

(ii) Serikali inashauriwa kufanya marekebisho ya sheria ili kuruhusu vyama kuungana na kusimamisha mgombea mmoja wa urais, ubunge na udiwani.

(iii) Sheria ya vyama vya siasa irekebishwe ili kuweke vigezo vya msingi vya kidemokrasia kwa ajili vyama kuvifuata wakati wa zoezi la uteuzi.

(iv) Vyama vya siasa vibanwe kisheria kushiriki vema kwenye uchaguzi kwa kuwasimamisha wagombea kwenye nafasi za uongozi katika ngazi zote.

(v) Utaratibu mzuri uliooneshwa na Tume katika kushughulikia rufaa na pingamizi unahitaji kukuzwa na kudumishwa.

# CHAPTER 6
# MWENENDO WA KAMPENI ZA UCHAGUZI

## 6.1 Utangulizi

Kampeni za uchaguzi ni kipengele muhimu cha mchakato wa uchaguzi wa Kidemokrasia kutoa nafasi kwa wagombea wa vyama vya siasa ya kuwafikia wapigakura kueleza ilani zao. Sura hii itajadili mwenendo wa kampeni za uchaguzi kwa ajili ya uchaguzi mwaka 2015. Sura imegawanywa katika sehemu kuu kumi kwa kuanza na utangulizi huu. Sehemu ya pili inajadili mifumo ya kisheria na kitaasisi kwa ajili ya kampeni za uchaguzi. Sehemu ya nne naya tano zinaelezea ufadhili wa kampeni ukifuatiwa na taratibu na mikakati ya kampeni. Sehemu ya sita na saba zinaelezea ilani ya uchaguzi na elimu ya wapigakura. Sehemu ya nane na ya tisa zinaelezea kuhusu taratibu za usalama katika mikutano ya kampeni na tathmini ya jumla ya mwenendo wa kampeni za uchaguzi.

## 6.2 Miongozo ya Kisheria na Kitaasisi kwa ajili ya Kampeni

Kampeni za kisiasa zinaongozwa na vyombo vikuu vitatu vya Kisheria na chombo kimoja cha ziada. Vyombo hivyo vikuu ni Sheria ya Taifa ya Uchaguzi Sura ya 343, Kifungu cha 124 (kitatumika kama Sheria ya Uchaguzi); Kanuni za Taifa za Uchaguzi za mwaka 2015 (zitatumika kama Kanuni); Na Sheria ya Gharama za Uchaguzi ya mwaka 2010 (itatumika kama Sheria ya Gharama za Uchaguzi). Chombo cha ziada ni Kanuni ya Maadili ya Uchaguzi, 2015 (itatumika kama Kanuni ya Maadili ya Uchaguzi wa mwaka 2015). Kanuni hii ya Maadili ya 2015 imetengenezwa chini ya kifungu cha 124A cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi ya mwaka 1985. Lengo kuu la vyombo hivi ni kuweka misingi ya mienendo ya kampeni za siasa ya amani na yenye ufanisi ili kuwa na uchaguzi huru na wa haki. Kwa mfano, huku kifungu cha 51(1) cha sheria ya uchaguzi kinatoa fursa sawa kwa wagombea na/au vyama vya kisiasa (au mawakala) kufanya kampeni, kifungu cha 21(1) cha Sheria ya Gharama za Uchaguzi kinazuia vitendo visivyo vya haki kama vile udhamini usio halali (rushwa, utoaji wa zawadi, ahadi, n.k). Hata hivyo, kuna mianya ya kufanya hayo kwa watu binafsi. Kifungu cha 21(2) kinaeleza kwamba "Itakapotokea mawakala au watu kwa niaba ya mgombea ndio waliofanya jambo lolote miongoni mwa hayo yaliyozuiwa, mgombea atalindwa kama atathibitisha kwamba hayo yamefanywa bila ya yeye kujua, au bila ya ridhaa au uthibitisho wake." Uchunguzi wa TEMCO unaonesha kuwa wagombea hutoa udhuru mbalimbali kuthibitisha kwamba vitendo vilivyozuiliwa (mf. rushwa) vilifanyika bila mgombea kujua wakati wa kampeni za uchaguzi.

Utekelezaji wa sheria za uchaguzi huwa na ufanisi zikihusisha taasisi nyingi zinazoelezwa na kanuni za kisheria. Taasisi hizi ni pamoja na: (a) Vyombo vya Utazamaji wa Uchaguzi, (b) Vyama vya siasa (c) Polisi. Mwenendo wa kampeni za uchaguzi za mwaka 2015 kwa ujumla zilichukuliwa kuwa bora na za amani. Kulikuwa na vyama vya siasa 22 vilivyoshiriki katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015. Takriban vyama vya siasa 6 viliweza kufanya kampeni za kisiasa kupitia utaratibu wa mikutano ya hadhara. Vyama viwili vya siasa miongoni mwa hivyo sita vilikuwa na ushindani mkubwa. Vyama hivyo vilikuwa CCM na CHADEMA.

## 6.3 Gharama za Kampeni

Gharama za kampeni zinaongozwa na Sheria ya Gharama za Uchaguzi. Kifungu cha 7(1) kinafafanua gharama za uchaguzi kama fedha zote zinazotumiwa au gharama zinazotumika

katika kufanyika na kuratibiwa kwa mchakato wa uteuzi, kampeni za uchaguzi, na chaguzi zinazofanywa na chama cha siasa, mgombea au serikali na inajumuisha gharama zote zinazohusu kampeni za uchaguzi. Utekelezaji wa Sheria ya Gharama za Uchaguzi una changamoto. Kuna mambo makuu matano yanayoufanya utekelezaji wa Sheria ya Gharama za Uchaguzi kuwa mgumu. Mambo hayo ni haya yafuatayo: - (a) Vyanzo vya fedha kwa ajili ya kampeni (b) Mipaka ya matumizi, (c) Utoaji wa taarifa za fedha, (d) namna ya uwajibikaji (e) mambo yanayokatazwa.

Kwanza, Chanzo cha msingi kimeelezwa wazi na Sheria ya Gharama za Uchaguzi. Kifungu cha 8(1) cha sheria kinaeleza kwamba, "kila chama cha kisiasa kinapaswa kufanya na kudhamini kampeni zake za uchaguzi kwa kutumia fedha zake kutoka vyanzo vilivyoelezwa chini ya kifungu cha sheria ya vyama vya siasa namba (13)1" Vyanzo vya fedha vinavyoelezwa na kifungu hiki ni hivi vifuatavyo;- Ada za uanachama; maslahi binafsi, michango binafsi, mapato ya uwekezaji wowote; mradi wowote ambao chama kina maslahi nao; ruzuku kutoka serikalini; michango na misaada kutoka vyanzo vyovyote. Zaidi ya hayo, kifungu cha 8(2) cha Sheria ya Gharama za Uchaguzi kinataja vyanzo vingine vya ziada vya fedha kwa ajili ya kampeni za uchaguzi. Kifungu kinaeleza kwamba, "Pamoja na vyanzo vilivyoelezwa katika sheria hii, mgombea anaweza kutumia fedha zake katika kipindi cha kampeni kama itaonekana kuwa ni muhimu au inahitajika kwa ajili ya kampeni za uchaguzi. Vyama vya siasa vilipokea misaada ya fedha na vitu kwa ajili ya kapeni za wagombea wao kama inavyooneshwa katika kifungu cha 8(1&2).

Hivyo, tarehe 18 Agosti 2015, Waziri Mkuu Mizengo Pinda alitoa agizo katika Gazeti la serikali akitaja kiwango cha gharama za uchaguzi kwa kujikita katika vigezo vilivyowekwa na sheria. Aliagiza shilingi za kitanzania bilioni 17 kuwa kiwango cha juu cha gharama za uchaguzi zinazopaswa kutumiwa na vyama vya siasa wakati wa kampeni za kisiasa. Kiwango cha juu kilichotumiwa na wagombea kinaonyeshwa katika Jedwali 6-1 hapo chini.

***Jedwali 6-1: Kiwango cha Juu cha Gharama ambacho Mgombea Anaweza Kutumia***

| Mgombea | Kigezo | Eneo | Kiwango cha juu |
|---|---|---|---|
| Urais | Aina ya Mgombea | HAKUNA | Bilioni 6 |
| Udiwani | Jiografia | A. Mjini | Milioni 4 |
| | | B. Kijijini | Milioni 6 |
| Ubunge | Idadi ya watu<br>Miundombinu ya Mawasiliano | A. Majimbo 60 kuanzia Ilala Dar hadi Kiwami Pemba | Milioni 33 |
| | | B. Mjimbo 53 kuanzia Chilonwa Dodoma hadi Ikungi Mkoa wa Singida | Milioni 44 |
| | | C. Majimbo 69 kuanzia maeneo ya Mtera Dodoma hadi Majimbo ya Singida Mashariki | Milioni 55 |
| | | D. Majimbo 43 kuanzia Bahi Dodoma hadi Madaba Mkoani Ruvuma | Milioni 66 |
| | | E. Majimbo 29 kuanzia Jimbo la Dodoma Mjini hadi Mtwara Vijijini Mkoani Mtwara | Milioni 77 |
| | | F. Majimbo 12 kuanzia Igunga hadi Mlimba Mkoani Morogoro | Milioni 88 |

Chanzo: Tangazo katika Gazeti la Serikali la tarehe 18 Agosti 2015

utekelezaji wa azma ya serikali juu ya gharama za uchaguzi halikuwa jambo rahisi. Kati ya 150 waangalizi wa muda mrefu wa TEMCO, ambao ni 117 (asilimia 78) walibainisha kwamba ilikuwa vigumu sana kwa wagombea na vyama kufichua kiasi cha fedha walichotumia katika kampeni za uchaguzi.

**6.4 Taratibu za Kampeni na Kanuni za Maadili**

Sheria inahitaji vyama vya siasa kuendesha kampeni za heshima. Sheria inabainisha yapi "wafanye" na yapi "wasifanye" wakati wa kampeni. Kati ya waangaliazi wa muda mrefu 150 waliokuwa katika majimbo ya uchaguzi, 27 (asilimia 18) waliona matukio ya vurugu, vitisho na uchochezi wakati wa kampeni. Matukio 8 kati ya matukio yote ya vurugu yalihusisha chama cha CCM na wagombea wake, hii ni sawa na asilimia 5.3; matukio 6 yalihusisha CHADEMA sawa na asilimia 4; na vyama vingine vilikuwa tukio moja tu, sawa na asilimia 0.7. Kwa ujumla waangalizi wa muda mrefu wa TEMCO walishuhudia wagombea na vyama vyao wakipeleka malalamiko yao juu ya matukio yapatayo 67 (asilimia 44.7) yahusuyo mapungufu mbalimbali katika kampeni ikiwamo vurugu.

Vyama vya siasa na wagombea wamekiuka Kanuni za Maadili kwa kiasi kikubwa. Ingawa Tume ya uchaguzi ilipiga marufuku matumizi ya vikundi vya usalama vya vyama vya siasa; maelekezo hayo hayakuzingatiwa na vyama husika. Matukio ya kuhusiana na uharibifu wa vifaa vya kampeni yalihusisha vyama vya CCM na CHADEMA. Katika mikutano ya kampeni ukiukwaji wa kanuni za maadili ulibainikakama ifuatavyo: (i) CCM (asilimia 48.7) na CHADEMA (asilimia 35.3). Matumizi ya ukabila katika mikutano ya kampeni ya CCM ilishuhudiwa na waangalizi wa muda mrefu 38 (asilimia 25.3).

Matumizi ya ukabila katika majimbo yalibainishwa na waangalizi wa muda mrefu 31 (asilimia 20.7). Matukio mengine yaliyoripotiwa na waangalizi hao yalikuwa upotoshaji wa taarifa na uongo. Kwa mfano: (i) CCM ilikuwa katika majimbo 30 (asilimia 20); (Ii) CHADEMA katika majimbo 25 (16.7 asilimia); (Iii) CUF katika majimbo 8 (asilimia 5.3). Pia matukio mengine yalikuwa uharibifu wa vifaa vya kampeni. Iliripotiwa kuwa katika mikutano ya kisiasa ya chama uharibifu wa vifaaulikuwa kama ifuatavyo: (i) CCM katika majimbo 73 (48.7 asilimia); CHADEMA katika majimbo 53 (35.3 asilimia); CUF katika majimbo 22 (asilimia 14.7).



*Mgombea wa urais CCM Dk John Pombe Magufuli Akihutubia Mkutano wa Hadhara wa Kisiasa*

Chama kilichopo madarakani kilituhumiwa kutumia rasilimali za serikali wakati wa kampeni za uchaguzi uliopita. Kufuatia uchaguzi mkuu wa 2015, waangalizi wa muda mrefu wa TEMCO walilipoti matukio yapatayo 46 (asilimia 30.7) ambapo CCM ilitumia rasilimali za serikali katika kampeni. Zaidi ya hapo, waangalizi 23 (asilimia 15.3) walishuhudia katika mikutano ya kampeni watumishi wa serikali wakinadi sera za chama tawala. Tabia hii hainaendani na matakwa ya usawa katika kampeni za uchaguzi kwa vyama vyote vya siasa. Katika majimbo 27 (asilimia 18) waangalizi wa TEMCO walishuhudia matumizi ya alama za uchochezi, matusi na ujumbe wa kuwadhalilisha vyama pinzani vya siasa au viongozi wao.



*Mgombea wa urais CHADEMA Bw Edward Lowassa Akihutubia Mkutano wa Hadhara wa Kisiasa*

Katika mwenendo wa kampeni za uchaguzi Tume ya Uchaguzi ilitoa onyo kadhaa kwa vyama vya siasa na wagombea juu ya mfululizo wa ukiukwaji wa kanuni na maadili ya uendeshaji wa mikutano ya kampeni. Tarehe 9 Septemba 2015 Tume ya Uchaguzi ilitoa taarifa kuwakumbusha viongozi wa vyama vya siasa na wagombea kufuata Kanuni za Maadili

kufuatia uvunjaji wa Kanuni na Maadili ya uendeshaji kampeni uliofanywa na mgombea urais wa CHADEMA mgombea urais pamoja na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Freeman Mbowe. Kwa mfano, Mheshimiwa Edward Lowassa aliomba kura kwa misingi ya udini akiwa Tabora. Katika tukio lingine Mheshimiwa Edward Lowassa na viongozi wa CHADEMA walitoa taarifa yenye utata kuhusu wizi wa kura. Hivyo mnamo tarehe 17 Oktoba 2015, Tume ya Uchaguzi ilitoa onyo rasmi kwa Mheshimiwa Duni Haji, mgombea mwenza wa urais wa CHADEMA kwa madai kuwa kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika uwanja wa Furahisha jijini Mwanza, kwamba Tume ya Uchaguzi imeongeza vituo hewa 20,000 vya kupigia kura (NEC, 2015).

### 6.5 Kampeni Hasi

Kanuni za Maadili zinakataza kampeni hasi katika aina zake mbalimbali. Hata hivyo, waangalizi wa muda mrefu wa TEMCO walibainisha matumizi ya kampeni hasi kwa vyama vya CCM na CHADEMA katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015. Jedwali 6-2linaonesha kwa ufupi maneno yaliyotumiwa kwenye kampeni hasi.

***Jedwali 6-2: Kampeni Hasi kwa Kupitia Maneno***

| Chama cha siasa | LTO kutoka | Kampeni Hasi |
|---|---|---|
| CCM | Arumeru Mashariki, Mbagala, Morogoro Mjini, Mtama, Hai, Moshi Mjini | *Lowassa ni mgonjwa sana na anaweza kufa muda wowote. Ikulu sio Mortuary ya kuhifadhi wafu* |
| CCM | Mbagala, Geita, | *Igizo lilionesha Lowassa ni mgonjwa sana mpaka anavishwa pampers* |
| ACT Wazalendo | Tunduma | *CHADEMA symbol was used by the killer regimes in history* |
| CCM | Tunduma, Kibamba | *Lowassa ni fisadi, mgonjwa na hawezi ongea kwa muda mrefu kwenye kampeni* |
| CUF | Mbagala | *BOT wametengeneza pesa bandia ili zitumike kipindi cha kampeni na uchaguzi ukimalizika tu hamtaziona hizo pesa bandia* |
| CUF | Mbagala | *Magufuli hata uwe mgoni vipi huwezi kumtongoza mkweo Kikwete* |
| CHADEMA | Ilemela | "..msimchague *Angelina Mabula .... hajaolewa, ameshindwa kuishi na mume, ni vigumu sana kuweza kuwatumikia kama mbunge* |
| CCM | Rombo | *Mgombea wa CHADEMA ni mchawi na alimuua mama yake ili apate ubunge* |
| NCCR- Mageuzi and CHADEMA | Vunjo | *Bora UKIMWI kuliko CCM, Bora EBORA kuliko Magufuli* |

Chanzo: Waangalizi wa muda mrefu wa TEMCO, 2015



*Ushahidi Unaonesha Hampeni Hasi, 2015*

Mwangalizi wa TEMCO huko Serengeti alibainisha moja ya kampeni hasi iliyorudiwa rudiwa sana katika mikutano ya CCM kuwa ni kuchafua utu wa mgombea wa urais wa UKAWA. CCM ilitohoa salamu ya UKAWA kutoka "Power!" kuwa "Pampers !, na kuwafundisha wanachama wao kujibu" Pampers! "Neno" pampers "ilitumika kumaanisha diapers ambazo hutumika kwa sababu za usafi kwa watoto au watu wagonjwa. Tukio jingine lilitokea Bunda Mjini ambapo mgombea wa CHADEMA, Esther Bulaya, alionya wakazi wa Bunda kuwa mgombea wa CCM, Bw Steven Wassira, "ni mzee sana na kwa hiyo watu hawapaswi kupiga kura kwa ajili yake kwa sababu yeye huishia kulala bungeni". Katika kulipiza kisasi, Mheshimiwa Wassira alijibu kwa kuwaambia watu kwamba hawapaswi kumpigia kura Bulaya kwa sababu yeye ni "malaya, kaolewa na mwanamke mwingine" (nyumba ntobhu) na yeye anakaa katika nyumba ya wageni.

Matukio hayo ya kampeni hasi hayakuwa ya amani,na kampeni hazikuwa huru na haki. Maneno kama hayo yalikuwa ni ya kuvunja moyo hasa ukizingatia bodi za kudhibiti uchaguzi hazikufanya mengi ili kuzuia kampeni hasi.

### 6.6 Mbinu na Mikakati ya Kampeni

Kampeni katika Tanzania kwa ujumla zinaratibiwa na Tume ya Uchaguzi. Ili kuhakikisha uendeshaji rahisi wa kampeni za uchaguzi Tume ya Uchaguzi ikishauriana na wadau wengine wa uchaguzi waliandaa ratiba ya kampeni za uchaguzi za rais,ubunge na udiwani.Tume ya Uchaguzi iliweka utaratibu ambapo kampeni za vyama vya siasa ingefanyika.

Kampeni za uchaguzi mkuu wa 2015 zilizinduliwa rasmi Agosti. Vyama vitano tu vya siasa vilifanya uzinduzi rasmi wa kampeni. CCM ilizindua kampeni zake za urais Agosti 24,2015 katika viwanja vya Jangwani jijini Dar Es Salaam wakati CHADEMA walifanya hivyo Agosti 29,2015 katika viwanja vya Jangwani jijini Dar Es Salaam, ACT wazalendo Agosti 30 katika

viwanja vya Zakhem jijini Dar Es Salaam,ADC tarehe 8 Septemba 2015 katika Pemba, Zanzibar, CUF tarehe 9 Septemba huko Kibanda Maiti, Zanzibar na TLP tarehe 13 Septemba 2015, Mwembeyanga jijini Dar Es Salaam.



Mgombea wa Urais wa ACT –Wazalendo katika Kampeni

Timu za kampeni ziliundwa na vyama vya siasa kwa mujibu wa kifungu cha 7 cha Sheria ya Gharama za Uchaguzi. Timu ya kampeni ya CCM iliundwa na wajumbe 32 wakati timu ya kampeni ya CHADEMA iliundwa na wajumbe 8 (Citizen, 19 Agosti na 3 Septemba, 2015). Mbinu na mikakati ya uendeshaji wa kampeni za mwaka 2015 ilijumuisha zaidi: (i) mikutano ya hadhara; (ii) kampeni za nyumba kwa nyumba; (Iii) kampeni ya mkononi, (iv) Teknolojia ya kisasa ya mawasiliano, (v) mijadala katika vyombo vya habari na matangazo; na mikakati kama vile matumizi ya maonyesho ya vikundi vya sanaa na kusafirisha wapigakura. Mikutano ya hadhara ilitumiwa sana na CCM, CHADEMA, ACT Wazalendo, na CUF. Jedwali 6-3 linaonesha mikakati ya kampeni kutumiwa na vyama mbalimbali vya siasa.

***Jedwali 6-3: Mbinu na Mikakati Iliyotumiwa na Vyama***

| S/No. | Mikakati | Vyama vya Siasa (%) | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | CCM | CHADEMA | ACT-W | CUF | NCCR-M | Others |
| 1. | Mikutano ya Hadhara | 147 (98) | 127 (84.7) | 98 (65.3) | 81 (54) | 23 (15.3) | 44 (29.3) |
| 2. | Vikundi vya Sanaa | 134 (89.3) | 79 (52.7) | 33 (22%) | 44 (29.3) | 12 (8%) | 16 (10.7) |
| 3. | Kampeni za Nyumba kwa Nyumba | 110 (73.3) | 89 (59.3) | 79 (52.7) | 64 (42.7) | 26 (17.3) | 62 (41.3) |
| 4. | Mitandao ya Kijamii | 81 (54%) | 59 (39.3) | 28 (18.7) | 29 (19.3) | 5 (3.3) | 10 (6.7) |
| 5. | Ujumbe mfupi wa maneno | 63 (42) | 44 (29.3) | 21 (14.0) | 19 (12.7) | 9 (6%) | 14 (9.3) |
| 6. | Vikundi lengwa katika maeneo muhimu | 83 (55.3) | 79 (52.7) | 62 (41.3) | 39 (26.3) | 11 (7.3) | 33 (22) |

Chanzo: Taarifa za Waangalizi wa TEMCO, 2015

Kama inavyoonekana katika Jedwali 6-3, mikutano ya hadhara ilitumiwa sana katika kampeni za vyama vikuu viwili vya siasa, ambavyo ni CCM (asilimia 98) na CHADEMA (asilimia 85). Ni wazi pia kwamba CCM ilitumia mbinu sita kwa ufanisi zaidi kuliko chama kingine chochote cha siasa. Uchunguzi wa TEMCO umeonesha uwiano chanya kati ya ufanisi katika matumizi ya mikakati mbalimbali ya kampeni na utendaji katika uchaguzi.



*Mgombea Urais, Hashim Rungwe Spunda, Kupitia Chama cha CHAUMMA wakati wa Kampeni*

### *6.6.1 Njia za Usafiri*

Ripoti ya waangalizi waTEMCO ilionesha njia kuu sita za usafirishaji hutumiwa na vyama vya siasa na wagombea wakati wa mikutano ya kampeni: misafara ya watu; ndege / helikopta; magari; pikipiki, baiskeli na kwa miguu kama inavyoonekana katika Jedwali 6-4.

***Jedwali 6-4: Njia za Usafiri kuelekea katika mikutano ya kampeni***

| S/No. | Njia za Usafiri | Vyama vya Siasa (%) | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | CCM | CHADEMA | ACT-W | CUF |
| 1 | Usafiri wa mabasi | 109 (72.7) | 32 (21.4) | N.A | 24 (16) |
| 2 | Usairi wa Ndege | 49 (32.7) | 53 (35.3) | N.A | 1 (0.7) |
| 3 | Usafiri wa Magari madogo | 140 (93.3) | 112 (74.7) | 69 (46.0) | 69 (46) |
| 5 | Usafiri wa Baiskeli | 53 (35.3) | 44 (29.3) | 28 (18.7) | 35 (23.3) |
| 6 | Usafiri kwa Miguu | 58 (38.7) | 47 (31.3) | 32 (21.3) | 38 (25.3) |

Chanzo: Ripoti za Waangalizi wa TEMCO, 2015

Kama inavyoonekana katika Jedwali 6-4, vyama vingi vya siasa vilitumia usafiri wa basi kama njia kuu ya usafiri wakati wa kampeni za uchaguzi. Wakati CHADEMA ilitumia ndege / helikopta mara nyingi zaidi (asilimia 35.3), CCM ilitumia usafiri wa aina hiyo kwa asilimia 32.7. CCM na CHADEMA walikuwa wamejipanga vizuri na kutumia njia mbalimbali za usafiri kuwafikia wapigakura. Kwa ujumla, uchunguzi wa TEMCO ulionesha kwamba vyama vilivyotumia rasilimali nyingi zaidi katika kampeni ndivyo vilivyokuwa na nafasi kubwa ya kushinda uchaguzi.



*Helikopta iliyotumiwa na wakati wa Kampeni*



*Helikopta iliyotumiwa na CCM wakati wa Kampeni*

Aidha, CCM na CHADEMA walitumia wasanii maarufu kama wajumbe wao maalum katika kampeni wakiwa na kauli mbiu. Kwa mfano, CCM walitumia kauli mbiu ya Mama Ongea na Mwanao; vile vile, CHADEMA ilianzisha kampeni inayojulikana kama Toroka Uje karibu siku thelathini kuelekea siku ya uchaguzi.



*Chanzo: Kikundi kampeni cha Mama Ongea na Mwanao*





*Chanzo: Kikundi cha kampeni cha Toroka Ujee*


**6.7 Ilani za Uchaguzi: Ajenda na Masuala Yaliyojitokeza katika Kampeni za Uchaguzi**

Jumla ya vyama vya siasa 22 vilivyoshiriki katika uchaguzi wa mwaka 2015, vyama vya siasa vinane vilisimamisha wagombea wa urais. Mgombea urais wa CHADEMA aliungwa mkono na vyama vya siasa vitatu ambavyo ni; Civic United Front (CUF), The National Convention for Construction and Reform – (NCCR-MAGEUZI) na National League for Democracy (NLD) chini ya mwavuli wa *Umoja wa Katiba ya Wananchi* (UKAWA). Kuibuka kwa UKAWA na kuhama kwa Edward Lowassa CCM na kuwa mgombea wa urais wa CHADEMA kuliufanya uchaguzi wa mwaka 2015 kuwa na ushindani wa hali ya juu kati ya vyama hivi viwili.Taarifa za waangalizi wa uchaguzi wa TEMCO zinaonesha kuwa vyama vinne tu nivyo viliandaa na kuzindua ilani zao. Vyama vingine havikuweza kuandaa ilani za uchaguzi na pia kufanya kampeni katika maeneo yote na kikamilifu ili kuelezea walichokuwa wanakisimamia.










*Ilani za Uchaguzi za baadhi ya Vyama, ACT-Wazalendo, CCM, CHADEMA na CUF*

Kulingana na ilani za vyama, kauli mbiu ya CCM ilikuwa Umoja ni Ushindi na ililenga kukabiliana na changamoto kubwa nne za (i) kuondooa umaskini, (ii) kushughulikia ukosefu wa ajira kwa vijana, (iii) kupambana na rushwa na ufisadi na (iv) kujenga uchumi wa viwanda. Vipaumbele vya ACT-Wazalendo vilikuwa ni (i) hifadhi ya jamii; (ii) ajira' (iii) afya (iv) elimu. CHADEMA ilikuwa na vipaumbele mbalimbali ikiwa ni pamoja na (i) upatikanaji wa katiba ya wananchi (ii) kujenga uzalendo (iii) kuimarisha nidhamu na uwajibakaji katika sekta ya umma ; (iv) kutumia watalaamu katika uendeshaji wa nchi.

Kampeni za CCM na vyama vya upinzani kwa pamoja vilionesha haja ya kupambana na rushwa na ubadhilifu wa mali ya umma. Jedwali 6-5 linaonesha mbinu mbalimbali zilizonyeshwa na vyama vikuu vya siasa katika kupambana na rushwa.

***Jedwali 6-5: Mbinu za Vyama vya Siasa katika Kupambana na Rushwa***

| Chama | Mbinu |
|---|---|
| ACT-Wazalendo | Kuzuia mtu yeyote aliyepatikana na makosa ya rushwa kufanya kazi au biashara na taaasisi za umma. |
| | Kutunga sheria ya kutaifisha mali za makampuni yatakayopatikana na hatia ya rushwa. |
| CCM | Kuunda mahakama maalum ya kushughulikia wala rushwa na mafisadi. |
| CHADEMA | Kuingiza masuala ya maadili na miiko ya viongozi katika katiba. |
| | Kuunda chombo huru kwa ajili ya kusimamia na kuchunguza viongozi na watumishi wa umma. |
| CUF | Kukuza uwazi |


Chanzo: Taarifa za Waangalizi wa TEMCO, 2015

Pamaoja na kwamba ilani za vyama vinne vikuu zilisisitiza mapambano dhidi ya rushwa na kuhuisha maadili nchini, waangalizi wa TEMCO walibaini kuwa suala hili halikupewa kipaumbele kikubwa katika kampeni. Taarifa za wanagalizi wa TEMCO zilionesha kuwa ACT-Wazalendo walikuwa na kauli mbiu 30, CCM walikuwa na 36, CHADEMA walikuwa na 32 na CUF walikuwanazo 24. Hata hivyo, hakukuwa na kauli mbiu hata moja kuhusu mapambano dhidi ya rushwa.

TEMCO ilibainisha kuwa ilani za vyama vikuuu vinne zilitilia mkazo uboreshaji wa huduma za jamii, matumizi ya sayansi na teknolojia katika nyanja za uzalishaji mali ili kuiwezesha nchi kufikia uchumi wa ngazi ya kati. TEMCO ilibainisha kuwa hakukuwa na tofauti kubwa ya

kiitikadi baina ya vyama katika mambo muhimu yanayohusu nchi. Tofauti ilikuwa kwenye vipaumbele na mikakati ya utekelezaji. Suala la Muungano, hasa muundo wa muungano, pia lilijitokeza katika ilani za vyama. CHADEMA waliahidi Muungano wa serikali tatu ambapo kutakuwa na serikali ya Muungano, ya Zanzibar na Tanganyika. Ilani ya CUF iliiegemea zaidi Zanzibar msisitizo ukiwa ni kuwa na mamlaka kamili kwa Zanzibar.

Timu za kampeni na wagombea walitumia muda mwingi kuelezea sifa za uongozi walizo nazo wagombea binafsi ambazo mpinzani wake hana. Vifaa mbalimbali vya kampeni kama mabango, stika, vipeperushi, kalamu, mabegi, vifungo, fulana na kanga vilikuwa na ujumbe kuhusu wagombea na siyo Ilani ya chama. Kampeni zilijikita katika kuwasifu wagombea wao, hasa, Dkt. John Pombe Magufuli, ambaye utendaji wake katika serikali alipokuwa Waziri wa maendeleo ya miundombinu ulionekana kuwa mzuri. Lifuatalo ni moja ya mabango ya kampeni.




*Moja ya Mabango ya Kampeni ya CCM*

Mgombea wa CCM alielezewa kama asiyekula rushwa, mchapakazi, mwaminifu na hivyo ni mtu sahihi wa kushughulikia matatizo sugu ya serikali yanayoikumba nchi. Kampeni za CCM pia zilifanya juhudi za kuelezea sifa mbaya za mgombea wa CHADEMA/UKAWA kuwa ni mwanasiasa mla rushwa mwenye uchu wa madaraka anayetaka kujinufaisha binafsi.


Vilevile, UKAWA walitumia muda mwingi katika kampeni zao kukosoa utendaji wa serikali ya CCM. UKAWA walidai kuwa CCM imesababisha umaskini, kuenea kwa rushwa, uzembe au kutowajibika, kupindisha sheria, 'kubebana' kisiasa, usimamizi mbaya wa uchumi, na kudorora kwa huduma muhimu za kiuchumi na kijamii. Kwa upande mwingine, kampeni za timu za CCM, zilijikita katika kumkosoa mgombea urais wa CHADEMA kuwa ana historia ya

ufisadi ilhali kampeni za CHADEMA/UKAWA zilijikita katika kumsifu mgombea wa urais binafsi Edward Lowassa. CHADEMA walidai kuwa mgombea wao aliweka rekodi ya kile alichokiita '*maamuzi magumu'* wakati wa uongozi wake akiwa Waziri Mkuu wa Nchi. Pia, wagombea na timu zao za kampeni hawakutumia muda mwingi kuelezea Ilani za vyama vyao. Ufuatao ni mfano mmojawapo wa bango la kampeni za UKAWA.




*Moja ya Mabango ya Kampeni ya UKAWA*

Vivyo hivyo, wagombea wa ubunge na udiwani hawakutumia muda mwingi kuzinadi Ilani za vyama vyao. Wagombea wengi waliahidi kutatua matatizo na changamoto mbalimbali zinazowazunguka wapigakura katika maeneo yao. Kwa mfano, Mwangaalizi wa TEMCO wa Chakechake alibainisha kuwa mgombea ubunge wa UDP aliahidi kujenga nyumba maalum na vituo vya kushughulikia waathirika wa madawa ya kulevya. Huko Mbulu, mgombea ubunge wa ACT-Wazalendo aliahidi kujenga madarasa ya shule za sekondari katika kila kata yakiwa na vifaa vyote muhimu vya kufundishia. Huko Bukoba, mgombea ubunge kupitia CHADEMA aliahidi kuwa meli mpya kwa ajili ya usafiri wa Bukoba-Mwanza itanunuliwa.




*Azimio la  Wazalendo la Chama cha ACT-Wazalendo*

Maudhui makubwa yaliyotawala kampeni za uchaguzi za chama tawala CCM na UKAWA yalikuwa *Mabadiliko*. CCM na CHADEMA walieleza kuwa hawakuridhishwa na  hali ya uendeshaji wa masuala ya umma hasa usimamizi wa huduma za jamii na kwamba wataleta mabadiliko ikiwa watachaguliwa.




*Kibonzo cha Kipaumbele cha Ajenda ya Uchaguzi wa 2015*

Ujumbe wa salamu ya kampeni ya UKAWA ulifanywa kwa kuzungusha mikono huku wakiimba *Lowassa = Mabadiliko…... Mabadiliko = Lowassa.*  Kwa upande wake, CCM waliahidi kumchagua Magufuli kwa mabadiliko ya kweli. Kauli mbiu iliyotumika ni *Chagua Magufuli kwa Mabadiliko ya Kweli.* Mgombea wa CCM, Dkt. John Magufuli, alibadilisha kifupisho cha CHADEMA chenye maana ya Movement for Change (yaani vuguvugu la mabadiliko - M4C) na kumaanisha 'Magufuli for Change' (yaani Magufuli kwa ajili ya mabadiliko - M4C). Kielelezo hapo chini inaonesha matumizi sawia ya M4C baina ya CCM na CHADEMA.

*Kauli Mbiu za Mabadiliko kwa Vyama vya CCM na CHADEMA*

**6.8 Elimu kwa Wapigakura**

Kikatiba, Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Tume ya Uchaguzi Zanzibar ndizo zenye mamlaka ya kutoa elimu kwa wapigakura na kusimamia na/au kuratibu asasi nyingine au watu wanaotoa elimu kwa wapigakura. Tume ilitoa idhini kwa Asasi za Kiraia (AZAKI) 447 kati ya 451 zilizooomba kutoa elimu ya mpigakura katika uchaguzi wa mwaka 2015. Idadi hii ya watoa elimu ilikuwa ndogo kulinganisha na ukubwa wa nchi. Kati ya waangalizi 150, 58(38.7%) walitoa taarifa kuwa AZAKI zilitoa elimu ya mpigakura. Umadhubuti wa utoaji wa elimu ya mpigakura unategemea mbinu inayotumiwa na watoaji. Mbinu zilizotumiwa na AZAKI kutoa elimu ya mpiga kura zimeonyeshwa kwenye Jedwali 6-6 hapo chini.

***Jedwali 6-6: Mbinu za Zilizotumiwa na AZAKI katika Kutoa Elimu kwa Mpigakura***

| Mbinu iliyotumika | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|
| Vipeperushi | 32 | 21.3 |
| Brosha | 29 | 19.3 |
| Mabango | 27 | 18 |
| Magazeti | 20 | 13.3 |
| Radio | 34 | 22.7 |
| Mitandao ya Kijamii | 19 | 12.7 |

Chanzo: Taarifa za Waangalizi wa TEMCO, 2015

Elimu iliyotolewa na AZAKI kwa wapigakura ilifagharamikiwa na wafadhili wakigeni. Hakukuwa na fedha kutoka serikalini kwa ajili ya AZAKI kutoa elimu ya mpigakura. Tume ya uchaguzi pia ilitoa elimu ya mpigakura kwa kutumia mbinu mbalimbali kama inavyoonekana kwenye Jedwali 6-7 hapo chini.

***Jedwali 6-7: Mbinu zilitumiwa na Tume ya Uchaguzi kutoa Elimu ya Mpigakura***

| Mbinu iliyotumika | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|
| Vipeperushi | 84 | 56.0 |
| Brosha | 70 | 46.7 |
| Mabango | 73 | 48.7 |
| Magazeti | 50 | 33.3 |
| Radio | 89 | 59.3 |
| Televisheni | 83 | 55.3 |
| Mitandao ya Kijamii | 43 | 28.7 |

*Chanzo: Taarifa za Waangalizi wa TEMCO, 2015*

Jedwali hapo juu linaonesha kuwa Tume ya Uchaguzi ilitoa elimu ya mpigakura katika maeneo mengi zaidi kuliko AZAKI. Pia, tofauti na AZAKI, Tume ilitumia televisheni katika kutoa taarifa na elimu kwa wapigakura. Vyama vya siasa pia vilifanya kazi ya kutoa elimu ya kupiga kura na kuhamasisha wafuasi wao wajitokeze kwenye michakato mbalimbali ya uchaguzi. Jedwali 6-8 hapo chini linaonesha uhusika wa vyama vya siasa katika kutoa elimu ya mpigakura. Jedwali hili linaonesha kuwa vyama vya siasa vilihusika zaidi kwenye utoaji elimu ya uraia kuliko watoaji elimu wengine.

***Jedwali 6-8: Uhusika wa Vyama vya Siasa kutoa Elimu ya Mpigakura***

| Chama | Kiwango cha Uhusika | |
|---|---|---|
| | Idadi | Asilimia |
| ACT-Wazalendo | 103 | 68.7 |
| CCM | 144 | 96.0 |
| CHADEMA | 125 | 83.3 |
| CUF | 91 | 60.7 |
| NCCR-Mageuzi | 29 | 19.3 |
| Vyama Vingine | 58 | 38.7 |

Chanzo: Taarifa za Waangalizi wa TEMCO, 2015

Kulikuwa pia na elimu ya mpigakura kwa makundi maalum ya wapigakura hasa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Kati ya waangalizi 150 wa uchaguzi wa TEMCO, 56 (37.3%) walitoa taarifa kuwa kulikuwa na elimu ya mpigakura kwa wajili ya wanawake na vijana, ila kwa upande wa walemavu utoaji elimu uliripotiwa na waangalizi kuwa 43(28.7%) tu. Mbinu zifuatazo zilitumika kutoa elimu ya wapigakura.

***Jedwali 6-9: Mbinu za Kutoa Elimu ya Mpigakura kwa Makundi Maalum***

| Njia iliyotumika | Kundi (%) | | |
|---|---|---|---|
| | Wanawake | Vijana | Walemavu |
| Programu za Radio | 42 (28) | 38 (25.3) | 28 (18.7) |
| Programu za Televisheni | 28 (19.7) | 32 (21.3) | 27 (18) |
| Vipindi vya Radio | 20 (30) | 27 (18) | 15 (10) |
| Vipindi vya Televisheni | 24 (16) | 19 (12.7) | 12 (8) |
| Matangazo ya Magazeti | 14 (9.3) | 18 (12) | 16 (10.7) |
| Vielelezo vinavyoonekana | 11 (7.3) | 9 (6) | 8 (5.3) |
| Vifaa vya kusafiri | 5 (3.3) | 7 (4.7) | 9 (6) |
| Sanaa | 19 (12.7) | 15 (10) | N.A |
| Nyengine | 1 (0.7) | 1 (0.7) | N.A |

Chanzo: Taarifa za Waangalizi wa TEMCO, 2015

Jedwali 6-9 hapo juu linaonesha kuwa mbinu zilizotumiwa kutoa elimu ya mpigakura kwa makundi maaalum zilikuwa nyingi ingawa hazikuenea katika sehemu kubwa ya nchi.

## 6.9 Taratibu za Kiusalama

Ili kampeni za uchaguzi ziweze kwenda vizuri, ni muhimu kuwa na uhakika wa ulinzi na usalama muda wote wa kampeni hasa kwa wagombea na timu zao za kampeni na wapigakura kwa ujumla. TEMCO ilifanya tathmini ya mwenendo wa kampeni na kung'amua yafuatayo:

(i) kati ya mikutano 3,242, 3240 ilifanyika kwa usalama na amani. (ii) kati ya mikutano ya hadhara 269, 218 ilivurigika; (iii) kati ya mikutano ya hadhara 71, 4 ilianza kabla ya saa mbili asubuhi; (iv) kati ya mikutano ya hadhara 829 iliyoanza kwa wakati, 797 ilimalizika baada ya saa kumi na mbili na (v) kati mikutano ya hadhara 2842, 2839 ilifanyika kwa muda uliopangwa.

Kwa kiwango kikubwa wagombea na vyama vya siasa vilizingatia kanuni na miiko ya maadili kwa ajili ya mwenendo wa vyama vya siasa na wagombea. Kutokana na hali hiyo, kampeni za uchaguzi za mwaka 2015 zilifanyika kwa amani. Vyombo vya kusimamia sheria vilitekeleza majukumu yao kwa weledi na maadili ya kazi zao. CEMOT waliripoti kwamba kati ya wahojiwa 3,794 walioulizwa kama walishuhudia zuio lolote la polisi katika mikutano ya hadhara ya kampeni, 3,674 (95.0%) walijibu kwamba hawakuona kitu kama hicho (CEMOT, 2015).

Mikutano ya hadhara iliyofanywa na wagombea urais ilipewa ulinzi wa kutosha. Wagombea urais wa CCM na CHADEMA waliwavutia watu wengi kwenye mikutano yao katika kipindi chote cha kampeni. Jeshi la polisi lilihakikisha kwamba askari polisi waliovaa sare walikuwapo kuhakikisha kunakuwa na utulivu, amani na usalama.




*Kielelezo 7: Polisi katika Moja ya Mikutano ya Kampeni*
*Chanzo: Taarifa za Waangalizi wa TEMCO, 2015*

Polisi walihimiza watu kutii sheria kupitia kauli mbiu yao ya *utii wa sheria bila shuruti, ulinzi shirikishi na Polisi Jamii.* Mkakati huu ilizaa matunda.



*Askari Polisi Akiwa katika Moja ya Mikutano ya Mashauriano na Jamii.*

Mbinu nyingine ya ulinzi wakati wa kampeni za mwaka 2015 ilikuwa ni matumizi ya vikundi vya ulinzi vya vyama. Miongoni mwa vikundi hivyo ni "Green Guards" cha CCM, "Blue Guards" cha CUF na "Red Brigade" cha CHADEMA. Vikundi hivi vilisababisha mgongano kati ya vyama vya siasa hasa baina ya CCM na CHADEMA kiasi cha kusababisha kifo cha mtu mmoja huko Tarime. Waangalizi wa TEMCO walibainisha kuwa vyama hivyo vitatu vilitumia vikundi vya ulinzi vya vyama kama ifuatavyo; CCM (76%), (ii) CHADEMA (55.3 %), (iii) CUF (22 %). Matumizi ya vikundi hivi vilipigwa marufuku kwa pamoja na msajili wa vyama vya siasa na Jeshi la Polisi nchini.

## 6.10 Tathmini ya Jumla ya Kampeni za Uchaguzi

Tathmini ya TEMCO ya uchaguzi mkuu wa 2015 umewasilishwa katika Jedwali 8.0 hapa chini.

***Jedwali 6-10: Tathmini ya Kampeni za Uchaguzi***

| **Aina na Mwenendo wa Kampeni** | **Daraja na Alama** | **Idadi** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|
| Mwenendo wa kampeni ulikuwa na kasoro chache ambazo hazikuathiri kwa namna yeyote matokeo ya uchaguzi. Kwa ujumla uchaguzi ulikuwa safi, huru na wa haki. | A (80 - 100%) | 42 | 28.0 |
| Kampeni za uchaguzi zilikuwa kwa kiwango kikubwa huru na haki lakini kulikuwa na kasoro chache ambazo kwa ujumla wake hazikuathiri kwa namna yeyote matokeo ya mwisho ya uchaguzi na haziathiri ushiriki na majaliwa ya wadau wa uchaguzi (vyama vya siasa, wagombea na wapigakura). | B (60 - 79%) | 88 | 58.7 |
| Kampeni ziliruhusu ushiriki huru wa wadau (vyama vya siasa, wagombea na wapigakura). Lakini kulikuwa na kasoro nyingi ambapo vyama vikuu na hasa chama tawala kilivunja sheria bila kuchukuliwa hatua na kulikuwa na upendeleo ambao uliathiri ushiriki na hatima ya baadhi ya wagombea na vyama. | C (50 - 59%) | 16 | 10.7 |
| Kampeni zilikuwa na kasoro nyingi na kutoheshimu sheria za uchaguzi, kanuni na maadili ya uchaguzi, kulikuwa na matatizo ya usimamizi, unyanyasaji na upendeleo. | D (40 - 49%) | 4 | 2.6 |
| Kampeni zilivurugwa au kusimamiwa vibaya kiasi kwamba haikuwa rahisi kuelewa kilichotendeka. Ilikuwa ni kama mwanafunzi aliyefeli mtihani. | E (1 - 39%) | 0 | 0 |
| Mwenendo wa kampeni uligubikwa na kasoro kubwa sana. Kulikuwa na matukio mengi ya fujo, vurugu, hujuma, rushwa na uchochezi kiasi cha baadhi ya wagombea kujitoa kwenye uchaguzi au kuchukua hatua zingine. Uchaguzi uliharibika. | F (0%) | 0 | 0 |
| Jumla | | 150 | 100.0 |

Chanzo: Taarifa za Waangalizi wa TEMCO, 2015

### 6.11 Hitimisho na Mapendekezo

#### *6.11.1 Hitimisho*

Kampeni za uchaguzi zilizofanywa na vyama vya siasa na wagombea kwa uchaguzi wa mwaka 2015 zilifanyika kwa kiwango kikubwa kwa kuzingatia sheria na kanuni za maadili zilizotolewa na Tume ya Uchaguzi. Ratiba kwa ajili ya kampeni katika majimbo ziliandaliwa kwa kushirikisha wadau wakiwemo wawakilishi wa Tume, vyama vya siasa na wagombea. Vyama vingi havikufuata ratiba ya kampeni. Hata hivyo, vyama vikuu vilijitahidi kufuata ratiba ya mikutano yao ya hadhara na mabadiliko yalifanyika tu baada ya taratibu mwafaka za kuahirisha mikutano hiyo kufanyika.

Ingawa sheria ya gharama za uchaguzi inaweka mipaka katika matumizi ya fedha za kampeni kwa vyama na wagombea wao, ushahidi wa mazingira ulionesha kuwa sheria haikuzingatiwa na usimamizi wa sheria hiyo haukuwa madhubuti. Mikakati ya kampeni kwa vyama vya siasa na wagombea wao ilikuwa tofauti hasa kwenye maeneo yaliyofikiwa na kiwango cha rasilimali zilizotumika. Vyama vikubwa vya CCM na CHADEMA vilifanya kampeni zilizokuwa na mbwembwe nyingi na zilizokuwa na watu wengi hasa kwenye mikutano ya wagombea Urais. Vyama vidogo havikuweza kufanya mikutano mikubwa. Vyama vinne vya CCM, CHADEMA, CUF na ACT-Wazalendo vilikuwa na siku maalum kwa ajili ya kuzindua kampeni na ilani za vyama vyao katika ngazi ya Taifa. Vyama viingine ikiwa ni pamoja na vile vilivyokuwa na wagombea Urais havikuweza kufanya hivyo.

Vyama vyote havikuweza kutoa msisitizo kwa makundi maalum hasa kwenye elimu ya mpigakura. Hakukuwa na tofauti kubwa ya kiitikadi katika ilani za vyama vya siasa vikubwa. Vyama vyote vikubwa vilikuwa na kauli mbiu ya "mabadiliko" wakati wa kampeni iliyoambatana na kutoa sifa nyingi kwa wagombea mahususi hasa wagombea urais. Kampeni hasi zilionekana kwenye baadhi ya majimbo na nyingi zilihusisha vyama vya CCM na CHADEMA. Pia, elimu ya mpigakura haikupewa msisistizo unaostahili na wadau wote. Vyombo vya ulinzi na usalama hasa jeshi la polisi vilihakikisha kuwa kampeni zinafanyika katika mazingira ya amani na usalama. Jeshi la polisi lilionesha weledi, uadilifu na umahiri wa hali ya juu katika kutimiza wajibu wao. Vurugu zilizotokea baina ya wafuasi wa CHADEMA na CCM huko Tarime zilisababisha mtu mmoja kupoteza maisha. Hili lilikuwa ni jambo halikutarajiwa katika kampeni za uchaguzi wa mwaka 2015.

#### *6.11.2 Mapendekezo*

Kwa kuzingatia taarifa zilizopatikana kuhusu mwenenendo wa kampeni za uchaguzi wa mwaka 2015, mapedendekezo yafuatayo yanatolewa:

(i) Vyama vya siasa vinatakiwa kuheshimu ratiba ya kampeni iliyokubaliwa na vyama vyote vinavyoshiriki kwenye uchaguzi;

(ii) Serikali inatakiwa kuweka mikakati itakayowezesha vyama vidogo kupata rasilimali za kuendesha kampeni na kutengeneza ilani za vyama vyao;

(iii) Sheria ya gharama za uchaguzi itazamwe upya kwa ajili ya kuiimarisha. Serikali iweke mifumo madhubuti kwa ajili ya kuhakikisha vyama vya siasa na wagombea vinaitekeleza sheria hiyo kikamilifu;

(iv) Elimu ya mpigakura ni muhimu katika kuwajengea uwezo wapigakura ili waweze kushiriki ipasavyo katika uchaguzi. Elimu ya mpigakura ni jambo nyeti kuachwa katika mikono ya AZAKI na wadau wa maendeleo. Serikali inahitaji kuona uwezekano wa kutengeneza mkakati endelevu wa kutoa elimu ya uraia ambayo elimu ya mpigakura ni sehemu yake;

(v) Vyama vya siasa na wagombea wao wanahimizwa kuacha kampeni hasi kwa kuwa haziendani na utamaduni wa kisiasa uliojengeka Tanzania;

(vi) Utendaji wa vyombo vya dola hasa Jeshi la Polisi unahitaji kukuzwa na kuendelezwa.

## CHAPTER 7
## VYOMBO VYA HABARI NA UCHAGUZI

### 7.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha tathmini ya utendaji wa vyombo vya habari kuhusiana na uchaguzi mkuu wa Tanzania wa mwaka 2015. Imegawanyika katika sehemu tano: sehemu ya kwanza ni utangulizi ikifuatiwa na sehemu ya pili ambayo inaangazia muktadha wa kisheria ulioongoza utendaji wa vyombo vya habari wakati wa uchaguzi wa mwaka 2015. Sehemu ya tatu inahusu habari na uandikishaji wa wapigakura kwa kutumia mfumo wa Biometric Voter Registration (BVR). Sehemu ya nne inazungumzia kwa undani uandishi wa habari za uchaguzi na hasa kampeni na mchakato wa upigaji kura. Sehemu ya tano inatoa mapendekezo ya maboresho na kuhitimisha sura.

### 7.2 Mfumo wa Kisheria na Uendeshaji wa Uchaguzi wa 2015

Kwa minajili ya kufuatilia na kutathmini utendaji wa vyombo vya habari katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, TEMCO iliangalia kiwango ambachi vyombo vya habari viliweza kuzingatia mwongozo wa Maadili na Mwenendo wa vyombo vya habari kwa ajili ya kuandika habari za uchaguzi, uliochapishwa na kugawiwa na Baraza la Habari Tanzania (MCT). MCT ilieleza kuwa Mwongozo huo wa Maadili na Mwenendo wa vyombo vya habari ulitengenezwa ili kuhakikisa vyombo vya habari vinajiendesha kwa kuzingatia taaluma na weledi, kuepuka upotoshaji, kuheshimu haki ya kusikilizwa na usawa, na kuwa kipaza sauti cha wapigakura wakati wote wa mchakato wa uchaguzi. Mwongozo huo wa Maadili na Mwenendo wa vyombo vya habari ulitumika kwa wakati mmoja na Mwongozo wa Maadili wa Wanataaluma wa Habari.




*Kituo cha kuuzia magazeti*

Wakati wa kuandaa mwongozo wa utendaji MCT ilizingatia dhima ya vyombo vya habari katika mchakato wa uchaguzi na athari mbaya ambazo zingeweza kujitokeza kwa kutumia

vibaya vyombo vya habari. Hata hivyo TEMCO ilibaini kuwa Mwongozo wa vyombo vya habari hakuwa na mashiko ya kisheria. Kwa hiyo, vyombo hivyo vilikuwa huru kuutumia au kutoutumia na hapakuwa na adhabu kwa kushindwa kuuzingatia mwongozo huo. Licha ya mapungufu hayo, kuwa na mwongozo wa maadili ilikuwa ni dalili ya kiwango cha juu cha kutaka kuhimiza weledi na kufanyakazi kama wapiga vita ufisadi na matendo maovu wakati wa uchaguzi ili kuhakikisha kuwa uchaguzi unakubalika, unakuwa huru na wenye kuzingatia haki. Ufuatialiji wa TEMCO ulibaini kuwa hapakuwa na mwongozo wa maadili kama huo kwa ajili ya mitandao ya kijamii kwenye intaneti, hali ambayo imefanya hili jukwaa linalokua na kukomaa kukosa usimamizi.

Kama moja ya juhudi za kusimamia mitadao ya kijamii, pamoja na juhudi zingine, mwanzo wa mwaka 2015 kukatungwa sheria ya Upatikanaji wa Habari na Sheria ya Mitandao. Sheria hizi kwa pamoja zinadhibiti matumizi na upatikanaji wa habari na kutoa mfumo wa adhabu kama kukitokea matumizi mabaya na tafsiri isiyo sahihi ya taarifa za kitakwimu.

Kuna sera nne ambazo kwa namna fulani zinashughulikia mambo ya uandishi wa habari, na ambazo moja kwa moja zinashughulikia masuala ya mawasilian, nazo ni: (i) Sera ya Utangazaji na Habari, (ii) Sera ya Taifa ya Mawasiliano ya Simu, (iii) Sera ya Taifa ya Habari na Teknololjia ya Habari, na (iv) Sera ya Taifa ya Huduma za Posta.

Sheria zingine ambazo huathiri uendeshaji wa vyombo vya habari moja kwa moja au kwa namna fulani ni pamoja na (i) Sheria ya Mamlaka ya Usimamizi wa Mawasiliano, yam waka 2010 ambayo hutoa leseni, kusimamia uendeshaji na upatikanaj wa taarifa, kufuatilia maudhui na ugawaji wa masafa kwa ajili ya vyombo vya habari vya utangazaji; (ii) Sheria ya Magazeti ya Mwaka 1976, ambayo huhusika na kutoa vitambulisho kwa waandishi wa habari na kufuatilia uchapishaji na maudhui ya magazeti; (iii) Sheria ya Huduma za Usalama wa Taifa ya mwaka 1996; Sheria ya Usalama ya mwaka 1970; Sheria ya Magereza ya Mwaka 1967; na Mwongozo wa Kudumu za Watumishi wa umma ambazo zinazuia kupata au kuchapisha taarifa bila ruhusa jambo linaloweza kuhatarisha siri za serikali na usalama wa nchi au za mashirika, na kuzuia waandishi wasifike maeneo wasiyoruhusiwa na kudhibiti upatikanaji wa habari; (iv) Sheria ya Polisi na Majeshi ya Mgambo, ambayo inaruhusu askari kuchukua mitambo ya uchapishaji, au kunyang'any vitendea kazi vya waandishi wa habari, kukagua vitambulisho vya waandishi wa habari na kuzuia waandishi kuhudhuria mikutano ambayo haikuruhusiwa; (v) Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 1985/2010 (vifungu 53 (1) –(40) inayotaka vyombo vya habari vya umma kutoa fursa sawa na ya haki wanapoandika habari za vyama vya siasa wakati wa uchaguzi. Vyombo vya habari visivyo vya serikali havidhibitiwi na sheria hii. TEMCO iliarifiwa kuwa hapakuwa na taarifa kwa vyombo vya habari kutoka tume ya uchaguzi ya kuvitaka kuandika habari kwa kuzingatia haki na usawa.

### 7.3 Habari na Uandikishaji Wapigakura (BVR)

Ufuatiliaji wa vyombo vya habari uliofanywa na TEMCO ulibaini kuwa Dar es Salaam ndiyo iliyotoa taarifa nyingi zaidi kuhusu uchaguzi ukilinganisha na mikoa mingine. Kwa mfano, wakati zoezi la uandikishaji wapigakura (BVR) likiendelaa kule Njombe, Mkambako na Wanging'ombe, Dar es Salaam ilichangia taarifa 138 juu ya uchaguzi katika jumla ya magazeti

nane yaliyofuatiliwa na TEMCO, wakati Njombe, Makambako, na Wanging'ombe zilichangia chini ya taarifa za habari 12 kila moja. Vyanzo vya habari juu ya uandikishaji wapigakura vilikuwa; (i) wasemaji wa Tume ya Uchaguzi, (ii) wapigakura waliohojiwa kwenye vituo vya uandikishaji; na (iii) wanasiasa na maafisa wa NGOs waliokuwapo kwenye vituo vya uandikishaji walioweza kuitisha mikutano ya waandishi wa habari. Hii ilidhihirisha uwezo mdogo wa waandishi wa kubuni vyanzo vyao binafsi vya habari na kukosa kufanya juhudi.

Udhaifu huohuo ulijionesha pia juu ya habari za BVR mkoani Dodoma ambayo awali ilichangia habari nyingi kwa sababu tu bunge lilikuwa limekutana na hivyo waandishi walipata urahisi wa kukusanya maoni kutoka vyanzo vya bunge. TEMCO ilibaini kuwa katika habari hizi hakuna iliyotokana na wananchi wa kawaida. Na hali ilibaki hivyo hivyo wakati wote wa uchaguzi kwa sababu vyombo vya habari vingi vinaendeshwa kutokea Dar es Salaam na hivyo kukosa wawakilishi mikoani.




***Kielelezo 7-1: Asilimia ya Habari za Uandikishaji Wapigakura***

Uandikishaji wapigakura kwa kutumia BVR uliingizwa na kutumika kwa mara ya kwanza kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka 2015. Kutokana na ugeni wa teknolojia hiyo na ukweli kuwa wapigakura wote walitakiwa kujiandikisha upya, ilitarajiwa kuwa vyombo vya habari vingelichukulia suala hili kama ni la maslahi ya kitaifa na kulifanya ni ajenda kubwa. TEMCO ilifuatilia vyombo vya habari vya utangazaji na magazeti, na ilifuatilia mitandao ya kijamii hali kadhalika kwa dhumuni la kutathmini kiwango cha umuhimu kilichotolewa kwa uandikshaji wapigakura na vyombo vya habari. TEMCO ilibaini kuwa kadri muda ulivyopita na hasa tulipoanza kukaribia uteuzi wa wagombea unaofanywa na Tume ya Uchaguzi (NEC) vyombo vya habari na mitandao ya kijamii vilionesha kutilia umuhimu wa juu suala la uandikishaji, baada ya kutambua kuwa ndio njia pekee ambao wananchi wanaweza kuitumia haki yao ya kuchagua viongozi, na kuwa ndio kizingiti kikuu cha kuhakikisha uchaguzi unakuwa huru na wa haki na ili uwe wa kukubalika pia. Lakini hilo bado halikuonesha kuwa vyombo vya habari viliandika habari nyingi zaidi juu ya uandikishaji wapigakura. Habari za uandikishaji ziliendelea kuwa chache ukilinganisha na masuala mengine ya uchaguzi. Wakati wa

kuhitimisha zoezi la uandikishaji (BVR) mwezi wa Agosti 2015 habari zinazohusiana na suala hilo zilifikia wastani wa asilimia 3 tu ya habari zote za uchaguzi na habari zingine.

Ufuatiliaji wa TEMCO ulibaini pia tabia ya muda mrefu ya kuishambulia Tume ya Uchaguzi (NEC) kwa kutumia katuni za kisiasa, maoni ya wahariri na makala za maoni kwa tuhuma za udhaifu katika usimamizi na kukosa matayarisho ya kutosha. Vyombo vya habari havikuweza kuipatia Tume ya Taifa fursa ya kutoa maelezo, kama ilivyo katika kanuni za maadili ya uandishi na mwongozi wa uandishi wakati wa uchaguzi. Usawiri wa BVR kwa kutumia picha na katuni ulikuwa, wakati mwingine, wenye kukashfu na kudhihaki. Katuni zilionesha NEC kama taasisi ambayo ilishindwa kujiongoza na kuituhumu kushirikiana na Chama cha Mapinduzi na serikali ili kuuharibu uchaguzi.














Magazeti mengi yalitumia katuni kuelezea hisia zao juu ya utendaji wa Tume ya Uchaguzi katika utekelezaji wa zoezi la uandikishaji wapigakura. Dhamira iliyotawala usawiri wa NEC kwa kutumia picha ilikuwa ya kukosa uwezekano wa kufanikisha zoezi kwa wakati. Katuni ziliakisi pia hisi za wadau wengine wa uchaguzi waliohofia kuwa uandikishaji wa kutumia BVR usingeweza kufanikiwa. Katuni nyingi zilisawiri zoezi la BVR kama lililoharibika na

kulifananisha na gari lisilokuwa na matairi, lililokwama na haliwezi kutembea. CCM na serikali walilaumiwa kwa sababu ya kuchelewesha uagizaji wa mashine za BVR na uandikishaji wapigakura. Na hili liliendelea kuwasilisha tuhuma za wadau wengine kuwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar hawakuwa wakifanya kazi yao kwa makini kama ilivyotarajiwa. Magazeti na vyombo vya habari vya utangazaji vilichapicha taarifa zilizoakisi hofu za vyama vya siasa kuwa uandikishaji kwa kutumuia BVR ungeweza kuchelewesha michakato mingine. (angalia kwa mfano *Nipashe, Mei 27, 2015: Uandikishaji BVR wazua hofu ratiba ya uchaguzi; Nipashe, Mei26, 2015, Selasini akerwa majibu ya serikali uandikishwaji wanafunzi, walimu; Mtanzania, Mei 27; Bavicha walia na NEC uandikishaji wapigakura kwa mfumo wa BVR*).

### *7.3.1 Habari za BVR katika Mitandao ya Kijamii*

Katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, na hususani wakati wa kuanza kwa zoezi la uandikishaji wapigakura (BVR), mitandao, hasa Facebook, Twitter na Instagram, vifanyakazi kubwa kwa niaba ya vyama vya siasa na wagombea kama majukwaa ya kimkakati ya kukusanya na kusambaza taarifa, kupatia mrejesho na kutathmini maoni ya watu na hisia zao. Vyama vya siasa vilitumia Facebook kuweka taarifa ambazo zilitumiwa na magazeti na vyombo vya habari vya utandazaji kwa ajili ya hadhira pana zaidi.

Vyama vya siasa na wagombea walianzisha kurasa na akaunti za Twitterna Facebook kwa minajili ya kuwasiliana na wafuasi na mashabiki wao na kuweza kuwafikia wapigakura wengi. Awali kabisa uandikishaji wa wapigakura haukuwa na mvuto mkubwa kwa watumiaji wa mitandao ya kijamii, sababu kubwa ni kuwa mitandao hiyo ni nyenzo ya kutoa taarifa papo kwa papo, huwasilisha matukio wakati yakitokea. Kama jambo halitokei karibu na mtu mwenye kutumia mtandao wa kijamii haliwezi kupata umuhimu na hivyo halitawekwa kwa ajili ya kushirikisha wengine. Utaona kuwa hii ilikuwa sababu mojawapo ya kuongezeka kwa habari za BVR uandikishaji ulipofika mkoani Dar es Salaam. Mitandao ya intaneti iliyo hafifu maeneo ya nje ya miji mikuu na hasa vijijini ilisababisha watu kupeana na kushirikishana taarifa kupitia mitandao ya kijamii. Uandikishaji wa wapigakura ulipoanza jijini Dar es Salaam likawa moja ya mada kuu katika mitandao ya kijamii. Baadhi ya watumiaji wa mitandao ya kijamii, japo wachache, walionesha ufahamu wao juu ya kupiga kura kama ni haki ya kisiasa na kiraia kwa kila mtu. Ujumbe katika Twitter na katika Facebook ulihamasisha watu wajitokeze kujiandikisha. Waliweka picha zilizoambatana na ujumbe uliowakumbusha watu kwenda kujiandisha na hatimaye wapige kura. Ujumbe mwingine wa picha ulionyea watumiaji wa Twitter na Facebook wakionyesha kadi zao za kupigia kura zikiambatana na ujumbe kama “Kura yangu nahitaji inipatie huduma bora ya afya kwa jamii yangu, panga foleni”- (with my vote I expect better health services for my community-stand in a queue for the card), au “tayari nasubiri kupiga kura- kura ni wajibu,” au “ukiipata, hongera mwulize mwenzako unacho?”




*Mitandao ya kijamii ikihimiza uandikishaji wa upigaji kuran*



Wapigakura Wakionesha Kadi zao Mpya

Baadhi ya watumiaji wa Twitter walianzisha kurasa maalumu #*Kijana Kujiandikisha* ukiwa na wafuasi ambao walikuwa wakiwahamasisha watu wengine kwenda kujiandikisha kwa ajili ya kupiga kura. Baadhi ya jumbe zilionesha wasiwasi kutokana na kuharibika haribika kwa mitambo ya BVR, muda mfupi wa uandikishaji, uandikishwaji wa wasiokuwa raia wa nchi na mambo mengine yaliyoharibu mchakato. Lakini kulikuwa na watumiaji wengine wa Twitter na Facebok walioonesha faida ya kujiandikisha na kuwakosoa wale waliojiandikisha kwa ajili ya kupata vitambulisho.

#### *7.3.2 BVR katika Vyombo vya Utangazaji wa Habari*


Mwenendo wa vyombo vya utangazaji wa habari katika kufuatilia habari za BVR haukutofautiana sana na ule wa magazeti. Habari nyingi za vyombo hivi zilipendelea maeneo ya mijini, hususani Dar es Salaam, Arusha, Mbeya na Mwanza. Habari zao kuhusu BVR zilitokana na taarifa kutoka kwa wanasiasa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Habari zinazotokana na matukio ya migogoro na kushindwa kwa mchakato zilipata nafasi kubwa zaidi kuliko habari za kuonesha mafanikio. TEMCO ilibaini kuwa vituo vya East Africa, Clouds na TBC vilikuwa msitari wa mbele kuhamasisha vijana kwenda kujiandikisha.

Siku ya tarehe 22 Julai, 2015, saa 3.48 asubuhi, rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Jakaya Mrisho Kikwete, akiwa katika ziara nchini Australia alituma ujumbe wa Twitter uliolenga kuwahamasisha Watanzania kujiandikisha. Ujumbe ulisomekahivi: "Kila Mtanzania ana fursa ya kushiriki kwenye maamuzi yahusuyo mustakabali wa nchi kupitia kura yake. Fursa hii inapatikana kwa kujiandikisha." Ujumbe huo ulitumwa upya na watumiaji wengine 56 kufikia saa kumi na dakika 51 jioni ya siku hiyo hiyo, huku watu 65 wakiuunga mkono na kuwa na maoni mengi. Siku hiyo hiyo Zito Kabwe, Mbunge wa Kigoma na kiongozi wa ACT-Wazalendo, alituma ujumbe wa Twitter kwa madhumuni hayo hayo. Hata hivyo, TEMCO iliona licha ya kuwapo kwa ujumbe kutoka kwa watu mashuhuri, magazeti na televisheni hazikutumia, ingawa zilizalisha mijadala mirefu na mikali ndai ya mitandao.

### 7.4 Habari Za Kampeni Na Mchakato Wa Kupiga Kura.

Wakati wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 Twitter na Facebook yalitoa fursa ya kutoa na kusambaza habari na picha papo kwa papo na hivyo kuwezesha urahisi wa kufuatilia matukio na michakato ya uchaguzi kipindi chote cha uchaguzi. Mitandao ya kijamii ilitumika kama

majukwaa ya kufanyia kampeni na propaganda. Vyama vya siasa, wagombea na hata wafuasi na washabiki wao walianzisha kurasa na akaunti kwenye Facebook na Twitter zilizotumika kushawishi kuungwa mkono, kushirikisha taarifa na kujenga mwamko kuhusu masula ya sera na mengine yahusuyo uchaguzi na siasa. TEMCO observation noted several cases of abuse. Some users resorted to posting of false information with the intention of discrediting rival political parties and candidates. Ufuatiliaji wa TEMCO uligundua matukio mbalimbali ya matumizi mabaya ya mitandao ya kijmii. Baadhi ya watumiaji walianza kusambaza habari zao upotoshaji kwa ajili ya kuwadhalilisha wapinzani na wagombea wao. Wafuatiliaji wa TEMCO walishuhudia uwepo wa matoleo maalumu ya kwenye Mitandao ya magazeti ya Nipashe, Mwananchi na Rai yakiwa na taarifa za upotoshaji na zisizo na kweli dhidi ya mgombea wa urais wa CHADEMA/UKAWA. TEMCO ilifuatilia suala hilo na kujua kuwa hata Baraza la Habari la Tanzania lilibaini pia suala hili na kulitolea taarifa katika moja ya machapisho yake ya wiki juu ya ufuatiliaji wa uchaguzi. TEMCO iliarifiwa pia kuwa wahariri wa magazeti husika walikanusha kuchapisha matoleo hayo ya kwenye mitandao.





***Kielelezo 7-2 Matumizi Mitandao kwa Wanasiasa/Vyama***

Ufuatiliaji wa TEMCO wa matumizi ya mitandao ya kijamii wa vyama vya siasa ulionesha kuwa baadhi ya vyama vya siasa viliitumia fursa hiyo vizuri zaidi kuliko vingine. CHADEMA ilikuwa na kurasa nyingi zaidi na wafuasi wengi zaidi katika Facebook ikifuatia na CCM na vyama vingine katika muungano wa UKAWA. Zito Kabwe wa ACT-Wazalendo alikuwa mwanasiasa mashuhuri zaidi kwa kuwa na kurasa nyingi za Facebook zilizoanzishwa kwa jina lake. Hata hivyo, bado si rahisi kuthibitisha kuwa mitandao ya kijamii inaweza kutumika kama nyenzo nzuri sana ya kampeni ya uchaguzi, kwa vile matumizi ya simu zinazoweza kutumia mitandao ya kijamii bado ni kwa Watanzania walioko mijini ambako intaneti ziko kwa uhakika na zina kasi ya kutosha.

### *7.4.1 Kampeni za Urais katika Television*

TEMCO ilifuatilia habari kuu za siku za vituo vitano vya televisheni. Channel Ten, Independent Television (ITV), Star TV na Mlimani TV. TEMCO iligundua kuwapo na hali ya vyombo vya habari kuwakweza wanasiasa binafsi badala ya vyama vyao vya siasa. Kwa mfano, Dr Wilbrod Slaa, Katibu Mkuu wa CHADEMA, alipata muda mwingi sana katika

televisheni zote ukilinganisha na wagombea wote wa uchaguzi kwa pamoja. Kama inavyoonyeshwa katika chati, hatuba ya Dr Slaa aliyotangazia umma kuacha uongozi wa CHADEMA kama katibu mkuu, akipinga kuteuliwa kwa Edward Lowasa kuwa mgombea wa CHADEMA ilitangazwa katika vituo vinne vya televisheni kwa wakati mmoja. Kwa nyongeza TBC 1 ilirudia matangazo ya hotuba hiyo siku hiyo hiyo jioni, kipindi kilimalizika usiku wa manane; Star TV iliomba fursa ya kufanya mahojiano siku tatu baadaye na kuwa na kipindi kilichodumu kwa takribani saa moja; na AZAM TV ilifanya kipindi kingine cha saa moja na Dr Slaa kufuatia hotuba ile ya kujitoa.




*Kielelezo 7-3: Vyama vya siasa katika televisheni*

### *7.4.2 Usawiri wa Uchaguzi kwa Picha na Katuni*

Matumizi ya picha na katuni katika magazeti na mitandao ya kijamii kuwasilisha matukio, vyama vya siasa na masuala anwai yahusuyo uchaguzi katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 hakumithilika. Picha na katuni vilitumika kwa wingi saa kusawiri mtu au dhana fulani. TEMCO ilibaini kuwa lilikuwa jambo la kawaida kuona kwenye kurasa za mbele za magazeti kuwa na picha zilizowafananisha wagombea wawili wa urais katika uwezo wao wa kuvutia wafuasi wengi sana kwenye mikutano ya uchaguzi, kitu kilichotumiwa kama ishara yakupendwa kwa chama cha siasa au wagombea wao wa urais.








Wafuatiliaji wa TEMCO waliona pia kuwa magazeti yalitumia picha kwa nia ya kupiga chuku kwa kuweka picha kubwa kubwa katika ukurasa wa mbele zikiambatana na maneno (vichwa vya habari) yaliyolenga wasomaji kuangalia ukubwa wa kundi la wahudhuriaji na mgombea.

Picha zilizo nyingi zilikuwa zikipigwa kutoka jukwaani, huku mpiga picha akisimama nyuma ya mgombea aliyekuwa akihutubia umati, au walikuwa wakitumia mitambo ya kupiga picha za angani. Katika mitandao ya kijamii picha zilitumika kuonesha ubaya wa mgombea, kumdhalilisha na kumuoanisha mgombea na ujumbe wenye taarifa hasi dhidi yake. Picha zilibadilishiwa matumizi na kutumika katika muktadha mpya kwa lengo la kukidhi haja za kipropaganda za watumiaji wa mitandao ya kijamii.

Katuni zilibebesha jukumu kubwa na muhimu katika kuelezea maoni ya wasanifu. Kundi moja la katuni lilisaili wagombea waliokuwa wakiweka ahadi mpya bila kufanya tathmini ya kama walifanikisha ahadi walizoziweka kipindi kilichopita. Kundi lingine lilikosoa serikali, CCM na NEK.

### *7.4.3 Magazeti*

Kielelezo 7-4 inaonesha idadi ya habari ndani ya magazeti zilizohusu uchaguzi. Matokeo ya ufuatiliaji wa TEMCO unabainisha utofauti wa uhabarishaji wa masuala mbalimbali kati ya magazeti na vyombo vya habari vya utangazaji. Ufananisho wa uandikaji wa habari za uchaguzi kabla ya kampeni Agosti 22 hadi Okotaba 24 na habari baada ya uchaguzi umeonesha kuwa habari zinazohusu uchaguzi zilipungua kwa asilimia kumi na tano mara baada ya uchaguzi kwisha.





***Kielelezo 7-4: Habari za Uchaguzi katika Magazeti (Januari-Novemba, 2015)***


### *7.4.4 Habari za Magazeti kwa Kuzingatia Dhamira*

Wakati wa kampeni za uchaguzi TEMCO ilibaini kuwa habari za uchaguzi zilizojitokeza pia katika makala zilihusu ilani za uchaguzi za vyama ya siasa vikubwa. Hata hivyo hilo halikufanyika kwa kuchapisha kurasa kwa kurasa kutoka ilani za uchaguzi zenyewe bali kwa kuandika habari kutoka kwa viongozi wakati wakihutubia mikutano ya uchaguzi. Kwa ujumla habari nyingi zilijikita kwenye mambo yasiyo ya msingi, hususanii habari zilizoelekea kudhalilisha wagombea wa urais, ubunge na udiwani. Kama inavyoonyeshwa katika Kielelezo 7-5 TEMCO ilibaini kuwa habari za kashfa ndizo zilizokuwa nyingi zaidi ya habari zingine zote za uchaguzi. Kwa mfano gazeti la Uhuru kwa muda mwingi lilijikita katika kuandika habari hasi dhidi ya mgombea urais wa CHADEMA, Edward Lowasa,(Agosti 7-Lowasa

Aipasua Vipande Ukawa; Septemba 14, -Lowassa hakujiuzulu, Alifukuzwa-Makamba; Agosti 1-Vuai: Lowasa ni Mroho wa Madaraka—amtaka aache Uwongo)




***Kielelezo 7-5: Habari za kashfa zilizojitokeza magazetini***




***Kielelezo 7-6: Yaliyojiri kweye mikutano ya hadhara***

## 7.5 Hitimisho na Mapendekezo

### *7.5.1 Hitimisho*

Mwenendo wa vyombo vya habari katika kipindi cha uchaguzi kwa ujumla ulionesha kiwango cha kutia moyo cha kuheshimu misingi ya maadili na weledi. Baraza la Habari la Tanzania lilitayarisha kanuni za maadili kwa lengo la kuongoza uandikaji wa habari za uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, ambalo lilikuwa ni jambo la kupongezwa. Hata hivyo baadhi ya vyombo vya habari walishikwa na wadau wenye nguvu kubwa za kisiasa na fedha., na badala ya kupaza sauti cha wapigakura kama ilivyoelekezwa katika kanuni za maadili ya uandishi wa habari vijijini. Majukwaa ya mitandao ya kijamii yaliendelea kutumika na kupendwa na vijana hasa katika maeneo ya mijini. Hata hivyo ilikuwa ni vigumu sana kuithibiti mitandao ya kijamii. Juhudi za mamlaka ya mawasiliano (TCRA) na hata za serikali za kutunga sheria ya makosa ya kimtandao ilikusudiwa kuzuia athari mbaya na matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii

hazikuwa na matokeo chanya. Kilichotokea ni kuwa matumizi mabaya ya mitandao yakihusisha pia kashfa dhidi ya wagombea, na upotoshaji wa habari uliendelea katika mitandao ya kijamii ukilinganisha na kwenye magazeti na vyombo vya habari vya utangazaji.

***7.5.2 Mapendekezo***

TEMCO inawasilisha mapendekeo yafuatayo kwa kuzingatia yaliyobainishwa na TEMCO katika ufuatiliaji wa mwenendo wa vyombo vya habari katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015;

(i) Vyombo vya habari vinawajibika kutenga muda na nafasi sawa kwa vyama vya siasa na wagombea wa nafasi mbalimbali; urais, ubunge na udiwani;
(ii) Serikali inawajibika kusimamia kikamilifu mitandao ya kijamii ili kuzuia matumizi mabaya hususanii ya kutoa taarifa potofu, ya kudanganya na za kupiga chuku kuhusiana na uchaguzi;
(iii) Vyombo vya habari vinatakiwa kuzingatia kanuni za maadili ya uandishi wa habari na hususani za wakati wa uchaguzi; na
(iv) Vyombo vya habari za utangazaji vinatakiuwa kuongeza vipindi kuhusiana na makundi maalumu ili kuongeza uwezekano wa wao kushiriki katika uchaguzi kama wagombea au wapigakura.

# CHAPTER 8
# USHIRIKISHWAJI WA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU KATIKA CHAGUZI

## 8.1 Utangulizi

Sura hii inatathmini ushirikishwaji wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika uongozi wa uchaguzi, zoezi la uandikishaji wa wapigakura , mpango wa elimu ya mpigakura, mchakato wa uteuzi wa wagombea, kampeni na upigaji wa kura. Matokeo ya utafiti huu yamepatikana kwa kupitia maandiko ya ripoti za waangalizi wa uchaguzi, ripoti za tume za uchaguzi, ripoti za vyombo vya habari, ripoti za TEMCO na sheria mbalimbali za uchaguzi. Matokeo ya utafiti huu yanawasilishwa na kujadiliwa katika vipengele kumi na moja utangulizi ukiwa umejumuishwa. Kipengele cha pili kinajikita katika muktadha wa sheria zilizowekwa kwa ajili ya kulinda makundi maalum na kipengele cha tatu kinahusu ushirikishwaji wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika uongozi wa chaguzi. Aidha kipengele cha nne kinaangalia ushirikishwaji wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika mchakato wa kujiandikisha kama wapigakura kwa mfumo mpya wa BVR. Kipengele cha tano kinahakiki mpango wa elimu ya mpigakura kwa makundi maalum, na kipengele cha sita kinashughulikia mambo ya nayohusiana na upendekezwaji wa wagombea kwa kuzingatia makundi maalum. Wakati kipengele cha saba kimeangazia ushirikishwaji katika kampeni za uchaguzi, kipengele cha nane kimeshughulikia ushirikishwaji wa makundi hayo maalum kama wapigakura. Vipenge tisa na kumi vimeshughulikia matokeo ya uchaguzi, matukio baada ya uchaguzi na maendeleo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Kipengele cha mwisho kimehitimisha sura hii na kutoa mapendekezo.

## 8.2 Muktadha wa Sheria Katika Kulinda Makundi Maalum.

Uchaguzi ni moja kati ya vipengele muhimu katika kukuza ushirikishwaji na uwajibikaji katika mifumo ya siasa za kidemokrasia. Ushirikishwaji wa makundi yote ya kijamii ni muhimu katika kuufanya uchaguzi uwe huru na wa haki.Tanzania imekuwa ikiendesha chaguzi kila baada ya kipindi cha miaka mitano (5) kabla na baada ya kuanzisha mfumo wa vyama vingi mwaka 1992. Haki za wanawake, vijana, watu wenye ulemavu na makundi mengine zinalindwa na katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Katika Ibara 12 (2) ya katiba inaeleza wazi kuwa kila mtu ana haki ya kutambuliwa na kuheshimiwa utu wake. Aidha, ibara ya 13 (4) inakataza kubaguliwa kwa mtu yeyote na mtu mwingine au utawala. Ibara ya 21 (1) inatoa haki kwa raia wote kushiriki katika maswala ya uongozi wa nchi ama moja kwa moja au kwa uwakilishi. Hata hivyo, licha ya kuwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu wanatambulika kuwa ni wadau muhimu katika mchakato wa kufanya maamuzi, bado ushirikishwaji wao katika mzunguko wote wa mchakato wa uchaguzi umeendelea kuwa finyu.

Kihistoria, ushirikishwaji wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika chaguzi umekuwa sio wa kiwango cha kuridhisha. Mara chache sana makundi haya huchaguliwa kama wagombea wa nafasi mbalimbali. Mara nyingi makundi haya, yanaandaliwa kuwa watoa burudani katika kampeni, walinzi, mawakala na wapigakura kuliko kuwa viongozi. Hata hivyo, zikiibuka vurugu kipindi cha uchaguzi, wanawake, vijana na watu wenye ulemavu huwa waathirika wakuu wa vurugu hizo. Matokeo ya ushirikishwaji finyu wa makundi haya yamepelekea kuibuka kwa mapambano ya kimaslahi yasiyokwisha yanayoendeshwa na

makundi mbalimbali yakidai usawa katika chaguzi na katika vyombo vya maamuzi. Moja ya matunda ya mapambano hayo kwa Tanzania ni uanzishwaji wa mkakati mahususi kwa wanawake, maarufu kama mfumo wa viti maalum kwa wanawake, kama inavyoelezwa katika ibara ya 66 (1) (b) na ibara 78 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka1977 na kifungu cha 86 cha sheria za uchaguzi (Sura ya 343) ya mwaka 1985.

Sheria hizo kwa pamoja zinaelekeza kuwa asilimia arobaini (40%) ya wajumbe wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lazima wawe wanawake. Chama lazima kipate asilimia tano ya kura zote za uchaguzi wa wabunge ili kiwe na sifa ya kutoa mbunge wa viti maalum (Tume ya Uchaguzi (NEC), 2015). Vile vile sheria inaagiza kuwa theluthi moja (1/3) ya madiwani waliochaguliwa katika kila Halmashauri iwe kwa ajili ya wanawake kupitia mpango wa viti maalum. Hata hivyo, ni vyema ifahamike kuwa mfumo huu wa viti maalum umelenga zaidi ushirikishwaji wa wanawake na hauko mahususi kwa vijana pamoja na watu wenye ulemavu.

Mwaka 2015, Watanzania walienda kwenye sanduku la kura kwa mtindo ambao unaweza ukatafsiriwa na wachambuzi wa kisiasa kuwa uchaguzi wa kipekee katika historia ya siasa za vyama vingi Tanzania. Upekee huo unaweza kufasiliwa na mambo makuu matatu; kwanza kuwepo kwa ushindani mkubwa ndani ya vyama vikubwa vya siasa , ambavyo ni, CHADEMA, CUF na CCM; Pili, Muungano wa vyama vya upinzani 'UKAWA' ambao ulichochea kiwango cha ushindani; na tatu ni kuongezeka kwa kiwango cha uelewa kwa vijana na wanawake juu ya umuhimu wa kushiriki katika mchakato wa uchaguzi. Miongoni mwa mambo yaliyochangia hali hii ni jitihada za wadau mbalimbali katika kuhamasisha uchaguzi jumuishi. Miongoni mwa wadau hao ni vyama vya siasa, asasi za kiraia (CSOs), vyombo vya habari, na taasisi nyinginezo. Hata hivyo, kiwango cha ushirikishwaji na ujumuishwaji wa makundi yenye mahitaji maalum katika uchaguzi wa mwaka 2015 hakifahamiki. Kwa hiyo, swali muhimu litakalojibiwa katika sura hii ni: Je, kwa kiwango gani makundi maalum na mahitaji yao yalizingatiwa katika mchakato wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2015?

### 8.3 Ushirikishwaji wa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu katika Usimamizi wa Uchaguzi

Ushirikishwaji wa makundi maalum katika usimamizi wa uchaguzi unaweza kutathiminiwa kwa kupima muundo wa tume za chaguzi, ambayo ni, Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), ambayo inasimamia uchaguzi wa muungano na wa serikali za mitaa Tanzania bara na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) inayoshughulikia chaguzi za Zanzibar.

Kwa ujumla, muundo wa NEC na ZEC katika ngazi ya makamishina inaonekana kupendelea zaidi wanaume kuliko wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa utofauti wa kijinsia katika uchaguzi wa mwaka 2015, ulikuwa mkubwa zaidi kwenye ZEC ukilinganisha na NEC. Hapakuwa na mwanamke hata mmoja kati ya makamishina wote saba wa ZEC tofauti na NEC ambayo walao ilikuwa na makamishina watatu wanawake kati ya saba. Hii inaashiria mabadiliko ukilinganisha na uchaguzi wa mwaka 2010 ambapo NEC walikuwa na makamishina wanawake wawili tu kati ya saba (Ripoti ya waangalizi wa Commonwealth, 2010).

Kwa bahati mbaya, vijana, na watu wenye ulemavu hawakupata fursa ya ukamishina katika NEC na ZEC. Katika ngazi za maafisa uchaguzi kwenye wilaya mbalimbali ushirikishwaji wa wanawake na vijana ulikuwa mkubwa. Kwa mfano, asilimia hamsini (50 %) na asilimia thelathini (30%) ya wasimamizi wa uchaguzi walioajiriwa katika Majimbo ya Kilolo na Mafinga walikuwa ni wanawake mtawalia[10]. Mwanza na Morogoro-Kilombero, zaidi ya nusu (61% and 53%) mtawalia, ya wasimamizi walioajiriwa walikuwa wanawake. Pia, asilimia 46% ya wazimamizi wa uchaguzi walikuwa ni vijana katika majimbo ya Morogoro[11]. Hata hivyo, watu wenye ulemavu hawakupata ushirikishwaji wenye tija kama wasimamizi wa uchaguzi katika ngazi ya wilaya. Watu watatu tu wenye ulemamavu katika jimbo la Mafinga na watano katika jimbo la kilombero waliajiriwa kuwa wasimamizi wa uchaguzi katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015[12]. Hii inaonesha kuwa ingawa ushirikishwaji wa wanawake na vijana katika ngazi ya wilaya umeonekana kuwa wa kuridhisha, ushirikishwaji wa watu wenye ulemavu bado umebakia kuwa mdogo.

## 8.4 Ushirikishwaji wa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu katika Zoezi la Uandikishwaji wa Wapigakura.

Zoezi la uandikishaji wa wapigakura mwaka 2015 limevutia makundi mengi ikiwa ni pamoja na makundi ya watu wenye mahitaji maalum. Kwa mujibu wa ripoti ya NEC, asilimia hamsini na tatu (53%) ya wapigakura waliojiandikisha ilikuwa ni wanawake. Jedwali 8-1 linaonesha kwa muhtasari idadi ya wapigakura waliojiandikisha kwa makundi katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 .

***Jedwali 8-1: Wapigakura Waliojiandikisha kwa Umri na kwa Jinsia katika Uchaguzi mkuu wa Mwaka 2015***

| Na | Umri | Me | Ke | Jumla | % Me | % Ke |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 18-35 | 6,155,613 | 6,738,964 | 12,894,576 | 27% | 30% |
| 2 | 36-50 | 2,744,422 | 2,946,247 | 5,690,668 | 12% | 13% |
| 3 | 50-na zaidi | 1,900,555 | 2,264,990 | 4,165,544 | 8% | 10% |
| Jumla | | 10,800,589 | 11,950,200 | 22,750,789 | 47% | 53% |

Chanzo: Ripoti yaTume ya Uchaguzi (NEC), 2015.

Ikiwa takwimu za vijana (wanawake na wanaume wenye umri kati ya miaka 18-35) zitawekwa pamoja, itaonesha kuwa zaidi ya nusu (57%) ya wapigakura waliojiandikisha walikuwa vijana. Kwa misingi hii, wanawake na vijana walijiandikisha kwa wingi katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015. Hii inamaanisha kuwa wanawake na vijana ndio waliokuwa wapigakura wengi zaidi katika uchaguzi wa mwaka 2015. Kwa bahati mbaya, daftari la wapigakura halikuonesha idadi ya watu wenye ulemavu waliojiandikisha, hivyo, ni vigumu kujua idadi ya watu wenye ulemavu waliojiandikisha kama wapigakura.

[10] RipotiRipoti ya Mkoa ya TEMCO (2015) –Iringa

[11] RipotiRipoti ya Mkoa ya TEMCO (2015)–Morogoro; RipotiRipoti ya Mkoa ya TEMCO (2015) - Mwanza

[12] RipotiRipoti ya Mkoa ya TEMCO (2015) -Iringa

## 8.5 Programu za Elimu ya Mpigakura Zilizolenga Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu.

Uchaguzi wa mwaka 2015 ulivutia asasi za kiraia 451. Watoaji wengine wa elimu ya mpigakura walikuwa ni pamoja na vyombo vya habari na vyama vya siasa kama moja ya majukumu yao ya msingi. Asasi mbalimbali za kiraia zilitoa elimu ya mpigakura Tanzania. Miongoni mwa asasi hizo ni; Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (Legal and Human Rights Center- LHRC), Chama cha Wanawake Wanasheria Tanzania (Tanzania Women Lawyers Association-TAWLA), Umoja wa Wanawake Wabunge (the Coalition of Women MPs (ULINGO), Wakala wa Kukuza Maendeleo Kigoma ( Development Promotion Agency - KDPA), *Femina Hip* pamoja na Taasisi zisizo za kiserikali Sumbawanga (Sumbawanga Non-Governmental Organizations (SUMANGO), Kituo cha Maendeleo ya watoto yatima cha Baraka (*BAGODE)*, na Chama cha Walemavu Tanzania (Association of PWDs -CHAWATA), kutaja baadhi tu. Kwa mfano, ULINGO waliendesha semina Iringa Mjini kwa ajili ya kuwajengea uwezo wanawake watiania wagombea ili waweze kushiriki uchaguzi kwa ushindani.Vilevile Chama cha Walemavu Tanzania (CHAWATA) waliendesha semina Iringa Mjini iliyowahusisha watu wenye ulemavu iliyolenga kuwajuza haki na wajibu wao katika kipindi cha uchaguzi. Kilolo, asasi mbili za kiraia zijulikanazo kama, FEMA na KARIBU ziliripotiwa kuendesha elimu ya mpigakura katika kata tatu; Ilula, Lugalo na Nyalumbu kati ya kata 24 za jimbo la Kilolo. Mafinga na Mufindi Kusini, kulikuwa na asasi moja ya kiraia inayojulikana kwa jina la *Restless Development Tanzania* ambayo iliripotiwa kutoa elimu ya mpigakura katika kata kadha wa kadha.

Huko Zanzibar, ZEC ilianzisha *Zanzibar Voter Education Reference Group* (ZANVERG) ambapo wajumbe wake walitokana na asasi za kiraia pamoja na taasisi za serikali zilizojumuisha Chama cha wanawake wanasheria wa Zanzibar (Zanzibar Female Lawyers Association ZAFELA), Chama Cha taasisi zisizo za kiserikali (Association of Non-governmental Organizations in Zanzibar (ANGOZA), Chama cha Walemavu Zanzibar, Jukwaa la Vijana Zanzibar (ZYF) na Ofisi ya msajili wa vyama vya Siasa Zanzibar (the Office of Registrar of Zanzibar ID Card (ZANID)[13]. Jumuiya ya Kitaifa ya Watu Walemavu wa Macho ya Zanzibar (ZANAB), Umoja wa Jinsia Zanzibar (ZGC) Jumuiya ya Waandishi wa Habari wanawake Tanzania (TAMWA) pia walihusishwa katika kutoa elimu ya mpigakura.[14]

## 8.6 Vyombo vya Habari

Vyombo vya habari (redio, runinga, magazeti na mitandao ya kijamii) havikuachwa nyuma katika kuhamasisha wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kushiriki kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka 2015. Kwa mfano; Runinga ya Africa Mashariki (The East Africa Television -EATV) kwa kushirikiana na Redio ya Afrika Mashariki (East Africa Radio) walianzisha kampeni ya kuwahamasisha vijana iliyokuwa inajulikana kwa jina la '*Zamu Yako 2015'* iliyolenga kuwahamasisha vijana kushiriki katika uchaguzi (The Guardian, February 2015). Kampeni ililenga kuongeza uelewa kwa vijana juu ya umuhimu wa kujiandikisha katika daftari

[13] RipotiRipoti ya Mkoa ya TEMCO -Mjini Magharibi
[14] RipotiRipoti ya Mkoa ya TEMCO - Mjini Magharibi

la kudumu la wapigakura kwa kuzingatia kuwa karibia asilimia sitini na nane 68% ya Watanzania ni vijana (The Guardian, February 2015).

Redio za kiraia Kigoma, kama vile Radio Joy and Kwizera huko Kasulu walishiriki katika shughuli muhimu ya kuelimisha wapigakura ili washiriki katika ngazi mbalimbali katika mchakato wa uchaguzi. Vilevile, Arusha, redio kama vile Sunrise, Triple A na Radio one ziliripotiwa kuwa ziliandaa program zilizolenga kuelimisha wapigakura. Asasi nyingine za kiraia kama vile TAMWA walitumia vyombo vya habari vya umma kama vile Shirika la Utangazaji la Tanzania (TBC), na vituo vya watu binafsi kama vile Runinga Huru (ITV), Runinga ya Afrika Mashariki (EATV), *Clouds TV* and Channel Ten kwa ajili ya kutoa elimu ya mpigakura

**8.7 Taasisi za Kimataifa**

Kulikuwa na programu mbalimbali za kujenga uwezo zilizoendeshwa na taasisi za kimataifa zilizokuwa na lengo la kuhamasisha na kuhakikisha kuwa makundi yote yanashiriki kwa usawa katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015. Baadhi ya taasisi hizo ni pamoja na; UNDP, UN-women, *Action Aid Tanzania* (AATZ), *Restless Development*, na BBC *Trust Fund.* Programu ya Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) inajulikana kama Mradi wa uwezeshaji kidemokrasia wenye lengo la kuunga mkono maendeleo ya kidemokrasia Tanzania katika mzunguko mzima wa uchaguzi. Pamoja na mambo mengine, program hii ililenga katika kuhakikisha kuwa ujumuishwaji wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika chaguzi na siasa unakuzwa kupitia uwezeshwaji wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu; kuimarisha jitihada za vyama vya siasa na kukuza ujumuishwaji wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu; kuwafunda wagombea wanawake ambao wanakaribia kuanza kampeni; kuwakumbusha wanaume kuhusu umuhimu wa ushiriki wa wanawake katika siasa na kuunga mkono na kuhakikisha kuwa miundo mbinu ya amani ya kitaifa inakuzwa ili kupunguza na kuzuia migogoro ya chaguzi na migogoro ya kijinsia inayolenga wanawake na wasichana (UNDP-DEP, 2013-2016).

Vilevile, taasisi inayoitwa Shirika la Msaada lijulikanalo kama Action Aid Tanzania (AATZ) lilishirikiana na Programu ya Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) kuandaa kongamano la kitaifa la wanawake watakaogombea katika nafasi mbalimbali za uongozi kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka 2015. Kongamano hilo liliwaleta pamoja zaidi ya wanawake 100, vijana na watu wenye ulemavu kutoka katika Mikoa yote ya Tanzania bara na visiwani ambao walishirikishana yanayowapasa kufanya pamoja na changamoto walizopitia wanawake *(*AATZ, 2015*)*. Katika kongamano hilo, Balozi na Rais wa Zamani wa Bunge la Umoja wa Afrika (UA) Mh. Getrude Mongela alikuwa miongoni mwa wazungumzaji wakuu aliwafundisha wanawake wagombea mbinu za kushinda uchaguzi. Kwa mfano aliwatia moyo wanawake wagombea kwa kusema kuwa;“Ninakubali kuwa kuna vikwazo mbalimbali katika vyama vya siasa kwa wanawake. Muwe makini kwa vyama vyenu……Wanaweza kuwapotosha kutoka kwenye nia asilia ya kuwa kiongozi” alisema Mh. Mongela (AATZ, 2015).




*Wanawake katika Programu ya Kujengewa Uwezo ya AATZ*

Mbali na hayo, *UN-women* waliwezesha asasi za kiraia kutoa elimu ya mpigakura katika kampeni ya kuelimisha wanawake kuhusu haki ya kuchagua wagombea ambao ni chaguo lao. Miongoni mwa asasi hizo za kiraia ni pamoja na ULINGO, TGNP and TAMWA. Pia UN-Women waligharamia maandalizi ya vipeperushi mbalimbali vilivyolenga kujenga uelewa kwa wanawake na makundi mengine kabla ya siku ya kupiga kura. Moja ya vipeperushi vya *UN-Women* kilikuwa kinasomeka kama ifuatavyo:

> “Ni haki ya kila mtu kuchagua mgombea anayempenda” Mume: “Mke wangu, weka kitambulisho chako vizuri ili uweze kumchagua Bwana Tabasamu awe kiongozi wetu.” Mke: “Ni haki yangu ya kikatiba kuchagua kiongozi ninayempenda.” kijana: “Mama yuko sahihi baba” (The Guardian, February 2015).

### 8.8 Vyama vya Siasa

Vyama vya siasa hususani CCM, CUF, CHADEMA na ACT- Wazalendo walikuwa ni wadau wakuu wa elimu ya mpigakura katika majimbo yote nchini. Hili lilifanyika katika mikusanyiko ya kampeni ambapo vyama viliwahamasisha mashabiki wao kujitokeza kwa wigi kupiga kura.



*Wakazi wa Kijiji cha Ugesa katika Kata ya Ihalimba Mufindi Kusini Wakimsikiliza Shabiki Mwenzao wa CHADEMA Akielezea jinsi ya Kupiga Kura.*

Wanawake na vijana walionekana kuhudhuria katika mikusanyiko mingi ya mikutano. Hata hivyo, wakati mikutano mingi ya CCM ikionekana kuhudhuriwa na wanawake wengi zaidi, mikutano ya CHADEMA ilihudhuriwa na vijana wengi zaidi.




*Timu ya Kampeni ya CHADMA katika Mkutano wa Kampeni Arusha.*[15]

Aidha, baadhi ya vyama vya siasa vilitoa upendeleo maalum kukidhi mahitaji ya watu wenye ulemavu katika mikutano yao ya kampeni. Hii ilionekana katika moja ya mikutano ya kampeni katika uwanja wa Mashujaa jimbo la Mafinga ambapo wataalamu wa lugha za alama

[15] RipotiRipoti ya Mkoa ya TEMCO-Arusha

walionekana wakiwaongoza watu wenye ulemavu wa macho ambao walihudhuria katika kampeni kama inayoonekana katika picha ifuatayo:




*Wasichana Wawili wenye Matatizo ya Kusikia Wakifuatilia kwa Makini Mgombea Ubunge wa CCM Mafinga kwa Msaada wa Mtaalam wa Lugha za Alama (Mfasiri)*

**8.9 Changamoto katika Utoaji wa Elimu ya Mpigakura**

Kulikuwa na changamoto mbalimbali zilizoathiri utoaji wa elimu ya mpigakura wakati wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2015. Kwa ujumla, ripoti za matokeo ya utafiti wa TEMCO mikoani zinaonesha kuwa kuna ushahidi finyu sana unaothibitisha kuwa elimu ya mpigakura ilitolewa kwa mawanda mapana sehemu za vijijini Tanzania. Vyombo vya habari vilifaidisha zaidi wakazi wa mijini. Programu za Redio zilikuwa haziwafikii wananchi waishio vijijini ambapo kuna mawanda madogo ya usikikaji wa vyombo vya habari. Kwa mfano; iliripotiwa kuwa mawanda madogo ya usikikikaji wa vyombo vya habari uliwanyima fursa ya habari watu wa jimbo la Kalambo katika Mkoa wa Rukwa. Vivyo hivyo kwa watu wa Kigoma, kwa mfano, Redio Joy na Kwezira ambazo ziliwekeza sana katika utoaji wa elimu ya mpigakura zilijikita zaidi katika manispaa ya Kigoma, Kasulu na sehemu chache za maenneo ya Muhambwe kwa mtawalia. Vilevile, iligundulika kuwa hata mtandao wa intaneti haukuwa na nguvu ya kutosha kuwawezesha watu wa tegemee kwenye mitandao ya kijamii (kama vile tovuti, wavuti, *instagram,viber* na *facebook*) kupata elimu hiyo [16].

Halikadhalika, elimu ya mpigakura iliyotolewa katika kampeni za vyama vya siasa ilitawaliwa mno na siasa, Kwa mfano, chama cha CHADEMA kilikuwa kinawaelekeza wafuasi wake kuwa wakapige kura kwa kutumia kalamu zao na kuacha kutumia za NEC kwa sababu zile za NEC zimechezewa ili kuharibu matokeo ya kura zao. Pia wafuasi hao wa CHADEMA walielekezwa namna ya kukunja karatasi ya kura ili kudhibiti mbinu zozote za wizi zilizopangwa kwa kutumia mkunjo wa karatasi ya kura na kubadilisha matokeo. Kulikuwa na

[16] RipotiRipoti ya Mkoa ya TEMCO -Kigoma

imani kuwa kama karatasi ya kura haitakunjwa kama walivyoelekezwa kuna hatari ya tiki kuhama kutoka kwa mgombea wa CHADEMA kwenda kwamgombea wa CCM. Kwa upande mwingine CCM walihimiza kuwa kama wafuasi wake hawatapigia chama chao watachunguza na kuwatambua. Mchakato wa BVR unawawezesha kujua wamempigia mgombea yupi. Hii ni baadhi tu ya mifano michache ya namna ambavyo vyama vya siasa vinaweza kutumia mikutano ya kampeni na vikao vidogovidogo kutoa taarifa zisizo za uhakika ili kuweza kujikusanyia kura.

### 8.10 Uteuzi wa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu

Uteuzi wa wagombea katika nafasi mbalimbali ulifanyika katika ngazi mbili, ambazo ni, uteuzi wa ndani ya chama na uteuzi wa mabaraza ya kusimamia uchaguzi (NEC na ZEC). Kwa ujumla, ujumuishwaji wa vijana na wanawake kama wagombea katika uchaguzi wa mwaka 2015 uliongezeka ukilinganisha na chaguzi zilizotangulia. Hata hivyo, idadi ya wanawake waliochaguliwa kama wagombea ilikuwa ndogo ukilinganisaha na ile ya wanaume. Pia, idadi ya wagombea wenye ulemavu ilikuwa hairidhishi kabisa katika vyama vyote.

#### *8.10.1 Uteuzi wa ndani ya Vyama vya Siasa.*

Kulikuwa hakuna mtindo mmoja wa uteuzi uliotumiwa na vyama vyote vya siasa. Kulikuwa kuna mitindo tofauti ya uteuzi kati ya jimbo moja na jingine na kati ya vyama vya siasa. Kwa mujibu wa ripoti za mikoani za TEMCO (2015), aina kuu mbili zilizotumika kupendekeza wagombea zilikuwa ni pamoja na kupiga kura za maoni na kuteua tu mgombea bila kupigiwa kura na wanachama (hand-picking style). Mfumo wa kupiga kura za maoni ambao ulionekana kuwa shirikishi ulitumiwa zaidi na vyama maarufu (CCM, CHADEMA na CUF) wakati mtindo wa kuteua na kumpendekeza mgombea bila kupigiwa kura ukitumiwa zaidi na vyama vidogo. Hata hivyo, baadhi ya vyama vidogo vilitumia pia mfumo wa kura za maoni katika kuteua wagombea ubunge; kwa mfano ACT- Wazalendo.



*Mke wa Raisi, Salma Kikwete Akiwa na Mke wa Mgombea Uraisi kwa Tiketi ya CCM, Janet Magufuli*

### *8.10.2 Uteuzi wa Mgombea Urais ndani ya Vyama vya Siasa*

Jumla ya vyama vinane vya siasa viliteua mgombea urais katika uchaguzi wa mwaka 2015. Vyama hivyo ni; CCM, CHADEMA, CUF, CHAUMMA, TLP, UPDP, ADC na NRA, ACT-Wazalendo. Tofauti na chaguzi zilizotangulia, uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 ulivutia idadi kubwa ya wanawake na vijana kutia nia ya kugombea nafasi mbalimbali ikiwemo nafasi ya urais. Kwa mfano, ndani ya CCM, wanawake waliotia nia ni pamoja na Dkt. Helena Elinawiga, Amina Salum Ali, Dkt. Mwele Malecela, Dkt. Asha Rose Migiro, Monica Mbega, Ritta Mlaki (TEMCO, 2015). Mbio hizo zilizokuwa na jumla ya wagombea arobaini na mmoja (41) zilivutia zaidi pale wanawake wawili (Asha-Rose Migiro na Amina Salum Ali) walipoweza kushindana hadi kufikia nafasi ya wagombea watano bora wa nafasi ya urais. Hata hivyo, Dkt. John Pombe Magufuli alishinda na kumchagua Waziri wa Nchi katika ofisi ya Makamu wa Rais (wa mambo ya Muungano) Bi, Samia Suluhu Hassan, kuwa mgombea mwenza katika uchaguzi wa rais wa Jamhuri ya muungano wa Tanzania. Hii ni mara ya kwanza katika historia ya siasa za Tanzania kuona mwanamke akichaguliwa kuwa mgombea mwenza katika nafasi ya Makamu wa Rais.




*Wagombea Watano Bora kwa Nafasi ya Urais ndani ya CCM*

Zaidi ya hayo, mwanamke mmoja Bi. Anna Mghwira kutoka ACT-Wazalendo aliteuliwa na NEC kuwa mgombea urais katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015.



*Mgombea Uraisi kwa Tiketi ya ACT-Wazalendo, Bi. Anna Mghwira*

***8.10.3 Uteuzi wa Wagombea Ubunge na Madiwani ndani ya Vyama vya Siasa.***

Kwa ujumla, mchakato wa kupendekeza na kuteua wagombea katika majimbo mengi uliwapendelea zaidi wanaume kuliko wanawake. Kwa mfano; Arusha, wagombea wote 25 waliofanikiwa kugombea udiwani walikuwa ni wanaume. Kilolo, kati ya wajumbe 103 wa CCM waliochukua fomu ili kupata ridhaa ya vyama vyao ya kugombea udiwani, 99 walikuwa wanaume na 4 tu ndio walikuwa wanawake.


*Mgombea Ubunge wa CCM Jimbo la Muleba Kusini, Anna Tibaijuka Akiwa katika Mkutano wa Kampeni*

Mufindi Kusini, jumla ya wajumbe 58 wa CCM waliochukua fomu za udiwani katika kata 11, kati yao 54 walikuwa wanaume na 4 walikuwa wanawake. Kama ilivyokuwa kwa CCM,

kiwango cha ushirikishwaji wa wanawake kwa CHADEMA kilikuwa chini sana katika halmashauri ya Kilolo. Kati ya wajumbe 76 wa CHADEMA waliochukua fomu ili kutafuta ridhaa ya vyama vyao kugombea udiwani, 74 walikuwa wanaume na 2 walikuwa wanawake. Wagombea waliopendekezwa walikuwa 24 ambapo wanaume walikuwa 22 na wanawake walikuwa wawili (2) tu, sawa na asilimia nane (8%).



*Mgombea Ubunge wa CHADEMA Jimbo la Kawe, Halima Mdee Akiwa katika Mkutano wa Kampeni*

Aidha, baadhi ya wabunge walioshinda viti maalum katika chaguzi zilizopita waliamua kugombea moja kwa moja majimboni. Kwa mfano Ester Bulaya (CHADEMA), Prudeciana Kikwembe (CCM), Mary Mwanjelwa (CCM), Suzan Kiwanga (CHADEMA), Magdalena Sakaya (CUF) and Suzan Lyimo (CHADEMA) (Mwananchi, 20, Aprili, 2015). Haya ni miongoni mwa matokeo mazuri ya programu za kujengea uwezo zilizoendeshwa na wadau mbalimbali kuhamasisha wanawake kugombea katika majimbo. Kwa mfano, Dkt. Mwanjelwa aliripoti kuwa programu mbalimbali za mafunzo ambazo zilitolewa kwao ikiwa ni pamoja na ile ya *UN-Women* na UNDP imewajengea ujasiri wa kutosha kuwawezesha kugombea katika majimbo (Mwananchi, 20, Aprili, 2015).

### *8.10.4 Changamoto za Mchakato wa Uteuzi wa Wagombea ndani ya Yyama.*

Kiwango cha ushirikishwaji wa makundi maalum kama wagombea katika kipindi cha uchaguzi wa mwaka 2015 kilikuwa kidogo sana. Tofauti na wanawake na vijana, uteuzi wa watu wenye ulemevu ulionekana kuwa mdogo mno. Pia, kulikuwa na malalamiko kuwa watu wenye ulemavu hususani wale wenye ulemavu wa ngozi walikuwa hawako huru kushiriki kikamilifu katika mchakato wa uchaguzi kwa kuogopa kutokana na mauaji ya kutisha ya watu wenye ulemavu wa ngozi nchini (Gazeti la Nipashe, Februari, 2015).




*Kampeni Dhidi ya Mauaji ya Albino.*

Ni katika jimbo la Lindi mjini tu ambapo Bw. Salum Barwany alichaguliwa kuwa mgombea akitetea kiti chake kupitia CUF.

### *8.10.5 Uteuzi wa NEC na ZEC*

Kwa ujumla, wanawake wachache tu ndio walishinda katika uteuzi ndani ya vyama na hivyo ni wachache tu ndio waliidhinishwa na NEC kugombea katika nafasi mbalimbali. Hata hivyo, ukilinganisha na chaguzi za mwaka 2005 na 2010 ambapo wanawake walikuwa asilimia 13 na 18 za wagombea wote wa ubunge mtawalia, katika uchaguzi wa 2015, asilimia 19 ya wagombea wote walikuwa wanawake. Licha ya ongezeko la wagombea wanawake kutoka asilimia 13 katika uchaguzi wa mwaka 2005 hadi asilimia 19 katika uchaguzi wa mwaka 2015 bado uwiano wa wagombea wanawake imeendelea kuwa mbali kutoka ile ya wanaume. Katika uchaguzi wa wabunge kwa mwaka 2015, 10% na 6% ya wagombea waliopendekezwa ndani ya CCM na CHADEMA walikuwa wanawake mtawalia. Jedwali 8-2 Iinaonesha idadi ya wagombea walioidhinishwa na NEC katika vyama vinne vya siasa.

***Jedwali 8-2: Wagombea Ubunge Waliochaguliwa kutoka katika Vyama vya Siasa, 2015***

| Na | Chama | Me | Ke | Asilimia ya Wanawake |
|---|---|---|---|---|
| | CCM | 241 | 26 | 10% |
| | CHADEMA | 181 | 11 | 6% |
| | CUF | 118 | 15 | 11% |
| | ACT | 179 | 30 | 14% |

Chanzo: NEC, 2015

### *8.10.6 Nafasi za Viti Maalum vya Wanawake*

Kulikuwa hakuna mtindo mmoja uliotawala katika uteuzi wa wanawake katika nafasi za viti maalum vya wanawake katika ngazi zote kwa vyama vyote vya siasa. Kila chama cha siasa kilikuwa na mtindo wake wa kuteua wanawake wa viti maalum. Kwa mfano kwa CCM,

mchakato wa upendekezaji wa wanawake wa viti maalum katika nafasi za viti maalum katika ngazi ya ubunge ilifanywa na baraza kuu la wanawake katika ngazi ya wilaya ambapo wanawake wawakilishi kutoka kila tawi la CCM ndani ya wilaya walipata nafasi ya kumchagua mgombea wampendaye kupitia utaratibu wa kupiga kura ya maoni. Vivyo hivyo katika ngazi ya Kata[17].

Kwa CHADEMA, uteuzi wa wanawake katika nafasi za viti maalum hususani katika ngazi ya ubunge ulifanyika kwa kupiga kura za maoni na wanawake wa CHADEMA kupitia BAWACHA au CHAVITA, kisha majina yalipelekwa katika ngazi ya kamati kuu kwa ajili ya upendekezaji wa mwisho. Hata hivyo katika maeneo mengine CHADEMA walitumia mbinu ya kuteua bila kuchaguliwa na wanachama (hand-picking style). Kwa vyama vilivyobakia, ni mtindo huu wa kuteua bila kupigiwa kura na wanachama ndio uliotawala. Katika baadhi ya vyama, wale ambao hawakupendekezwa katika vyama vyao waliamua kuhamia kwenye vyama vingine. Kwa mfano; huko Arusha, wagombea 19 kati ya 24 ambao hawakupendekezwa kugombea kupitia CCM walihamia CHADEMA. [18].

Mchakato wa kupendekeza wanawake wa viti maalum katika baadhi ya vyama ulionekana kuharibika kutokana na tuhuma za rushwa na upendeleo. Kwa mfano; Mwenyekiti wa zamani wa UKAWA nyanda za juu kusini Bw. Jacob Kalua alielezea kutoridhishwa kwake na mchakato wa upendekezwaji wa wanawake wa viti maalum akilalamika kuwa baadhi ya wanawake waliopendekezwa hawajawahi kuwa wanachama hai wa chama (The Citizen, 13 Novemba, 2015).

Pia, tuhuma za upendeleo ziliibuliwa pia katika Mkoa wa Iringa ambapo baadhi ya viongozi wa CHADEMA waliripoti kuwa Iringa ilipewa nafasi tatu ambazo zilihusisha wagombea ambao walijiunga kwenye chama katika dakika za mwisho wakati maeneo kama Songwe ambapo CHADEMA ilishinda viti vitatu hawajapewa hata nafasi moja. Katibu wa CHADEMA wa Mbarali, Bw. Nicolaus Lyaumi pia alilalamika kuwa hao waliochaguliwa kwenye nafasi za viti maalum hawakustahili kwasababu walikuwa hawajulikani na wanachama wa Mkoa wa Mbeya (The Citizen, 13 Novemba, 2015).

### *8.10.7 Uteuzi wa Wanawake wa Viti Maalum Katika Ngazi ya Tume ya Uchaguzi*

Tume zote (NEC na ZEC) zimepewa mamlaka kisheria kupendekeza majina ya wagombea yaliyopelekwa kwao na vyama ya siasa vyenye usajili. Mgawanyo wa viti maalum kati ya vyama vyenye sifa unazingatia kanuni maalum iliyoelezwa katika sheria za uchaguzi za Tanzania. Katika uchaguzi wa wabunge wa Muungano, kulikuwa na viti maalum vya wanawake 113 (40%) ya wa bunge wote katika bunge ambavyo vilitakiwa kugawanywa kwa vyama vya siasa vilivyopata angalau 5% ya kura zote za ubunge. Viti hivyo viligawanywa kwa vyama vya siasa kwa uwiano wa asilimia za kura walizopata katika uchaguzi wa wabunge.

---

[17] RipotiRipoti Mkoa ya TEMCO - Mwanza
[18] RipotiRipoti Mkoa ya TEMCO -Arusha

Kwa uchaguzi wa udiwani, sheria inaagiza moja ya tatu (1/3) ya madiwani waliochaguliwa katika kila wilaya iwe kwa ajili ya viti maalum vya wanawake. Kwa misingi hii, jumla ya kata katika uchaguzi wa mwaka 2015 zilikuwa 3,957. Ambapo kulikuwa na jumla ya viti 1,406 vilivytakiwa kugawanywa kwa vyama mbalimbali vya siasa kwa uwiano wa kura walizopata katika uchaguzi wa udiwani.

### *8.10.8 Ushirikishwaji katika Kampeni za Uchaguzi*

Kampeni za uchaguzi wa mwaka 2015 zilivuta makundi yote hususanii wanawake na vijana. Kwa mujibu wa ripoti za mikoani za TEMCO, mahudhurio ya wanawake, vijana na watu wenye ulimevu yalikuwa makubwa. Kwa mfano; katika jimbo la Mjini Magharibi, wengi wa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu walihudhuria mikutano ya kampeni hususanii ya UKAWA na CCM[19]. Pia, Kigoma mikutano mingi ya kampeni ilitawaliwa na wanawake zaidi kuliko wanaume[20]. Hata hivyo, iliripotiwa kuwa baadhi ya wanawake walipewa motisha kama vile pesa na nguo ili washawishike kuhudhuria. Pia, ilionekana kuwa mahudhurio kati ya wanawake na vijana yalitofautiana kutoka chama kimoja na kingine. Kwa mfano; katika majimbo ya Rukwa wanawake walihudhuria kwa wingi zaidi kuliko wanaume[21]. Katika majimbo ya Njombe, vijana walitawala kwa wingi zaidi katika mikutano ya kampeni ya CHADEMA[22].



*Mgombea Uraisi kwa Tiketi ya ACT-Wazalendo, Ms. Anna Mghwira, Akihutubia mkutano wa Kampeni*

## 8.11 Vitendo vya Ubaguzi dhidi ya Wanawake

Wakati wa kampeni, kulikuwa na matukio ya ubaguzi hususani dhidi ya wagombea wanawake. Kwa mfano, katika jimbo la Ilemela, mgombea wa CHADEMA Bw. Hyness Kiwia alinukuliwa

[19] RipotiRipoti Mkoa ya TEMCO -Mjini Magharibi
[20] RipotiRipoti Mkoa ya TEMCO -Kigoma
[21] RipotiRipoti Mkoa ya TEMCO -Rukwa
[22] RipotiRipoti Mkoa ya TEMCO -Njombe

akisema mambo yafuatayo katika mikutao yake ya kampeni."Msimchague Anjelina Mabula…………..hajaolewa, ameachika. Sasa kama alishindwa kuongoza ndoa yake, hata nafasi ya ubunge hataiweza….."[23]



*Mgombea ubunge kwa tiketi ya CCM jimbo la Ilemela, Angelina Mabula katika Mkutano wa Kampeni*

Hii ni kinyume na sheria ya maadili ya uchaguzi ya mwaka 2010, kifungu cha 124 A cha sheria ya uchaguzi ibara ya 1. ya mwaka 1985 inayoelekeza vyama vyote vya siasa, viongozi wa serikali, wapigakura pamoja na tume ya uchaguzi kuzingatia maadili ya uchaguzi. Hasa hasa, kifungu 2.2 (b) kinazuia wagombea kutumia matusi, vitisho, udhalilishaji wa aina yoyote ile dhidi ya mgombea mwingine[24].




*Mgombea Mwenza wa Uraisi kwa Tiketi ya CCM, Samia Suluhu Hassan katika Moja ya Mikutano ya Kampeni*

[23] RipotiRipoti ya Mkoa ya TEMCO-Mwanza
[24] (ibid)

Vilevile, wagombea wanawake walipata nafasi finyu ya kusikika katika vyombo vya habari ukilinganisha na wanaume. Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na umoja wa wanawake Tanzania (TAMWA), wagombea wanawake walipata asilimia kumi na moja (11%) tu ya mawanda ya machapisho katika vyombo vya habari Septemba na Octoba 2015 ukilinganisha na wagombea wa kiume[25].

**8.12 Ushirikishwaji wa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu kama Wapigakura**

Mwitikio wa wapigakura ulikuwa mkubwa katika uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 kuliko ilivyokuwa katika uchaguzi wa mwaka 2010. Wengi wa Watanzania wanawake kwa wanaume vijana, wengi wao wakiwa ndio mara yao ya kwanza kupiga kura walijitokeza kwa wingi kupiga kura. Kwa mujibu wa NEC wengi wa wapigakura waliojiandikisha walikuwa wanawake na vijana (The Citizen, 26 Octoba, 2015). Iliripotiwa zaidi kuwa hata mazingira ya kupigia kura yalikuwa mazuri ambapo wanawake wajawazito, wanawake wenye watoto wadogo na watu wenye ulemavu walipewa kipaumbele katika zoezi la upigaji kura[26].




*Mwanamke Kikongwe Akipiga Kura yake ya Kumchagua Rais katika Uchaguzi wa Tarehe 25 Octoba, 2015*

**8.13 Matokeo ya Uchaguzi kwa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu**

Uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 kwa kiasi fulani umeongeza idadi ya wanawake waliochaguliwa moja kwa moja kutoka katika majimbo. Katika chaguzi zilizofanyika wakati wa chama kimoja kuanzia 1965-1980 hapakuwa na mwanamke yeyote aliyechaguliwa kutoka jimbo lolote Tanzania. Mwanamke mmoja tu alichaguliwa mwaka 1985 na wawili mwaka1990. Katika chaguzi nne zilizopita tangu kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi

[25] http//www.thehabari.com/wanahabari-waliminya-sauti-za-wanawake-uchaguzi-mkuu-tamwa

[26] RipotiRipoti Mkoa ya TEMCO Rukwa

Tanzania 1992, idadi ya wanawake waliochaguliwa moja kwa moja kutoka majimboni ilikuwa ndogo sana, 8 (3.4%) mwaka 1995, 12 (5.2%) mwaka 2000, 17 (7.3%) mwaka 2005 na 21 (8.7%) mwaka 2010. Katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 idadi ya wabunge waliochaguliwa moja kwa moja kutoka majimbo imeongezeka na kufikia 25 sawa na asilimia (9.5) kama inavyooneshwa kwenye Jedwali 8-3.

***Jedwali 8-3: Wanawake Waliochaguliwa Kupitia Viti vya Majimboni***

| Na | Jina | Chama cha Siasa | Jimbo | Mkoa |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Jenista Mhagama | CCM | Peramiho | Ruvuma |
| 2 | Janeth Mbene | CCM | Ileje | Mbeya |
| 3 | Angelina Mabula | CCM | Ilemela | Mwanza |
| 4 | Mary Chatanda | CCM | Korogwe Urban | Tanga |
| 5 | Mary Nagu | CCM | Hanang’ | Manyara |
| 6 | Margreth Sitta | CCM | Urambo | Tabora |
| 7 | Bona Kalua | CCM | Segerea | Dar es Salaam |
| 8 | Hasna Mwilima | CCM | Kigoma South | Kigoma |
| 9 | Mboni Mhita | CCM | Handeni Rural | Tanga |
| 10 | Hawa Ghasia | CCM | Mtwara Rural | Mtwara |
| 11 | Bahati Ali Abeid | CCM | Mahonda | Kaskazini Unguja |
| 12 | Dr. Ashatu Kijaji | CCM | Kondoa | Dodoma |
| 13 | Dr. Pudesiana Kikwembe | CCM | Kavuu | Katavi |
| 14 | Stella Martin Manyanya | CCM | Nyasa | Ruvuma |
| 15 | Lolesia Bukwimba | CCM | Busanda | Geita |
| 16 | Mwantakaje Haji Juma | CCM | Bububu | Mjini Magharibi |
| 17 | Prof. Anna Tibaijuka | CCM | Muleba South | Kagera |
| 18 | Saada Mkuya Salum | CCM | Welezo | Mjini Magharibi |
| 19 | Ester Bulaya | CHADEMA | Bunda | Mara |
| 20 | Pauline Gekul | CHADEMA | Babati | Manyara |
| 21 | Suzan Kiwanga | CHADEMA | Mlimba | Morogoro |
| 22 | Halima Mdee | CHADEMA | Kawe | Dar es Salaam |
| 23 | Ester Matiko | CHADEMA | Tarime Urban | Mara |
| 24 | Naghenjwa Kaboyoka | CHADEMA | Same East | Kilimanjaro |
| 25 | Magdalena Sakaya | CUF | Kaliua | Tabora |

Chanzo: Ripoti za Waangalizi wa TEMCO, 2015

Kati ya wagombea 1,250 waliogombea viti majimboni, 237 sawa na asilimia 19 walikuwa wanawake. Kati ya wanawake 237 waliogombea, ishirini na tano tu (25) sawa na asilimia 10.5 ndio walioshinda. CCM ilipata 18 (sawa na asilimia 69.2), CHADEMA viti 6 (sawa na asilimia 23.1) na CUF viti 2 (sawa na asilimia 7.7). Kuna ongezeko kidogo la wanawake waliogombea viti vya majimboni ukilinganisha na uchaguzi wa mwaka 2010 ambapo kati ya wagombea 1036 wanawake walikuwa 191 (sawa na asilimi 18.4). Vile vile kwa kupitia mfumo wa viti maalum, wanawake wengi zaidi walichaguliwa kuwa wabunge na wengine madiwani. Jedwali 8-4

linaonesha idadi ya viti maalum vilivyopatikana katika chama husika kulingana na idadi ya kura walizoshinda katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015.

***Jedwali 8-4: Wanawake Wabunge na Madiwani Waliochaguliwa Kupitia Mfumo wa Viti Maalum***

| Chama cha Siasa | Idadi ya Wabunge | Idadi ya Madiwani |
|---|---|---|
| CCM | 66 | 1,021 |
| CHADEMA | 37 | 280 |
| CUF | 10 | 70 |
| ACT-Wazalendo | - | 6 |
| NCCR-Mageuzi | - | 6 |

Chanzo: NEC, 2015

Licha ya matumaini yaliyokuwepo, wanawake walipata asilimia tisa (9%) tu ya wabunge wote waliochaguliwa moja kwa moja kutoka majimboni. Baadhi ya wanawake wasingeweza kushinda majimboni na katika kata na hata katika mbio za urais kutokana na sababu mbalimbali miongoni mwa sababu hizo zikiwa ni ushindani mkali uliokuwepo, mfumo dume majimboni, kipato kidogo kwa wagombea wanawake, na mawanda finyu ya kusikika kwa wanawake katika vyombo vya habari. Licha ya hizi kasoro za kijamii na kitamaduni, muktadha wa kisheria ulitoa haki sawa kwa wanawake na wanaume katika uchaguzi wa wabunge na madiwani.




*Mgombea Urais kwa Tiketi ya ACT-Wazalendo Akiingia katika Uwanja wa Mashujaa Dodoma kwa Ajili ya Kufanya Kampeni.*

## 8.14 Mwelekeo Baada ya Uchaguzi

### *8.14.1 Uteuzi wa Rais kwa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu*

Kwa kujua umuhimu wa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu, rais mpya aliyechaguliwa Tanzania aliwashirikisha vijana, wanawake na watu wenye ulemavu katika Baraza Lake. Wanawake 22 waliteuliwa kuwa mawaziri. Hawa ni pamoja na, Angelina Mabula, Jenister Mhagama, Ummy Mwalimu, Dkt. Suzan Kolimba, Stella Manyanya, Anastazia Wambura, Prof. Joyce Ndalichako na Angela Kairuki. Pia, rais alimchagua mtu mwenye ulemavu Bw.

Posi Abdallah kuwa waziri msaidizi. Vile vile, mwanamke mmoja (Dkt. Tulia Akson Mwansasu) kuwa mbunge, na baadae alichaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano.

## 8.15 Hitimisho na Mapendekezo

### *8.15.1 Hitimisho*

Matokeo ya utafiti huu kama yalivyowasilishwa katika sura hii yanaashiria kuwa kuna safari ndefu kwa makundi maalum kushirikishwa kikamilifu katika michakato ya uchaguzi hususani kama wagombea na hatimaye kuibuka washindi. Hata hivyo, ukilinganisha na chaguzi zilizotangulia kuanzia mwaka 1995, uchaguzi wa mwaka 2015 kwa kiasi fulani umepiga hatua mbele katika ushirikishwaji wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika ngazi mabalimbali za mchakato wa uchaguzi. Matokeo pia yanaonesha kuwa elimu ya mpigakura haikuwa ya kutosha, na kwa kiwango kikubwa ilijikita zaidi mijini, na hivyo kuacha sehemu kubwa ya majimbo ya vijijini yakiwa hayajaelimishwa kuhusu haki na wajibu wao katika mchakato wa uchaguzi.

### *8.15.2 Mapendekezo*

Sura hii inapendekeza yafuatayo:

(i) Vyama vya siasa vinapaswa kuangalia upya demokrasia ndani ya vyama vyao katika mchakato wa uteuzi wa wagombea hususani wale wa viti maalum vya wanawake;

(ii) Vyama vya siasa vinapaswa kufasili sera ya upendeleo maalum itakayotoa fursa kwa makundi maalum kugombea nafasi mbalimbali za uongozi;

(iii) Serikali inapaswa kuendesha elimu ya mpigakura ambayo italenga makundi yote yaliyoko mijini na vijijini mwa Tanzania na

(iv) Serikali inapaswa iweke sheria itakayoongoza kuchaguliwa kwa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu kama wagombea ndani ya vyama vyao.

## CHAPTER 9
## MCHAKATO WA KUPIGA KURA, KUHESABU KURA NA KUTANGAZA MATOKEO

### 9.1 Utangulizi

Sura hii inajikita katika shughuli za siku ya uchaguzi: Kupiga kura, kuhesabu kura kutangaza matokeo pamoja na matukio na mambo mengine baada ya uchaguzi. Sura imegawanywa katika sehemu 11, ikiwa inaanza na utangulizi huu. Sehemu ya pili inahusu uandaaji wa vituo vya kupigia kura na maandalizi ya upigaji kura. Sehemu ya tatu inahusu masuala ya utaratibu wa polisi na usalama katika siku ya uchaguzi. Sehemu ya nne inajikita katika utendaji wa wasimamizi wa uchaguzi na sehemu ya tano inahusu mchakato wa kuhesabu kura na kubandika matokeo. Sehemu ya sita inaangazia utangazaji wa chaguzi za udiwani, ubunge na urais. Sehemu ya saba inajadili mahudhurio ya wapigakura yakifuatiwa na matukio na mambo mengine baada ya uchaguzi katika Sehemu ya nane. Malalamiko ya uchaguzi ni mada ya sehemu ya tisa ikifuatiwa na tathimini ya jumla ya shughuli za siku ya uchaguzi katika sehemu ya kumi. Hitimisho na mapendekezo yanatolewa katika sehemu ya mwisho.

### 9.2 Uandaaji wa Vituo vya Kupigia Kura na Maandalizi ya Kupiga Kura

Ripoti za waangalizi wa uchaguzi wa TEMCO zinaonesha kwamba vituo vingi vya kupigia kura viliandaliwa katika majengo ya umma kama vile shule na ofisi za serikali za mitaa. Ripoti pia zinaonesha kuwa katika kituo kikuu kimoja cha kupigia kura, kulikuwa na vituo vingi vya kupigia kura. Kwa ujumla, katika maeneo ambayo hakukuwa na majengo ya umma kwa ajli ya kuandalia vituo vya kupigia kura, mahema yalijengwa na kufanywa kuwa vituo vya kupigia kura, hasahasa, katika maeneo ya pembezoni mwa miji. Vibanda vya kupigia kura vilitengenezwa kwa kutumia mbao laini ambazo zinaweza kujengwa na kubomolewa ndani ya dakika chache.



*Utengenezaji wa Vibanda vya Kupigia Kura*



*Wapigakura Wakikagua Majina yao kwenye Orodha ya Majina Iliyobandikwa Nje ya Kituo cha Kupigia Kura*

Ripoti za waangalizi wa TEMCO zinaonesha kwamba wasimamizi wa uchaguzi na wadau wengine walikagua vifaa vya uchaguzi kabla ya kuvifungua vituo vya kupigia kura ili kuhakikisha kwamba kila kitu kipo.




*Rais Kikwete Akitumbukiza Karatasi yaKura katika Boksi la Kura katika Kituo cha Kupigia kura*

Vifaa vya uchaguzi ni pamoja na daftari la kudumu la mpigakura, maboksi ya kura, karatasi za kura za urais, ubunge na udiwani, muhuri, wino wa muhuri, wino usiofutika, fomu (Na.13, 14, 15, 16, 17, 18, 19, na 20); tepu za kufungia maboksi ya kura, selo-tepu, pini za kubania karatasi, wembe; bahasha (Na. 2A, 2B, 2C, 3A, 3B, 3C, 4, 5A, 5B, 5C, 6A, 6B, 6C, 7A, 7B, na 7C);

karatasi za majaribio, kalamu, taa zenye betrii, vibanda vya kupigia kura; na fomu za matokeo (Na.21A, 21B, 21, C, sehemu A na B).



*Mgombea Urais wa CCM Dkt. John Joseph Magufuli katika Kituo cha Kupigia Kura*


Ripoti za TEMCO zinaonesha kuwa zaidi ya theluthi mbili ya vifaa vya uchaguzi vilikuwepo kama inavyoonyeshwa katika Jedwali 9-1.

***Jedwali 9-1: Kufaa kwa Vifaa vya Uchaguzi***

| Kufaa kwa vifaa vya uchaguzi | Aina ya vifaa vya uchaguzi | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Orodha ya wapigakura | Karasi za kura | Mihuri | Wino | Fumu | Kalamu |
| Vinafaa | 93.6 | 95.3 | 92.7 | 95.3 | 93.0 | 92.6 |
| Vinafaa na kwa kiasi fulani vibovu | 2.7 | 1.1 | 3.4 | 0.9 | 1.5 | 1.3 |
| Havifai | 0.3 | 0.5 | 0.6 | 0.5 | 0.6 | 0.8 |
| Havikuwepo | 3.4 | 3.1 | 3.3 | 3.3 | 4.9 | 5.3 |
| Jumla | 100.0 | 100.0 | 100.0 | 100.0 | 100.0 | 100.0 |

Chanzo: Ripoti za Uwandani za Waangalizi wa TEMCO, 2015

Ripoti za waangalizi wa TEMCO zinaonesha maboksi ya kura za uchaguzi wa urais, ubunge na udiwani yalipangwa katika namna ambayo wapigakura waliweza kuyabainisha kwa urahisi, kama inavyoonyeshwa katika Jedwali 9-2




*Mgombea Urais wa CHADEMA Bw. Edward Lowassa katika Kituo cha Kupigia Kura*

***Jedwali 9-2: Mpangilio wa Maboksi ya Kura katika Vituo vya Kupigia Kura***


| Mpangilio wa Maboksi ya Kura katika vituo vya kupigia kura | Asilimia | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Ndiyo | Hapana | Hakuna | Jumla |
| Maboksi ya kura yalipangwa kama inavyotakiwa | 86.0 | 9.0 | 5.0 | 100 |
| Maboksi ya kura yaliwekwa karibu na msimaizi mkuu kwa ajli ya kusimamia kwa urahisi | 77.4 | 14.0 | 8.6 | 100 |
| Maboksi ya kura yalionekana kuwa matupu | 94.2 | 1.0 | 4.8 | 100 |

Chanzo: Ripoti za Uwandani za Waangalizi wa TEMCO, 2015

## 9.3 Ufunguaji wa Vituo vya Kupigia Kura na Upigaji Kura

Ripoti za waangalizi wa TEMCO zinaonesha kwamba vituo vingi vilifunguliwa dakika chache kabla ya saa 1:00 asubuhi, muda ambao ulikuwa rasmi kwa upigaji kura. Ripoti za TEMCO zinaonesha kuwa vituo vya kupigia kura 4,157 kati ya 7,316 vilifunguliwa kati ya saa 1:00 asubuhi na 1:29 asubuhi, sawa na asilimia 56.7 na vituo vya kupigia kura 83, sawa na asilimia 1.1, vilifunguliwa baada ya saa 2:00 asubuhi kama inavyoonyeshwa katika Kielelezo 9-1.

*Kielelezo 9-1: Muda wa Kufungua Vituo vya upigia kura*




| | Not Opened | 6.00 – 6.29 am | 6.30 – 6.59 am | 7.00 – 7.29 am | 7.30 – 7.59 am | 8.00 am or more | DK |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| % | 0.1 | 22.2 | 16.28 | 56.82 | 2.71 | 1.13 | 0.77 |
| Frequencies | 7 | 1624 | 1191 | 4157 | 198 | 83 | 56 |


Chanzo: Ripoti za Uwandani za Waangalizi wa TEMCO, 2015

Ilishuhudiwa pia kuwa vituo vya kupigia kura vichache vilichelewa kidogo kufunguliwa kutokana na sababu mbalimbali kama vile kuchelewa kupokea vifaa vya uchaguzi au matatizo ya kiutendaji. Tume ya Taifa ya Uchaguzi iliahirisha uchaguzi katika vituo vya kupigia kura vya Kimara Stopover, Kimara Temboni, Saranga na Sinza jijini Dar es Salaam kutokana na kuchelewa kusambaza vifaa vya uchaguzi.

Ripoti za TEMCO zilionesha kwamba upigaji kura ulifanyika katika hali ya amani. Aidha, ripoti zinaonesha kwamba utaratibu wa hatua-nne za upigaji kura katika vituo vya kupigia kura ulizingatiwa. Hatua hizo ni pamoja na; (i) Wapigakura kuangalia majina yao katika orodha ya majina iliyobandikwa nje ya vituo vya kupigia kura ili kuhakikisha kwamba wako katika vituo sahihi; (ii) ukaguzi wa vitambulisho vya mpigakura uliofanywa na maafisa wa uchaguzi na mawakala wa vyama vya siasa kabla ya mtu kuruhusiwa kuendelea na upigaji kura; (iii) mpigakura kupewa karatasi tatu zenye muhuri za kupigia kura ili aende katika kibanda cha kupigia kura akapige kura (iv) Uchovyaji wa kidole cha mpigakura katika wino usiofutika. Ripoti za TEMCO zinaonesha kwamba wapigakura wote walipanga mstari wakisubiri zamu zao kupiga kura. Hata hivyo, mahali pengi mama wajawazito au wanaonyonyesha, wazee na walemavu walipewa kipaumbele kwa kuruhusiwa kupiga kura bila kupanga mstari.

Vilevile, ripoti za waangalizi wa TEMCO zilionesha kwamba, kwa ujumla iliwachukuwa wapigakura wengi muda wa kati ya dakika moja na dakika tano kupiga kura kuanzia muda ambao walihudumiwa na Msimamizi wa Uchaguzi mpaka kumaliza upigaji kura wenyewe kama inavyoonyeshwa katika Kielelezo 9-2

*Kielelezo 9-2: Muda Aliotumia kila Mpigakura Kupiga Kura*




| | 1-5 minutes | 6-10 minutes | 11-15 minutes | 16-20 minutes | 21-30 minutes | More than 30 minutes | Did not answer |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| F | 6,273 | 810 | 46 | 7 | 8 | 9 | 163 |
| % | 85.74 | 11.07 | 0.63 | 0.1 | 0.11 | 0.12 | 2.23 |

Chanzo: Ripoti za Uwandani za Waangalizi wa TEMCO, 2015

Ripoti za TEMCO pia zinaonesha kuwa ingawa kulikuwa na mfumo wa kukagua vitambulisho vya mpigakura kabla ya kuwaruhusu kupiga kura, ukaguzi wa vitambulisho vya mpigakura ulikabiliwa na changamoto kadhaa, tazama katika Jedwali 9-3.

*Jedwali 9-3: Changamoto katika Kubaini Vitambulisho vya Wapigakura*


| Changamoto | Asilimia | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Ndiyo | Hapana | Waliokkosa majina | Jumla |
| Wapigakura waliokosa majina yao katika daftari la kudumu la mpigakura waliruhusiwa kupiga kura | 2.5 | 31.2 | 66.25 | 100 |
| Wasio na vitambulisho vya mpigakura waliruhusiwa kupiga kura | 0.5 | 31.6 | 67.85 | 100 |
| Wapigakura wenye vitambulisho vya kupigia kura na waliosajiliwa hawakuruhusiwa kupiga kura | 1.07 | 30.0 | 68.92 | 100 |
| Wapigakura hawakukaguliwa kama wana alama ya wino kabla ya kupiga kura | 4.7 | 26.3 | 68.89 | 100 |

Chanzo: Ripoti ya Uwandani ya Waangalizi wa TEMCO

### 9.4 Kufungwa kwa Vituo vya Kupigia Kura

Ripoti za waangalizi wa TEMCO zinaonesha kuwa vituo vingi vya kupigia kura vilifungwa rasmi saa 10:00 jioni, muda ambao ulikuwa rasmi kama inavyoonyeshwa katika Kielelezo 9-3.

*Kielelezo 9-3: Muda wa Kufungwa kwa Vituo vya Kupigia Kura*



| | Before 4.00pm | 4.00pm | 4:01 - 4:59 pm | 5:00 – 5:59 pm | 6:00 – 6:59 pm | 7:00 PM | After 7:00 pm | DK |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| F | 260 | 4931 | 1124 | 400 | 173 | 38 | 119 | 271 |
| % | 3.55 | 67.4 | 15.36 | 5.47 | 2.36 | 0.52 | 1.63 | 3.7 |

Chanzo: Ripoti ya Uwandani ya Waangalizi wa TEMCO

Kwa ujumla, mchakato wa upigaji kura ulienda vizuri katika vituo vingi vya kupigia kura vilivyoshuhudiwa na TEMCO. Hata hivyo, ripoti zinaonesha matukio machache ambapo baadhi ya vituo vya kupigia kura vilifungwa kwa muda kutokana na sababu kadhaa kama inavyoonyeshwa katika Jedwali namba 10.4. Kati ya vituo vya kupigia kura 7,316 vilivyoshuhdiwa na TEMCO, vituo vya kupigia kura 56 (asilimia 0.8) vilifungwa kwa muda kutokana na vurugu kati mashabiki wa vyama vinavyogombania kinyang'anyiro; vituo vya kupigia kura 222 (asilimia tatu) kwa sababu ya kupungukiwa na vifaa vya kupigia kura; na vituo vya kupigia kura 37 (asilimia 0.5) kwa sababu ya hali ya hewa mbaya.

Kama ilivyotakiwa na sheria ya uchaguzi, vyama vingi maarufu vya siasa vilisambaza mawakala wa vyama katika vituo vya kupigia kura. Waangalizi wa TEMCO walibaini kuwa mawakala wa vyma wengi walitoka CCM na CHADEMA/UKAWA. Kati ya vituo vya kupigia kura 6,579, CCM ilikuwa na mawakala 6,475 (asilimia 98), CHADEMA/UKAWA ilikuwa na mawakala 6,351 (asilimia 97), na vyama vingine vilikuwa na jumla ya mawakala 4,585 (asilimia 70).

**9.5 Utaratibu wa Polisi na wa Usalama katika Siku ya Uchaguzi**

Ripoti za waangalizi wa TEMCO zinaonesha kuwa katika vituo vingi vya kupigia kura kulikuwa na askari polisi au maafisa usalama. Kuwepo kwa utaratibu huu wa usalama kulichangia sana katika kumaliza mchakato wa upigaji kura kwa amani. Ripoti zinaonesha kuwa kati ya vituo 7,316 vya kupigia kura, vituo vya kupigia 6,416 (asilimia 87.7) vilikuwa na wastani wa kati ya askari polisi wenye sare mmoja hadi watu



*Mkuu wa Jeshi la Polisi, Tanzania, Mr. Ernest Mangu*

Hata hivyo, ripoti zinaonesha kuwa katika baadhai ya maeneo kulikuwa na usalam zaidi, hali ambayo kwa namna fulani "iliwaogopesha" baadhi ya wapigakura, kama ilivyoripotiwa katika jimbo la Sengerema ambako iliripotiwa kwamba kulikuwa na idadi kubwa mno ya askari wenye silaha waliosambazwa katika Siku ya Kupiga Kura. Hali kadhalika katika jimbo la Nyamagana ambako ofisi za manispaa ambako kura zilijumlishiwa, askari polisi wengi walilidna mageti makuu yote ya majengo hayo, na hivyo kuzuia watu ambao walikuwa na mahitaji ya huduma nyingine kuingia.



*Afisa usalama aliyevaa sare akifuatilia kwa karibu uhesabuji wa kura katika moja ya vituo vya kupigia kura huko Nyamagana.*



*Magari matano ya askari yakifanya doria katika barabara siku ya uchaguzi katika jimbo la Nyamagana*

**9.6 Utendaji wa Wasimamizi wa Uchaguzi katika Siku ya Uchaguzi**

Kwa mujibu wa ripoti za uwandani za waangalizi wa TEMCO, utendaji na mwenendo wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ulikuwa wa kuridhisha kwa kiasi kikubwa, kama ambavyo unaweza kuoneshwa kwa kuzingatia viwango vya maandalizi ya kutosha katika kuendesha chaguzi za mwaka 2015. Hili lilikuwa bayana kabisa katika (i) kununua na kusambaza kwa wakati vifaa vya uchaguzi; (ii) kuajiri, kutoa mafunzo na kusambaza wasimamizi wa uchaguzi (iii) kutoa matangazo ya mara kwa mara ya taarifa mpya kuhusiana na maandalizi ya uchaguzi,

ikiwa ni pamoja na changamoto ambazo Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilizokumbana nazo; (iv) kufanya kazi kwa ukaribu sana na wadau wengine wa uchaguzi katika kipindi chote cha uchaguzi; na (v) utangazaji wa matokeo ya uchaguzi wa urais kwa wakati kama ilivyopangwa.

Ni muhimu kufahamu kwamba utendaji mzuri wa jumla wa wafanyakazi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ulichangiwa na ufanisi wa wafanyakazi muhimu kwa utendaji katika kusimamia chaguzi, kama inavyoonyeshwa katika sifa zao za kielimu katika Jedwali 9-4.

***Jedwali 9-4: Sifa za Wasimaizi Wakuu wa Uchaguzi***

| Sifa za kielimu | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|
| Elimu ya msingi | 1 | 0.7 |
| Elimu ya sekondari | 9 | 6 |
| Elimu ya sekondari ya juu | 7 | 4.7 |
| Stashahada | 11 | 7.3 |
| Stashahada ya juu | 9 | 6 |
| Shahada | 96 | 64 |
| Shahada ya uzamili | 10 | 6.6 |
| Wasio na elimu | 7 | 4.7 |
| Jumla | 150 | 100 |

Chanzo: Ripoti za Uwandani za Waangalizi wa TEMCO

Kama inavyoonyeshwa katika Jedwali 9-4 Wasimamizi Wakuu wa Uchaguzi (asilimia 70) walikuwa wahitimu wa vyuo vikuu na asilimia saba kati ya hao walikuwa na elimu ya kiwango cha uzamili. Ni asilimia 18 tu ya waangalizi waliokuwa na elimu ya sekondari.

## 9.7 Mchakato wa Kuhesabu Kura na Kubandika Matokeo

Kwa mujibu wa ripoti za waangalizi wa TEMCO, mchakato wa kuhesabu kura katika vituo vingi vya kupigia kura ulifanyikia pale pale ambapo upigaji kura ulifanyikia. Kati ya vituo vya kupigia kura 7,316, vituo vya kupigia kura 6,961 (asilimia 95.1) vilifanya zoezi la kuhesabu kura pale pale katika eneo la kupigia kura na vituo vya kupigia kura 49 tu (asilimia 0.67) ndivyo vilihesabia kura zake mahali pengine. Aidha, ripoti za waangalizi wa TEMCO zinaonesha kuwa katika vituo vingi vya kuhesabia kura, zoezi la kuhesabu kura lilishuhudiwa na wadau muhimu wa uchaguzi kama inavyoonyeshwa katika Jedwali 9-5.

***Jedwali 9-5: Kuwepo kwa Wadau Muhimu wa Uchaguzi wakati wa Mchakato wa Kuhesabu Kura***

| **Wadau waliokuwepo katika kituo cha kuhesabia kura** | **Idadi** | **%** |
|---|---|---|
| Msimamizi Mkuu wa kituo peke yake | 163 | 2.2 |
| Msimaizi mkuu wa kituo na askari polisi | 352 | 4.8 |
| Msimamizi mkuu wa kituo, askari polisi na mawakala wa vyma | 6,624 | 89.7 |
| Wengine | 245 | 3.3 |
| Jumla | 7,384 | 100.0 |

Chanzo: Ripoti za Uwandani za Waangalizi wa CEMOT



*Mchakato wa kuhesabu kura katika moja ya vituo vya kupigia kura huko Nyamagana*



*Wasimamizi wa uchaguzi wakiyafunga maboksi ya kura baada ya kuhesabu kura katika moja ya viuto vya kupigia kura katika jimbo la Nyamagana.*

Taarifa kutoka katika ripoti za waangalizi wa TEMCO zinaonesha pia matukio ya urudiaji wa kuhesabu kura uliofanywa katika baadhi ya vituo vya kupigia kura. Kati ya vituo vya kuhesabia kura 7,316 vilivyoshuhudiwa na TEMCO, urudiaji wa kuhesabu kura ulitokea katika vituo 1,834 (asilimia 25). Ripoti zinaonesha pia kwamba malalamiko machache yalisikika kabla matokeo hayajatangazwa katika vituo vya kuhesabia kura 177 (asilimia 2.4) kama inavyoonyeshwa katika Jedwali 9-6

***Jedwali 9-6: Urudiaji wa Kuhesabu Kura na Malalamiko Yaliyosikika kabla ya Kutangazwa kwa Matokeo***

| Uhesabuji wa kura uliorudiwa | Idadi | % | Malalamiko yaliyosikika | Idadi | % |
|---|---|---|---|---|---|
| Ndiyo | 1,834 | 25.1 | Ndiyo | 177 | 2.4 |
| Hapana | 5,198 | 71.1 | Hapana | 6,790 | 92.8 |
| Hakuna | 284 | 3.8 | Hakuna | 349 | 4.8 |
| Jumla | 7,316 | 100.0 | Total | 7,316 | 100.0 |

Chanzo: Ripoti za Uwandani, Waangalizi wa TEMCO, 2015

Ripoti za waangalizi wa TEMCO zinaonesha kuwa kati ya vituo vya kuhesabia kura 7,316 vilivyoshuhudiwa, matokeo ya uchaguzi katika vituo vya kuhesabia kura 6,756 yalibandikwa nje ya vituo vya kuhesabia kura mara tu baada ya kuhitimisha zoezi la kuhesabu kura kama sheria ya uchaguzi inavyosisitiza. Ripoti zinaonesha kuwa katika vituo vya kuhesabia kura 43 tu (asilimia 0.6) ndiko ambako matokeo ya uchaguzi hayakubandikwa kama inayooneshwa katika Jedwali 9-7.

***Jedwali 9-7: Kubandikwa kwa Matokeo ya Uchaguzi katika Vituo vya Kuhesabia Kura***

| Matokeo ya uchaguzi yaliyobandikwa katika vituo vya kupigia kura | Idadi | % |
|---|---|---|
| Ndiyo | 6,756 | 92.3 |
| Hapana | 43 | 0.6 |
| Hakuna jibu | 517 | 7.1 |
| Jumla | 7,316 | 100 |

Chanzo: Ripoti za Uwandani, Waangalizi wa TEMCO, 2015

### 9.8 Utangazaji wa Matokeo ya Uchaguzi

Utangazaji wa matokeo ya uchaguzi wa urais, ubunge na udiwani ni jukumu la Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Wasimamizi Wakuu wa Uchaguzi na Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi, mtawalia. Kwa kufuata utaratibu huo, matokeo ya uchaguzi wa urais yanajumlishwa katika ngazi ya taifa baada ya kukusanywa kutoka katika majimbo yote; matokeo ya uchaguzi wa ubunge yanajumlishwa katika ngazi ya jimbo na yale ya uchaguzi wa udiwani katika ngazi ya kata.



*Rais Anayemaliza Muda wake, J. M. Kikwete Akimpongeza Mrithi wake Mhe. John Pombe Magufuli*

Tarehe 29 Oktoba, 2015, siku nne baada ya siku ya uchaguzi, Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Jaji (mstaafu) Damian Lubuva alimtangaza Dkt. John Pombe Magufuli, mgombea urais wa CCM kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akiwa amejikusanyia kura 8,882,935 (asilimia 58.46). Bw. Edward Ngoyai Lowasa, mgombea urais wa CHADEMA alijikusanyia kura 6,072,848 (39.97%) na alikuwa mshindi wa pili. Matokeo ya uchaguzi kwa wagombea wanane wa urais yanaonyeshwa katika Jedwali 9-8.

***Jedwali 9-8: Matokeo ya Uchaguzi wa Urais Tanzania***

| Mgombea | Chama cha Siasa | Kura | % |
|---|---|---|---|
| John Pombe Magufuli | Chama Cha Mapinduzi | 8,882,935 | 58.46 |
| Edward Ngoyai Lowassa | Chama cha Demokrasia na Maendeleo | 6,072,848 | 39.97 |
| Anna Elisha Mghwira | Alliance for Change and Transparency | 98,763 | 0.65 |
| Lutalosa Yembe | Alliance for Democratic Change | 66,049 | 0.43 |
| Hashim Rungwe Spunda | Chama cha Ukombozi wa Umma | 49,256 | 0.32 |
| Machmillan Elifatio Lyimo | Tanzania Labour Party | 8,198 | 0.05 |
| Janken Malik Kasambala | National Reconstruction Alliance | 8,028 | 0.05 |
| Fahmi Nassoro Dovutwa | United People's Democratic Party | 7,785 | 0.05 |
| Kura batili/hazikujazwa | | 402,248 | – |
| Jumla | | 15,596,110 | 100 |

Chanzo: Tume ya Taifa ya Uchaguzi, 2015

Kuhusiana na chaguzi za ubunge, kama ilivyooneshwa katika Jedwali 9-9, vyama vya siasa vitano vilivyoweza kujinyakulia viti vya ubunge ni: CCM, CHADEMA, CUF, NCCR-Mageuzi na ACT-Wazalendo. Kati ya majimbo 264, CCM ilishinda majimbo 195 (asilimia 73.9), CHADEMA ilishinda majimbo (35 (asilimia 13.3) na CUF ilishinda majimbo 32 (12.1). NCCR-Mageuzi na ACT-Wazalendo kila kimoja kilishinda kiti kimoja cha ubunge (asilimia 0.4). Vyama vya siasa vinavyounda muungano wa UKAWA, ambavyo ni CHADEMA, CUF, na NCCR-Mageuzi kwa pamoja vilishinda majimbo 68 (asilimia 25.7).

***Jedwali 9-9: Matokeo ya Uchaguzi wa Ubunge, 2015***[27]

| Chama | Kura | Viti | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Waliochaguliwa | Wanawake | Jumla |
| CCM | 8,495,488 | 195 | 66 | 261 |
| CHADEMA | 4,720,881 | 35 | 37 | 72 |
| CUF | 1,274,911 | 32 | 10 | 42 |
| ACT-Wazalendo | N.A | 1 | 0 | 1 |
| NCCR-Mageuzi | N.A | 1 | 0 | 1 |
| Other political parties | N.A | 0 | 0 | 0 |
| Jumla | N.A | 265 | 113 | 378 |

Chanzo: Ripoti za Uwandani, Waangalizi wa TEMCO, 2015

### 9.9 Mahudhurio ya Wapigakura

Ikilinganishwa na chaguzi za mwaka 2010 zilizofanyika nchini Tanzania, mahudhurio katika uchaguzi wa mwaka 2015 yalikuwa mazuri kwa ujumla. Wakati ambapo mahudhurio katika uchaguzi wa mwaka 2010 yalikuwa kama asilimia 43 ya wapiga kura waliojiandikisha, mahudhurio ya uchaguzi wa mwaka 2015 yalikuwa asilimia 67.3, ongezeko la asilimia 24.3. Ongezeko hili kubwa katika mahudhurio linaweza kuelezwa kwa kuzingatia sababu mbailmbali: (i) ushindani mkali kati ya CCM na vyama vya siasa vinavyounda umoja wa UKAWA; (ii)shauku ya mabadiliko katika maeneo yote ya maisha; (iii) idadi kubwa ya wapigakura ambao ni mara yao ya kwanza kupiga kura waliotaka kutumia haki yao ya kuchagua viongozi; (iv) kuongezeka kwa mwamko wa wapigakura juu ya haki zao za kisiasa na kiraia; na (v) kuisha kwa muhula wa rais aliyekuwa madarakani.

Pamoja na kuwepo kwa mahudhurio mazuri yanayoridhisha ya wapigakura, idadi kubwa ya wapigakura waliojiandikisha, takribani milioni saba, hawakujitokeza kupiga kura siku ya uchaguzi. Utazamaji wa TEMCO unaliona hili kama tatizo la kitaifa na suala la kufikiriwa na wadau wote wa uchaguzi ili kuunda mikakati ya kukuza ufanisi wa kisiasa, mwamko na uelewa wa wapigakura.

### 9.10 Hali na Matukio Baada ya Uchaguzi

Kwa mujibu wa ripoti za waangalizi wa TEMCO, katika vituo vingi vya kupigia kura kulikuwa na hali ya utulivu na shamlashamla, hususani baada ya kubandikwa na kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi katika ngazi mbalimbali, kama inavyoonyeshwa katika Jedwali 9-10.

[27] Ukiacha majimbo nane ambayo yaliahirisha uchaguzi wa ubunge.

*Jedwali 9-10: Matokeo ya Mwitikio wa Watu*

| Mwitikio | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|
| Walikuwa wakisherehekea, wakiimba na kucheza | 117 | 78.0 |
| Walikuwa watulivu na watiifu | 25 | 16.7 |
| Walikuwa wanahofia kuzuka kwa vurugu | 4 | 2.7 |
| Walikuwa na hasira na wenye vurugu | 1 | 0.7 |
| Matokeo yalitolewa watu walipoodoka | 1 | 0.7 |
| Hakuna majibu | 2 | 1.2 |
| Jumla | 150 | 100.0 |

Chanzo: Ripoti za Uwandani, Waangalizi wa TEMCO

Kama ilivyooneshwa katika Jedwali 9-10, majimbo 177 kati ya majimbo 150, watu waliyapokea matokeo ya uchaguzi kwa nyimbo na shangwe. Kwa ujumla, hali ilibaki kuwa tulivu katika kipindi chote cha kuhesabu kura. Matukio ya mwitiko wa jazba na vurugu hayakuwa na maana. Kiwango cha jumla cha kuyakubali matokeo ya uchaguzi kinaonyeshwa pia na ripoti zinazoonesha kuwa kati ya majimbo 150 yaliyoshuhudiwa na TEMCO ni majimbo 14 tu (asilimia 9.3) ndiyo ambayo wagombea walitoa malalamiko ya matokeo ya uchaguzi, huku majimbo 135, sawa na asilimia 90, yakiwa yameridhishwa na matokeo yake ya uchaguzi.

Hata hivyo, CHADEMA na vyama vingine vya siasa vya umoja wa UKAWA vilikataa kuyakubali matokeo ya uchaguzi wa rais. Mgombea wa urais wa CHADEMA alitoa kauli nyingi kwa umma akidai kuwa CCM na serikali wamempora ushindi wa uchaguzi. Kinyume chake, wakati CHADEMA inakataa kuyatambua matokeo ya uchaguzi wa urais, iliyakubali matokeo ya ubunge. CHADEMA walisusia sherehe za kumtangaza mshindi wa urais, sherehe za kumwapisha rais mteule na uzinduzi wa Bunge la 11 uliofanywa na Rais Dkt. John Pombe Magufuli tarehe 11 Novemba, 2015.



*Rias Mteule Dkt. John Pombe Magufuli Akiapishwa na Jaji Mkuu kuwa Rais wa Awamu ya 5 wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*

Siku ya uzinduzi wa Bunge vyama vya upinzani, hususani vile vinavyounda UKAWA, vilitoka nje ya Bunge kama ishara ya kutoyatambua matokea ya urais na kama ishara ya kupinga kuwepo kwa Rais wa Zanzibar, Dkt. Ali Mohamed Shein, ambaye aliendelea kuwa madarakani, wakidai kuwa ni kinyume na katiba.



*Rais John Pombe Magufuli Ameshikilia Alama za Taifa baada ya Sherehe za Kuapishwa*



*Rais na Amiri-Jeshi Mkuu wa Jeshi akikagua Jeshi la Kutoa Heshima baada ya Sherehe za Kuapishwa*



*Warithi wa Amani: Somo kwa Demokrasia za Afrika 1985-2015, Marais Wastaafu watatu Wakifurahi baada ya Kuapishwa kwa Rais J.P. Magufuli, kuwa Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.*




*Sehemu ya Marais kutoka Nchi za Jirani Wakishuhudia Sherehe za Kuapishwa kwa Rais wa Awamu ya 5 wa Tanzania. Rais Uhuru Kenyatta hayupo kwenye Mstari*

## 9.11 Malalamiko ya Uchaguzi wa Urais na Ubunge

Sheria ya Tanzania inazuia uwezekano wa kuyapinga matokeo ya uchaguzi wa urais katika mahakama za kisheria. CHADEMA ilipeleka malalamiko Tume ya Taifa ya Uchaguzi ikidai kusitishwa kwa utangazaji wa matokeo ya urais, ikitaka kurudiwa kwa uchaguzi wa urais Tanzania bara. Hata hivyo, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilijibu kwa kusema kuwa malalamiko ya uvunjifu wa taratibu za uchaguzi yaliyoelezwa yalipaswa kupelekwa kwa wasimamizi wakuu wa uchaguzi. Kwa hiyo, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilitupilia mbali malalamiko hayo. na iliendelea kutangaza matokeo ya urais kama ilivyopangwa.

Kuhusiana na matokeo ya uchaguzi wa ubunge, kuna malalamiko mengi yaliyofikishwa mahakama kuu, kama inavyoonyeshwa katika Jedwali 9-11.

***Jedwali 9-11: Malalamiko Yaliyofikishwa Makahama kuu Dhidi ya Matokeo ya Uchaguzi wa Ubunge***

| | Jina la Mlalamikaji | Chama cha Siasa | Jimbo |
|---|---|---|---|
| 1 | Frederick Mwakalebela | CCM | Iringa Mjini |
| 2 | Murtaza Mangungu | CCM | Kilwa Kaskazini |
| 3 | Stephen Kiruswa | CCM | Longido |
| 4 | Juma Manguya | CCM | Kilwa Kusini |
| 5 | James Lembeli | CHADEMA | Kahama |
| 6 | Ezekiel Wenje | CHADEMA | Nyamagana |
| 7 | Benedicto Mutungirehi | CHADEMA | Kyerwa |
| 8 | Emmanuel Godfrey | CHADEMA | Njombe |
| 9 | William Mungai | CHADEMA | Mafinga |
| 10 | Zella Abraham | CHADEMA | Mbeya Vijijini |
| 11 | Fanuel Mkisi | CHADEMA | Vwawa |
| 12 | Amina Mwidau | CUF | Pangani |
| 13 | David Kafulila | NCCR-Mageuzi | Kigoma Kusini |

Chanzo: Mahakama Kuu ya Tanzania, 2016

## 9.12 Tathimini ya Jumla ya Shughuli za Siku ya Uchaguzi

Kwa ujumla, shughuli za siku ya kupiga kura zilifanywa vizuri na kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zilizopo za uchaguzi. Vifaa vya kutosha vya uchaguzi vilisambazwa kwa wakati. Ripoti za waangalizi wa TEMCOzinaonesha kuwa shughuli za siku ya uchaguzi zilifanywa kama ilivyopangwa ukiachilia mbali upungufu mdogo ambao haukuathiri sana michakato ya kupiga kura na kuhesabu kura kama inavyooneshwa katika

Jedwali 9-12.

*Jedwali 9-12: Tathtimini ya Shughuli za Siku ya Uchaguzi*

| Mchakato wa kupiga na kuhesabu kura ulivyokuwa | Alama na madaraja | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|---|
| Mchakato wa kupiga na kuhesabu kura ulikuwa na dosari chache sana ambazo hazikuathiri matokeo ya jumla ya chaguzi. Kwa ujumla, mchakato wa kupiga na kuhesabu kura ulikuwa safi, huru na haki. | A (80 – 100%) | 5,630 | 76.6 |
| Mchakato wa kupiga na kuhesabu kura ulikuwa huru na wa haki kwa ujumla lakini kulikuwa na dosari ambazo kwa ujumla wake hazikuathiri chochote matokeo ya mwisho ya uchaguzi na hazikuathiri bahati za wadau (vyama vya siasa, wagombea na wapigakura). | B (60-69%) | 1,595 | 21.7 |
| Mchakato wa kupiga na kuhesabu kura ulitoa uhuru wa ushiriki kwa wadau (vyama vya siasa, wagombea na wapigakura) lakini kulikuwa na mifano mingi ambapo vyama vikubwa au, hasahasa chama tawala, kilivunja kanuni za uchaguzi bila kupewa adhabu, na kulikuwa na upendeleo ambao uliathiri matokeo ya baadhi ya wagombea na vyama vyao. | C (50-59%) | 117 | 1.6 |
| Mchakato wa kupiga na kuhesabu kura uliharibiwa na hitilafu nyingi zinazohusiana na kutokufuata baadhi ya sheria, kanuni na maadili ya uchaguzi, matatizo ya kiusimamizi na matukio kadhaa ya vitisho na upendeleo. | D (40-49%) | 7 | 0.1 |
| Mchakato wa kupiga na kuhesabu kura ulivurugwa au ulisimamiwa vibaya kiasi kwamba haikuwezekana tena kuelewa ni nini kilichotokea. Ilikuwa kana kwamba ni mwanafunzi aliyefeli mtihani. | E (1-39%) | 0 | 0.0 |
| Mwenendo kupiga na kuhesabu kura uliharibiwa na uvunjaji mkubwa wa kanuni za uchaguzi. Kulikuwa na mtukio mengi ya vurugu, rushwa na chokochoko kiasi kwamba baadhi ya wagombea walimua kujitoa katika uchaguzi au kuchukua hatua nyingine. Siku ya kupiga kura iliahirishwa. | F (0%) | 1 | 0.0 |
| Jumla | | 7,350 | 100 |

Chanzo: Ripoti za Uwandani, Waangalizi wa TEMCO, 2015

## 9.13 Hitimisho na Mapendekezo

### *9.13.1 Hitimisho*

Kwa ujumla, taarifa kutoka katika ripoti za waangalizi wa TEMCO zinaonesha kuwa shughuli za siku ya uchaguzi, hususani kupiga kura, kuhesabu kura na utangazaji wa matokeo ya uchaguzi wa mwaka 2015 vilimalizika vizuri na kwa mafanikio. Vifaa vya uchaguzi vilisambazwa katika majimbo yote mapema na viliwasilishwa katika vituo vya kupigia kura kama ilivyopangwa. Kati ya majimbo 264, ni majimbo sita tu ndiyo yaliahirisha uchaguzi kutokana na kufariki kwa wagombea na majimbo mawili (asilimia 0.75) yaliahirisha uchaguzi kwa sababu ya matatizo ya karatasi za kura. Kuhusiana na chaguzi za wabunge, uchaguzi uliahirishwa katika kata 26 (asilimia 0.65) tu kati ya kata 3,957. Sababu za kuahirishwa kwa uchaguzi katika kata hizo ilikuwa ni pamoja na matatizo ya karatasi za kupigia. kura na vifo

vya wagombea. Ripoti za waangalizi wa TEMCO zinaonesha kuwa shghuli za uchaguzi kwa ujumla wake zilifanyika vizuri na zilikuwa na uvunjaji mdogo sana wa kanuni ambao haukuondoa kukubalika kwa zoezi la uchaguzi, huru na haki ya shughuli za siku ya uchaguzi

### *9.13.2 Mapendekezo*

Kutokana na taarifa za waangalizi wa muda mrefu na waangalizi wa muda mfupi wa TEMCO kuhusiana na shughuli za siku ya uchaguzi, yaani kuandaa vituo vya kupigia kura, uhakiki wa vifaa vya uchaguzi, kufungua vituo vya uchaguzi, kupiga kura, kuhesabu kura na utangazaji wa matokeo, yametolewa mapendekezo yafuatayo:

(i) Kuna haja ya wadau wa uchaguzi kuongeza zaidi elimu ya mpigakura kama njia mojawapo ya kuongeza mahudhrurio ya wapigakura. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, pamoja na mafanikio ya kuwa na mahudhurio ya wapigakura zaidi ya asilimia 67, asilimia 33 ya Watanzania (milioni saba) ambao walijiandikisha kupiga kura hawakujitokeza kupiga kura.

(ii) Kuna haja ya wadau wa uchaguzi kutilia mkazo zaidi elimu muhimu kuhusiana na mchakato wa kuupiga kura ili kupunguza zaidi idadi ya kura zinazoharibika, ambazo idadi yake ni takribani kura 402,248 (asilimia 2.58) ya kura za urais;

(iii) Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatakiwa kuhakikisha kwamba maadalizi ya kituo cha kupigia kura yanaboreshwa ili kuhakikisha kuwa mchakato wa kupiga kura unakuwa rafiki kwa watu wenye mahitaji maalumu, wasimamizi wa uchaguzi, waangalizi wa uchaguzi, mawakala wa vyama vya siasa na wadau wengine.

(iv) Tume ya Taifa ya Uchaguzi ihakikishe kwamba vituo vya kupigia kura vinawekwa katika majengo ya umma yenye viwango vinavyokubalika. Mahali ambapo vibanda vya muda vinatakiwa kujengwa, Tume inapaswa kufuata muundo unaofanana ili kufikia viwango vizuri vya usiri wa kura, hifadhi nzuri ya kura na usalama wa kura zilizopigwa;

(v) Tume ya Taifa ya Uchaguzi ihakikishe kuwa zana na vifaa vya uchaguzi viwe katika viwango vya juu ili kurekebisha baadhi changamoto zilizobainika hususani vifaa vinavyohusiana na utoaji wa mwanga, wino na mihuri.

(vi) Serikali na Tume ya Taifa ya Uchaguzi vinatakiwa kupitia upya mafao na hali ya ustawi wa wasimamizi wa uchaguzi wanaofanya kazi siku ya uchaguzi, ikiwa ni pamoja na kuliangalia suala la kuongeza malipo; na,

(vii) Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatakiwa ichukue hatua za kupata taarifa mpya na kuboresha usahihi wa daftari la kudumu la wapigakura ili kupunguza suala la wapigakura kukosa majina yao katika dafatari hilo katika siku ya uchaguzi.

## CHAPTER 10
## UCHAGUZI ZANZIBAR: UTATA NA CHANGAMOTO

### 10.1 Utangulizi

Zanzibar ilifanya uchaguzi wake siku moja pamoja na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 25 October 2015. Kwa mantiki hiyo, wapigakura wa Zanzibar walishiriki katika chaguzi mbili kwa wakati mmoja kwa ajili ya Zanzibar na Jamhuri ya Muungano, wakipiga kura zipatazo tano; ambapo kura mbili zaidi zilipigwa na wakazi wa Tanzania bara. Wazanzibari walipiga kura kumchagua Rais wa Zanzibar, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Madiwani katika uchaguzi wa Zanzibar, lakini pia walimchagua Rais wa Jamhuri ya Muuangano na Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muuangano wa Tanzania wakiwakilisha majimbo ya visiwani Zanzibar. Uchaguzi wa mwaka 2015 haukifika mwisho baada ya Tume ya Uchaguzi Zanzibar kufuta matokeo ya uchaguzi huo. Sura hii inatathmini uchaguzi wa Zanzibar 2015 na mgogoro uliojitokeza baada ya kufutwa kwa matokeo yake.

Sura hii ina utangulizi mfupi wa historia ya siasa za Zanzibar ambazo zimekuwa zikikabiliwa na ushindani mkubwa, ukataaji wa matokeo kwa walioshindwa uchaguzi na vurugu. Sehemu ya pili itaangazia nafasi ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa katika uchaguzi wa 2015. Sehemu ya tatu inachambua mamlaka na uhusiano kati ya ZEC na NEC na jinsi ambavyo wahusika wa nje walivyoingilia mgogoro huo mara baada ya matokeo kufutwa. Tathmini ya jumla ya mchakato wa uchaguzi Zanzibar inatolewa kutokana na ripoti ya timu ya waangalizi wa TEMCO waliotazama kila hatua ya uchaguzi visiwani humo.

### 10.2 Siasa za Zanzibar Kabla ya Uhuru


Siasa za ushindani visiwani Zanzibar zilianza miaka ya 1950, kipindi ambacho kinatazamwa kama kilele cha harakati za ukombozi. Vyama vikuu katika harakati hizi vilikuwa Zanzibar Nationalist Party (ZNP), kilichoanzishwa mwaka 1955; Afro Shiraz Party (ASP), kilichoanzishwa mwaka 1957; Zanzibar and Pemba Peoples' Party (ZPPP) kilichoanzishwa mwaka 1959 na Umma Party cha mwaka 1963. Chaguzi za kabla ya uhuru zilitawaliwa na migawanyiko katika misingi ya rangi na matabaka, mambo ambayo yalitafsiri pia ufuasi ndani ya vyama vya siasa. Hivyo basi, chaguzi hizi zilikuwa na ushindani mkubwa sana. Mwaka 1957 viti vya uwakilishi sita vilikuwa vikigombaniwa katika Baraza la Kutunga Sheria (LEGCO). Uchaguzi huu ulivuta hisia kubwa sana za ushindani kati ya ASP na ZNP pamoja na jumuiya za kikabila na kidini.  ASP ilishinda viti vyote vitano na kiti kilichobaki hakikwenda kwa ZNP bali kilikwenda kwa Jumuiya ya Kidini ya Wahindi. Mnamo Januari 1961, uchaguzi wa kugombea uhuru ulifanyika ambapo viti 22 vilishindaniwa. ASP ilishinda viti 10 dhidi ya viti 9 vya ZNP na ZPPP ilijinyakulia viti 3. Katika Uchaguzi huu, chama cha wachache cha ZPPP kilipata umuhimu mkubwa sana pale ambapo viti vyake viwili viliendа ZNP na kiti kimoja kikaenda ASP. Pande zote mbili zikawa zimefungana kwa viti 11 na hapakuwa na mshindi.

Katika kujaribu kuepuka kufungana tena, utawala wa kikoloni uliongeza jimbo la uchaguzi katika eneo la Mtambile Pemba ili kufanya majimbo yawe 23 katika uchaguzi wa marudio. Uchaguzi huo uliofanyika June 1961 ASP ilibakiza majimbo yake 10 na ZNP ikapata viti 10 wakati ZPPP ilibakiza viti vyake vitatu. Viti viwili vya ZPPP vikaenda ZNP na kiti kimoja

kikaenda ASP.  Hivyo basi, ushirikiano wa NZP/ZPPP uliibuka na ushindi wa viti 12 dhidi ya11 vya ASP. Kwa mujibu wa Ramadhani (2000), uchaguzi wa June 1961 ulifuatiwa na vurugu zilizosababisha vifo vya Waafrika 65 na Waarabu watatu. Watu wasiopungua 350 walipata majeruhi na watu wengi zaidi walikamatwa na polisi. Matukio hayo ya vurugu yakalazimu kuitishwa kwa kongamano la kikatiba, mjini Lancaster 1962. ASP waliwataka Waingereza wacheleweshe kutoa uhuru kwa Zanzibar na uchaguzi urudiwe wakati ushirika wa ZNP/ZPPP walioibuka washindi walisisitiza wakabidhiwe uhuru.

Utawala wa Kikoloni wa Waingereza uliitisha uchaguzi mwingine 1963 huku wakiongeza majimbo mapya 8. Katika uchaguzi huu ASP ilipata viti 13, ZNP 12 na ZPPP viti 6. Kwa mujibu wa baadhi ya wachambuzi, kwa jinsi majimbo hayo mapya yalivyogawanywa, yalikusudia kutoa ushindi wa wazi kwa ushirika wa ZNP/ZPPP (Ramadhani 2000: 60, Othman 2006: 125). Hoja hii inapata mashiko kutokana na ukweli kwamba ingawa ASP ilipata asilimia 54.21% ya kura zote katika uchaguzi wa 1963 lakini ilipata viti 13 tu kati ya jumla ya viti 31. Hali hii iliwapa wafuasi wa ASP sababu ya kuhisi kuwa walifanyiwa hila za kiuchaguzi na utawala wa kikoloni. Hali hii ilipelekea kukosekana kwa uhalali wa uchaguzi uliowapa ushirika wa ZNP/ZPPP ushindi. Hata hivyo utawala wa kikoloni ilitoa uhuru kwa Serikali liyoundwa na ushirika ZNP/ZPPP. Sultani Jamshid akawa kiongozi wa kwanza ya Zanzibar huru.

Wakiamini kuwa uchaguzi wa 1963 haukuwa halali, na kwamba ZNP/ZPPP hawakuwa na lengo la kuwaingiza ASP kwenye ushirika wa serikali yao, kundi la Waafrika wakaongoza mapinduzi January 1964 ambayo yaliuondoa utawala wa ZNP/ZPPP na kuuweka utawala wa ASP madarakani.



*Hayati Abeid Amani Karume*

Abeid Karume akawa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi lililoundwa na wajumbe 30. Matumaini ya Waarabu kuurudisha utawala wao Zanzibar yalipotea mara baada ya Zanzibar kuungana na Tanganyika tarehe 26 April 1964. Zanzibar ikawa sehemu ya Tanzania lakini yenye uhuru katika utawala wake wa ndani. Baaada ya Mapinduzi, Katiba iliwekwa kando, vyama vya siasa vilipigwa marufuku isipokuwa ASP, na Rais Karume akatangaza uchaguzi usifanyike kwa miaka 50 ili kuimarisha mapinduzi na kuondoa historia ya udhalimu iliyodumu kwa karne na karne dhidi ya Waafrika (Mapuri 1996: 66).

**10.3 Kurudishwa kwa Mfumo wa Vyama Vingi**

Pamoja na kwamba chaguzi za chama kimoja zilifanyika mwaka 1980, 1985 na 1990 (baada ya ASP kuungana na TANU kuunda CCM mwaka 1977) lakini uchaguzi wenye ushindani ulirejea mara baada ya kurudishwa kwa mfumo wa vyama vingi mwaka 1992. Mwaka huu ulishuhudia kurejea kwa wanasiasa Maalim Seif Sharif Hamad, Hamad Rashid Mohamed, Shaaban Khamis Mloo na Ali Haji Pandu ambao walikuwa maafisa wa ngazi za juu serikalini lakini wakafukuzwa CCM mwaka 1988. Wanasiasa hawa walianzisha Chama cha Wananchi (CUF) ambacho kilikuwa chama kikuu cha upinzani.

Uchaguzi wa kwanza wa vyama vingi ulifanyika tarehe 22 Octoba mwaka 1995. Ushindani ulikuwa wa karibu sana kati ya CCM na CUF na Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) ilimtangaza mgombea wa CCM Salmin Amour kama mshindi katika uchaguzi huo kwa asilimia 50.2 dhidi ya asilimia 49.8 alizopata mgombea wa CUF Seif Sharif Hamad. Matokeo haya ya urais yalipingwa vikali sana. CCM pia ilishinda viti 26 na CUF viti 24 vya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Pamoja na kwamba CUF hawakuridhishwa na matokeo, hawakuweza kufungua kesi mahakamani kwa sababu ya Kifungu cha 37 cha Katiba ya Zanzibar kinachozuia kuhoji matokeo ya urais yaliyotangazwa na ZEC. Hivyo basi, CUF iliamua kutumia mbinu mbadala kama vile maandamano na kuvuruga shughuli za Baraza la Wawakilishi ili kuelezea masikitiko yao na kutaka haki. Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Madola (Commonwealth) Chief Emeka Anyaoku na mjumbe wake maalum Dr. Moses Anafu waliingilia kati mgogoro huu na kujaribu kuleta usuluhishi. Makubaliano ya awali kati ya CCM na CUF yalisainiwa Aprili 1999 jijini Dar es Salaam na maafikiano ya mwisho yalisainiwa Juni 1999 yakijulikana kama Mwafaka I. Mwafaka I ulilenga kuleta mageuzi ya kidemokrasia kwa lengo la kutengeneza uwiano wa kiushindani wakati wa uchaguzi. Pamoja na mambo mengine Muafaka I uligusia uhuru wa ZEC na kutofungamana na taasisi yeyote, kuwa na daftari la kudumu la wapigakura, na marekebisho ya Katiba na Sheria za Uchaguzi (Mbunda, 2010: 11-12).



*Makatibu Wakuu, Phillip Mangura wa CCM (kushoto) na Seif Sharif Hamad wa CUF Wakitia saini Mwafaka I Mwaka 1999, Dar es Salaam.*

Katika uchaguzi wa mwaka 2000, mgombea wa CCM Amani Abeid Karume alishinda kwa tofauti ya asilimia 67 dhidi ya asilimia 33 za Seif Sharif Hamad wa CUF. CCM pia ilishinda jumla ya viti 34 za Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi dhidi ya viti 16 walivyoshinda CUF. Hata hivyo, CUF waligoma kuyakubali matokeo ya uchaguzi huo na kumtambua Karume kama Rais aliyechaguliwa kihalali. Zanzibar ikarudi kwenye mgogoro. CUF walipanga maandamano nchi nzima tarehe 26 na 27 Januari 2001 kupinga matokeo ya uchaguzi huo. Jeshi la polisi lilipamabana vikali na waandamanaji, wakifyatua risasi za moto na kusababisha vifo na majeruhi. Baada ya matukio haya, CCM na CUF walilazimika kurudi kwenye meza ya majadiliano yaliyozaa Mwafaka II. Moja ya mafanikio ya Mwafaka II ni kuanzishwa kwa daftari la kudumu la wapigakura Zanzibar. Katika uchaguzi wa 2005 mgombea Urais wa CCM Amani Abeid Karume alishinda tena kwa asilimia 53.2 ya kura zote dhidi ya 46.1 alizopata Seif Sharif Hamad. CCM pia ilishinda viti 30 dhidi ya 19 za CUF. Matokeo haya pia yalikataliwa na CUF waliodai kuwa ZEC ilitengeneza matokeo ili kuipa ushindi CCM.

### 10.4 Serikali ya Umoja wa Kitaifa

Wazo la kuwa na Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK) lilitokana na ukweli kwamba mfumo wa uchaguzi wa mshindi-huchukua-yote ulikuwa chanzo cha migogoro ya kiuchaguzi. Mara baada ya uchaguzi wa Mwaka 2005 ambao pia ulilalamikiwa, CCM na CUF waliamua kuanza majadiliano kuanzia tarehe 1 Februari 2007 mjini Dodoma, wakiwa na lengo la kugawana madaraka. Mazungumzo yaliendelea kimyakimya kwa zaidi ya mwaka mmoja ndipo 17 Machi 2008 mazungumzo hayo yalivunjika.



*Rais Mstaafu Amani Karume Akimkaribisha Maalim Seif Sharif Ikulu katika Mazungumzo Yaliyopelekea Kuundwa kwa SUK*

Taarifa zilieleza kuwa, mahasimu hao wa kisiasa walikuwa wamekubaliana kugawana madaraka lakini hawakukubaliana mpangilio huo uanze lini. Miezi nane baadae, wakati CCM na CUF wakiendelea kuvutana Rais Amani Karume na Maalim Seif walikutana rasmi tarehe 5

Novemba 2009 na kusaidia kufanikiwa kwa mchakato huo wa kugawana madaraka katika kile kilichoitwa maridhiano (Killian & Mbunda 2010: 125).



*Rais Mstaafu wa Zanzibar Akishikana Mikono na Maalim Seif Sharif Hamad. Anayeangalia pembeni ni Jusa Ladhu wa CUF.*

Maridhiano hayo yalipelekea kubadilishwa kwa katiba ambayo ilitaka kura ya maoni ifanyike ili kurasmisha kuwepo kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK). Kura ya maoni ilipigwa mwezi Julai 2010 ambapo asilimia 66.4 ya wapigakura wote waliridhia kuwepo kwa SUK baada ya uchaguzi wa tarehe 31 Octoba 2010.

Katika uchaguzi huo wa tarehe 31 Octoba 2010, mgombea wa CCM Ali Mohammed Shein alishinda kwa asilimia 50.11 dhidi ya mpinzani wake Seif Sharif Hamad aliyepata kura 49.14. Katika Baraza la Wawakilishi CCM ilipata viti 28 na CUF ikashinda viti 22. Matokeo haya yalipelekea kuundwa kwa SUK. Rais Ali Mohammed Shein alimteua Seif Sharif Hamad kuwa Makamo wa Kwanza wa Rais na Seif Ali Iddi kuwa Makamo wa Pili wa Rais. Serikali ya Umoja wa Kitaifa ilikuwa na Mawaziri 19 na Manaibu Waziri 7. CCM walishika wizara 11 ikiwemo Wizara ya Nchi- Ofisi ya Rais; Wizara ya Fedha; Wizara ya Tawala za Mikoa na Vikosi Maalum; Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais; Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati; Wizara ya Uwezeshaji, Huduma za Jamii, Wanawake na Watoto; Wizara ya Elimu na Ufundi; Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Kazi na Utumishi wa Umma; Wizara ya Kilimo na Maliasili na Wizara nyingine mbili zisizo maalumu.

Kwa upande wao CUF walisimamia wizara 8 zikiwemo; Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais; Wizara ya Katiba na Sheria; Wizara ya Afya; Wizara ya Mawasiliano na Miundombinu; Wizara ya Mifugo na Uvuvi; Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko; Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo; na Wizara moja isiyo Maalum. Kulikuwa na jumla ya Manaibu waziri 7 na CCM ilikuwa na manaibu waziri wanne ambao ni Naibu Waziri wa

Miundombinu na Mawasiliano; Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo; Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko; na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Kwa upande wao CUF walikuwa na manaibu waziri watatu ambao ni Naibu Waziri wa Elimu na Ufundi; Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba , Maji na Nishati; na Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili.

### 10.5 Faida na Mapungufu ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa

Faida nyingi sana za kisiasa zilihusianishwa na mgawanyo wa madaraka uliowekwa rasmi katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar. Kwa kuanzia, SUK ilitazamwa kama chombo cha kupunguza hali ya kutokuaminiana baina ya mahasimu hao wa kisiasa visiwani humo na kujenga misingi ya ushirikiano. Hivyo basi, CCM na CUF walianza kufanya kazi pamoja pale ambapo Rais Shein alipomteua Maalim Seif kuwa Makamu wa Rais. Na baadae Rais, Makomu wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais wakakaa pamoja na kuteua Mawaziri 19 na Manaibu Waziri 7 kutoka vyama vyote viwili.

Pili, ahadi ya kuundwa kwa SUK iliondoa uadui uliokuwa ukitawala chaguzi za nyuma kiasi kwamba ZEC ikaweza kusimamia uchaguzi kwa weledi na kusifiwa na waangalizi wa ndani na nje takribani miezi mitatu tu tangu kura ya maoni ifanyike (TEMCO 2010: 109). Pia, kwa mara ya kwanza, Seif Sharif Hamad wa CUF aliyeshindwa katika uchaguzi wa Rais aliyakubali matokeo ingawa kulikuwa na tofauti ndogo sana ya kura.

Hata hivyo, kwa muundo wake SUK haikuweza kujenga mazingira ya kudumu ya kuaminiana baina ya vyama hivi viwili. Kikatiba (Kifungu cha 42), mpango wa kugawana madaraka katika SUK unaishia kwenye Mawaziri na Manaibu tu ambao hugawiwa kutokana na uwiano wa viti vya Baraza la Wawakilishi. Mamlaka nyingine za uteuzi kama vile Makatibu Wakuu, Wakurugenzi, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya huachwa kwa Rais ambaye pia analindwa na Kifungu cha 52 cha Katiba ya Zanzibar kutofuata ushauri wowote katika kutekeleza majukumu yake. Makamu wa Kwanza wa Rais kwa upande wake hajapewa majukumu maalum kikatiba isipokuwa kama kifungu cha 39(5) kinavyoeleza, atakuwa mshauri mkuu wa Rais na atamsaidia Rais kufanya kazi yeyote atakayopangiwa.

Hivyo basi, SUK ilipata malalamiko mengi ikiwemo suala la kupanua uwigo wa kugawana madaraka. Kwa jamii iliyogawanyika kama ya Zanzibar, sio wananchi wote wananufaika na matunda ya utawala. Hivyo basi, wakati vyama hivi vya siasa vikijiandaa na uchaguzi, lengo kubwa lilikuwa kushinda kiti cha Urais ili kupata mgao mkubwa wa madaraka ya nchi. Kuwa wa pili katika uchaguzi ilimaanisha kukubali kumsaidia Rais aliyeshinda kutekeleza dira yake.

### 10.6 Uchaguzi wa 2015 Zanzibar

#### *10.6.1 Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar: Mamlaka na Muundo*

Chaguzi za Zanzibar husimamiwa na ZEC. ZEC inaundwa na kifungu cha 119(1) cha Katiba ya Zanzibar ikiwa na wajumbe saba. Mwenyekiti wa ZEC ni mteule wa Rais kati ya watu wenye sifa za kuwa majaji wa Mahakama Kuu, au mtu yeyote mwenye heshima katika jamii. Wajumbe wawili wanateuliwa na Rais kutokana na mapendekezo ya kiongozi wa shughuli za Serikali katika Baraza la Wawakilishi, na wajumbe wawili wengine huteuliwa na rais kwa kuzingatia mapendekezo ya Kiongozi wa Upinzani katika Baraza la Wawakilishi. Kisha, Rais

wa Zanzibar huteua wajumbe wengine wawili kutoka katika majaji wa Mahakama Kuu kama anavyoona inafaa. Makamu Mwenyekiti wa ZEC huchaguliwa na wajumbe wa ZEC kutoka miongoni mwao.

Mamlaka ya ZEC yapo kisheria na yameainishwa katika Katiba ya Zanzibar na Sheria ya Uchaguzi No. 11 ya 1984, na Sheria ya Kura ya Maoni No. 6 ya 2010. ZEC ina mamlaka ya kusimamia uchaguzi wa Rais, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na madiwani, uchaguzi wa serikali za mitaa na kusimamia kura za maoni Zanzibar. ZEC pia ina jukumu la kupitia mipaka ya majimbo, kutunza na kuboresha daftari la kudumu la wapigakura, na kuendesha elimu ya mpigakura visiwani Zanzibar.

### *10.6.2 Uhusiano wa ZEC na NEC*

Uhusiano kati ya ZEC na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) unapaswa kutazamwa katika mjadala huu. Kisheria, tume hizi mbili zina maeneo yao ya kufanya kazi. Wakati ZEC husimamia uchaguzi wa Zanzibar, NEC husimamia uchaguzi wa Rais na Wabunge wa Jamhuri ya Muungano Bara na visiwani, lakini pia inasimamia uchaguzi wa madiwani Tanzania Bara. Hata hivyo, kuna ushirikiano rasmi kati ya Tume hizi mbili katika kazi zake. Kwa mfano, kifungu cha 74(13) cha katiba ya Jamhuri ya Muungano kinatamka kuwa NEC itakuwa inashauriana na ZEC katika kutekeleza majukumu yake.

Ushirikiano kati ya ZEC na NEC upo katika kuandikisha wapigakura ambapo wapigakura ambao wanakidhi vigezo vya ukaazi Zanzibar huorodheshwa katika daftari la kudumu ZEC. Kifungu cha 12A (1) cha Sheria ya Uchaguzi kinaweka wazi kuwa Sheria ya Zanzibar inayohusiana na utunzaji wa daftari la kudumu la wapigakura itatumika pia kusajili wapigakura wa Rais na Wabunge wa Jumahuri ya Muuangano. NEC inawasajili tu wale wapigakura ambao hawakukidhi vigezo vya kupiga kura katika uchaguzi wa Zanzibar kama kifungu cha 12A (2) kinavyotanabaisha. Hata hivyo, katika uchaguzi wa Octoba 2015, ingawa ZEC na NEC walitumia kituo kimoja lakini kila tume ilikuwa na upande wake na wapigakura walipaswa kumaliza kupiga kura katika uchaguzi mmoja kabla ya kwenda kupiga katika uchaguzi mwingine. Wapigakura pia walichovya vidole viwili tofauti katika wino kuashiria kuwa walimaliza kupiga kura. Ikumbukwe kuwa kuna baadhi ya wapigakura walioenda tu vituoni ili kupiga kura ya Rais wa Jamahuri ya Muungano.

Uhusiano wa NEC na ZEC ulichunguzwa kwa karibu zaidi mara baada ya kubatilishwa kwa matokeo kwa misingi ya ukikwaji wa taratibu za uchaguzi. Moja ya kanuni zilizokiukwa ni kuwa ZEC iligundua kukosekana kwa uwiano kati ya karatasi za kura na watu waliojiandikisha kupiga kura hasa katika vituo vya Pemba. Hii ni tuhuma nzito sana inayoathiri uhalali na kuaminika kwa matokeo ya uchaguzi. Hata hivyo, Mwenyekiti wa NEC Jaji Damian Lubuva alisisitiza kuwa chaguzi hizi zilisimamiwa katika mazingira tofauti. Moja ya mambo yanayochukuliwa kama ushahidi wa hoja hii ni kuwa ZEC iliongeza majimbo manne katika uchaguzi, lakini NEC iliamua kubaki na majimbo 50 ya mwaka 2010 Zanzibar.

### *10.6.3 Uandikishaji Wapigakura*

Mara nyingi hatua hii ya uchaguzi hughubikwa na vurugu kubwa Zanzibar. Mwezi June 2015 wakati uandikishaji wapigakura kwa kutumia BVR unaendelea, Mawaziri na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kutoka CUF walisusia bajeti wakilalamikia mchezo mchafu katika zoezi la uandikishaji. Gazeti la Mwananchi liliripoti kuwa viongozi wa CUF walituhumu kuwepo kwa urasimu wa makusudi uliowekwa na Serikali ya Mapinduzi ili kuwanyima watu vitambulisho vinavyotumika wakati wa kujiandikisha.



*Uandikishwaji wa Wapigakura*

### *10.6.4 Ugawaji wa Majimbo*

Kwa mujibu wa kifungu cha 120 (4) cha Katiba ya Zanzibar, ZEC imepewa mamlaka ya kupitia majimbo yote ya Zanzibar na kuyafanyia marekebisho ya kiidadi, majina, na mipaka kila baada ya miaka 8 hadi 10. Hivyo basi, mwezi Julai 2015 Mwenyekiti wa ZEC Jecha Salim Jecha alitangaza kwa vyombo vya habari kuwa ZEC ilifanya mapitio ya majimbo ya Zanzibar kwa kushirikisha vyama vya siasa, viongozi wa serikali wanaoshughulika na serikali za mitaa na utawala wa mikoa, jeshi la polisi, viongozi wa kuchaguliwa na asasi za kiraia. Matokeo yake, majimbo mapya manne yaliongezwa katika mkoa wa Mjini Magharibi likiwemo Pangawe, Kijitoupele, Welezo na Mtopepo. Majimbo mawili yalibadilishwa majina kama vile Mjimkongwe likaitwa Malindi na Kwamtipula likaitwa Shaurimoyo. Pia kuna Shehia na Kata ambazo zilibadilika kitu kilichopelekea kubadilika kwa vituo tofauti na ilivyokuwa 2010. Takwimu za TEMCO zinaonesha kuwa asilimia 4.5 ya waangalizi wa muda mrefu (LTOs) walisema kuwa pamekuwa na ongezeko la kata za wagombea udiwani Zanzibar, kuashiria kuwa kulikuwa na ongezeko la kata wakati wa mapitio ya majimbo. Hata hivyo, takwimu zinaonesha kuwa majimbo sita ( asilimia 27.3 ya majimbo yote) yalilalamikiwa katika mchakato wa kuongeza majimbo mapya. Malalamiko yaliyorekodiwa kwenye ripoti za waangalizi wa TEMCO yanaeleza kuwa majimbo yote yaliongezwa kwenye ngome ya CCM Unguja tu na sio kwenye ngome ya CUF.




*Mwenyekiti wa ZEC Akiongea na Vyombo vya Habari*

***10.6.5 Uteuzi wa Wagombea kwa Vyama vya Siasa na ZEC***

Chaguzi za Zanzibar zina upekee kwa kuwa na vyama vikuu viwili vinavyoshindana ingawa mwaka 2015 kulikuwa na vyama 18 viliyosimamisha wagombea. CCM na CUF vilivutia wagombea wengi sana katika mchakato wa uteuzi wa ndani. Hivyo basi vyama hivi vilitumia mfumo wa kura za wazi katika nafasi zote ili wanachama wachague wagombea waliopendwa zaidi.




*Mgombea wa CCM Dr. Ali Mohamed Shein Akikabidhiwa Fomu na Mwenyekiti wa ZEC*

Uteuzi wa wagombea wa viti maalum ulitofautiana kati ya chama na chama. Uteuzi wa ndani ya CCM na CUF ulisimamiwa na tawi la wanawake katika ngazi za wilaya na mikoa. CCM na CUF walitumia kura za wazi kwa wanachama wakati vyama vingine vilitumia njia mchanganyiko.




*Mgombea wa CUF Maalim Seif Sharif Hamad baada ya Kuchukua Fomu kutoka kwa Mwenyekiti wa ZEC*

Waangalizi wa TEMCO pia waligundua kuwa vyama vyingine vya siasa vilikuwa na wafuasi wachache kiasi kwamba wanachama wao wachache sana walichukua fomu za kugombea nafasi mbalimbali. Baadhi ya nafasi kama vile udiwani hazikupata wagombea au waliojitokeza walikuwa wachache sana. Kwa ujumla, ripoti za waangalizi wa TEMCO zinaonesha kuwa uteuzi wa wagombea ndani ya vyama ulienda vizuri kwa kuwa vyama vya siasa vilijaribu kuzuia migawanyiko ya ndani. Takwimu zinaonesha kuwa ndani ya CCM asilimia 9.1 ya malalamiko yalirekodiwa katika uteuzi wa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na asilimia 4.5 katika uteuzi wa madiwani. Hakuna malalamiko yaliyorekodiwa kwa upande CUF.

ZEC kwa upande wake iliwapitisha wagombea wote waliopendekezwa na vyama vyao vya siasa. Hata hivyo, kutokana na ushindani wa kisiasa visiwani Zanzibar kati ya CCM na CUF wagombea walitarajiwa kuweka pingamizi dhidi ya wapinzani wao. Kwa mfano, CUF waliweka pingamizi mara mbili dhidi ya wagombea wa CCM katika nafasi ya ujumbe wa Baraza la Wawakilishi, lakini pingamizi hizi zilitupiliwa mbali na ZEC. Ripoti za waangalizi wa muda mrefu wa TEMCO zinaonesha kuwa zoezi la uteuzi ndani ya vyama ulifanyika vizuri japo ulikuwa na mapungufu machache kama inavyoonyeshwa katika Jedwali 10-1.

*Jedwali 10-1: Tathmini ya Uteuzi wa Wagombea ndani ya Vyama vya Siasa*

| Maelezo | Daraja | Idadi ya Marudio | Asilimia |
|---|---|---|---|
| Uteuzi ambao japo una mapungufu kadhaa, ni mapungufu ya kawaida na yasiyoweza kuathiri matokeo ya uteuzi. Ni uteuzi safi na wa kiungwana. | A (80 - 100%) | 12 | 54.6 |
| Uteuzi ambao kwa jumla ni huru na haki, lakini bado kuna mapungufu ambayo yanaweza kuathiri sudi za baadhi ya wagombea. | B (60 - 79%) | 9 | 40.9 |
| Uteuzi wenye kuruhusu wadau wote (vyama, wagombea, wanachama) washiriki, lakini kukawepo matukio mengi ya kutozingatia sheria na kanuni za uteuzi (na kutoadhibiwa kwa hilo), na ukawepo upendeleo unaoathiri mafanikio ya baadhi ya wagombea. | C (50 - 59%) | 1 | 4.5 |
| Uteuzi uligubikwa na dosari nyingi kutokana na ukikwaji wa baadhi ya sheria, kanuni, udhaifu wa kiuendeshaji (management), na uwepo wa vitisho (Intimidation), na upendeleo. | D (40 - 49%) | 0 | 0.00 |
| Uteuzi umevurugika au kuborongwa (mismanaged) kiasi kwamba inashindikana kwa wadau kuwakubali walioteuliwa. Ni kama mwanafunzi aliyefeli mtihani. | E (1 - 39%) | 0 | 0.00 |
| Mwenendo wa uteuzi katika vyama vingi ulikuwa mbaya sana. Kulikuwepo upendeleo mkubwa, mizengwe na rushwa kiasi kwamba baadhi ya wagombea waliamua kujiondoa katika uchaguzi au kuchukua hatua za kisheria au nyinginezo. Uteuzi umekuwa kama mimba iliyoharibika. | F (0%) | 0 | 0.00 |
| Total | | 22 | 100.0 |

Chanzo: Taarifa za Waangalizi wa TEMCO, 2015

### *10.6.6 Kampeni za Uchaguzi*

Vyama vikuu CCM na CUF vilikuwa na sera zilizoelezeka kinagaubaga zikijumuisha pamoja na mambo mengine mambo ya uchumi, kijamii na haki za binadamu. Hata hivyo, ushindani wa dhati kati ya vyama hivi viwili ulijionesha hasa katika `misemo ya kampeni waliyoitumia ili kuwateka wapigakura. Kwa upande wa CUF misemo yao ilikuwa "Mamlaka kamili" ikitafsiriwa kama kuirudishia Zanzibar hadhi yake ya dola. Hata hivyo, msemo/kauli hii ilitafsiriwa kama dhamira ya kuvunja muungano. Msemo mwingine wa CUF ni kuifanya Zanzibar iwe Singapore ya Afrika ya Mashariki kiuchumi. CCM kwa upande wao walikuwa na misemo mingi pia. Mbali na msemo wa Umoja ni Ushindi, walihimiza pia msemo wao wa "Mapinduzi Daima".

Mikutano ya kampeni iliibua utata kwa kiasi chake. CCM kwa mfano, walishikilia msimamo wao wa siku nyingi dhidi ya CUF. Iliripotiwa na waangalizi wa TEMCO kuwa Mwenyekiti wa chama wa mkoa wa Mjini Magharibi aliongea bila kupepesa macho akiwa kwenye mkutano Fuoni Kibonde Mzungu, jimbo la Dimani kwamba CUF ni sawa tu na ZNP ya miaka ya 1950 na 1960, na kwamba wao CCM hawapo tayari kuwaachia madaraka ya nchi watu waliowapindua miaka 50 iliyopita. Kiongozi huyu wa Chama aliongeza kuwa CCM haikuwa tayari kuiacha Serikali ya Mapinduzi iende kwa karatasi za kura tu. Vilevile, waangalizi wa TEMCO walimnukuu mgombea wa nafasi ya Ujumbe wa Baraza la Wawakilishi DR.

Mwinyihaji Makame katika mkutano wa kampeni Fumba akisema kuwa Maalim Seif Sharif Hamad, ambaye alikuwa mgombea urais wa CUF hatakuja atawale Zanzibar maishani mwake.

Vitendo vya ubaguzi wa rangi na ukabila vilirekodiwa na waangalizi wa TEMCO lakini kwa kiasi kidogo sana. Kwa mfano, kati ya waangalizi wa TEMCO 22 wa muda mrefu visiwani Zanzibar, asilimia 18.2 tu waliripoti vitendo vya ukabila katika mikutano ya kampeni. Moja ya matukio ya ovyo yaliyofanywa kwa kasi sana ni kuharibu nyenzo za kampeni kama vile mabango. Kwa mfano, takwimu za TEMCO zinaonesha kuwa asilimia 54.5 ya waangalizi wote 22 waliokuwa Zanzibar waliripoti kuona mabango yakiwa yameharibiwa. Hata hivyo ni vyema tukiri kuwa pamoja na uchokozi uliojitokeza katika mikutano, kampeni zote ziliisha kwa amani.

Kama iliyooneshwa katikaJedwali 10-2, ripoti za waangalizi wa TEMCO zinaonesha kuwa kwa ujumla mchakato wa kampeni ulikuwa wa amani, ingawa kulikuwa na mapungufu ambayo katika ujumla wake hayakuathiri mwenendo wa kampeni, kwa kuzifanya zisiwe huru na haki.

***Jedwali 10-2: Tathmini ya Mchakato wa Kampeni***

| Maelezo | Daraja | Idadi ya Marudio | Asilimia |
|---|---|---|---|
| Kampeni ambao japo zina mapungufu kadhaa, ni mapungufu ya kawaida na yasiyoweza kuathiri matokeo ya uchaguzi. Ni kampeni safi na za kiungwana. | A (80 - 100%) | 8 | 36.4 |
| Kampeni ambazo kwa jumla ni huru na haki, lakini bado kuna mapungufu ambayo yanaweza kuathiri sudi za baadhi ya wadau (vyama, wagombea, wapigakura). | B (60 - 79%) | 13 | 59.1 |
| Ni kampeni zenye kuruhusu wadau wote (vyama, wagombea, wanachama) washiriki, lakini kukawepo matukio mengi ya kutozingatia sheria na kanuni za kampeni (na kutoadhibiwa kwa hilo), na ukawepo upendeleo unaoathiri mafanikio ya baadhi ya wagombea na vyama vyao. | C (50 - 59%) | 0 | 0.0 |
| Kampeni zilizogubikwa na dosari nyingi kutokana na ukikwaji wa baadhi ya sheria, kanuni, udhaifu wa kiuendeshaji (management), na uwepo wa vitisho (Intimidation), na upendeleo. | D (40 - 49%) | 1 | 4.5 |
| Kampeni zimevurugika au kuborongwa (mismanaged) kiasi kwamba inashindikana kujua nini kinaendelea. Ni kama mwanafunzi aliyefeli mtihani. | E (1 - 39%) | 0 | 0.00 |
| Mwenendo wa kampeni za wagombea wengi ulikuwa mbaya sana. Kulikuwepo fujo nyingi, kuhujumiana, na rushwa kiasi kwamba baadhi ya wagombea waliamua kujiondoa katika uchaguzi au kuchukua hatua nyinginezo. Kampeni zimekuwa kama mimba iliyoharibika. | F (0%) | 0 | 0.00 |
| Total | | 22 | 100.0 |

Chanzo: Taarifa za Waangalizi wa TEMCO, 2015




*Mkutano wa CUF wa Kampeni ya Urais ChakeChake*

Vyama vikuu vya siasa Zanzibar vilitumia mbinu tofauti tofauti za kampeni. Kwa mujibu wa ripoti za waangalizi wa TEMCO, vyama vya siasa, hasa CUF na CCM walitumia njia zozote zile kuhakikisha mikutano yao inahudhuriwa kwa wingi. Hivyo basi, watu walikuwa wakisafirishwa kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa boti au magari, huku pia wakitumia vikundi vya sanaa, muziki na burudani nyinginezo. Hii ilikuwa ni mbinu ya kisaikolojia ya kuvutia wahudhuriaji wengi huku wakijaribu kuwashinda wapinzani wao. Vyama hivi pia vilikuwa na vipaza sauti vyenye uwezo mkubwa sana.





*Kushoto: Lori likiwa limebeba wafuasi wa CCM Bububu. Kulia: lori likiwa limebeba wafuasi wa CUF- Mkoani*

*10.6.7 Maandalizi ya Siku ya Uchaguzi*

Maandalizi ya siku ya uchaguzi Zanzibar yalienda vizuri. Ripoti za waangalizi wa TEMCO zinaonesha kuwa orodha ya wapigakura ilibandikwa vituoni ikiwa inasomeka vizuri na kwa kuzingatia alfabeti tarehe 18 Oktaba 2015- siku saba kabla ya siku ya kupiga kura kama sheria inavyoelekeza. Takwimu za wangalizi wa TEMCO zinaonesha pia kuwa asilimia 60 ya vifaa vya kupigia kura vilisambazwa siku moja kabla ya siku ya kupiga kura na asilimia 31.8 vilisambazwa siku ya uchaguzi.




*Masanduku ya Kura katika mojawapo ya Vituo vya Kupigia Kura*

Usambazwaji wa vifaa vya kupigia kura ulifanywa na maafisa wa ZEC wakiambatana na walinzi. Kwa ujumla, vifaa vyote vilivyohitajika katika uchaguzi vililetwa kwenye vituo ilipofika saa 12 asubuhi, ingawa vifaa vichache tu vilikosekana. Kwa mujibu wa waangalizi wa TEMCO, malalamiko yaliyojitokeza ni kukosekana kwa fomu ya kujazia matokeo ya urais wa Jamhuri ya Muungano. Waangalizi wa TEMCO walilipoti pia kuwa, mpangilio wa vituo vya kupigia kura ulifanyika kwa mujibu wa taratibu za uchaguzi Zanzibar.


*10.6.8 Kufunguliwa kwa Vituo vya Kupigia Kura*

Ripoti za waangalizi wa TEMCO kwa Unguja na Pemba zinaonesha kuwa vituo vilikuwa tayari saa 12 asubuhi na vilifunguliwa katika muda uliowekwa kisheria, ambao ni saa 1 kamili asubuhi. Waangalizi wa TEMCO hawakurekodi kituo chochote kilichofunguliwa zaidi ya muda uliowekwa kisheria.




*Mgombea wa Urais wa CCM, Dkt Ali Mohamed Shein Akitumia Haki yake ya Kupiga Kura*

Kwa mujibu wa waangalizi wa TEMCO, zoezi la kupiga kura lilikwenda vizuri kabisa. Pamoja na maafisa wa ZEC, vituo vilikuwa na polisi wenye sare lakini ambao hawakuwa na silaha waliokuwa wakilinda usalama; mawakala waliowakilisha vyama vya siasa na wagombea, na waangalizi wa uchaguzi. Mbali na kufuatilia mchakato wa kupiga kura mawakala walitumika pia kuwatambua wapigakura kwa kuwa walikuwa wanatoka maeneo hayo. Zoezi hili lilikuwa muhimu sana ili kuhakikisha kuwa waliopiga kura wote walistahili kutokana na majina na picha zao kwenye kitabu cha wapigakura. Zoezi la upigaji kura lilifungwa saa kumi jioni isipokuwa pale tu ambapo wapigakura walikuwa bado wamejipanga kwenye mistari.




*Mgombea Urais wa CUF, Mh. Seif Sharif Hamad Akitumia Haki yake ya Kupiga Kura*

### *10.6.9 Kuhesabu Kura*

Zoezi la kuhesabu kura lilianza mara tu baada ya kukamilika kwa zoezi la kupiga kura. Kura zilichambuliwa vizuri kwa kutenganisha kura halali na kura zilizoharibika kwa mujibu wa kanuni na taratibu. Kwa ujumla, takwimu za TEMCO zinaonesha kuwa hapakuwa na malalamiko juu ya maamuzi ya kura halali na zilizoharibika.




*Mgombea Urais wa ADC, Mh. Hamad Rashid Mohamed Akiitumia Haki yake ya Kupiga Kura*

Takwimu za TEMCO zinaonesha pia kuwa kwa nchi nzima, asilimia 2.42 tu ya malalamiko yalirekodiwa kabla ya matokeo hayajatangazwa. Namba hii ni ndogo sana kuweza kuathiri matokeo ya uchaguzi wote.

### *10.6.10 Kutangazwa kwa Matokeo na Matukio baada ya Uchaguzi*

Ripoti za Waangalizi wa TEMCO zinaonesha kuwa matokeo ya uchaguzi wa madiwani, wawakilishi na urais yalitangazwa katika ngazi za kata, jimbo na ngazi ya taifa katika mpangilio huo. Ripoti hizi zinaonesha pia watu walipokea matokeo kwa shangwe na nderemo, hasa kwa wale walioshinda. Hapakuwa na matukio ya kuashiria kuwepo kwa vurugu. Tathmini ya waangalizi wa TEMCO siku ya uchaguzi imeonyeshwa katika Jedwali 10-3.

***Jedwali 10-3: Tathmini ya Siku ya Kupiga Kura***

| Maelezo | Daraja | Idadi ya Marudio | Asilimia |
|---|---|---|---|
| Upigaji kura ambao ulikuwa na mapungufu kadhaa, ni mapungufu ya kawaida na yasiyoweza kuathiri matokeo ya uchaguzi. Ni upigaji kura safi na wa kiungwana. | A (80 - 100%) | 480 | 66.2 |
| Upigaji kura ambao kwa jumla ni huru na haki, lakini bado kuna mapungufu ambayo yanaweza kuathiri kwa kiasi sudi za baadhi ya wadau (vyama, wagombea, wapigakura). | B (60 - 79%) | 218 | 30.0 |
| Ni upigaji kura wenye kuruhusu wadau wote (vyama, wagombea, wanachama) washiriki, lakini kukawepo matukio mengi ya vyama vikubwa au chama tawala kutozingatia sheria na kanuni za kampeni (na kutoadhibiwa kwa hilo), na ukawepo upendeleo unaoathiri mafanikio ya baadhi ya wagombea na vyama vyao. | C (50 - 59%) | 24 | 3.2 |
| Upigaji kura uligubikwa na dosari nyingi kutokana na ukikwaji wa baadhi ya sheria, kanuni, udhaifu wa kiuendeshaji (management), na uwepo wa vitisho (intimidation), na upendeleo. | D (40 - 49%) | 4 | 0.6 |
| Upigaji kura umevurugika au kuborongwa (mismanaged) kiasi kwamba inashindikana kujua nini kinaendelea. Ni kama mwanafunzi aliyefeli mtihani. | E (1 - 39%) | 0 | 0.00 |
| Mwenendo wa upigaji kura ulikuwa mbaya sana. Kulikuwepo fujo nyingi, kuhujumiana, na rushwa kiasi kwamba baadhi ya wagombea waliamua kujiondoa katika uchaguzi au kuchukua hatua nyinginezo. Upigaji kura umekuwa kama mimba iliyoharibika. | F (0%) | 0 | 0.00 |
| Total | | 22 | 100.0 |

Chanzo: Taarifa za Waangalizi wa TEMCO, 2015

Kwa kuzingatia hatua zote muhimu za uchaguzi, tathmini ya jumla ya TEMCO katika uteuzi wa wagombea, kampeni, michakato ya kupiga na kuhesabu kura pamoja na kutangazwa kwa matokeo imewasilisha katika Jedwali 10-4.

*Jedwali 10-4: Tathmini ya Jumla ya Mwenendo wa Uchaguzi*

| Maelezo | Daraja | Idadi ya Marudio | Asilimia |
|---|---|---|---|
| Mwenendo wa uchaguzi ulikuwa na mapungufu kadhaa, ni mapungufu ya kawaida na yasiyoweza kuathiri matokeo ya uchaguzi. Ni upigaji kura safi na wa kiungwana. | A (80 - 100%) | 11 | 50.0 |
| Ni uchaguzi ambao kwa jumla ni huru na haki, lakini bado kuna mapungufu ambayo yanaweza kuathiri kwa kiasi sudi za baadhi ya wadau (vyama, wagombea, wapigakura). | B (60 - 79%) | 11 | 50.0 |
| Ni uchaguzi wenye kuruhusu wadau wote (vyama, wagombea, wanachama) washiriki, lakini kukawepo matukio mengi ya vyama vikubwa au chama tawala kutozingatia sheria na kanuni za kampeni (na kutoadhibiwa kwa hilo), na ukawepo upendeleo unaoathiri ushiriki au mafanikio ya baadhi ya wagombea na vyama vyao. | C (50 - 59%) | 0 | 0.00 |
| Uchaguzi uligubikwa na dosari nyingi kutokana na ukikwaji wa baadhi ya sheria, kanuni, na udhaifu wa kiuendeshaji (management), na kuwepo kwa vitisho (intimidation), na upendeleo. | D (40 - 49%) | 0 | 0.0 |
| Uchaguzi umevurugika au kuborongwa (mismanaged) kiasi kwamba inashindikana kujua nini kinaendelea. Ni kama mwanafunzi aliyefeli mtihani. | E (1 - 39%) | 0 | 0.00 |
| Mwenendo wa uchaguzi ulikuwa mbaya sana. Kulikuwepo fujo nyingi, kuhujumiana, na rushwa kiasi kwamba baadhi ya wagombea waliamua kujiondoa katika uchaguzi au kuchukua hatua nyinginezo. Uchaguzi umekuwa kama mimba iliyoharibika. | F (0%) | 0 | 0.00 |
| Total | | 22 | 100.0 |

Chanzo: Taarifa za Waangalizi wa TEMCO, 2015

Kama ilivyooneshwa katika Jedwali 10-4, tathmini ya jumla ya TEMCO juu ya utazamaji wa uchaguzi wa Zanzibar inaonesha uchaguzi ulikuwa safi, huru na haki ambao ulizingatia matakwa ya wapigakura.

### 10.7 Kubatilishwa kwa Matokeo ya Uchaguzi

Wakati ZEC walipokuwa wakiendelea kutangaza matokeo kutoka majimboni, na kabla ZEC haijamtangaza mshindi wa uchaguzi wa Rais, kuna mlolongo wa matukio ambao ulibadilisha mtiririko ulioonekana kwenda katika mpangilio mzuri. Tarehe 26 Oktoba 2015, CUF walitoa tamko kwa umma wakidai kuwa mgombea wao Seif Sharif Hamad alishinda uchaguzi huo kwa silimia 52.87 dhidi ya asilimia 47.13 za mpinzani wake Dkt. Ali Mohammed Shein wa CCM. Sehemu ya tamko hilo ambalo halikusainiwa lenye kichwa cha habari "Chama cha Wananchi CUF chashinda uchaguzi wa kihistoria Zanzibar" linasomeka kama ifuatavyo:

> Mpaka kufikia saa 3:30 asubuhi hii, Maalim Seif Hamad, mgombea urais wa CUF Zanzibar amepata kura 200,077 dhidi ya mpinzani wake Dkt Ali Mohamed Shein wa CCM aliyepata kura 178,363. Hivyo CUF imepata ushindi wa jumla ya kura 21,714 sawa na asilimia 52.87 dhidi ya asilimia 47.13.... Wananchi wa Zanzibar wameongea... Sasa hakuna shaka Maalim Seif ameshinda uchaguzi wa rais Zanzibar na chama tawala kimeangushwa kwa mara ya kwanza tangu 1977 [sic].

Tarehe 28 Oktoba 2015 Mwenyekiti wa ZEC, Jecha Salim Jecha akatangaza kufutwa kwa matokeo ya uchaguzi huo akitangaza kwamba tarehe ya marudio ya uchaguzi itatajwa baadae. Katika tamko lake kwa vyombo vya habari, Mwenyekiti wa ZEC alieleza kuwa kubatilishwa kwa matokeo hayo ya uchaguzi kunatokana na matatizo ambayo Tume ilikumbana nayo wakati wa kusimamia uchaguzi ikiwemo:

1. Tofauti kati ya makamishina wa Tume ambazo zilipelekea kuvua mashati na kuanza kupigana;
2. Kugundulika kwa kasoro za taratibu hasa Pemba ambako ilibainika kura zilikuwa nyingi kuliko idadi ya wapigakura katika daftari la kudumu. Vilevile, uhesabuji kura Pemba haukufanyika vituoni kwa mujibu wa sheria ambapo masanduku ya kura yalisafirishwa kwingineko;
3. Kuna kundi la vijana lililokuwa likiwazuia wafuasi wa vyama vingine kupiga kura Pemba;
4. Vyama vya siasa vilipola madaraka ya ZEC ya kutangaza matokeo ya Rais;
5. Mawakala wa vyama waliondolewa vituoni kwa nguvu kitu ambacho kiliathiri uhalali wa matokeo. Mwenyekiti wa ZEC alitolea mfano wa mawakala wa TADEA;
6. Fomu za awali za matokeo Pemba zilikuwa zimefutwafutwa na kuandikwa upya kitu kilichozipotezea kuaminika.

Tamko la kubatilishwa matokeo yote ya uchaguzi Zanzibar kama yalivyotolewa na Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi yaliwashtua CUF, Waangalizi wa uchaguzi na jumuiya ya kimataifa.




*Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar, Jecha Salim Jecha*

Uongozi wa CUF ulikutana tarehe 7 Novemba 2015 kujadili uamuzi huo na baadae wakatoa tamko. Katika tamko lao, CUF walidai kuwa mchakato wa uchaguzi kuanzia kwenye kupiga kura, kuhesabu kura na kutangaza matokeo ulienda vizuri kabisa. Kwa mujibu wa tamko lao, matokeo ya uchaguzi huu yalisubiri tu kuidhinishwa na ZEC katika kituo cha taifa cha kujumlishia matokeo, ambapo matokeo ya majimbo 31 kati ya 54 yalikuwa yamekwisha idhinishwa. CUF walilikosoa tamko la ZEC la kufuta matokeo wakidai halikuwa na nguvu ya vifungu vya kisheria au kikatiba. CCM kwa upande wao walikubaliana na uamuzi wa ZEC.

Uamuzi wa ZEC pia ulipata upinzani kutoka Jumuiya ya Wanasheria Zanzibar (ZLS) na Jumuiya ya Wanasheria wa Tanganyika (TLS). Jumuiya za kimataifa kama vile Jumuiya ya

Madola, Jumuiya ya Umoja wa Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), Umoja wa Afrika na Umoja wa Ulaya walishtushwa sana na hatua ya ZEC na wakatoa tamko lililoelezea uchaguzi ulikuwa wa amani na uliendeshwa kwa mujibu wa sheria. Jumuiya hizi za kimatifa ziliwataka ZEC kutoa ushahidi wa sababu zilizowafanya wabatilishe uchaguzi na kutatua mgogoro uliotokana na kitendo hicho kabla haujafika mbali.



*Mwenyekiti wa ZEC Akitoa Tamko Linalohusiana na Uchaguzi*

Swali la msingi linaloulizwa ni kama ZEC ina mamlaka ya kisheria kufuta matokeo ya uchaguzi Zanzibar. Kwa mujibu wa CUF, ZEC haina mamlaka ya kufuta matokeo yote ya uchaguzi isipokuwa tu kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 74 cha Sheria ya Uchaguzi ambapo mchakato wa upigaji kura unaweza kuahirishwa mpaka siku ya pili yake kama pakitokea vurugu. Taarifa zinaonesha hapakuwa na vitendo vya vurugu vilivyotokea katika kituo chchote Zanzibar na hakuna msimamizi wa kituo aliyeahirisha uchaguzi. Kama matatizo yangetokea kwenye vituo mawakala walitakiwa kujaza fomu kwa mujibu wa kifungu cha 76(1) cha Sheria ya Uchaguzi wa Zanzibar Namba 11 ya 1984.

Eneo lingine lililogubikwa na utata ni kama kweli tamko la Mwenyekiti wa ZEC lilikuwa na uhalali wa kisheria. Katiba ya Zanzibar kifungu cha 119 (10) inayapa uhalali maamuzi yote ya ZEC endapo tu yametolewa kwa kuzingatia akidi inayohusisha Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti na wajumbe wanne. Kifungu cha 3(1) na 3(2) vya Sheria ya Uchaguzi Zanzibar vinahalalisha matangazo yote yatolewayo na ZEC na kusainiwa na Mwenyekiti au Mkurugenzi wa Uchaguzi. Hata hivyo, Kifungu cha 3(2) kinataka matangazo hayo yawe yamepata kukubaliwa na Tume ya Uchaguzi, kwa maana ya akidi ya kikatiba. Kuna wasiwasi kama maamuzi ya kufutwa kwa matokeo ya uchaguzi yaliyotamkwa na Mwenyekiti wa ZEC yalifikiwa na akidi au yalikuwa maamuzi yake binafsi.

Mwisho, hoja inaweza kutolewa kuwa ZEC imepewa mamlaka ya kikatiba ya kusimamia uchaguzi, ambayo yanajumuisha pia kufuta matokeo ya uchaguzi, lakini mazingira yaliyopelekea kufutwa kwa uchaguzi wa 2015 yalileta mashaka makubwa. Ni muhimu

tukatambua kuwa, kiwango cha uvunjifu wa taratibu za uchaguzi kilichosemwa katika uchaguzi wa 2015 hakiwezi kulinganishwa na kile cha mwaka 2000 ambapo TEMCO walilazimika kuuita uchaguzi huo kama mimba iliyoharibika. Mpaka sasa ZEC wameshindwa kutoa ushahidi wa madai yake ya tuhuma za uvunjwaji wa taratibu za uchaguzi huku waangalizi wa uchaguzi wa ndani na nje wakisema uchaguzi ulienda vizuri. Hata hivyo, uamuzi wa ZEC ulileta mkanganyiko mkubwa wa kikatiba uliohitaji ufafanuzi wa kisheria wa Mahakama Kuu. Kwa bahati mbaya hakuna mtu, kundi au taasisi yeyote iliyoenda mahakamani kutaka ufafanuzi huo.

### 10.8 Utatuzi wa Migogoro baada ya Uchaguzi

Kubatilishwa kwa matokeo ya uchaguzi, na msisitizo wa ZEC kuwa uchaguzi huo utarudiwa kulipandisha joto la kisiasa visiwani Zanzibar. Kwa kuzingatia ufanisi wa majadiliano ya ana kwa ana huko nyuma CCM na CUF walienda kwenye meza ya majadiliano kujaribu kutafuta suluhu ya mgogoro huo. Viongozi wa CCM na CUF walikutana mara kadhaa kujaribu kutatua mkwamo wa kisiasa. Maelezo ya majadiliano hayakuwekwa wazi lakini tarehe 11 Januari 2016 aliyekuwa mgombea Urais wa CUF aliita vyombo vya habari. Kwa mshangao wa wengi, Seif Sharif Hamad aliurudia msimamo wa CUF kuwa alishinda uchaguzi wa tarehe 25 Oktoba 2015 kwa jumla ya asilimia 52.84. Maalim Seif aliendelea kusema kuwa CUF hawakuwa tayari kushiriki uchaguzi wa marudio. Katika kumbukumbu ya sikukuu ya Mapinduzi, Dkt Shein aliwaasa Wazanzibari kujiandaa na uchaguzi wa marudio kama utakavyotangazwa na ZEC. Dkt Shein aliwataka Wazanzibari kutambua uhuru wa ZEC na kuheshimu maamuzi yake. Hatimaye Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ilitangaza marudio ya uchaguzi huo kuwa tarehe 20 Machi 2016. Uchaguzi wa marudio ulifanyika kama ilivyopangwa, na kwa mujibu wa ZEC hakuna Chama cha siasa kilichoomba rasmi kujitoa katika uchaguzi. Hata hivyo baadhi ya vyama vya siasa ikiwemo CUF walitangaza kutoshiriki uchaguzi wakiwaasa wafuasi wao kutokupiga kura. Vyama vilivyoshiriki katika uchaguzi ni ADC, AFP, CCK, CCM, SAU na TADEA. CCM ilipata ushindi mnono sana katika matokeo ya uchaguzi wa marudio ikishinda kila nafasi iliyogombaniwa ikiwemo asilimia 91.4 za urais wa Zanzibar. Kwa mujibu wa ZEC asilimia 67.9 ya wapigakura walijitokeza katika uchaguzi wa marudio. Matokeo haya hayakulazimisha kuundwa kwa SUK kwa kuwa hakuna chama kilichopata asilimia 10 ya kura za Rais wala kiti katika Baraza la Wawakilishi kama Katiba ya Zanzibar inavyofafanua .Rais Shein hakuteua Makamu wa Kwanza wa Rais. Hata hivyo, Rais aliwateua mawaziri watatu miongoni mwa wagombea wa urais ili kuleta ishara ya kuwepo kwa serikali ya mseto.

#### *10.8.1 Kuingilia Mgogoro wa Zanzibar*

Kwa masilahi ya amani, mgogoro wa uchaguzi wa Zanzibar ulivuta hisia za wahusika wa kimataifa na wa ndani ya nchi. Nafasi ya Serikali ya Jamhuri ya Muuangano kwa Zanzibar ni ngumu kuifikilia. Kwa upande mmoja Serikali ya Muungano inaonekana kama mhusika wa nje katika mgogoro wa Zanzibar. Vyombo vya habari vilimripoti Rais wa Muungano Dkt. John Magufuli akihimiza kuwa viongozi wa Zanzibar watafute suluhu wao wenyewe. Katika mkutano wake na Dkt Shein na Maalim Seif Sharif Hamad katika nyakati tofauti Ikulu ya Dar es Salaam, Rais Magufuli alitoa hisia kuwa mazungumzo yaliendelea vizuri. Hata hivyo, Serikali ya Muungano inaangaliwa pia kama sehemu ya mgogoro wa Zanzibar kwa kuwa chama tawala cha CCM ndicho kinachoongoza pande zote mbili za muungano. Kwa maneno

mengine, CCM inahusika moja kwa moja na kile kinachotokea Bara na Zanzibar. Kwa kuzingatia hoja hii, tunaweza kusema kuwa Serikali ya Muungano haijashiriki ipasavyo kuzuia au kutatua mgogoro wa Zanzibar.

Wafadhili na Jumuiya ya Kimataifa wana rekodi nzuri ya kuzisukuma Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zaznibar kutafuta suluhu ya migogoro ya uchaguzi visiwani humo. Kwa mfano, baada ya mgogoro wa uchaguzi wa Rais 1995, wafadhili walishikilia misaada iliyokusudiwa kwenda Zanzibar. Denmark ilishikilia msaada wa chanjo ya watoto wakati Finland ilishikilia msaada wa maji mjini Zanzibar (Bakari 2000: 269). Vilevile Norway iliondoa msaada wake uliokusudiwa kufadhiri mradi wa uhifadhi wa mazingira Zanzibar (Ibid). Kufuatia mgogoro wa matokeo ya 2015, Marekani waliondoa msaada usio na riba wa Dola za kimarekani 472.8 ambao ni sawa na trilioni 1, msaada wa Mradi wa Changamoto ya Milenia uliokusudiwa kusaidia miradi ya kusambaza umeme Tanzania. Marekani iliondoa msaada huu ili kuilazimisha Serikali ya Mungano na Chama cha Mapinduzi kutafuta suluhisho katika mgogoro wa Zanzibar. Kwa ujumla, jumuiya za kimataifa zimezuiwa na mambo mawili kuweza kuingilia moja kwa moja mgogoro wa Zanzibar. Mosi, ukweli kuwa Zanzibar ni sehemu ya jamhuri ya muungano wa Tanzania, kuingilia mambo yake itatafsiriwa kama kuingilia uhuru wa Tanzania. Pili, mgogoro huo haukufikia kiwango cha vurugu kiasi cha kuilazimisha jumuiya ya kimatifa kuingilia kwa mantiki ya kuzuia uvunjivu wa haki za binadamu.

## 10.9 Hitimisho na Mapendekezo

### *10.9.1 Hitimisho*

Uchaguzi Zanzibar wa Oktoba 2015 ulianza kwa ahadi pevu. Waangalizi wa ndani na nje na wadau wengine walitegemea kuona uchaguzi wa amani, ambao ungesimamiwa kwa weledi mkubwa na ZEC. Uchaguzi huo ulitarajiwa kuendeshwa katika mazingira ya kuaminiana kama ilivyokuwa mwaka 2010 hasa kutokana na Serikali ya Umoja wa Kitaifa iliyoundwa baada ya kura ya maoni ya Julai 2010. Mgawanyo wa madaraka ulitazamiwa kama suluhisho la kudumu la migogoro ya uchaguzi inayoikumba Zanzibar ambayo ililetwa na mfumo wa mshindi-huchua-vyote uliotumika kabla ya 2010. Hivyo basi SUK ilitazamwa kama chombo cha kujenga imani na kuaminiana na kuruhusu mabadilishano ya madaraka kwa amani. Hata hivyo, kubatilishwa kwa matokeo ya Oktoba 2015 kunatoa picha tofauti. Hata hivyo, kufutwa kwa matokeo ya uchaguzi wa 2015 na kususiwa kwa uchaguzi wa marudio kumeathiri SUK.

### *10.9.2 Mapendekezo*

Uchaguzi wa marudio kama ulivyotangazwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kufuatia kufutwa kwa matokeo ya uchaguzi wa Oktoba 2015, ulifanyika na matokeo yalitangazwa. CUF iligoma kushiriki uchaguzi huo ikiruhusu CCM kushinda nafasi zote zilizoshindaniwa kuanzia Urais, wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Udiwani. Kwa masilahi ya Zanzibar yenye amani na chaguzi za kuaminika siku za mbeleni, tungependa kupendekeza yafuatayo:

(i) Katiba na Sheria za uchaguzi Zanzibar zifanyiwe marekebisho ili kuonesha kinagaubaga mamlaka ya ZEC na mazingira yanayoweza kupelekea maamuzi makubwa kama vile kufuta uchaguzi mkuu;

(ii) Vyama vya siasa pamoja na wagombea urais kuheshimu mamlaka ya ZEC kutokana na vifungu vya Katiba ya Zanzibar na sheria husika;

(iii) Wadau wote, hasa CCM na CUF kutunza utulivu na kujizuia kuleta vurugu au kutoa matamko yanayoweza kuhamasisha au kuongeza mivutano na migogoro isiyo na maana;

(iv) Wanaolalamikia kitendo cha kufutwa kwa matokeo ya uchaguzi wa tarehe 25 Oktoba 2015 kutafuta suluhu kupitia vyombo vya kisheria vilivyowekwa ili kutunza amani na utangamano wa kisheria;

(v) Uongozi wa juu wa Jamhuri ya Muungano kuangalia namna ya kutatua migogoro ambayo inaweza kumomonyoa utengamano wa jamii sio tu kwa visiwani bali hata Tanzania bara;

(vi) Wapenda amani wote wakiwemo Jumuiya za kimataifa, wadau wa maendeleo, viongozi wa kidini, asasi za kiraia, marais wastaafu, vyombo vya habari na wananchi wote washiriki katika kuleta mapatano ili kuleta suluhu katika mgogoro wa Zanzibar utokanao na uchaguzi wa Oktoba 2015;

(vii) Makamishina wa ZEC kuwajibika kutokana na mazingira yaliyopelekea kubatilishwa kwa uchaguzi;

(viii) Mamlaka za uteuzi kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya watumishi wa ZEC waliosababisha kufutwa kwa matokeo ya uchaguzi ya Oktoba 2015.

# CHAPTER 11

# UHURU, HAKI NA KUAMINIKA KWA UCHAGUZI WA MWAKA 2015

## 11.1 Utangulizi

Ushiriki katika chaguzi ni sehemu ya haki za kisiasa na kiraia zinazotolewa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya Watanzania wote. Ni kwa msingi huu na kwa kuzingatia vipengele vingine vya sheria kwamba tarehe 25 Oktoba 2015 Watanzania walipiga kura kuwachagua wagombea wa nafasi za urais, ubunge, na udiwani. TEMCO, waangalizi wa uchaguzi wa kitaifa, ambao walitazama na kutathmini uchaguzi wa kwanza (1995), wa pili (2000), wa tatu (2005) na wa nne (2010) walipata tena ridhaa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kutazama uchaguzi wa mwaka 2015.

Sura hii inahitimisha ripoti ya utazamaji wa uchaguzi wa mwaka 2015, na kuweka msingi wa tathmini ya uchaguzi. Inaelezea kwa muhtasari masuala makuu yaliyojitokeza katika kila kipengele cha mzunguko wa uchaguzi, yaani utengaji wa mipaka ya maeneo ya uchaguzi; uandikishaji wa wapigakura; uteuzi wa wagombea; kampeni; na upigaji kura, kuhesabu kura, kutangaza matokeo na matukio yaliyojiri baada ya uchaguzi. Sura hii pia inaelezea kwa muhtasari mbinu iliyotumika kukusanya habari na taarifa.

## 11.2 Muhtasari wa Masuala Makuu

Ripoti hii ya utazamaji wa uchaguzi imeibua masuala mengi yaliyojitokeza wakati waangalizi wa TEMCO walipokuwa wakifuatilia uchaguzi. Katika sehemu hii masuala haya yameelezewa kwa muhtasari.

### *11.2.1 Njia na Mbinu za Utazamaji wa Uchaguzi*

Utazamaji wa uchaguzi wa mwaka 2015 ulifanyika kwa hatua mbili. Hatua ya kwanza ilihusisha mchakato wa uandikishaji wa wapigakura ambao kwa mara ya kwanza ulitumia teknolojia ya BVR. Hatua ya pili ilihusisha vipengele vingine katika mzunguko wa uchaguzi. Katika hatua ya kwanza waangalizi wa muda mrefu 163 walihudhuria na kufuzu mafunzo ya utazamaji wa uchaguzi na walipangiwa maeneo ya kutazama kwa siku 21 katika halmashauri 140 katika serikali za mitaa, kata 1,216, na vituo 9,728 vya kuandikisha wapigakura Tanzania Bara; na wilaya 11, shehia 88 na vituo 704 vya kuandikisha wapigakura huko Zanzibar. Seti mbili za madodoso ziliandaliwa na zilitumika kukusanya taarifa mahsusi za uchaguzi.

Katika hatua ya pili jumla ya waangalizi wa muda mrefu 150 waliteuliwa na kupewa mafunzo na kupangiwa kazi kwa muda wa siku 44 kutazama kampeni na kukusanya taarifa za yaliyojiri kabla ya kampeni. Masuala haya ni kama vile utengaji wa majimbo na maeneo ya uchaguzi (majimbo na kata), uteuzi ndani ya vyama vya siasa, na uteuzi wa wagombea uliofanywa na Tume. Waangalizi walitumia seti mbili za madodoso: (i) dodoso la CEMOT lililokuwa na maswali funge yaliyododosa kuhusu yaliyojiri kabla ya uchaguzi. Taarifa hizi ziliwasilishwa kwa mtandao kwa kutumia fomu za Magpi na kufanyiwa uchambuzi; na (ii) dodoso la TEMCO lililokuwa na maswali funge na ya wazi kwa ajili ya kukusanya taarifa na takwimu zilizohusu masuala yaliyojiri kabla ya kuanza kwa kampeni, na wakati wa kampeni na zilitumika katika kuandaa ripoti ya uchaguzi. Siku ya uchaguzi waangalizi waliangalia zoezi la upigaji kura, kuhesabu kura, kutangaza matokeo na yaliyojiri baada ya uchaguzi. Aidha, siku ya uchaguzi

waangalizi wa muda mfupi 7,350 walipangiwa kuangalia vituo 7,350 vya kupigia kura katika majimbo 150 Tanzania Bara (6,646) na Zanzibar (704). Waangalizi wa muda mfupi walikuwa na seti mbili za madodoso: (i) dodoso la CEMOT la kukusanya taarifa na takwimu siku ya uchaguzi. Dodoso hili lilikuwa na maswali funge 69. Majibu yaliwasilishwa kwenye kituo cha habari cha CEMOT (Election Observation Centre-EOC) kwa kutumia njia ya ujumbe mfupi wa simu "sms"; (ii) dodoso la TEMCO lilikuwa na maswali funge kwa ajili ya siku ya uchaguzi. Waangalizi wa TEMCO pia waliongea na wasimamizi wa uchaguzi katika ngazi mbalimbali pamoja na viongozi wa vyama vya siasa ili kupata taarifa na data za uhakika juu ya mchakato wa uchaguzi. Katiba ya Jamhuri ya Muungano na Katiba ya Zanzibar zilichambuliwa ili kuupa nguvu uchambuzi.

Kwa minajili ya tathmini ya uchaguzi wa Tanzania wa mwaka 2015, taarifa na takwimu zilichambuliwa ili kubaini kama hatua zote za mchakato wa uchaguzi zilizingatia matakwa na viwango vya kimataifa vya uchaguzi ulio huru, wa haki na kuheshimika. Waangalizi wa TEMCO walitoa alama (0-100) kwa kila moja ya hatua muhimu kama vile utengaji wa mipaka ya majimbo na kata, uandikishaji wa wapigakura, uteuzi wa wagombea, kampeni, na upigaji kura kwa kutumia mizania ya madaraja sita kama ifuatavyo:

(i) asilimia 80-100% au daraja 'A', kumaanisha uchaguzi wenye upungufu kidogo ambao usingeweza kuathiri matokeo ya ujumla ya uchaguzi. Uchaguzi wa namna hii hupewa "Cheti cha Uchaguzi Safi, Huru na wa Haki";
(ii) asilimia 60-79 au daraja 'B', kumaanisha uchaguzi (au hatua ya uchaguzi) ambao kwa ujumla ni huru na haki lakini bado ulikuwa na upungufu ambao uliathiri mafanikio ya baadhi ya wadau wa uchaguzi (wapigakura, wagombea na vyama vya siasa). Uchaguzi wa namna hii hupewa "Cheti cha Uchaguzi Huru na wa Haki, Wenye Walakini";
(iii) asilimia 50-59 au daraja 'C', kumaanisha kwamba uchaguzi ulitoa fursa kwa wadau kushiriki bila vikwazo lakini kuna matukio mengi ambapo vyama vikubwa, na hasa chama tawala, vilivunja sheria bila kuchukuliwa hatua. Hii ni kumaanisha kuwa uchaguzi unapewa cheti cha "Uchaguzi Huru Usio wa Haki";
(iv) asilimia 40-49 au daraja 'D', kumaanisha mchakato wa uchaguzi ambao ulikuwa na matukio mengi ya vitisho, vurugu, upendeleo na rushwa. Uchaguzi wa aina hii hupewa "Cheti cha Uchaguzi Usio Huru na Usio wa Haki";
(v) asilimia 1-39 au daraja 'E', kumaanisha uchaguzi (au hatua ya uchaguzi) wenye matatizo lukuki ya menejimenti na ukiukwaji kiasi kwamba wadau wa uchaguzi (wapigakura, wagombea, na vyama vya siasa) wanakataa au wanaelekea kukataa matokeo ya uchaguzi. Uchaguzi wa aina hii hupewa "Cheti cha Uchaguzi Uliovurugwa"; na
(vi) asilimia 0 au daraja 'F', kumaanisha uchaguzi (au hatua ya uchaguzi) ambao umeshindwa kabisa katika vigezo vya usimamizi, uzingativu wa sheria, kanuni na taratibu kiasi kwamba haufikii mwisho uliotarajiwa. TEMCO huupa uchaguzi wa namna hii "Cheti ya Uchaguzi Ulioharibika".

### *11.2.2 Muktadha wa Kisiasa na Mazingira ya Uchaguzi*

Siasa za Tanzania kuelekea uchaguzi wa mwaka 2015 zilitawaliwa na matukio kadhaa yaliyoathiri siasa. Kwanza, ufa dhahiri miongoni mwa wapigakura na wadau wakuu wa

uchaguzi juu ya Katiba Inayopendekezwa ulijitokeza. Chama cha Mapinduzi na wafuasi wake waliiunga mkono Katiba Inayopendekezwa wakati vyama vya upinzani kwa mwavuli wa Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA) waliipinga Katiba inayopendekezwa. Muundo wa Muungano ndio ulikuwa kiini cha mvutano. Wakati CCM walitaka muundo uliopo wa serikali mbili uendelee, UKAWA walipigia chapuo muundo wa serikali tatu.

Pili kuundwa kwa UKAWA kutokana na vyama vinne vya siasa, yaani CHADEMA, CUF, NCCR-Mageuzi na NLD ambapo walitakiwa kusimamisha mgombea mmoja katika ngazi zote. Tatu, inayohusiana na hiyo ilikuwa ni kushindikana kwa "makubaliano ya hiari" kati ya Rais Jakaya Kikwete na TCD yaliyolenga kuboresha haki na uwazi katika uchaguzi wa 2015, ikiwemo: (i) kuundwa kwa tume huru ya uchaguzi; (ii) kushiriki kwa wagombea binafsi katika uchaguzi; (iii) asilimia 50+1kama kiwango cha chini cha ushindi katika nafasi ya urais badala ya mfumo wa wengi wape; (iv) uwezekano wa kupinga matokeo ya urais mahakamani; na (v) kusitisha mchakato wa mabadiliko ya katiba mpaka baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2015.

Sababu ya nne inahusiana na utaasisishaji wa vyama vya siasa. Chama cha Mapinduzi kiliendeleza ubabe wa kutawala ulingo wa siasa Tanzania tangu nchi kupata uhuru mwaka 1961 kikiendelea kushinda chaguzi zote za urais na kuwa na wingi wa viti bungeni, katika Baraza la Wawakilishi na katika mabaraza ya kutunga sheria kwenye uchaguzi wa serikali za mitaaa katika halmashauri. Wakati huohuo kasi ndogo ya ukuaji wa demokrasia ndani ya vyama vya siasa ilichangia kuongezeka kwa ukosefu wa uvumilivu kwa fikra kinzani na kusababisha baadhi ya wanachama kufukuzwa na kisha wao kuunda vyama vingine vya siasa. Vyama viwili vya siasa, ACT-Wazalendo na ADC, ni matokeo ya mafarakano na migogoro ndani ya CHADEMA na CUF. Ndani ya CCM kulikuwa na ushindani mkali baina ya wanachama waliotaka kupata tiketi ya chama kusimama katika ngazi mbalimbali za uchaguzi. Mathalani, wanachama 42, wakiwemo mawaziri 14, walichukua fomu za kuomba uteuzi wa nafasi ya urais, kitu ambacho hakikuzoeleka. Pia yalijitokeza matukio yasiyotarajiwa kufuatia mchakato wa uteuzi ndani ya CCM na vyama vya siasa vinavyounda UKAWA, hasa CHADEMA na CUF. Mawaziri wakuu wastaafu wawili Edward Ngoyai Lowasa na Frederick Tluway Sumaye pamoja na Kingunge Ngombale Mwiru, naibu waziri mmoja na wenyeviti watatu wa CCM mkoa walijitoa na kujiunga na CHADEMA. Edward Lowassa aliteuliwa kuwa mgombea urais kwa tiketi ya vyama vinavyounda UKAWA. Baadhi ya viongozi wakuu wa CHADEMA na CUF walijitoa ndani ya vyama vyao wakipinga mchakato wa uteuzi wa mgombea urais ndani ya umoja. Katibu Mkuu wa CHADEMA, Dkt. Wilbroad Slaa, aliyesimamishwa na CHADEMA kugombea urais mwaka 2010 alitarajiwa kusimama tena kwa tiketi ya chama mwaka 2015, alijiuzulu kwa aibu, akatangaza kujitoa katika siasa moja kwa moja. Pia Mwenyekiti wa CUF, Prof. Ibrahim Haruna Lipumba, aliamua kujivua nafasi yake lakini akabakia kuwa mwanachama. Ujumla wa ushindi wa kishindo wa CCM katika siasa za Tanzania uliogusiwa awali unaendelea kusababisha kukosekana kwa uwiano wa nguvu katika ulingo wa siasa. Katika uchaguzi wa mwaka 2010 CCM ilikuwa na viti 186 vya ubunge na 28 katika Baraza la Wawakilishi Zanzibar; CUF ilikuwa na viti 24 vya ubunge na 22 vya Baraza la Wawakilishi Zanzibar; CHADEMA ilikuwa na viti 23; NCCR-Mageuzi ilikuwa na viti 4; UDP kiti 1 na TLP kiti 1. Wingi wa viti katika Bunge na Baraza la Wawakilishi ulikuwa pia

na athari katika kupata rasilimali za serikali kwa vyama vya siasa hupata ruzuku kwa kadri ya wingi wa viti bungeni.

### *11.2.3 Mfumo wa Kisheria na Kitaasisi*

Mfumo wa kisheria na kitaasisi unaotawala uchaguzi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania unatokana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977. Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 1985 pamoja na marekebisho yake inatoa dira inayoongoza uchaguzi wa rais na wabunge. Chaguzi za serikali za mitaa hufanyika chini ya sheria ya uchaguzi wa serikali za mitaa (the Local Authorities Elections Act (CAP 292) ya 1979) na sheria zinazohusiana. Vilevile chaguzi za serikali ya Muungano hutawaliwa na Sheria ya Gharama za Uchaguzi Na. 6 ya mwaka 2010, yenye vifungu vinavyohusiana na ugharamiaji wa uchaguzi ikiwa na lengo la kudhibiti matumizi ya fedha na kuzuia vitendo vya uhalifu. Sheria ina vipengele vinavyohusiana na matumizi, usimamizi na uwajibikaji katika fedha za uchaguzi. Chaguzi Zanzibar huongozwa na Katiba ya Zanzibar (1984) na Sheria Na. 11 ya mwaka 1984 pamoja na marekebisho yake.

NEC imepewa majukumu ya kikatiba ya kusimamia uchaguzi wa Muungano. Makamishina wa Tume huteuliwa na Rais wa Jamhuri na hutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria. Baadhi ya wadau wa uchaguzi hawaridhishwi na sheria ya uchaguzi ya Tanzania. Kuna hisia na hoja kuwa sheria ina upungufu, ikiwemo: (i) NEC haina uhuru wa kutosha wa kutekeleza majukumu yake bila upendeleo. Hoja hii inatokana na ukweli kuwa mwenyekiti, makamu wake na mkurugenzi wa uchaguzi wote huteuliwa na rais ambaye ni mwenyekiti wa chama cha siasa na wakati fulani huwa ni mgombea katika uchaguzi; (ii) NEC haijiri wafanyakazi wake badala yake inategemea wafanyakazi wa serikali za mitaa ambao hufanya kazi kwa ridhaa ya rais. Utiifu wa wafanyakazi hawa ni kwa mwajiri wao na sio kwa Tume; (iii) sheria hairuhusu mgombea binafsi, inawataka wagombea kuteuliwa na vyama vyao na hivyo kukandamiza haki za kisiasa na za kiraia; (iv) sheria inawabagua *Diaspora* kujiandikisha kama wapigakura na hata kusimama kama wagombea; (v) wafungwa wanaotumikia adhabu ya chini ya miezi sita na watu waliolazwa hospitali kwa matibabu hunyimwa fursa ya kupiga kura. Pamoja na kuwa sheria haiwabagui wala kuwakosesha sifa za kujiandikisha na kupiga kura, haiweki kipengele maalum kwa ajili ya utekelezaji wa haki hizo; na (vi) muundo na nyenzo za utekelezaji wa Sheria ya Gharama za Uchaguzi ya mwaka 2010 havitoshelezi.

Kwa ujumla, sheria inayotawala uchaguzi Tanzania sio kandamizi wala ya kibaguzi. Sheria ya uchaguzi na mpangilio wa kitaasisi kwa kiasi kikubwa unatoa uhuru wa kushiriki katika uchaguzi. Mfumo wa kisheria na mpango wa kitaasisi haupingani na viwango vya kimataifa vya uchaguzi. Hata hivyo, baadhi ya vifungu vya sheria vinahitaji kupitiwa upya ili kuongeza imani ya wadau wakuu wa uchaguzi katika mfumo wa sheria na taasisi ili kufikia chaguzi za kuheshimika, zilizo huru na za haki.

### *11.2.4 Usimamizi wa Michakato ya Uchaguzi*

Usimamizi wa michakato ya uchaguzi Tanzania ni jukumu la NEC na ZEC. Kuelekea uchaguzi wa mwaka 2015, NEC ilikamilisha baadhi ya shughuli muhimu zilizotoa mweleko wa uchaguzi. Baadhi ya shughuli hizo zilikuwa ni: (i) ununuzi na usambazaji wa vifaa vya

uchaguzi, ikiwemo mashine za BVR; (ii) uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura kwa kutumia teknolojia ya BVR; (iii) kutoa mafunzo kwa maafisa wa uchaguzi katika ngazi ya taifa, mkoa, wilaya na kata; na (iv) kuandaa na kusambaza kanuni za maadili kwa vyama vya siasa na wagombea pamoja na zile za waangalizi wa uchaguzi. Kwa ujumla, NEC ilifanya kazi zake kikamilifu, kwa weledi na ustadi licha ya kukumbwa na changamoto ya upungufu wa rasilimali na shinikizo kubwa kutoka kwa wadau mbalimbali wa uchaguzi.

### 11.3 Tathmini ya Michakato ya Mzunguko wa Uchaguzi

Vipengele muhimu katika mzunguko wa uchaguzi vilivyokamilishwa kabla ya uchaguzi wa mwaka 2015 vilikuwa ni utengaji wa mipaka ya maeneo ya uchaguzi, kuandikisha wapigakura, kampeni, kupiga kura, kuhesabu kura na matukio ya baada ya uchaguzi.

#### *11.3.1 Utengaji wa Mipaka ya Maeneo ya Uchaguzi*

Majimbo mapya 25 ya uchaguzi yalianzishwa na kufanya idadi ya majimbo yote kufikia 264 ikilinganishwa na 239 yaliyokuwepo. Kata ziliongezeka kutoka 3,339 mwaka 2010 mpaka 3,957 mwaka 2015. Upangaji wa majimbo mapya ulifanyika kwa uwazi, bila upendeleo na kwa mujibu wa sheria kwa kuzingatia idadi ya watu na mipaka ya kijiografia na kiutawala. Hakukuwa na malalamiko miongoni mwa wadau wa uchaguzi dhidi ya namna ambavyo mipaka ya majimbo ilivyotengwa. Ripoti za waangalizi wa TEMCO hazioneshi matukio wala ushahidi wa hila au “uchakachuaji” (“gerrymnaering”) ambao ungeweza kugeuza matokeo ya uchaguzi.

#### *11.3.2 Mchakato wa Uandikishaji wa Wapigakura*

TEMCO iliona kuwa NEC iliandikisha jumla ya wapigakura 23,161,440 (asilimia 96.9) ikilinganishwa na watu 23,913,184 waliokadiriwa. Haya yalikuwa ni mafanikio makubwa ikizingatiwa kuwa NEC ilikuwa kwa kiasi fulani na upungufu wa rasilimali na ilikuwa chini ya shinikizo kubwa kutoka kwa wadau mbalimbali wa uchaguzi. Ingawa hakuna sheria Tanzania inayowalazimishwa wenye umri wa miaka 18 kujiandikisha, mwitikio wa watu ulikuwa mzuri, kuonesha kuwa watu wana mwamko wa haki zao za kisiasa na kiraia. Ripoti za waangalizi wa TEMCO zinaonesha kuwa mchakato wa uandikishaji wapigakura kwa kutumia teknolojia ya BVR ulichukua muda mrefu kumalizika na zoezi la utambuzi wa wapigakura wenye sifa lilikuwa na mianya mingi. Tuhuma za uandikishwaji wa wageni zinaashiria upungufu huu. Kama ilivyokwishagusiwa, *Diaspora* na watu wanaotumikia vifungo vya chini ya miezi sita hawakuruhusiwa kujiandikisha.

#### *11.3.3 Uteuzi ndani ya Vyama*

Matokeo ya utazamaji wa TEMCO yanaonesha kuwa uteuzi wa wagombea ndani ya vyama vya siasa haukufikia viwango vya kidemokrasia. Njia kuu nne za uteuzi zilitumika: (i) uamuzi wa viongozi wa juu wa chama (handpicking), (ii) kutuma maombi, (iii) kusubiri wanaohama vyama, (iii) njia mtambuka au demokrasia nusu (iv) njia ya demokrasia na ushirikishwaji. Njia ya uamuzi wa viongozi wa juu wa chama ilitumika kwa viongozi kuchagua wagombea waliowataka wao. Njia hii ilitumiwa na vyama vidogo vya siasa hasa vile visivyokuwa na viti bungeni au kwenye halmashauri na vyenye ofisi Dar es Salaam na katika mikoa michache. Njia ya kutuma maombi ilikuwa ni mbinu mpya ambapo baadhi vya vyama hasa vidogo vilitangaza

nafasi za maombi katika ngazi ya jimbo na kata. Njia ya kusubiri wanaohama vyama vyao ilitumiwa na baadhi ya vyama vya siasa kutengeneza nafasi kwa viongozi waliokosa uteuzi ndani ya vyama vyao. Mbinu hii ilitumiwa na vyama vya siasa vinavyounda UKAWA. Kwa namna fulani njia hii ilidhoofisha nguzo za michakato ya kidemokrasia ya uteuzi. Njia mtambuka ilikuwa na chembechembe za ushirikishwaji ingawa viongozi wa vyama vya siasa walikuwa na uamuzi wa mwisho. Njia ya kidemokrasia ilitumika kwa kiasi kikubwa na CCM na CUF hasa kwa upande wa Zanzibar ambapo wagombea walitakiwa kuchukua fomu za kugombea nafasi mbalimbali, ikiwemo urais. Uteuzi ulifanyika kwa kuzingatia sifa na kura kwa vigezo vilivyowekwa na chama. Baadhi ya vyama vya siasa vilitumia njia za kiimla kwa kiasi fulani kwa kuwa Tanzania haina sheria inayoviwezesha vyama kuunda umoja au ushirikiano wakati wa uchaguzi. Kwa ujumla ripoti za waangalizi wa TEMCO zinabainisha kuwa baada ya miaka 23 ya kuwepo kwake, vyama vya siasa Tanzania havijajigeuza kuwa taasisi za kidemokrasia na havijafanikiwa kufanya kazi ya msingi ya kulea, kukuza na kuibua viongozi. Pia kasi ya kujenga na kuimarisha demokrasia ndani ya vyama ni ndogo.

### *11.3.4 Uteuzi wa NEC*

NEC imepewa mamlaka ya kuteua wagombea waliopendekezwa na vyama vya siasa kusimama katika nafasi mbalimbali za uwakilishi katika uchaguzi. NEC pia ina uwezo wa kusikiliza na kushughulikia pingamizi zinazowekwa na wagombea, wasimamizi wa uchaguzi, wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi na Msajili wa Vyama vya Siasa. Yeyote asiyeridhishwa na uamuzi katika ngazi moja anaruhusiwa kukata rufaa katika ngazi inayofuatia na hatimaye NEC. Mwaka 2015 wagombea 10 wa nafasi ya urais walichukua fomu za kugombea kutoka NEC. Hata hivyo ni wagombea nane (mwanamke mmoja [asilimia 12.5] na wanaume saba) ndio waliotimiza vigezo na matakwa ya sheria kusimama kama wagombea kwa nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Upande wa uchaguzi wa wabunge, wagombea 1,218 (wanaume 985 na wanawake 233 [asilimia 19.1]) waliteuliwa na NEC. Uchaguzi wa madiwani ulikuwa na wagombea 10,879 (wanaume 10,191 na wanawake 679 [asilimia 6.3]). NEC ilipokea na kutoa uamuzi juu ya rufaa zote zilizopokelewa kama inavyotakiwa na sheria ama kwa kukubaliana na uamuzi wa ngazi za chini au kuubatilisha. Uamuzi wa NEC wa kuwarudisha kwenye kinyang'anyiro wagombea wote wa ubunge waliokuwa wameenguliwa na wasimamizi wa uchaguzi ulisifiwa sana na wadau wa uchaguzi, wakiwemo waangalizi wa uchaguzi. Rufaa zilizosikilizwa na Tume ni pamoja na zile zilizohusu majimbo nane ya uchaguzi, yaani, Tandahimba, Mwanga, Wanging'ombe, Handeni Mjini na Kasulu Mjini. NEC pia ilitolea uamuzi rufaa 70 kuhusiana na uchaguzi wa madiwani. Kinyume na ilivyokuwa katika uchaguzi wa mwaka 2010 ambapo wagombea ubunge 16 wa CCM na 500 wa udiwani walipita bila kupingwa, majimbo ambayo wagombea wake walipita bila kupingwa yalipungua sana katika uchaguzi wa mwaka 2015.

Kwa ujumla, NEC ilishughulikia mchakato wa uteuzi kwa mujibu wa sheria na kwa namna ambayo iliviridhisha vyama vya siasa. Ni vizuri kuzingatia kuwa wanawake walioteuliwa na NEC walikuwa wachache sana na hii inaleta maswali mengi juu ya tija ya mipango mingi ya uwezeshaji iliyolenga kuwajengea wanawake umahiri na ujasiri wa kushiriki katika michakato ya kisiasa.

### *11.3.5 Kampeni*

Ripoti za Waangalizi wa TEMCO zinaonesha mambo chanya na hasi yaliyofanywa na vyama vya siasa katika kuendesha kampeni za uchaguzi. Kwa upande wa mambo chanya, ripoti zinaonesha yafuatayo: (i) ratiba ya kampeni za uchaguzi wa rais iliandaliwa na vyama vyote viliizingatia kwa kiasi kikubwa. Hata hivyo wakati mwingine ratiba hiyo ilifanyiwa marekebisho; (ii) vyama vitatu tu vya siasa CCM, CHADEMA/UKAWA na ACT-Wazalendo viliweza kuzindua kampeni za uchaguzi kwa ngazi ya taifa ikiwemo ilani za uchaguzi; (iii) vyama viwili tu vya siasa CCM na CHADEMA/UKAWA vilivutia umati katika mikutano yao ya kampeni ambayo ilitawaliwa kwa kiasi kikubwa na amani na utulivu; na (iv) polisi waliovaa sare walionekana katika mikutano ya kampeni za uchaguzi wa wagombea urais.

Kwa upande wa mambo hasi, ripoti za waangalizi wa TEMCO zinabainisha yafuatayo: (i) ingawa kwa ujumla kampeni ziliendeshwa kwa amani, kulikuwa na madai kuwa migongano kati ya wafuasi wa vyama vikuu viwili vya siasa ilisababisha kifo cha raia huko jimboni Tarime; (ii) licha ya matukio machache ya mikutano ya kampeni kuendeshwa zaidi ya muda uliopangwa, yaani saa 12 jioni, polisi kwa ujumla walikuwa wavumilivu na hivyo kuepusha migongano; (iii) ratiba ya mikutano ya kampeni za ubunge na udiwani zilizokubaliwa kwa pamoja na vyama vyote vya siasa, haikufuatwa kikamilifu; (iv) kampeni zilijielekeza zaidi k kwa wagombea kujikweza binafsi na jazba badala ya kujielekeza katika taasisi (vyama vya siasa) na ilani za uchaguzi; (v) ushahidi wa kimazingira unaonesha kuwa vyama viwili CCM na CHADEMA/UKAWA vilitumia pesa zaidi ya viwango vilivyowekwa na Sheria ya Gharama za Uchaguzi katika kuendesha kampeni zao za urais. Hata hivyo ni vigumu kuthibitisha kwa uhakika; (vi) vyama vingi vya siasa vilikuwa dhahiri hohehahe ukiacha tu CCM na CHADEMA/UKAWA, hivyo, uwanja haukuwa sawa, na hii inaweza kuathiri usawa katika uchaguzi; (vii) matukio machache ya kampeni hasi, ikiwemo matumizi ya lugha chafu, za kudhalilisha na za kuudhi katika mikutano ya kampeni; na (viii) matumizi makubwa ya lugha za asili katika baadhi ya maeneo na katika kampeni za ubunge na udiwani yalijitokeza, kinyume na sheria na kanuni za maadili ya vyama vya siasa.

### *11.3.6 Kupiga Kura, Kuhesabu Kura na Kutangaza Matokeo*

TEMCO ilituma jumla ya waangalizi 7,350 kuangalia shughuli za siku ya uchaguzi ikiwemo kupiga kura, kuhesabu kura na kutangaza matokeo. Pia TEMCO ilifaidika na data iliyotokana na Kituo cha Utazamaji wa Uchaguzi [Observation Centre (EOC)] kilichoratibiwa na CEMOT. Ripoti za waangalizi wa TEMCO kuhusu siku ya uchaguzi zinaonesha yafuatayo: (i) jumla ya vituo 6,080 vya kupigia kura (asilimia 94) vilifunguliwa saa 1.00 asubuhi au kabla, ambao ulikuwa muda rasmi wa kufungua na vituo 249 (asilimia 4) vilifunguliwa kuanzia saa 1.31 asubuhi mpaka saa 2.00 asubuhi. Ni vituo 115 tu vya kupigia kura (asilima 2) ndivyo vilivyofunguliwa kuanzia saa 2.01 na kuendelea; (ii) kati ya vituo vilivyokuwa na waangalizi wa TEMCO, vituo 6,615 (asilimia 90) vilikuwa na vifaa vya kupigia kura vya kutosha, na vituo 735 (asilimia 10) vilikuwa na upungufu, hasa mihuri; (iii) majina ya wapiga kura 1,323 (asilimia 18) kati ya vituo 7,350 vya kupigia kura yalikuwa yanakosekana kwenye orodha ya wapigakura; (iv) kati ya vituo 7,350 vya kupigia kura, CCM ilikuwa na mawakala 7,203 (asilimia 98), CHADEMA/UKAWA ilikuwa na mawakala 7,129 (asilimia 97), na vyama vingine vya siasa vilikuwa na mawakala 5,145 (asilimia 70); (v) vituo 6,883 vya kupigia kura

(asilimia 95) kati ya vituo 7,350 vilikuwa na polisi waliovaa sare; (vi) vituo 6,762 vya kupigia kura (asilimia 92) kati ya 7,350 vilifikika kwa urahisi na watu wenye ulemavu; (vii) kati ya vituo 7,350 vya kupigia kura katika vituo 7,276 (asilimia 99) maafisa uchaguzi walihakiki vitambulisho vya waiga kura; (viii) dalili za kampeni zilijidhihirisha katika vituo 294 vya kupigia kura (asilimia 4); (ix) katika vituo 6,542 vya kupigia kura (asilimia 89) maafisa uchaguzi walihakiki alama za wino katika vidole; (x) katika vituo 3,161 vya kupigia kura (asilimia 43) wapigakura walikuwa bado kwenye foleni kufikia saa 10 jioni, muda rasmi wa kufunga; na (xi) mtu wa mwisho katika foleni alipiga kura kati ya saa 11.00 na 11.30 jioni katika vituo 824 vya kupigia kura (asilimia 11.2).

Shughuli ya kuhesabu kura ilianza mara tu baada ya mtu wa mwisho kupiga kura. Ripoti za waangalizi wa TEMCO zinaonesha kuwa: (i) kati ya vituo 7,350 vya kupigia kura, vituo 3,014 (asilimia 41) vilivyokuwa na waangalizi wa TEMCO vilibadilishwa kuwa vituo vya kuhesabia kura kati ya saa 10.30 na saa 11.00 jioni; (ii) katika vituo 1,764 (asilimia 24) kura zilianza kuhesabiwa kuanzia saa 11.00 jioni; (iii) Waangalizi wa TEMCO walishuhudia matokeo yakibandikwa nje ya vituo vya kupigia kura kama ifuatavyo: uchaguzi wa urais vituo 7,056 (asilimia 96); uchaguzi wa ubunge vituo 6,762 (asilimia 92); na udiwani vituo 7,056 (asilimia 96). Waangalizi wa TEMCO walishuhudia mvutano baada ya matokeo ya ubunge kucheleweshwa katika majimbo ya Mbagala, Kinondoni, Ubungo, Kibamba, Kawe, Mbozi, Temeke, Simanjiro na Babati na wakati mwingine vurugu zilitokea.

### 11.4 Tathmini ya Michakato yote ya Uchaguzi

Waangalizi wa TEMCO walifanya tathmini huru ya michakato muhimu minne ya mzunguko wa uchaguzi ili kuangalia uadilifu na kuaminika kwa uchaguzi. Michakato hiyo ni uandikishaji wa wapigakura, uteuzi, kampeni, na shughuli za siku ya kupiga kura. Tathmini ya michakato mitatu ilihusisha waangalizi wa muda mrefu pekee wakati shughuli za siku ya kupiga kura zilihusisha waangalizi wa muda mfupi na waangalizi wa muda mrefu. Tathmini ya kila moja ya mchakato huu ilifanywa kwa kuangalia mzani wa alama 0-100 kama ilivyoanishwa katika sura ya nane ya ripoti hii. Baada ya hapo, daraja stahiki lilitolewa ikianzia “A” mpaka “F”. Matokeo ya tathmini yanaoneshwa katika Jedwali 11-1.

***Jedwali 11-1: Tathmini ya Michakato yote ya Uchaguzi***

| Mchakato wa uchaguzi | Alama na daraja | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | A (80-100) | | B (60-79) | | C (50-59) | | D (40-49) | | E (1-39) | | F (0) | |
| | Idadi | % | Idadi | % | Idadi | % | Idadi | % | Idadi | % | Idadi | % |
| Uandikishaji wapigakura[28] | 24 | 14.9 | 112 | 69.6 | 24 | 14.9 | 1 | 0.6 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Uteuzi wa wagombea | 61 | 40.4 | 68 | 45.6 | 16 | 10.5 | 5 | 3.5 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kampeni | 42 | 28.0 | 88 | 58.7 | 16 | 10.7 | 4 | 2.6 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Siku ya uchaguzi[29] | 5,630 | 76.8 | 1,595 | 21.5 | 117 | 1.6 | 7 | 0.1 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Wastani | 1,439 | 40.0 | 466 | 48.9 | 43.3 | 9.43 | 4.25 | 1.7 | 0 | 0 | 0.25 | 0 |

Chanzo: Ripoti zaWaangalizi wa TEMCO, 2015

[28] Tathmini ilifanywa na Waangalizi 161 waliopelekwa majimboni kufuatilia uandikishaji kwa kutumia teknolojia ya BVR.

[29] Tathmini ilifanywa na waangalizi 7,350 wakiwemo 6,600 wa TEMCO na 750 wa CEMOT.

Takwimu katika Jedwali 11-1 zinaonesha kuwa takriban asilimia 90 ya majibu yote yalitoa alama 60-100, sawa na daraja A (asilimia 40.0) au daraja B (asilimia 48.9), kuonesha kuwa, kwa ujumla, hatua nne za michakato ya uchaguzi zilikuwa na vigezo vya uchaguzi ulio huru, wa haki na wenye uadilifu, kukiwa na matukio machache ya ukiukwaji ambayo yasingeweza kuathiri kwa namna yoyote uadilifu wa michakato ya uchaguzi. Takriban asilimia 10 ya majibu yote yalitoa alama 40-59, au daraja C (asilimia 9.43) au D (asilimia 1.7), kuonesha kuwa michakato ya uchaguzi ilikuwa na matukio machache sana ya ukiukwaji. Tathmini hii ilichangia katika uamuzi wa kutoa cheti stahiki cha uchaguzi wa Tanzania wa mwaka 2015.

**11.5 Uchaguzi wa Zanzibar**

TEMCO ilisikia, kushangazwa na kushtushwa na taarifa ya Mwenyekiti wa ZEC, Jecha Salim Jecha, ya kufuta uchaguzi kwa kile alichosema kuwa ni "ukiukwaji wa hali ya juu wa sheria na taratibu za uchaguzi". Matukio mahsusi yaliyonukuliwa na bosi wa ZEC yalikuwa ni pamoja na vitisho kwa wapigakura katika ngome za vyama vya siasa, vyama kupoka mamlaka ya ZEC ya kutangaza matokeo ya urais, tofauti ambazo zilijitokeza na kusababisha wajumbe wa ZEC kupigana, na idadi ya wapigakura katika baadhi ya vituo vya kupigia kura ilizidi idadi ya wapigakura waliojiandikisha, hasa Pemba.

Waangalizi 22 wa muda mrefu na 704 wa muda mfupi walipangiwa kutazama uchaguzi Zanzibar na wale wa muda mrefu walikaa siku 43 kabla ya uchaguzi. Watazamaji hawa waliangalia michakato ya siku ya uchaguzi, yaani upigaji kura, kuhesabu kura, kutangaza matokeo na matukio ya baada ya uchaguzi. Ripoti zao zilionesha kuwa michakato ya kabla na baada ya uchaguzi ilifanyika kwa weledi, katika mpangilio mzuri na kwa amani na uliwaridhisha wadau wengi. Hivyo basi, uamuzi wa kufuta uchaguzi uliotolewa wakati tayari matokeo ya uchaguzi yalikuwa yakiendelea kutangazwa na ZEC ulikuwa unashangaza kabisa..

TEMCO pia ilishitushwa na tamko lisilosainiwa lililotolewa kwa umma na CUF tarehe 26 Oktoba, 2015 lenye somo "CUF yapata ushindi wa kihistoria katika uchaguzi wa Zanzibar" ("The Civic United Front Wins Historic Victory in Zanzibar Election"). Tamko hili lilitafsiriwa kama kujitangazia matokeo na hivyo kuvunja sheria na lilitajwa na ZEC kama mojawapo ya sababu za kufuta uchaguzi. Katika hali kama hii, uamuzi wa ZEC na tamko la CUF yanaacha maswali mengi. Mambo haya mawili yalisababisha mjadala mkali na wasiwasi kwa wadau wa uchaguzi ikiwemo vyama vya siasa, wagombea urais, na waangalizi wa uchaguzi wa kitaifa na wa kamataifa. Timu ya Utazamaji wa Uchaguzi ya TEMCO inaendelea kufuatilia hali ya siasa ya Zanzibar.

**11.6 Tathmini ya Jumla ya TEMCO na Uamuzi juu ya Uchaguzi wa 2015**

Tathmini hii ya ujumla imejikita katika vigezo viwili vya uchaguzi vinavyoshabihiana: (i) mfumo wa kisheria na kitaasisi unaoongoza chaguzi Tanzania; (ii) ufanisi wa michakato minne katika uchaguzi, yaani uandikishaji wa wapigakura, uteuzi wa wagombea, kampeni na shughuli ya siku ya uchaguzi. Waangalizi wa TEMCO walifanya tathmini huru ya ufanisi wa michakato ya uchaguzi wa mwaka 2015. Tathmini hii inatoa taswira ya jumla kuhusiana na jinsi ambavyo uchaguzi ulikuwa huru, wa haki na wa kuaminika kama inavyoonekana katika Jedwali 11-2.

*Jedwali 11-2: Tathmini ya Jumla ya Uchaguzi wa Mwaka 2015*

| Maelezo | Alama na daraja (%) | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|---|
| Mchakato wa uchaguzi ulikuwa na matukio machache ya ukiukwaji ambayo hayakuathiri kabisa matokeo ya jumla ya uchaguzi. Kwa ujumla, uchaguzi ulikuwa safi, huru na wa haki na uliakisi matakwa ya wananchi. | A (80-100) | 78 | 52.0 |
| Mchakato wa uchaguzi ulikuwa kwa ujumla huru na haki lakini bado kulikuwa na upungufu ambao ungeweza kuathiri mafanikio ya baadhi ya wadau (vyama vya siasa, wagombea na wapigakura). | B (60-79) | 67 | 44.7 |
| Mchakato wa uchaguzi uliruhusu ushiriki wa wadau (vyama vya siasa, wagombea na wapigakura) lakini kulikuwa na matukio ya vyama vikubwa, hasa chama tawala kuvunja sheria bila kuchukuliwa hatua, na kulikuwa na upendeleo ambao uliathiri mafanikio ya baadhi ya vyama vya siasa na wagombea. | C (50-59) | 5 | 3.3 |
| Mchakato wa uchaguzi uligubikwa na upungufu mwingi ukihusisha kutozingatia sheria, kanuni na taratibu na matukio ya vitisho na upendeleo. | D (40 - 49%) | 0 | 0.0 |
| Mchakato wa uchaguzi ulivurugika au uliendeshwa vibaya kiasi kwamba haikuwezekana kufahamu kilichotokea. Ni kama mwanafunzi aliyefeli mtihani. | E (1 - 39%) | 0 | 0.0 |
| Mchakato wa uchaguzi ulifanyika hovyo. Kulikuwa na matukio mengi ya vurugu, rushwa na vitisho kiasi kwamba baadhi ya wagombea waliamua kujitoa au kuchukua hatua nyingine. Uchaguzi wote ni kama mimba iliyoharibika. | F (0%) | 0 | 0.0 |
| Jumla | | 150 | 100.0 |

Chanzo: Ripoti za Waangalizi wa TEMCO, 2015

Tathmini ya jumla ya TEMCO inaonesha kuwa ufanisi wa vipengele vya uchaguzi katika mzunguko mzima katika majimbo 78 (asilimia 52) ulistahili cheti cha “uchaguzi safi, huru na haki”; majimbo 67 (asilimia 44.7) yalistahili cheti cha uchaguzi “huru na haki wenye walakini”; majimbo matano (asilimia 3.3) yalistahili cheti cha uchaguzi “huru lakini sio wa haki”. Kwa ujumla, uchaguzi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 2015 ulistahili cheti cha “uchaguzi safi, huru na wa haki”. Hata hivyo, kwa kuzingatia hisia na hoja za msingi za wadau mbalimbali wa uchaguzi kuhusiana na uhuru wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, upungufu katika mfumo wa kisheria na mpango wa kitaasisi ulioonekana katika mwenendo wa vipengele vinne vya mzunguko wa uchaguzi, TEMCO inaupa uchaguzi wa Tanzania wa mwaka 2015 cheti cha “UCHAGUZI HURU NA WA HAKI WENYE WALAKINI”.

### 11.7 Mapendekezo

Kwa kuzingatia matokeo ya utazamaji wa uchaguzi uliofanywa na TEMCO, mapendekezo yanatolewa kwa wadau mbalimbali wa uchaguzi kwa nia ya kuimarisha ufanisi wa uchaguzi siku zijazo.

### *11.7.1 Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*

Serikali inashauriwa kuangalia uwezekano wa kufanya uboreshaji mkubwa wa sheria kwa lengo la:

(i) Kuongeza imani ya wadau wa uchaguzi kwa Tume za uchaguzi hasa uteuzi wa makamishina na mkurugenzi wa uchaguzi na haja ya Tume kuwa na wafanyakazi wake yenyewe;

(ii) Kurekebisha sheria ili kuruhusu mgombea binafsi, kupinga matokeo ya urais mahakamani na kuruhusu *Diaspora* kushiriki katika chaguzi;

(iii) Kufikiria kubadilisha mfumo wa "wengi-wape" na kuwa na mfumo wa kura za uwiano. Hii itaongeza wigo wa ushiriki wa vyama vya siasa katika uchaguzi wa wabunge na madiwani;

(iv) Kupitisha sheria itakayoanzisha mamlaka huru ya kufuatilia na kuratibu kampeni na matumizi ya fedha kwenye uchaguzi;

(v) Kufikiria kuoanisha database za NEC, NIDA, Wizara ya Mambo ya Ndani, Afya na nyinginezo zenye mrengo unaofanana;

(vi) Kutengeneza na kutekeleza mpango kamambe wa elimu ya uraia utakaoongeza utoaji wa elimu ya mpigakura;

(vii) Kuchukua hatua za kuimarisha taasisi za makuzi ya vijana ili kusimamia tabia zao na kuwafanya wawe na subira, raia wema wenye uwezo wa kuzuia jazba zao;

(viii) Kuchukua hatua za kusimamia mitandao ya kijamii wakati wa uchaguzi ili kuepuka upotoshwaji wa habari;

(ix) Kufanyia marekebisho Sheria ya Vyama vya siasa ili kuwa na kipengele kitakachoruhusu vyama vya siasa kuunda umoja/ushirikiano kwa minajili ya uchaguzi; na

(x) Kuchukua hatua za kuwa na sheria itakayovilazimisha vyama vya siasa kuwa na kiwango cha chini cha wagombea katika nafasi ya urais, ubunge na udiwani.

### *11.7.2 Tume ya Taifa ya Uchaguzi*

Kwa kuzingatia mamlaka ya kikatiba iliyopewa, pamoja na nafasi yake katika kusimamia uchaguzi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na haja ya kuhakikisha uchaguzi wa kuaminika, huru na wa haki, TEMCO inapendekeza NEC kufikiria uwezekano wa:

(i) Kuanza maandalizi ya kura ya maoni kupitisha Katiba Inayopendekezwa kwani daftari la kudumu la wapigakura limekwishakamilika;

(ii) Kufanya maboresho ya mara kwa mara katika daftari la kudumu la wapigakura kama inayoainishwa na sheria;

(iii) Kutengeneza mpango wa muda wa kati wa menejimeneti kusaidia uboreshaji wa ufanisi;

(iv) Kutengeneza mfumo wa TEHAMA utakaowezesha kupigaji kura kwa mtandao pamoja na kuheshabu kura; na

(v) Kukasimu mamlaka ya kutoa vibali kwa waangalizi wa muda mfupi wa uchaguzi kwa wasimamizi wa uchaguzi.

### *11.7.3 Vyama vya Siasa*

Vyama vya siasa ni wadau wakubwa wa uchaguzi. TEMCO inapendekeza kuwa vyama vya siasa vifanye yafuatayo:

(i) Kuendesha mambo yao kwa misingi ya sheria za uchaguzi, kanuni na taratibu;
(ii) Kufuata njia sahihi katika kudai haki, mathalani mahakama;
(iii) Kuchukua hatua za kujenga na kuimarisha demokrasia ndani ya vyama hasa wakati wa uteuzi wa wagombea wa nafasi mbalimbali;
(iv) Kuchukua hatua zitakazovutia ushirikikwanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika uchaguzi; na,
(v) Kujitahidi kuwa asasi za kujifunza zenye uwezo wa kujiendeleza na kuwa na itikadi zitakazorithishwa kutoka kizazi kimoja kwenda kingine na kujiepusha na kirusi cha kukweza nafsi.

### *11.7.4 Vyombo vya Habari*

Vyombo vya habari vilifanya kazi kubwa sana ya kuelimisha wapigakura wakati wa uchaguzi wa mwaka 2015. Licha ya mchango wao wa kufanikisha uchaguzi inapendekezwa kuwa:

(i) Vyombo vya kujisimamia kama MCT na Jukwaa la Wahariri viendelee na kazi nzuri vinayoifanya kulinda na kutetea heshima ya taaluma miongoni mwa wadau wao lakini viende mbele zaidi na kuwa na uwezo wa kuchukua hatua za kinidhamu kwa wanaovunja kwa makusudi kanuni za maadili;
(ii) Hatua za makusudi zichukuliwe na wamiliki wa vyombo vya habari kuwaongezea uwezo waandishi na wahariri kuhusu uandishi wa habari za uchaguzi;
(iii) Mitandao ya kijamii ni jukwaa muhimu la kubadilishana uzoefu wa masuala ya uchaguzi. Hata hivyo kwa sababu ya uchanga na mwenendo wake, ni lazima mitandao hii idhibitiwe na iratibiwe; na
(iv) Vyombo vya habari vya umma vitoe fursa sawa kwa wagombea na vyama vya siasa.

### *11.7.5 Asasi za Kiraia*

Utaoaji wa elimu ya mpigakura na utazamaji wa uchaguzi kwa kiasi kikubwa ulitegemea asasi za kiraia. Ili kuwafanya wadau hawa kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi, yafuatayo yanapendekezwa:

(i) Waendeleze imani yao kwa wananchi kwa kufanya kazi bila upendeleo na kwa usawa;
(ii) Wawe na mbinu za utafutaji wa rasilimali sio tu kutoka kwa wahisani bali pia kutoka vyanzo vya ndani ili kuimarisha uhuru wao na kupunguza dhana ya utegemezi;
(iii) Zijiepushe na mtindo wa "zimamoto" katika kutoa elimu ya mpigakura na zijitahidi kufikia maeneo ya vijijini; na
(iv) Zitengeneze mpango-kazi na mbinu za utoaji wa elimu ya mpigakura ambazo ni shirikishi, zinazoruhusu mjadala badala ya imla.

### *11.7.6 Wapigakura*

Kama ilivyokuwa kwa chaguzi zilizopita, uchaguzi wa mwaka 2015 ulitoa fursa kwa wapigakura kutekeleza haki yao ya msingi ya kisiasa na kiraia. Ingawa idadi ya wapigakura waliojitokeza mwaka 2015 iliongezeka kufikia asilimia 67.34 kutoka asilimia 42.84 ya mwaka 2010, zaidi ya asilimia 33 ya Watanzania, sawa na wapigakura milioni saba, hawakupiga kura.

Licha ya kuwa kupiga kura sio lazima, na kushindwa kupiga kura sio kosa la jinai, raia makini wanatarajiwa kushiriki katika michakato ya uchaguzi kama kielelezo cha utimilifu wa wajibu wao wa kiraia. TEMCO inapendekeza yafuatayo:

(i) Watanzania waendelee kutekeleza wajibu wao wa kupiga kura na kuchaguliwa katika nafasi za uongozi.

## MAREJEO


Bakari, M. (2001). The democratization process in Zanzibar: A retarded transition. PhD Thesis, Hamburg: Institute of African Studies.

Bakari, M. (2001). *The democratisation process in Zanzibar: A retarded transition.* Hamburg: Institute for African Affairs.

Butahe, F., & Yamola, I. (2014). Rushwa yaitesa CCM kuelekea Urais 2015. *Mwananchi,* December 30, 2014.

Butahe, F., & Elias, P. (2014). Chenge, Tibaijuka, Kilaini, Walipuliwa Mabilioni ya IPTL" *Mwananchi*, November 27, http://www.mwananchi.co.tz/habari/Kitaifa/-/1597296/2536642/-/sohek6z/-/index.html

Chidawali, H., & Chebwete, R. (2014). CCM beats opposition despite decline. *Citizen,* 18, December. http://www.thecitizen.co.tz/News/CCM-beats-Opposition-despite-decline/-/1840392/2560666/-/iviub/-/index.html

Donor Countries (1995). *The presidential and house of representatives elections*. Statement of Donor Countries Cooperating in the Social Economic Development of Tanzania, released on 22nd October

Gray, H. (2015). The Political economy of grand corruption in Tanzania. *African Affairs,* Vol. 114, No. 456, pp. 382-403.

IFES (International Foundation for Electoral Systems) (1995). *Republic in transition: 1995 elections in Tanzania and Zanzibar*. Washington D.C.

Killian, B., & Mbunda, R. (2010). Elections and conflict in Zanzibar. In *When elephants fight: Preventing and resolving election-related conflicts in Africa*. Johannesburg: Global Print.

Kimboy, F. (2014). Political parties found wanting in funds audit. *Citizen,* 29 October. *http://www.thecitizen.co.tz/News/CCM-fails-test-in-party-subsidy-accounting-/-/1840406/2503280/-/pj1r9k/-/index.html*

Makoye, K. (2014). Anti-poaching operation spreads terror in Tanzania. June 6.http://www.ipsnews.net/2014/01/anti-poaching-operation-spread-terror-tanzania/

Mapuri, O. R. (1996). *Zanzibar, the 1964 revolution: Achievement and prospects*. Dar es Salaam: TEMA Publishers

Mbunda, R. 2009. Resolution or containment? An evaluation of direct negotiation and third-party facilitation in the Zanzibar conflict M.A. Dissertation: University of Dar es Salaam.

Mosoba, T. (2015). Man arrested, questioned after Tshs. 720 million found in his hotel room. *Citizen*, 12 July.

National Electoral Commission (2011). “Igunga by-election result”.

Othman, H. (2006). Political succession in Zanzibar. In Peter, C. M., & Kopsieker, F. (eds). *Political succession in East Africa: In search for a limited leadership*. Nairobi: Kituo Cha Katiba and Fredrich Ebert Stiftung- Kenya.

Ramadhani, A. S. L. (2000). The political situation of Zanzibar: Institutional and legal framework. In Maliyamkono, T. L. (ed). *The political plight of Zanzibar*. Dar es Salaam: TEMA Publishers.

REDET (Research for Education and Democracy in Tanzania) (2012). *Consolidation of the government of national unity in Zanzibar,* Dar es Salaam: REDET.

RGZ (1984). *Elections Act No. 11 of 1984 with 2004 amendments*. Government Printer: Zanzibar.

SMZ (1984). *Katiba ya Zanzibar ya 1984 - Toleo la 2010*. Kiwanda cha Uchapishaji Chuo Kikuu cha Elimu Chukwani: Zanzibar.

TEMCO (2000). *Report of the Tanzania election monitoring committee on the 2000 general elections in Tanzania*. Dar es Salaam: University of Dar es Salaam.

TEMCO (2010). *Report on the 2010 general Zanzibar elections*. Dar es Salaam: University of Dar es Salaam.

TEMCO (2015). *Interim report on the Tanzania 2015 general election*. TEMCO Observation Mission: Dar es Salaam.

URT (2008). *The Constitution of the United Republic of Tanzania of 1977*. Government Printer: Dar es Salaam

World Bank (2015). *Tanzania Mainland poverty assessment: Executive summary*. http://www.wds.worldbank.org/external/default/WDSContentServer/WDSP/IB/2016/03/18/090224b082e47cf0/1_0/Rendered/PDF/Executive0summary.pdf

ZEMOG (1995). *Monitoring of elections report by the Zanzibar Elections Monitoring Group (ZEMOG), 1995*.

## VIAMBATISHO

***Kiambatanisho namba 1: Orodha ya Asasi shiriki za TEMCO 2015***

| Na. | Asasi | Mahali ilipo |
|---|---|---|
| 1 | Action for Development Forward (ADF) | Dar es Salaam |
| 2 | Action for Justice in Society (AJISO) | Moshi |
| 3 | African Family Action Plan | Dar es Salaam |
| 4 | African International Group of Political Risk Analysis (PORIS) | Dar es Salaam |
| 5 | Agency for Co-operation and Research in Development (ACORD) | Mwanza |
| 6 | Agenda Participation 2000 | Dar es Salaam |
| 7 | Amani the Foundation of Life (AFL) | Mbeya |
| 8 | Amka Kazinga | Bukoba |
| 9 | Art for Development Company Limited | Bagamoyo |
| 10 | Association of Women for Democracy | Dar es Salaam |
| 11 | Association of Journalists and Media Workers (AJM) | Dar es Salaam |
| 12 | Association of Non-Governmental Organizations of Zanzibar (ANGOZA) | Zanzibar |
| 13 | Baraza Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA | Dar es Salaam |
| 14 | B'villea Community Services | Mbeya |
| 15 | Campaign for Good Governance (CGG) | Dar es Salaam |
| 16 | Centre Against Gender Based Violence | Dar es Salaam |
| 17 | Centre for Civil Society and Strategic Studies (CCSSS) | Dar es Salaam |
| 18 | Centre For Community Initiatives and Awareness | Dar es salaam |
| 19 | Centre for Informal Sector Promotion (CISF) | Moshi |
| 20 | Chama Cha Saidia Jamii-Kilombero (CHASAJAKI) | Ifakara |
| 21 | Chama cha Wafugaji Muheza (CHAWAMU) | Muheza |
| 22 | Chama Cha Walemavu Tanzania - Kigoma | Kigoma |
| 23 | Chama cha Walimu Tanzania (CWT) | Dar es Salaam |
| 24 | Chama cha Wastaafu na Wazee Lindi (CHAWALI) | Lindi |
| 25 | Chama Cha Wastaafu Wilaya ya Kisarawe (CHAWAKI) | Kisarawe |
| 26 | Chambani Development Society (CHADESO) | Mkoani Pemba |
| 27 | CHAWAKATA | Bukoba |
| 28 | Children Dignity Forum | Dar es Salaam |
| 29 | Children in Need Outreach (CINO) | Lindi |
| 30 | Christian Council of Tanzania (CCT) | Dar es Salaam |
| 31 | Christian Professionals of Tanzania (CPT) | Dar es Salaam |
| 32 | Civic Education Teachers' Association (CETA) | Dar es Salaam |
| 33 | Coast Region NGOs Network (CORNNET) | Mlandizi-kibaha |
| 34 | Community Development for All (CODEFA) | Kisarawe |
| 35 | Community Services Tanzania - COSETA | Dar es Salaam |
| 36 | Dar es Salaam Business School, Mzumbe University | Dar es Salaam |
| 37 | Department of Fine and Performing Arts ,UDSM | Dar es Salaam |
| 38 | Department of Political Science and Public Administration, UDSM | Dar es Salaam |
| 39 | Development and Relief Foundation ( DRF) | Bukoba |
| 40 | Development for Accountability for Tanzania | Bagamoyo |
| 41 | Development of Sustainable Community Based Activities (DESCOBA) | Dar es Salaam |
| 42 | District Organization for Aids Control and Orphans Right (DOACO) | Wete Pemba |
| 43 | Eastern and Southern Africa University Programme (ESAURP) | Dar es Salaam |

| Na. | Asasi | Mahali ilipo |
|---|---|---|
| 44 | Environature | Dar es Salaam |
| 45 | Environment Conservation for Social Development | Mkuranga |
| 46 | Environmental Conservation for Social Development ( ECOSODE) | Pwani |
| 47 | Environmental Protection and Humanitarian Agency (EPHA) | Kigoma |
| 48 | Forum for African Women Educationalists (FAWE) | Dar es Salaam |
| 49 | Guluka Kwalala Youth Environment Group | Dar es Salaam |
| 50 | Haki Mtoto Foundation | Dodoma |
| 51 | Hakielimu | Dar es Salaam |
| 52 | Health and Environmental Rehabilitation Organization of Tanzania | Dar es Salaam |
| 53 | Huruma Women Group | Dar es Salaam |
| 54 | Institute of Development Studies , UDSM | Dar es Salaam |
| 55 | Jamoja Trust | Moshi |
| 56 | Jikomboe Integral Development Association (JIDA) | Tabora |
| 57 | Jumuiya ya Sanaa ya Elimu ya Ukimwi na Mazingira (JSEUMA) | Mkoani Pemba |
| 58 | Jumuiya ya Wahitimu wa Chuo cha Demokrasia Zanzibar (JUWADEZA) | Zanzibar |
| 59 | Kagera Development and Credit Revolving Fund (KADETFU) | Bukoba |
| 60 | Kagera Environmental Care | Bukoba |
| 61 | Kagera Youth Empowerment Network | Bukoba |
| 62 | Kanyigo Aids Prevention Foundation | Kanyigo-bukoba |
| 63 | Kashai Development Initiative Organization (KADEI) | Bukoba |
| 64 | Kibaha Network of Civil Society Organizations (KNCSO) | Kibaha |
| 65 | Kidike Environmental Conservation Club | Chakechake Pemba |
| 66 | Kigoma Paralegal Aid Centre (KIPACE) | Kigoma |
| 67 | Kigoma Women Development Group | Kigoma |
| 68 | Kikundi Cha Wanawake Kilimanjaro Kupambana na Ukimwi (KIWAKKUKI) | Moshi |
| 69 | Kilimanjaro Women Information Exechange and Consultancy Organization (KWIECO) | Moshi |
| 70 | Kinga za Haki za Binadamu/Haki Za Raia (DHR) | Mbeya |
| 71 | Kinondoni Youth Parents Counselling Centre (KNYPC) | Dar es Salaam |
| 72 | Kiziba Development Initiatives | Bukoba |
| 73 | Kongwa Alliance Development Trust (KADET) | Mbeya |
| 74 | Lindi Support Agency for Welfare (Lisawe) | Lindi |
| 75 | Lindi Women's Paralegal Aid Centre | Lindi |
| 76 | Lisawe on Poverty Alleviation | Lindi |
| 77 | Liwale Farmer's Association (LIFA) | Liwale- lindi |
| 78 | Lumemo Farmers Club | Ifakara |
| 79 | Makambako Environmental Community Society | Makambako |
| 80 | Mapambano Centre for Children Rights | Mkuranga |
| 81 | Mara Youth NGO | Mara |
| 82 | Matumaini Women and Care of Children | Kigoma |
| 83 | Mbeya Older Persons Care (MOPEC) | Mbeya |
| 84 | Mbeya Paralegal Unit (MBEPAU) | Mbeya |
| 85 | Mbeya Women Organization for Preventing HIV/Aids | Mbeya |
| 86 | Mbeya Youth Development Organization | Mbeya |

| Na. | Asasi | Mahali ilipo |
|---|---|---|
| 87 | Mbinga Development and Environment Action (MBIDEA) | Mbinga |
| 88 | Mbulu Environmental Society Organization ( MBESO ) | Manyara |
| 89 | Merit Social Foundation (MESOF) | Mbeya |
| 90 | Micheweni Islamic Development Environmental Conservation and Aids Control (MIDECAC) | Micheweni Pemba |
| 91 | MIICO | Mbeya |
| 92 | Millennium Aids Herbalist Programme (MAHP) | Dar es Salaam |
| 93 | Mkoani Poverty Eradication Society (MPESO) | Mkoani Pemba |
| 94 | Moses Foundation Tanzania (MFT) | Dar es Salaam |
| 95 | Mowers Planters and Cleaners (MOPLAC) | Bukoba |
| 96 | Mshikamano and Advancement Women Organization | Dar es Salaam |
| 97 | Mtwara Region NGOs Network (ENGO) | Mtwara |
| 98 | Muheza District Paralegal Centre | Muheza |
| 99 | Multiple Education Centre (MEC) | Dar es Salaam |
| 100 | Mushrooming Legal, Economic and Environmental Aid for Community | Morogoro |
| 101 | Muungano wa Vijana Tanzania (MUVITA) | Dar es Salaam |
| 102 | MUVIKA | Bukoba |
| 103 | National Association of Education | Mbeya |
| 104 | National Youth Information Centre (NICE) KIGOMA | Kigoma |
| 105 | Ndela Kituo cha Maendeleo ya Vijana Kigoma | Kigoma |
| 106 | NGO Network for Dodoma Region (NGONDEDO) | Dodoma |
| 107 | Nyengedi Environment Development and Diseases Control | Lindi |
| 108 | Oak Tree Tanzania | Mbeya |
| 109 | Pamoja Aids and Environmental Foundation | Dar es Salaam |
| 110 | Patronage in Environmental Management and Health Care Warriors | Lindi |
| 111 | Peace House Foundation Ltd. | Moshi |
| 112 | Pemba Awareness for Land Use and Environment Society (PALESO) | Pemba |
| 113 | Pemba Environmental Gender and Advocacy Organization | Pemba |
| 114 | Pemba Investment and Youth Development Organization (PIYDO) | Wete Pemba |
| 115 | Pemba Press Club | Pemba |
| 116 | Pemba Rapid Development Organization (PRADO) | Wete Pemba |
| 117 | Peoples' Development Forum (PDF) | Dar es Salaam |
| 118 | People's Organization Transparency Agency (POTA) | Bukoba |
| 119 | Policy Mirror | Dar es Salaam |
| 120 | Ruaha University College | Iringa |
| 121 | Ruangwa Non-Governmental Organization Network (RUANGONET) | Ruangwa |
| 122 | Ruangwa Organization of Poverty Alleviation | Ruangwa-Lindi |
| 123 | Rural and Urban Development Initiatives (RUDIT) | Mkuranga |
| 124 | Rural Initiatives and Relief Agency | Magu |
| 125 | Rural Women Development Initiative (RUWODI) | Bagamoyo |
| 126 | Ruvuma Network of Organizations Working With HIV/Aids (RUNOWA) | Songea |
| 127 | Sanganigwa Children's Home | Kigoma |
| 128 | Self-Help Development Community (SEDECO) | Songea |
| 129 | SHIKWAUKI | Kilwa masoko |
| 130 | Shinyanga Civil Society Organization (SHINGONET) | Shinyanga |

| Na. | Asasi | Mahali ilipo |
|---|---|---|
| 131 | Sinangoa Disabled Group ( SDG) | Dar es Salaam |
| 132 | Society for Rural Development Initiatives (SRDI) | Dar es Salaam |
| 133 | Songea Network of Non-Governmental Organization (SONNGO) | Songea |
| 134 | South Region Civil Society Organization Network | Zanzibar |
| 135 | Taaluma Women Group (TWG) | Dar es Salaam |
| 136 | Taasisi ya Nyumba ya Haki (House of Justice) | Dar es Salaam |
| 137 | Tanganyika Law Society | Dar es Salaam |
| 138 | Tanzania Action for Coastal Education Advocacy | Kibaha |
| 139 | Tanzania Episcopal Conference (TEC) | Dar es Salaam |
| 140 | Tanzania Home Economics Association (TAHEA) | Dar es Salaam |
| 141 | Tanzania Journalists Association (TAJA) | Dar es Salaam |
| 142 | Tanzania Media and Youth Development Association (TAMEADA) | Songea |
| 143 | Tanzania Muslim Professional Association (TAMPRO) | Dar es Salaam |
| 144 | Tanzania Organization for Permaculture Promoters (TOPP) | Dar es Salaam |
| 145 | Tanzania Private Sector Foundation (TPSF) | Dar es Salaam |
| 146 | Tanzania Transparency Journalist Association | Dar es Salaam |
| 147 | Tanzania Women for Self Initiatives | Dar es Salaam |
| 148 | Tanzania Women Graduate Federation (TWGF) | Dar es Salaam |
| 149 | Tanzania Women Impact Foundation | Dar |
| 150 | Tanzania Women Lawyers Association (TAWLA) | Dar es Salaam |
| 151 | Tanzania Young Farmers Club (TAYFAC) | Dar es Salaam |
| 152 | Tanzania Youth Team for Campaign Against Aids (TAYOTA) | Dar es Salaam |
| 153 | Tanzania Youth Vision Association (TYVA) | Dar es Salaam |
| 154 | TCCIA Kigoma | Kigoma |
| 155 | The Institute of Peace and Conflict Studies (IPCS) | Dar es Salaam |
| 156 | Tumaini Trust Fund | Dar es Salaam |
| 157 | Uelekeo Tanzania (UTZ) | Dar es Salaam |
| 158 | Umoja wa Maendeleo Kaskazi Mtende Unguja (UMAKAMU) | Zanzibar |
| 159 | Umoja wa Wawezeshaji Kioo Kigoma | Kigoma |
| 160 | Urban West Civil Society Network | Zanzibar |
| 161 | Vitongoji Environmental Conservation on Association (VECA) | Chakechake-Pemba |
| 162 | Wamata Head Office | Dar es Salaam |
| 163 | Wazee Wastaafu Kigoma (WAWAKI) | Kigoma |
| 164 | Wete Environmental Conservation Club (WECOC) | Wete-Pemba |
| 165 | White Orange Youth (WOY) | Moshi |
| 166 | Women and Children Improvement Agency (WOCHIA) | Dar es Salaam |
| 167 | Women and Community Development (MUDUGU-WACOD) | Kisarawe |
| 168 | Women in Law and Development in Africa (WILDAF) | Dar es Salaam |
| 169 | Women Initiatives of Tabora | Tabora |
| 170 | Women Law Association Centre | Dar es Salaam |
| 171 | Youth Against Poverty Trust Fund (YAP) | Dar es Salaam |
| 172 | Youth Development Society | Wete-Pemba |
| 173 | Youth Environment Rescue Organization Tanzania (YEROTAN) | Dar es Salaam |
| 174 | Youth Service Volunteers Society | Dar es Salaam |
| 175 | ZAM Foundation | Dar es Salaam |

| Na. | Asasi | Mahali ilipo |
|---|---|---|
| 176 | Zanzibar Association of the Disabled | Zanzibar |
| 177 | Zanzibar Female Lawyers Association (ZAFELA) | Zanzibar |
| 178 | Zanzibar Law Society (ZLS) | Zanzibar |
| 179 | Zanzibar Legal Services Centre (ZLSC) | Zanzibar |
| 180 | Zanzibar National Association of the Blind (ZANAB) | Zanzibar |
| 181 | Zanzibar Paralegal Organization | Zanzibar |
| 182 | Zanzibar Women Cooperation (ZAWCO) | Zanzibar |
| 183 | Zanzibar Youth Education Development Environment Supporters | Zanzibar |

***Kiambatanisho namba 2: Maadili ya Waangalizi Uchaguzi wa TEMCO***

Kuonesha tabia njema na kuvaa mavazi nadhifu kama njia ya kuakisi heshima na haiba ya TEMCO wakati wote.

Kutii sheria, taratibu na miongozo yote inayoongoza chaguzi, kama zilivyopitishwa na vyombo vinavyoratibu uchaguzi, NEC na ZEC au vinginevyo.

Muda wote kutokuonesha upendeleo au kuegemea upande wowote hususani wa kisiasa wakati wa kutekeleza majukumu uliyopewa na ni marufuku kutoa matamko yanayoakisi kuegemea uongozi wa Taifa, vyama vya siasa au wagombea na hata kuhusiana na jambo lolote linaloshindaniwa katika mchakato wa uchaguzi.

Taarifa na nyaraka zote zinazohusiana na zilizopatikana wakati wa kipindi cha utazamaji wa uchaguzi husika inabidi ziwe siri na mali ya TEMCO na hivyo inabidi ziwasilishwe kwa TEMCO tu.

Ni marufuku kwa waangalizi wa uchaguzi wa TEMCO kutoa matamko au maoni kwenye vyombo vya habari kuhusiana na wanayoyashuhudia katika kutimiza wajibu wao. Ni Mwenyekiti wa TEMCO na Kiongozi Mkuu wa waangalizi au Naibu wake wanaoruhusiwa kutoa baadhi ya matamko na maoni kwenye vyombo vya habari juu ya zoezi la utazamaji.

Waangalizi hawapaswi kukwaza au kuingilia sehemu yoyote ya mchakato wa uchaguzi, ikiwa ni pamoja na kabla ya mchakato wa kupiga,kuhesabu kura ,kujumlisha na kutangaza matokeo na michakato inayoendelea baada ya uchaguzi.

Waangalizi wa TEMCO wanaweza kuwasilisha au kutoa ushauri kuhusu suala au masuala yanayohitaji ufuatiliaji au kuchukuliwa hatua za haraka na maafisa uchaguzi lakini uwasilishaji au ushauri huu kamwe haupaswi kuingilia, kukwaza na hata kutolewa katika mkitadha wa kutoa maelekezo kwa maafisa hawa wa uchaguzi.

Waangalizi watawajibika kukaa kwenye sehemu waliyopangiwa kufanya utazamaji siku nzima ya upigaji kura, ikiwa ni pamoja na kutazama zoezi zima la kupiga kura, kuhesabu kura, kujumlisha kura na kutangazwa kwa matokeo.

Waangalizi watafikia mahitimisho ya utazamaji kwa misingi ya yale waliyoyashuhudia wakati wa utazamaji na pia takwimu na vielelezo watakavyokuwa wamevipata.

Waangalizi wanapaswa kuwa makini na kuchukua tahadhari wakati wakitimiza wajibu wao kwani usalama wao ni muhimu kuliko kitu chochote kile.

Waangalizi watapaswa kuwa na vitambulisho vitakavyotolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi, NEC na ile ya Zanzibar yaani ZEC. Waangalizi watapaswa kuvionesha kwa mamlaka husika

wakati wowote wakihitajika kufanya hivyo. Pia wakati wote waangalizi wa TEMCO wanawajibika kuwa wamevaa mavazi maalum ya TEMCO.

Waangalizi watapaswa kujiheshimu na kutenda kazi zao kwa kujituma na kwa uadilifu na weledi wakati wote.

Waangalizi wote wanawajibika kuhudhuria mikutano yote itakayoitishwa na TEMCO; na watapaswa kuwepo katika vituo walivyopangiwa, na kufuata maelekezo yote watakayopewa na uongozi wa TEMCO.

Waangalizi watapaswa kujiepusha na vitendo ambavyo vinaweza kuibua hisia za kupendelea chama cha siasa au mgombea yeyote anayeshiriki kinyang'anyiro cha uchaguzi husika.

*Kiambatanisho namba 3: Mgawanyo wa Waangalizi wa TEMCO*

| Mkoa | Jina la Mwangalizi | Jimbo | Kata | Idadi ya STOs |
|---|---|---|---|---|
| 1. Arusha | Annmarie Nkelame (REOC) | Arusha | 25 | 50 |
| | Baraka Leader | Karatu | 14 | 44 |
| | Dr.Mbeba Benjamin | Arumeru West | 27 | 44 |
| | Fransisca Silayo | Arumeru East | 26 | 50 |
| | Marietha Kaijage | Monduli | 20 | 44 |
| 2. Dar Es Salaam | Dr. Rose Shayo (REOC) | Ilala | 16 | 45 |
| | Dr. Richard Mbunda | Segerea | 9 | 50 |
| | Anna Mgalla | Temeke | 13 | 45 |
| | Perpetua Bilizonzi | Mbagala | 10 | 44 |
| | RithaKalokola | Kawe | 10 | 50 |
| | Rusa Allen | Ubungo | 8 | 50 |
| | Shani Adam | Kibamba | 6 | 44 |
| 3. Dodoma | Agape Kakumbula | Mpwapwa | 15 | 46 |
| | Christabella Bushiri | Mtera | 22 | 46 |
| | Dr.Rasul A. Minja (REOC) | Dodoma Town | 41 | 46 |
| | Elly Ahimidiwe | Kongwa | 22 | 46 |
| | Martin Kihunrwa | Kondoa Town | 8 | 46 |
| 4. Geita | Ferdinand Lutatenekwa (REOC) | Geita Town | 12 | 50 |
| | Christina Mbilinyi | Busanda | 22 | 45 |
| | Alban Hokororo | Bukombe | 17 | 44 |
| | Patrick Mlinga | Chato | 23 | 45 |
| 5. Iringa | Prof.Bernadeta Killian | Iringa Town | 18 | 50 |
| | Evelyine Missingo | Kilolo | 24 | 45 |
| | Fortunata Sarmo | Mufindi North | 11 | 45 |
| | Denis Kamugisha | Mafinga Town | 9 | 44 |
| 6. Kagera | Faustine Rwelamila (REOC) | Bukoba Town | 14 | 50 |
| | Elizabeth Bitegela | Biharamulo | 17 | 45 |
| | Godfrey Benson | Karagwe | 23 | 45 |
| | KetrinaMakobwe | Kyerwa | 24 | 45 |
| | Lusubilo Mwaisunga | Muleba South | 25 | 46 |
| | Peter Enos | Ngara | 22 | 45 |
| 7. Katavi | Dr.Hamza Kondo (REOC) | Mpanda Town | 15 | 46 |
| | ConsolatiaBarongo | Katavi | 6 | 46 |
| | Alex William | Kavuu | 9 | 46 |
| 8. Kigoma | Deogratius Kisinda | Muhambwe | 19 | 45 |
| | Gibson B. George | Kasulu Town | 15 | 45 |
| | Shaaban Simba (REOC) | Kigoma Town | 19 | 50 |
| | Ibrahim A. Rwenza | Kigoma North | 16 | 45 |
| | Graceana Roman | Kigoma South | 16 | 45 |
| 9. Kilimanjaro | Audax B. Kweyamba | Hai | 17 | 43 |
| | Prof. Ernest T. Mallya (REOC) | Moshi Town | 21 | 50 |
| | Miza Haji | Same East | 14 | 43 |

| Mkoa | Jina la Mwangalizi | Jimbo | Kata | Idadi ya STOs |
|---|---|---|---|---|
| | Neema Richard | Vunjo | 16 | 50 |
| | Leonard Haule | Rombo | 28 | 44 |
| 10. Lindi | Sixbert Khamsini | Liwale | 20 | 46 |
| | Rajab Ali | Nachingwea | 36 | 46 |
| | Rubalatuka B. Josephat | Mtama | 20 | 46 |
| | Ali S. Mwaimu (REOC) | Lindi Town | 20 | 46 |
| | Thomas H. Moshi | Kilwa North | 13 | 46 |
| 11. Mara | Kulwa Mgawe | Bunda Town | 14 | 50 |
| | Elizabeth Massanja | Tarime Town | 8 | 50 |
| | Davis Benjamin Kato | Serengeti | 31 | 44 |
| | Furaha Julius | Butiama | 18 | 44 |
| | Norvin S. Mujwahoki | Rorya | 26 | 44 |
| | Prof. Mohabe Nyirabu (REOC) | Musoma Town | 16 | 44 |
| 12. Manyara | Dr.Leons Kimaryo(REOC) | Babati Town | 8 | 46 |
| | JechaVuaiJecha | Hanang' | 33 | 46 |
| | Mahyoro Kalokola | Mbulu Town | 17 | 46 |
| | Mariasemeni Festo | Simanjiro | 18 | 46 |
| 13. Mbeya | Dr. Bashiru Ally (REOC) | Mbeya Town | 36 | 50 |
| | Naumi Shemweta | Mbarali | 20 | 45 |
| | NdamlaniGosbert | Rungwe | 29 | 46 |
| | Neema Mukandala | Ileje | 18 | 45 |
| | Rashid Abdalla | Vwawa | 18 | 45 |
| | Rev. Raphael Haule | Tunduma | 15 | 45 |
| | Salma Hassan | Lupa | 20 | 46 |
| | Titus Gindo | Kyela | 33 | 46 |
| 14. Morogoro | Dr.Victoria Makulilo (REOC) | Morogoro Town | 29 | 46 |
| | Hoti Ramadhani | Morogoro South East | 14 | 46 |
| | Hysintha Musaroche | Gairo | 18 | 46 |
| | Ishengoma Gosbert | Mikumi | 17 | 46 |
| | Pavin Msigula | Kilombero | 19 | 46 |
| | Soud B Ayoub | Ulanga East | 21 | 46 |
| | Hildergada Mashauri | Kilosa | 23 | 46 |
| 15. Mtwara | Lucas Kisasa (REOC) | Mtwara Town | 18 | 46 |
| | Salma Saadat | Mtwara Rural | 21 | 46 |
| | Tambila Bukungu | Newala Town | 16 | 46 |
| | Tatu G. John | Nanyumbu | 17 | 46 |
| | Vicky K. Moshi | Ndanda | 16 | 46 |
| | Theresia Kessy | Masasi | 14 | 46 |
| 16. Mwanza | Anita Kisasira | Ilemela | 19 | 50 |
| | Dr. Ambrose T. Kessy (REOC) | Nyamagana | 18 | 50 |
| | Eva Maduhu | Kwimba | 15 | 44 |
| | Malingo Kinsweni | Magu | 25 | 44 |
| | Peter A. Bana | Sengerema | 26 | 44 |

| Mkoa | Jina la Mwangalizi | Jimbo | Kata | Idadi ya STOs |
|---|---|---|---|---|
| | Rweyemamu Sylivester | Ukerewe | 25 | 44 |
| 17. Njombe | Penina Petro | Njombe North | 13 | 46 |
| | BaumbaChogero (REOC) | Makambako | 12 | 46 |
| | Respicius S. Damian | Makete | 23 | 46 |
| 18. Pwani | Ahmad Haji | Chalinze | 15 | 46 |
| | Dr.Denis Gatambwa (REOC) | Kibaha Town | 14 | 46 |
| | Dr. Jacob Lisakafu | Mafia | 8 | 46 |
| | Regina Kabwogi | Mkuranga | 25 | 46 |
| | Renatus Mkinga | Rufiji | 13 | 46 |
| 19. Rukwa | Ramadhani Kingi (REOC) | Sumbawanga Town | 19 | 46 |
| | Happiness Malleyeck | Nkansi North | 17 | 46 |
| | Amina T. Ali | Kalambo | 23 | 46 |
| 20. Ruvuma | William John (REOC) | Songea Town | 21 | 45 |
| | Oscar Tarimo | Nyasa | 20 | 45 |
| | Anita Philbert | Tunduru North | 24 | 45 |
| | Fridolin Henjewele | Peramiho | 16 | 50 |
| | Happy Israel | Mbinga Town | 19 | 45 |
| 21. Simiyu | Dr. Edwin Babeiya (REOC) | Bariadi East | 22 | 46 |
| | Brenda Kalokola | Meatu | 16 | 46 |
| | Dr. Emmanuel Elia | Busega | 15 | 46 |
| | Kemilembe Mukyanuzi | Maswa West | 17 | 46 |
| 22. Singida | Dionis Ndamgoba (REOC) | Singida Town | 18 | 46 |
| | Bernadetha E. Choma | Iramba East | 17 | 46 |
| | Adrophina Salvatory | Iramba West | 20 | 46 |
| | Hadija K. Mwendah | Manyoni West | 13 | 46 |
| | Penina Nkinga | Singida East | 13 | 46 |
| 23. Shinyanga | Christonsia Reginald (REOC) | Shinyanga Town | 17 | 45 |
| | Abdalla J Abdalla | Kishapu | 29 | 45 |
| | Indamo Mziray | Msalala | 18 | 44 |
| | Joswam Kamara | Kahama Town | 20 | 50 |
| 24. Tabora | Joseph Ibreck (REOC) | Tabora Town | 29 | 46 |
| | Janeveva Emmanuel | Igalula | 11 | 46 |
| | Dr. Charles Saana | Sikonge | 20 | 46 |
| | Patricia Reginald | Urambo | 18 | 46 |
| | Suleimani Abubakari | Nzega Rural | 19 | 46 |
| | Emmanuel Momburi | Igunga | 16 | 46 |
| 25. Tanga | Matrona Kabyemela (REOC) | Tanga Town | 27 | 46 |
| | Anold Temba | Lushoto | 15 | 46 |
| | Jamila M. Juma | Bumbuli | 18 | 46 |
| | Tatu Kibakaya | Pangani | 14 | 46 |
| | Phillemon S. Mutashubirwa | Kilindi | 21 | 46 |
| | Renatus Rweshabula | Handeni Town | 12 | 46 |
| | Sophia Derick | Korogwe Town | 11 | 46 |

| Mkoa | Jina la Mwangalizi | Jimbo | Kata | Idadi ya STOs |
|---|---|---|---|---|
| 26. Pemba North | Antony Kija (REOC) | Kojani | 10 | 32 |
| | Joyce Mwacha | Mgogoni | 8 | 32 |
| | Dr. Philemon Lugumiliza | Micheweni | 8 | 32 |
| | Deborah Mbalilaki | Konde | 7 | 32 |
| 27. Unguja North | John Kihamba (REOC) | Chaani | 8 | 32 |
| | GoodluckMshana | Nungwi | 9 | 32 |
| | Anita Masaki | Donge | 9 | 32 |
| | Sophia Komba | Mahona | 9 | 32 |
| 28. Pemba South | Ishengoma J. Katabaro (REOC) | Chake Chake | 7 | 32 |
| | Kandi S. Mwambo | Wawi | 7 | 32 |
| | Devotha Mkongwa | Chambani | 7 | 32 |
| | Victor W. Rugumamu | Mtambile | 8 | 32 |
| 29. Unguja South | Faraja Ndumbaro(REOC) | Chwaka | 11 | 32 |
| | Felister Frank | Uzini | 16 | 32 |
| | Matogwa Armstrong | Makunduchi | 13 | 32 |
| 30. Unguja Town | Frida Ilomo | Dimani | 8 | 32 |
| | Asha Aboud (REOC) | Kiembesamaki | 4 | 32 |
| | Lucius Mugisha | Bububu | 6 | 32 |
| | Jocelyn Mkilima | Chumbuni | 6 | 32 |
| | Jackson Juma Coy | Mpendae | 4 | 32 |
| | Ezra E. Mbangwa | Jang'ombe | 5 | 32 |
| | Shafii D. Kanju | Kikwajuni | 10 | 32 |
| Jumla | | | 2550 | 6600 |

***Kiambatanisho namba 4: Wanachama wa CCM waliochukua Fomu za Kuteuliwa kugombea Urais ndani ya Chama***

| Na. | Jina | Nafasi Aliyokuwanayo |
|---|---|---|
| 13 | Ally Abeid Karume | Former Ambassador |
| 14 | Amina Salum Ali | AU Ambassador |
| 41 | Amos Robert | Not available |
| 12 | Amos Siyantemi | CCM Secretariat officer |
| 40 | Antony Chalamila | Not available |
| 29 | Asha Rose Migiro | Minister for Constitutional and Legal Affairs |
| 34 | Athuman Mwariko | Painter, Sculptor and Cultural Scientist |
| 22 | Augustine Mahiga | Former Tanzania Permanent Representative to the UN |
| 18 | Bernard Membe | Minister for Foreign Affairs and International Cooperation |
| 26 | Bonephace Ndenga | Businessman |
| 33 | Boniface Ndego | Not available |
| 9 | Charles Makongoro Nyerere | EALA member |
| 2 | Edward Ngoyai Lowassa | Former Prime Minister, Member of Parliament |
| 25 | Eldoforce Bihelo | Farmer |
| 3 | Frederick Tluway Sumaye | Former Prime Minister |
| 15 | Godwin Mwapongo | High Court Advocate |
| 20 | Hamis Kigwangalla | Member of Parliament |
| 27 | Hans Kitine | Former Chief of Intelligence Services |
| 39 | Helena Elinawinga | Not available |
| 19 | January Makamba | Deputy Minister for Communication, Science and Technology |
| 6 | John Pombe Magufuli | Minister of Works |
| 36 | Joseph Chagama | Not available |
| 17 | Lazaro Nyalandu | Minister for Natural Resource and Tourism |
| 16 | Leons Mulenda | Civil Servant |
| 21 | Luhaga Mpina | Member of Parliament |
| 31 | Maliki Malupu | Postgraduate student at Mzumbe University |
| 8 | Mark Mwandosya | Minister of State, President’s Office |
| 30 | Mathias Chikawe | Minister for Home Affairs |
| 28 | Mizengo Pinda | Prime Minister, United Republic of Tanzania |
| 1 | Mohammed Gharib Bilal | Vice President United Republic of Tanzania |
| 32 | Monica Mbega | Former Deputy Minister for Finance |
| 35 | Muzzammil Kalokola | Chairperson, Mwalimu Nyerere Ideology Conservation Society |
| 23 | Mwele Malecela | Director General of National Institute for Medical Research |
| 5 | Mwigulu Lameck Nchemba | Deputy Minister for Finance |
| 37 | Patrick Chokala | Former diplomat and Press Secretary to presidents Mwinyi and Mkapa |

| Na. | Jina | Nafasi Aliyokuwanayo |
|---|---|---|
| 24 | Peter Nyalali | Retired soldier |
| 38 | Ritha Ngowi | Community Development Officer |
| 7 | Samuel John Sitta | Minister for Transport, Former Speaker |
| 11 | Sospeter Muhongo | Former Minister for Energy and Minerals |
| 4 | Stephen Massatu Wassira | Minister for Agriculture, Food and Cooperative |
| 10 | Titus Kamani | Minister for Livestock and Fisheries Development |
| 42 | William Ngeleja | Former Minister for Energy and Minerals |

*Kiambatanisho namba 5: Mapendekezo ya TEMCO ya Kuboresha Mchakato wa Chaguzi wa 2000*

| Aina ya mapendekezo | Mapendekezo | Mamlaka husika | Hatua zilizochukuliwa | Maoni |
|---|---|---|---|---|
| Usimamizi wa michakato ya uchaguzi | NEC na ZEC inabidi ziundwe upya ili ziweze kuaminiwa na wadau wote wa uchaguzi, hasa vyama vya siasa na wapiga kura kabla ya uchaguzi wa mwaka 2005 | Serikali ya jamhuri ya Muungano wa Tanzania | Utaratibu wa muundo mpya wa NEC na ZEC umewekwa bayana katika Katiba mpya iliyopendekezwa | Utekelezaji wa mabadiliko yaliyochukuliwa unasubiri matokeo ya kura ya maoni juu ya Katiba iliyopendekezwa |
| | Uhusiano wa NEC na ZEC katika kusimamia uchaguzi rais wa Jamhuri ya Muungano na wabunge unahitaji kutafsiriwa upya ili kuodoa mkanganyiko uliopo kwa sasa | Serikali ya jamhuri ya Muungano wa Tanzania na serikali ya mapinduzi Zanzibar | Uhusiano ulitafsiriwa upya | Hakuna tena utata katika uhusiano kati ya NEC na ZEC |
| | Sheria za uchaguzi zinatakiwa kutoa njia sahihi ya kuweka mipaka ya majimbo ya uchaguzi ili kupunguza malalamiko na upendeleo | NEC na ZEC | Mfumo wa kisheria ulitafsiriwa upya | Uwekaji wa mipaka ya majimbo unaongozwa na mfumo uliofanyiwa marekebisho |
| | Mpango wa elimu ya uraia na elimu ya mpiga kura unaoendeshwa na NEC na ZEC unatakiwa kuwa endelevu badala ya kusubiri hadi kipindi cha uchaguzi | NEC, ZEC na wadau wengine wa uchaguzi | Bado hakuna hatua thabiti za kutoa elimu kwa mpiga kura | Utoaji elimu ya mpiga kura bado hauridhishi |
| | Ajira za wasimamizi wa uchaguzi (RECs, ROs, AROs na PAROs) zinatakiwa kutangazwa kwenye vyombo vya habari. Uteuzi wa wa wasimamizi wa uchaguzi kutoka serikalini inabidi ukomeshwe ili kuondoa mianya ya upendeleo katika michakato ya uchaguzi | NEC | Hakuna hatua zilizochukuliwa | Hakuna |
| | Sheria ya sasa ya Mzanzibari mkaazi inahitaji kupitiwa kwa kuwa inakandamiza uhuru wa kikatiba wa raia wa kusajiliwa kama wapiga kura | Serikali ya Mapinduzi Zanzibar | Hakuna hatua zilizochukuliwa | Hakuna |
| | Tunapendekeza kutolewa kwa elimu ya urais kwa vikosi vya ulinzi na usalama ili viweze kutambua haki za kiraia za wananchi, ikiwa | Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania | Mpango wa elimu ya uraia kwa vikosi vya ulinzi na usalama ulianzishwa | Programu hizi zimesaidi kwa kiasi fulani kuboresha uhusiano baina na vyombo hivi na raia |

| Aina ya mapendekezo | Mapendekezo | Mamlaka husika | Hatua zilizochukuliwa | Maoni |
|---|---|---|---|---|
| | ni pamoja na makundi mbalimbali kama vyama vya siasa | | | |
| | | | | |
| Uandikishaji wapiga kura | Ipo haja ya kupanua wigo wa elimu ya mpigakura ili kuhakikisha kuwa inatolewa kabla ya kipindi cha uchaguzi. | NEC, ZEC na wadau wengine wa uchaguzi | Hakuna hatua zilizochukuliwa kuboresha utoaji wa elimu kwa mpiga kura | Utoaji wa elimu kwa mpiga kura bado hauridhishi |
| | Uteuzi wa maafisa uandikishaji unatakiwa kuwa wazi na unatakiwa kuhusisha wadau muhimu kama asasi za kiraia na vyama vya siasa | NEC | Hakuna hatua zilizochukuliwa | Hakuna |
| | Ipo haja ya kuhakikisha kuwa maafisa uandikishaji na wapiga kura wanapatiwa mafunzo ya kutosha | NEC na ZEC | Mafunzo ya maafisa hawa yamekuwa yakiboreshwa | Mafunzo kwa maafisa hawa yanaridhisha kwa kiasi |
| | Ni vyema operesheni ya kukusanya kodi isiende sambamba na zoezi la kuandikisha wapiga kura | Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania | Opreseheni hizi zilikomeshwa | Hakuna tena mwingiliano |
| | Ipohaja ya kufanyika kwa sensa ya watu na makazi | Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania | Sensa ilifanyika | Hakuna |
| | Kuna haja ya kutoa orodha ya wapiga kura kwa wakati | NEC na ZEC | Uandaaji na ubandikaji wa hizi orodha bado hauridhishi | Kasi ya NEC na ZEC katika kubandika orodha hizi bado hairidhishi |
| | Zoezi la kuandikisha wapiga kura inabidi liendelee hadi hatua ya uteuzi wa wagombea ndani ya vyama | NEC na ZEC | Hakuna hatua zilizochukuliwa | Hakuna |
| | | | | |
| Uteuzi wa wagombea na Kampeni | NEC inatakiwa kutafuta wataalamu wa kushauri namna bora ya kuajiri watumishi wa serikali za mitaa kama wasimamizi wa uchaguzi | NEC | Hakuna hatua zilizochukuliwa | Hakuna |
| | | NEC | | Hakuna |

| Aina ya mapendekezo | Mapendekezo | Mamlaka husika | Hatua zilizochukuliwa | Maoni |
|---|---|---|---|---|
| | NEC inatakiwa kutathmini zuio lake la matumizi ya lugha za asili wakati wa michakato ya uchaguzi | | Hakuna hatua zilizochukuliwa | |
| | Ipo haja ya kuandaa kongamano la kitaifa kujadili nafasi ya viongozi wa vyama vya siasa katika nyanja za siasa | NEC na ZEC | Makongamano kadhaa yaliyoandaliwa na NEC na ZEC yamefanyika | Uhusiano baina ya vyombo vya kusimamia uchaguzi na viongozi wa dini ni mzuri |
| | . NEC ifanye mapitio ya matumizi ya vyombo vya habari vya serikali na iandae utaratibu bora wa kuwezesha kutoa fursa sawa kwa vyama vyote vinanvyoshiriki katika michakato ya uchaguzi | Vyombo vya habari vya umma; Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania | Hakuna hatua zilizochukuliwa | Vyama vya upinzani bado vinabanwa katika kutumia vyombo vya habari vya serikali |
| | Suala la ruzuku za serikali kwa ajili ya kampeni za uchaguzi linatakiwa kuangaliwa vizuri ili kuwezesha mazingira bora baina ya vyama vyenye raslimali na vyama maskini | Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania | Hakuna hatua zilizochukuliwa | Hakuna |
| | Matumizi ya lugha ya matusi yakomeshwe | NEC na ZEC | Hakuna hatua zilizochukuliwa | Matumizi ya lugha ya matusi wakati wa uchaguzi bado yanashuhudiwa |
| | Muda wa kufunga shughuli za kampeni unatakiwa kupitiwa upya kwakuwa saa kumi na mbili jioni inaweza kuwa muda wa mapema zaidi katika baadhi ya maeneo na kuwa muda wa jioni sana katika maeneo mengine. | NEC | Hakuna hatua zilizochukuliwa | Hakuna |
| | | | | |
| Kupiga kura, huhesabu kura na kutangaza matokeo | Wasimamizi wa vituo vya kupigia kura wanatakiwa kuwa na maadalizi ya kabla ili kuondoa changamoto kwa wapiga kura siku ya kupiga kura | NEC na ZEC | Uandaaji wa madaftari ya wapigakura umeboreshwa kwa kiwango fulani | Daftari la kudumu la mpiga kura lipo wazi kwa wapiga kura kabla ya siku ya uchaguzi |
| | Elimu ya mpiga kura inabidi itolewe na mamlaka husika kwa usahihi na kwa kina ikiwa ni pamoja na NEC, ngazi zote za | NEC, ZEC na wadau wengine wa kisiasa | Hakuna hatua madhubuti zilizochukuliwa | Utoaji wa elimu ya mpiga kura kwa wadau wote wa uchaguzi bado hauridhishi |

| Aina ya mapendekezo | Mapendekezo | Mamlaka husika | Hatua zilizochukuliwa | Maoni |
|---|---|---|---|---|
| | serikali, vyombo vya habari, asasi za kiraia, vyama vya siasa n.k | | | |
| | Ajira za wasimamizi wa uchaguzi na wasaidizi wao inabidi zizingatie misingi ya weledi badala ya utaratibu wa upendeleo | NEC | Hakuna hatua zilizochukuliwa | hakuna |
| | Mafunzo kwa wasimizi wa uchaguzi na wasaidizi wao yanatakiwa kutolewa kwa wakati, ikiwezekana wiki moja kabla ya siku ya uchaguzi ili kuwapa muda zaidi wa kuelewa sheria, kanuni na taratibu za uchaguzi | NEC na ZEC | Mafunzo ya maafisa uchaguzi yameboreshwa na yanaridhisha | Mafunzo yanayotolewa kwa maaisa ya uchaguzi yamekuwa yanatosheleza kuwawezesha kusimamia vizuri michakato ya uchaguzi |
| | NEC inatakiwa kuhakikisha kuwa vituo vyote vya kupigia kura vipo katika mazingira yanayoridhisha ili kuhakikisha kuwepo kwa mazingira ya usiri na kuwakinga wapiga kura dhidi ya mvua na jua kali. | NEC | Ubora wa vituo vya kupigia kura umeboreshwa kiasi | Ubora wa vituo vingi vya kupigia kura umekuwa unaridhisha |
| | NEC inatakiwa kuboresha mtandao wake wa mawasiliano ili kuhakisha kuwa matokeo ya uchaguzi yanatangazwa mapema sana iwezekanavyo | NEC | Utumiaji wa mifumo na vifaa vya Tehama umeboresha kwa kiwango fulani utangazaji wa matokeo kwa haraka | Pamoja na maboresho kidogo, tabia ya kuchelewesha utangazaji wa matokeo bado imekithiri |
| | | | | |
| Ushiriki wa wanawake katika uchaguzi | Vyama vya siasa vishurutishwe kuzingatia masuala ya usawa wa kijinsia katika michakato yake ya ndani, hasa katika masuala ya uongozi | Vyama vya siasa | Uwnja wa kijinsia umeboleshwa katika vyama vya siasa | Pamoja na maboresho kidogo bado hakuna usawa wa kijinsia katika ngazi za juu za uongozi wa vyama vya siasa |
| | Sheria ya taifa ya uchaguzi itoe mamlaka kwa NEC ya kuchunguza michakato ya uteuzi wa wagombea ndani ya vyama ikiwa ni pamoja na vigezo vilivyotumiwa wakati wa uteuzi wa wagombea | Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania | Hakuna hatua zilizochukuliwa | Hakuna |
| | NEC inatakiwa kufuatilia michakato ya kisiasa ndani ya vyama vya siasa ili | NEC | Hakuna hatua zilizochukuliwa | Hakuna |

| Aina ya mapendekezo | Mapendekezo | Mamlaka husika | Hatua zilizochukuliwa | Maoni |
|---|---|---|---|---|
| | kuhakikisha kuwa vyama vya siasa vinakomesha vitendo vya rushwa na unyanyasaji wa kijinsia na ubaguzi wowote kwa misingi ya kabila au jinsia | | | |
| | Serikali, vyama vya siasa na jamii kwa ujumla kufanya maboresho kuhusu nafasi ya mwanamke katika uchaguzi. | Wadau wote wa uchaguzi | Wadau wote wa uchaguzi wamefanya jitihada mbalimbali za kuongeza ushiriki wa wanawake katika uchaguzi | Bado idadi ya wagombea wanawake katika ngazi ya ubunge na udiwani ni ndogo |
| | | | | |
| Rushwa katika Uchaguzi | Vyama vya siasa vinatakiwa kutumia michakato kubalifu zaidi wakati wa uteuzi wa wagombea sambamba na utaratibu wa kupiga kura | Vyama vya siasa | Utaratibu wa uteuzi wa wagombea unatofautiana baina ya vyama | Mbali na CCM, uteuzi wa wagombea katika vyama vya upinzani hauna mchakato wa kina |
| | Sheria ya takrima na kampeni za mlango kwa mlango zinatakiwa kufanyiwa marekebisho | NEC na ZEC | Takrima ilipigwa marufuku | Japokuwa takrima ilipigwa marufuku, vitendo vya kampeni ya mlango kwa mlango bado vinashudiwa katika uchaguzi |
| | Wagombea wanatakiwa kuzingatia ilani za vyama vyao wakati wa kujinadi kwa wapiga kura | Vyama vya siasa, wagombea | Hakuna hatua madhubuti zilizochukuliwa | Tabia ya wagombea kutokuzingatia ilani za uchaguzi za vyama vyao bado ipo |
| | Wagombea wanatakiwa kuheshimu taratibu za maadili wakati wa michakato ya uchaguzi | Wagombea | Hakuna hatua madhubuti zilizochukuliwa | Hakuna hatua za kina kuwezesha utekelezaji wa kanuni hizi |
| | Vyama vya siasa vinatakiwa kuwa na uwazi na kueleza ukweli kuhusu viongozi wake wanaojihusisha na rushwa | Vyama vya siasa | Hakuna hatua zilizochukuliwa | Vyama vya siasa vimekuwa mstari wa mbele kukemea rushwa ndani ya serikali lakini havifanyi vivo hivyo juu ya vitendo vya namna hiyo ndani ya vyama |
| | Ipo haja ya kubadili sheria ya vyama vya siasa ili kuvitaka vyama kubainisha vyanzo vyake vya fedha vya ndani na nje ya nchi | Serikali ya jamhuri ya Muungano wa Tanzania | Sheria ya gharama za uchaguzi ilitungwa mwaka 2010 | Utekelezaji wa sheria hii umekuwa hauridhishi |
| | | | | |

| Aina ya mapendekezo | Mapendekezo | Mamlaka husika | Hatua zilizochukuliwa | Maoni |
|---|---|---|---|---|
| Vyombo vya habari | Upo umuhimu kwa vyombo vya habari kuhakikisha kwamba viwango vya ubora wa kitaaluma vya uandishi wa habari vinaboreshwa kabla ya chaguzi zinazofuata | Vyombo vya habari vya umma na binafsi | Hatua kadhaa za kuboreshw viwango vya taaluma na ujuzi vya waandishi wa habari zimechukuliwa | Pamoja na maboresho kadhaa, bado viwango vya kitaaluma vya waandishi wa habari wengi ni vidogo |
| | Vyombo vya habari vya umma vinatakiwa kuepuka upendeleo | Vyombo vya habari vya umma | Hakuna hatua madhubuti zilizochukuliwa | Vyama vya upinzani bado vinavilaumu vyombo vya habari vya umma kwa kuwa na upendeleo |
| | NEC inatakiwa kuwa na mpango endelevu wa elimu kwa wapiga kura kabla ya uchaguzi mkuu na uchaguzi wa serikali za mitaa | NEC | Hakuna hatua madhubuti zilizochukuliwa | Hakuna |
| | NEC ikemee vitendo vya vyombo vya habari vya umma kufanya upendeleo wa chama kimoja | NEC, Vyombo vya habari vya umma | Hakuna hatua madhubuti zilizochukuliwa | Hakuna |
| | Tume ya utangazaji Tanzania inatakiwa kuandaa vigezo vya wajibu wa watangazaji binafsi wa masuala ya uchaguzi kwa lengo la kuhakikisha kwamba vyombo binafsi vya utangazaji vinatoa fursa sawa kwa vyama vyote | Tume ya Utangazaji Tanzania | Hakuna hatua zilizochukuliwa | Hakuna |

*Kiambatanisho namba 6: Mapendekezo ya TEMCO ya Kuboresha Mchakato wa Chaguzi 2005*

| Aina ya mapendekezo | Mapendekezo | Mamlaka husika | Hatua zilizochukuliwa | Maoni |
|---|---|---|---|---|
| Usimamizi wa michakato ya uchaguzi | Ipo haja ya kuchukua hatua za kuiwezesha NEC kuwa huru | NEC, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania | Hakuna hatua madhubuti zilizochukuliwa | Hakuna |
| | NEC ihusishe wadau wengine katika utoaji wa elimu kwa mpiga kura | NEC, wadau wengine wa uchaguzi | Hakuna hatua madhubuti zilizochukuliwa | Utoaji wa elimu ya mpiga kura bado hauridhishi |
| | NEC iimarishe mahusiano ya karibu kati yake na kitengo cha TEHAMA ili kukabiliana na changamoto mbali mbali hasa zile zinazotokana na BVR | NEC | Ukaribu kati ya NEC na kitengo cha TEHAMA umeongezeka | Matumizi ya mifumo na vifaa vya TEHAMA yamesaidia kuongeza ufanisi wa NEC |
| | | | | |
| Uandikishaji wapiga kura | Ajira za maafisa uchaguzi zizingatie vigezo vya weledi | NEC | Hakuna hatua madhubuti zilizochukuliwa | Hakuna |
| | Daftari la kudumu la wapiga kura liboreshwe | NEC | Hakuna hatua madhubuti zilizochukuliwa | Zoezi la kuboresha daftari la kudumu la mpiga kura bado si endelevu |
| | | | | |
| Uteuzi wa wagombea na kampeni | Gharama za kampeni za uchaguzi zifanyiwe mapitio kwa lengo la kusaidia vyama vidogo | NEC, Vyama vya siasa,Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania | Hakuna hatua madhubuti zilizochukuliwa | Hakuna |
| | Gharama za uchaguzi ziwe wazi | NEC, Vyama vya siasa, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania | Sheria ya gharama za uchaguzi ilitungwa mwaka 2010 | Utekelezaji wa sheria hii bado hauridhishi |
| | | | | |
| Kupiga kura, kuhesabu kura na kutangaza matokeo | NEC ihakikishe kwamba daftari la kudumu la mpiga kura lina taarifa sahihi | NEC | Japo bado yapo magungufu kadhaa, NEC imechukua hatua madhubuti kuhakikisha usahihi wa taarifa za mpiga kura | Pamoja na mapungufu kadhaa, usahihi wa taarifa za mpiga kura katika mfumo wa BVR unaridhisha |
| | Muda wa kufungua na kufunga kituo cha kupigia kura uongozwe hadi saa | NEC | Hakuna hatua madhubuti zilizochukuliwa | Hakuna |

| Aina ya mapendekezo | Mapendekezo | Mamlaka husika | Hatua zilizochukuliwa | Maoni |
|---|---|---|---|---|
| | mbili asubuhi na saa kumi na moja jioni | | | |
| | NEC needs to ensure that its website is and remains up to date | NEC | Hakuna hatua madhubuti zilizochukuliwa | Tofuti hii imekuwa si ya kutegemewa sana |
| | | | | |
| Vyombo vya habari | Sekta ya vyombo vya habari iwekeze katika uandishi wa kiuchunguzi | Sekta ya vyombo vya habri | Hakuna hatua madhubuti zilizochukuliwa | Kiwango cha uandishi wa kiuchunguzi bado kiko chini |
| | Kuwe na mazingira rafiki kwa utendaji kazi wa vyombo vya habari | Vyombo vya habari | Hakuna hatua madhubuti zilizochukuliwa | Hakuna |
| | Vyombo vya habari vinatakiwa kuyafikia maeneo ya mijini na vijijini | Vyombo vya habari | Hakuna hatua madhubuti zilizochukuliwa | Bado vyombo vingi vya habari vinajikita maeneo ya mijini |
| | Vyombo vya habari viweke vigezo vya haki na heshima vinapojadili masuala ya kabila, rangi na jinsia | Vyombo vya habari | Vigezo hivi vimezingatiwa kwa kiwango cha juu | Hakuna |
| | Wadau wa kisiasa watumie fursa ya vyombo vya habari kujinadi | Vyama vya siasa | Matumizi ya vyombo vya habari hasa kwa vyama vya siasa yameimarika sana | Pamojana ongezeko la matumizi ya vyombo vya habari, vyombo hivi vimekuwa na tabia ya upendeleo |

*Kiambatanisho namba 7: Mapendekezo ya TEMCO ya Kuboresha Mchakato wa Chaguzi 2010*

| Aina ya mapendekezo | Mapendekezo | Mamlaka husika | Hatua zilizochukuliwa | Maoni |
|---|---|---|---|---|
| Usimamizi wa michakato ya uchaguzi | Uteuzi wa makamishna wa NEC unatakiwa kuwa wazi na usio na mlengo wa upendeleo wa kisiasa | NEC, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania | Hakuna hatua madhubuti zilizochukuliwa | Hakuna |
| | Mamlaka ya rais kuteua maafisa mbalimbali kama vile mkurugenzi wa uchaguzi na wakuu wa vyombo vya habari vya umma utazamwe upya | Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania | Hakuna hatua madhubuti zilizochukuliwa | Hakuna |
| | Iwepo mipaka ya majukumu katika utekelezaji wa sheria ya gharama za uchaguzi. | Msajili wa vyama vya siasa; NEC | Hakuna hatua madhubuti zilizochukuliwa | Hakuna |
| | Ipo haja ya kuuelimisha umma juu ya sheria ya gharama za uchaguzi | Msajili wa vyama vya siasa; NEC | Hakuna hatua madhubuti zilizochukuliwa | Kiwango cha uelewa wa sheria hii kwa wadau wengi wa uchaguzi bado kipo chini |
| | Vyama vya siasa viboreshe na kuimarisha uwepo wake katika maeneo ya vijijini | Vyama vya siasa | Hakuna hatua madhubuti zilizochukuliwa | Bado vyama vingi vya siasa vina tabia ya kuonekana kuwa hai tu wakati wa kipindi cha uchaguzi |
| | Vyama vya siasa viongeze uwezo wake wa usimamizi wa fesha ili kusadia utekelezaji wa sheria ya gharama ya uchaguzi | Vyama vya siasa | Hakuna hatua madhubuti zilizochukuliwa | Vyama vya siasa bado havitii sheria hii |
| | Vyama vya siasa na wagombea viheshimu utawala wa sheria | Vyama vya siasa | Vyombo vya dola vimekuwa makini kuhakisha utawala wa sheria unaheshimiwa | Usingatiaji wa utawala wa sheria wakati wa uchaguzi umekuwa ni wa kiwango cha kuridhisha |
| | | | | |
| Uandikishaji wa wapiga kura | Daftari la kudumu la mpiga kura liboreshwe mara kwa mara | NEC | Hakuna hatua madhubuti zilizochukuliwa | Bado zoezi la kuboresha daftari la wapiga kura si endelevu |
| | Usimamizi wa uchaguzi uongozwe na misingi ya weledi ili kuhamasisha ushiriki wa Wananchi wengi katika michakato ya uchaguzi | NEC | NEC has tried much to professionally manage elections<br>NEC imejitahidi kwa kiwango cha kuridhisha katika | Pampja na mapungufu kadhaa, NEC imekuwa imajitahidi kusimamia uchaguzi kwa kutumiamisingi ya weledi. |

| Aina ya mapendekezo | Mapendekezo | Mamlaka husika | Hatua zilizochukuliwa | Maoni |
|---|---|---|---|---|
| | | | kusimamia uchaguzi kwa weledi | |
| | Utoaji elimu ya mpiga kura uwe endelevu | NEC, ZEC, wadau wengine wa uchaguzi | Hakuna hatua madhubuti zilizochukuliwa | Utoaji wa elimu ya mpiga kura hauridhishi |
| | Ipo haja ya kuchochea uanzishwaji wa redio za jamii hasa maeneo ya vijijini | Wadau wote wa uchaguzi | Idadi ya redio za jamii katika maeneo ya vijijini imeongezeka sana | Redio hizi zimekuwa tegemeo la wengi katika utoaji elimu ya ,piga kura hasa maeneo ya vijijini |
| | | | | |
| Uteuzi wa wagombea na kampeni | Mgombea anayepita bila kupingwa apigiwe kura | NEC | Hakuna hatua madhubuti zilizochukuliwa | Hakuna |
| | Vyama vya siasa vichukue hatua madhubuti kukomesha vitendo vilivyo kinyume na sheria wakati wa uteuzi wa wagombea ndani ya vyama | Vyama vya siasa | Hakuna hatua madhubuti zilizochukuliwa | Bado rushwa imekithiri wakati wa uchaguzi |
| | Ipo haja ya kuongeza kipindi cha kampeni ili kuwafikia wapiga kura wengi | NEC | Hakuna hatua madhubuti zilizochukuliwa | Hakuna |
| | Kuna haja ya kubadili sheria za uchaguzi ili kuruhusu mgombea binafsi | Msajili wa vyama vya siasa; NEC | Suala la mgombea binafsi limependekezwa katika katiba mpya iliyopendekezwa | Japo suala hili limeongelewa katika katiba iliyopendekezwa bado kuna dukukduku juu ya masharti magumu ya kuwa mgombea binafsi |
| | Hatua za dhati zichukuliwe ili kuondoa upendeleo wa kimfumo wakati wa uchaguzi | NEC, Msajili wa vyama vya siasa; NEC | Hakuna hatua madhubuti zilizochukuliwa | Bado vyama vya upinzani vinalalamikia upendeleo wa kinfumo |
| | Vyama vya siasa na wagombea wazingatie na kuheshimu kanuni za maadili | Vyama vya siasa na wagombea | Japo hakuna usimamizi madhubuti kutoka NEC, kanuni za maadili zimekuwa zinaheshiwa kwa kiwango kikubwa | Wakati mwingine vyama vimekuwa vinakiuka haya maadili |
| | Vyama vya siasa vijiepushe na matumizi ya lugha za matusi, | Vyama vya siasa | Hakuna hatua madhubuti zilizochukuliwa | Matumizi ya lugha ya matusi bado ni makubwa |

| Aina ya mapendekezo | Mapendekezo | Mamlaka husika | Hatua zilizochukuliwa | Maoni |
|---|---|---|---|---|
| | kuchochea vurugu, ikiwa na pamoja na kukiuka sheria na kanuni za uchaguzi | | | |
| | Vyama vya siasa viandae ilani za uchaguzi zinazojitosheleza | Vyama vya siasa | Upo utofauti baina ya vyama katika uandaaji wa ilani za uchaguzi | Vyama vingi vya siasa bado ni dhaifu katika kuandaa ilani za uchaguzi |
| | | | | |
| Kupiga kura, Kuhesabu kura na kutangaza matokeo | Kuna haja ya kufanya utafiti kubaini chanzo cha mwitikio mdogo wa wananchi katika uchaguzi | Wadau wa uchaguzi | UNDP ilifanya ilifadhili utafiti huu mwaka 2011 | Mapungufu ya utafiti huu ni kwamba haukuwekwa wazi kwa wadau wengi wa uchaguzi |
| | Mchakato wa kutangaza matokeo ufanyike kwa haraka na kwa ufanisi | NEC | Matumizi ya BVR ni mojawapo ya mikakati ya kuboreshwa kwa utangazaji wa matokeo haraka | Bado ucheleweshaji wa kutangaza matokeo ni tatizo sugu |
| | Matokeo ya urais yapingwe mahakamani | NEC, Vyam vya siasa, wagombea | Suala hili limezngatiwa katika Katiba iliyopendekezwa | Hakuna |
| | | | | |
| Ushiriki wa wanawake katika uchaguzi | Ushiriki zaidi wa wanawake katika vyombo vya maamuzi upewe kipaumbele | Wadau wote wa uchaguzi | Usawa wa kijinsia umepewa kipaumbele zaidi | Pamoja na mafanikio haya, bado nafasi ya mwanamke katika vyombo vya maamuzi ni ndogo |
| | Vyama vya siasa viandae mikakati ya kuchochea ushiriki wa wanawake katika uchaguzi wakiwa kama wapiga kura au wagombea | Wadau wote wa uchaguzi | Usawa wa kijinsia umepewa kipaumbele zaidi | Pamoja na mafanikio haya, bado nafasi ya mwanamke katika vyombo vya maamuzi ni ndogo |
| | Uteuzi wa wanawake katika nafasi za viti maalum uwe wazi na shirikishi | Vyama vya siasa, NEC | Hakuna hatua madhubuti zilizochukuliwa | Uteuzi wa wanawake katika nafasi hizi umetawaliwa na vitendo vya rushwa na upendeleo |
| | | | | |
| Rushwa Wakati wa Uchaguzi | Vyama vya siasa vijiepushe na vitendo vya rushwa | Vyama vya siasa, wagombea, NEC, Msajili wa vyama vya siasa , polisi | Hakuna hatua madhubuti zilizochukuliwa | Pamoja na uwepo wa sheria ya gharama za uchaguzi, vitendo vya rushwa wakati wa uchaguzi bado vimekithiri |
| | | | | |

| Aina ya mapendekezo | Mapendekezo | Mamlaka husika | Hatua zilizochukuliwa | Maoni |
|---|---|---|---|---|
| Vyombo vya Habari | Vyombo vya habari vya serikali vitoe fursa kwa vyama vya upinzani bila upendeleo | Vyombo vya habari vya umma | Hakuna hatua madhubuti zilizochukuliwa | Vyombo vya habari vya uma bado vinalalamikiwa na vyama vya upinzani kwamba vinapendelea chama tawala |
| | Uhuru wa wahariri uheshimiwe | Wamiliki wa vyombo vya habari | Hakuna hatua madhubuti zilizochukuliwa | Bado hakuna uwazi wa kutosha juu ya jambo hili |
| | Vyombo vya habari vishirki vya kutosha katika utoajielimu ya mpiga kura | Vyombo vya habari | Hakuna hatua madhubuti zilizochukuliwa | Vyombo vya habari havijashiriki vya kutosha katika kutoa elimu kwa mpiya kura |
| | Vyombo vya habari vizingatia kanuni za maadili | Vyombo vya habari | Uzingatiaji wa kanuni hizi umekuwa wa kuridhisha | Kwakuwa vyombo vya habari vinakuwa vimegawanyika wakati wa uchaguzi, kanuni hizi za maadili zimekuwa wakati mwingine zinavunjwa |
| | Kuna haja ya kuwa na sheria ya uhuru wa vyombo vya habari inayotoa fursa kwa vyombo vya habari vya serikali kuchunguzwa | Vyombo vya habari, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania | Mchakato wa kupata sheria hii bado unaendela | Pamoja na mafanikio haya, bado nafasi ya mwanamke katika vyombo vya maamuzi ni ndogo |
| | Kuna haja ya kuboresha sekta ya uandishi wa habari kwa kuanzisha mafunzo mbalimbali | Vyombo vya habari | Hakuna hatua madhubuti zilizochukuliwa | Kiwango cha weledi katika tasnia ya habari bado kiko chini |

*Kiambatanisho namba 8: Sekretarieti ya TEMCO, 2015*


| | |
|---|---|
| <br>Prof. Rwekaza S. Mukandala<br>Mwenyekiti wa TEMCO na Kiongozi Mkuu wa Timu ya Waangalizi wa Uchaguzi | <br>Dr Benson Bana<br>Meneja wa TEMCO na Naibu Kiongozi Mkuu wa Timu ya Waangalizi wa Uchaguzi |
| <br>Dr. Deogratius Rugaimukamu<br>Mchambuzi wa Takwimu | <br>Dr. Lupa Ramadhani<br>Mchambuzi wa Masuala ya Kisiasa |

| | |
|---|---|
| <br>Ms. Judith Kapinga<br>Mchambuzi wa Masuala ya Kisheria | <br>Ms. Perpetua John Bilinzozi<br>Mtaalam wa Teknolojia ya Habari |
| <br>Ms. Shani Adam<br>Afisa Utawala Msaidizi | <br>Ms. Sandra Tetty<br>Afisa Utawala |


Mr. Dunia Nassoro
Mhasibu


Mr. Charles Kayoka
Mchambuzi wa Vyombo vya Habari


Captain Patrick
Mtaalam wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano


Julius David
Mhudumu wa Ofisi